

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Tisa – Tarehe 11 Februari, 2022

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha kwa kipindi cha nusu mwaka 2021/2022 (*Monitory Policy Statement-Mid-Year Review) 2021/2022*).

Taarifa ya mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka 2020/2021 (*The Annual Report of Bank of Tanzania for the Year, 2020/2021*).

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:

Taarifa ya mwaka ya shughuli zilizotekelwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Taarifa ya mwaka ya shughuli zilizotekelizwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea. Katibu!

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali. Tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Lindi Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 92

Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya – Lindi

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH Aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Lindi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa Dugange majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Jimbo la Lindi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi. Mara baada ya kukamilika kwa ujenzi huo na kuanza kutoa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

huduma, miundombinu ya Hospitali ya Rufaa ya sasa itakuwa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuimarisha na kuboresha huduma za afya kwa wananchi Serikali tayari imekwishaipatia Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga kituo cha afya kwenye eneo la Kimkakati na lenye mahitaji makubwa. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah swalii la nyongeza.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, kwa kutuwezesha fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mapenzi yake mema, lakini naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Lindi Mjini tuna kata 20 lakini kata 13 ziko katikati ya Mji, lakini ukiangalia wananchi wale, katika kata 13 zaidi ya watu 70,000 wanakosa mahali pa kukimbilia kwa maana ya kituo cha afya. Sasa ninaomba kuiuliza Serikali watatusaidiaje kuhakikisha kwamba tunapata Kituo cha Afya Lindi Mjini kuwasaidia wakazi wa kata 13 waishio Lindi Mjini?

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pili katika Kata ya Kitumbikwela upande wa pili wa bahari pana kituo cha afya lakini bado hakijakamilika, wanawake wanapata changamoto wakati wa kujifungua na wanapolazimika kufanyiwa upasuaji, kivuko wakati mwingine kinakuwa kina changamoto.

Kwa hiyo, ninaomba kuiuliza Serikali ni lini wataweza kutusaidia kuboresha Kituo cha Afya cha Kitumbikwela ili wanawake wajawazito waweze kuhudumiwa pale? Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Jimbo la Lindi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Hamida Mohamed kwa kuwasemea kwa dhati kabisa wananchi wa Lindi Mjini na mimi nimhakikishie kwamba Serikali hii sikivu ya Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan tutaendelea kushirikiana naye na kuhakikisha kwamba wananchi wa Lindi wanapata maendeleo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vituo vya afya katika Jimbo la Lindi Mjini; ni kweli kwamba wana vituo vya afya vichache. Lakini Serikali tumeshatoa fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya cha Mnazimoja, lakini tumepeleka fedha kwa ajili ya kujenga Hospitali kubwa ya kisasa ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini bado tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea kujenga vituo vya afya katika kata za kimkakati ambazo hazina vituo vya afya.

Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba Serikali inafahamu changamoto hiyo na mipango inaanndaliwa kuhakikisha Manispaa ya Lindi tunapata vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Kitumbikwela ni kweli Kata ya Kitumbikwela ipo upande wa pili wa bahari na njia kuu ya kuvuka pale ni kwa kutumia mapantoni lakini pia na boti. Kwa hiyo, kwa kweli tunahitaji kuboresha kituo kile cha afya ndio maana tulianza ujenzi kwa awamu ya kwanza, sasa tutakwenda kujenga miundombinu iliyobakia zikiwemo wodi na majengo mengine kwa awamu ya pili ili kuhakikisha huduma zinakwenda vizuri. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwantumu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Spika, ahsante; kwa kuwa Serikali inajenga Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya nchi nzima na kwa kuwa baadhi ya hospitali za Wilaya ni kongwe.

Je, Serikali haioni haja ya kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati hospitali za wilaya ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Pangani? (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mwantumu Zodo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumekuwa na Hospitali za Halmashauri kongwe ambazo zilijengwa miaka mingei. Zipo ambazo zimejengwa baada ya uhuru mapema, lakini zipo ambazo, zilijengwa hata kabla ya uhuru na kwa kweli miundombinu yake sasa ni chakavu. Lakini pia haziendani na kiwango cha hospitali za halmashauri ambazo sasa tunazhitaji. Kwa kutambua hilo Serikali tumefanya tathmini ya hospitali zote za Halmashauri kongwe na tumekwisha ziainisha. Tunaweka mpango, baada ya kukamilisha hospitali za Halmashauri 28, sasa tutakwenda kukarabati na kupanua hospitali zile kongwe ikiwepo Hospitali hii ya Pangani. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, sasa aulize swalii lake.

Na. 93

Uhaba wa Watumishi katika Idara ya Elimu - Mkoa wa Lindi

MHE. TECLA M. UNGELE aliuliza:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza uhaba wa watumishi katika Idara ya Elimu katika Mkoa wa Lindi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais -TAMISEMI ilifanya tathmini ya mahitaji ya walimu katika shule za msingi na sekondari nchi nzima na kubaini kuwa Mkoa wa Lindi unauhitajii jumla ya walimu wa shule za msingi 4,760 na waliopo ni 3,544 ikiwa ni upungufu wa walimu 1,216 sawa na asilimia 25.5 ya mahitaji. Kwa upande wa shule za sekondari, Mkoa wa Lindi unahitaji walimu 4,580 na waliopo ni 1,682 na upungufu ni walimu 2,898 sawa na asilimia 63.3 ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo nchini kote Serikali imetoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuhakikisha wanafanya msawazo wa walimu katika maeneo yao.

Pili, Serikali inakamilisha muongozo wa walimu wa kujitolea, utakaotumika kuwapata walimu wanaojitolea katika shule zenyenye uhitaji mkubwa. Walimu hao wanaojitolea watatambulika rasmi kuititia mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kupata chanzo sahihi cha kurejea utendaji kazi wao.

Tatu, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeomba kibali cha kuajiri walimu 10,000 katika shule za msingi na sekondari nchini ikiwemo Mkoa wa Lindi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Tecla Ungele swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. TECLA M. UNGELE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi katika Mkoa wa Lindi na hii inaleta ufaulu hafifu kwa wanafunzi katika masomo hayo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupatikana walimu wa sayansi kwa haraka iwezekanavyo kunusuru shida hiyo? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia naona kwenye majibu kuna upatikanaji/kibali cha kuajiri walimu 10,000. Katika hilo naomba sana Serikali watupe kipaumbele Mkoa wa Lindi, kwa sababu tuna changamoto kubwa ya walimu. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa na upungufu wa walimu wa sayansi katika shule zetu za sekondari nchini kote na tumefanya tathmini, kubaini mahitaji ya walimu wa sayansi angalau kuwezesha shule zetu kuwa na walimu wanaoweza kutosheleza mahitaji ya wanafunzi. Ndio maana katika ajira zilizopita asilimia 75.5 ya walimu wote walioajiriwa walikuwa ni walimu, wa masomo ya sayansi na utaratibu wa kuendelea kutoa kipaumbele kwa walimu wa sayansi katika ajira zinazofuata utaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la kibali cha walimu katika halmashauri hiyo kupewa kipaumbele katika walimu 10,000, tutawapa kipaumbele na kazi iliyofanyika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tumeainisha Mikoa yote yenye upungufu mkubwa zaidi wa walimu na watumishi wengine. Mikoa hiyo na Halmashauri hizo zitapewa kipaumbele wakati wa kuajiri watumishi hao. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mkundi swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru; Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ina upungufu wa watumishi zaidi ya 1,700 wa kada ya ualimu. Kwa sababu za kijiografia watumishi wengi wamekuwa wakipangangiwa wanaripoti baadaye wanaondoka.

Sasa Serikali haioni sababu za msingi na kwa sababu maalum kutoa kipaumbele kwa watu wenye taaluma ya ualimu, wazawa wa Ukerewe wakaajiriwa na wakapangangiwa eneo la Ukerewe kuweza kuwasaidia watu wa jamii ile? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto ya baadhi ya watumishi hasa wanaojiriwa katika maeneo ya Halmashauri za vijijini kuomba uhamisho mapema mara baada ya kuajiriwa. Lakini mambo mawili yamefanyika Serikalini; la kwanza, katika ajira zilizopita tulihakikisha kila anayeomba ajira anaomba ajira kwa maana ya shule husika na Halmashauri husika. Tulikubaliana katika mikataba kwamba lazima wakae angalau miaka mitatu katika vituo vyao vile ambavyo wameajiriwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, suala hilo litakuwa endelevu tutahakikisha kwamba mtumishi yeoyote anayeajiriwa, akishaajiriwa katika Halmashauri na shule hiyo lazima akae angalau miaka mitatu ili kuepusha wimbi la kuhama kwa maeneo ya vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala la kuwa na watumishi wazawa ni jambo jema na tumeendelea pia kuwapa kipaumbele. Lakini pia tunapenda utaifa kwa maana ya kwamba, waalimu wanaotoka Ukerewe waende maeneo mengine, lakini wanaotoka maeneo mengine waende pia Ukerewe ili kujenga utaifa wa nchi yetu, badala ya kuwa na watu wa aina moja katika eneo lile. Lakini tutaendelea kuhanakisha kwamba waalimu wanaopangiwa maeneo hayo, wanabaki na pia tunaendelea kudhibiti sana uhamisho katika maeneo hayo, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Husna Sekiboko swali la nyongeza.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana; pamekuwa na wimbi la vijana wengi waliomaliza vyuo vya elimu, kujitolea kwenye shule zetu za TAMISEMI.

Je, Serikali imejipanga vipi ku-*accommodate* vijana hao katika kibali cha ajira kilichotoka cha kuajiri vijana 10,000? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Swali hilo pia ni mahususi kwa takwimu hizo alizozitaja Mheshimiwa Mbunge. Kama unayo majibu tusaidie lakini kama huna majibu lije kama swali la msingi. Maana liko mahususi kwa ajili ya hizi nafasi ambazo zimetoka sasa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumekuwa na walimu wanaojitolea katika shule zetu za Serikali, lakini pia na watumishi wa kada nyingine wakiwemo watumishi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wataalam wa afya. Utaratibu ambao umewekwa na Serikali ni kuhakikisha wakati tunakwenda kutoa ajira kupertia vibali vyta Serikali, wale waalimu ambao wanatambulika rasmi wanajitolea katika shule zile wanapewa kipaumbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ndio maana kwenye jibu langu la msingi nimesema kwamba tunakwenda kuweka utaratibu wa kutumia mfumo wa kielektroniki, ambao utawatambua rasmi walimu na watumishi wengine wanaojitolea ili wapewe kipaumbele kwenye ajira zinazofuata. Kwa hiyo, hili tumelichukua tunaendelea kulifanya kazi ili kuweza kurahisisha utendaji wake. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana.

Halafu Waheshimiwa Wabunge ninavyoelekeza maswali kwamba yaulizwe kama maswali ya msingi na kuipa nafasi Serikali ili itoe majibu mahususi kwa ajili ya wananchi tunaowawakilisha, niliona chombo cha habari fulani hivi kama kimeonesha kwamba Mbunge kauliza swali gumu, ndio maana Waziri kapewa nafasi ya kuja kujibu likiletwa swali kama swali la msingi. Jambo hilo hakuna uhalisia kwa sababu mimi hapa mbele, pamoja na shughuli zingine kazi yangu ya msingi ni kusimamia Kanuni. Kwa hiyo, maswali ya nyongeza lazima yaendane na swali la msingi. (*Makof*)

Kwa hiyo, yakiwa kidogo yametoka maana yake Serikali haitaweza kujibu majibu yale ambayo wananchi wetu wanataka kuyasikia kutoka Serikalini. Kwa hiyo, sio kwamba kuna swali gumu hapa ndani ambalo linaweza kumshinda Waziri ye yote kujibu. Hoja ni kwamba, lazima swali la nyongeza liendane na swali la msingi hiyo ndiyo hoja.

Kwa hiyo, niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge saa nyingine hivi vyombo vyta habari, hata sisi wenyewe tunaweza kuwa tunahusika huko kuonyesha kwamba tunafanya kazi nzuri. Lakini Wabunge mnafanya kazi nzuri hata bila maswali magumu. (*Makof*)

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Omar Issa Kombo Mbunge wa Wingwi sasa aulize swalı lake.

Na. 94

Kugawa Miradi ya Maendeleo ya Muungano Zanzibar

MHE. OMAR ISSA KOMBO aliuliza: -

Je, Serikali inatumia utaratibu gani wa kugawa miradi ya maendeleo kama shule, barabara na afya inayotokana na Muungano na ina mkakati gani wa kuyapa kipaumbele maeneo ya vijijini ikiwemo Jimbo la Wingwi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Dkt. Jaffo majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi kama ifuatavyo:-

(a) Serikali zetu zote mbili Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zina dhamira ya dhati ya kuhakikisha kuwa utaratibu wa kugawa miradi ya maendeleo ya Muungano kama shule, barabara na afya unafanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizokubaliwa na pande zote mbili za Muungano. Vipo vigezo vinavyotumika katika kutoa fedha za kugharamia miradi ya Muungano kama vile Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo na Sheria nyinginezo zinazotumika kwa pande mbili za Muungano.

(b) Sambamba na hilo, Serikali kupitia misaada ya kibajeti (*general budget support*) hugawa fedha hizo kwa kigezo kilichokubalika kutumika cha asilimia 4.5 kwa Serikali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Mapunduzi ya Zanzibar. Aidha, fedha hizo hugawanywa kwenye miradi ya maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele veya Serikali ya Mapunduzi ya Zanzibar.

(c) Kwa upande wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Tanzania (*TASAF*) Awamu ya *Tatu Mzunguko* wa Pili uliozinduliwa Februari, 2020, shilingi bilioni 112.9 zimepangwa kutumika Zanzibar ikiwemo katika miradi ya kijamii ambapo kipaumbele ni kwenye maeneo yenye mahitaji zaidi.

(d) Serikali itaendelea kutekeleza vigezo na tatatibu zilizokubaliwa na pande mbili za Muungano pamoja na kuimarisha majadiliano na mashirikiano kwa lengo la kuhakikisha kuwa miradi inayokubaliwa inatatua changamoto zinazowakabili wananchi waliopo maeneo ya vijiji wakiwemo wa Jimbo la Wingwi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Omar Issa Kombo swali la nyongeza.

MHE. OMAR ISSA KOMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu, lakini pamoja na majibu mazuri nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine Wabunge kutoka Zanzibar, pamoja na majukumu mengine tunatakiwa kuwaeleza wananchi wa Zanzibar juu ya umuhimu na faida za Muungano wetu. Kwa kujua hilo, je, Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haionti ipo haja ya kuwashirikisha Wabunge kutoka Zanzibar katika uibuaji wa vipaumbele veya miradi inayotokana na fedha za Muungano?

Pili, Mheshimiwa Waziri katika Mkutano wa Nne aliniaihidi kwenda Jimboni kwangu kutembelea vijiji vya Mjini Wingwi na Sizini.

Je, ananiahidi ni lini tutakwenda kutekeleza ahadi hiyo? Ahsante. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri wazi kwamba kwa kweli Wabunge kutoka Zanzibar wamekuwa na kipaumbele sana cha kushughulikia changamoto za wananchi wa Zanzibar akiwemo ndugu yangu Omar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba niliahidi kwenda ni kweli, bahati nzuri nilishafika Zanzibar mpaka Jimbo la Nungwi, Jimbo la Amani na maeneo mengine, lakini nikuhakikishie kwamba ahadi yangu ya kufika katika eneo lako la kazi lipo pale pale tutaenda kuchapa kazi ondoa hofu katika hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kushirikisha Wabunge wa Zanzibar naomba niwashukuru, hata hii ajenda ukiangalia fedha za *Covid*, Wabunge wa Zanzibar mlileta fedha mahsusii hapa wakati mchakato wa barabara ulipokuwa ukifanyika ndio maana hata suala zima la fedha za *Covid* unaona kwamba zaidi ya shilingi bilioni 231 zimeenda upande wa Zanzibar lengo ni kuona kwamba hisia za Wabunge wa Zanzibar zimeonekana kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba yale Wabunge wanayoyachangia humu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo lazima iwe shirikishi.

Mheshimiwa Spika, hiyo, hilo jambo ni zuri, tutaendelea kuboresha zaidi jinsi gani Wabunge watashiriki vizuri katika kuibua hoja mbalimbali. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, Mbunge wa Mvomero sasa aulize swali lake.

Na. 95

Ujenzi wa Barabara ya Mzumbe hadi Mgeta

MHE. JONAS V. ZEELAND aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya kutoka Mzumbe hadi Mgeta?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas Van Zealand, Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo: -

Barabara ya Mzumbe – Mgeta yenyeye urefu wa kilometra 26 ni sehemu ya barabara ya Mkoa ya Sangasanga – Langali – Luale hadi Kikeo yenyeye urefu wa kilometra 59.16 na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

Mheshimiwa Spika, Ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mzumbe - Mgeta yenyeye urefu wa kilometra 26 imeanza kutekelezwa kwa awamu ambapo mwaka 2020 Serikali ilikamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami wa kipande cha mita 400 kuanzia Mzumbe na katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali inaendelea na ujenzi wa kipande kingine cha mita 700 kwa shilingi 216,800,000 na kazi ilianza Novemba, 2021 na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2022. Sehemu iliyobaki itaendelea kujengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iendelee kupitika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 kiasi cha shilingi 664,557,000 kimetengwa kwa kazi hiyo. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, swali la nyongeza.

MHE. JONAS V. ZEELAND: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nichukue nafasi hii niipongeze Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa changamoto ya barabara iliyopo Mzumbe kwenda Mgeta inafanana kabisa na changamoto ya barabara kutoka Turiani kwenda Mziha mpaka Handeni.

Je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami kutoka Turiani kwenda Mziha hadi Handeni?

Swali la pili, kwa kuwa tuna barabara ambayo ndiyo inasafirisha mazao ya wananchi wetu kutoka Kata ya Kibati, Pemba na Wilaya jirani ya Kilindi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuiongezea bajeti hii barabara ili iweze kutengenezwa kwa kiwango cha kuridhisha na iweze kupitika nyakati zote, lakini pia na kujenga daraja ambalo ni muhimu sana linalounganisha Wilaya ya Kilindi na Wilaya ya Mvomero katika Kata ya Kibati na Kata ya Kinde? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri naona maswali matatu hapo yameulizwa, lakini anaruhusiwa kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kwa hiyo jibu swali la kwanza na swali la pili.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE.ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee pongeze alizozitoa kwa Serikali kuendelea kufanya kazi katika barabara ambayo ameisema katika swali lake la msingi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika barabara aliyoisema ambayo inaanzia Magole – Turiani – Mziha, kipande cha Mziha - Handeni ambacho bado hakijajengwa barabara hii imetengewa bajeti katika mwaka huu wa fedha. Hivyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira kadri fedha zitakapopatikana barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Tanga - Turiani hadi Handeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Kibiti ambayo inaenda Kilindi, Tuko kwenye kipindi cha bajeti, ameomba bajeti iongezwe ili tuweze kujenga kwa kiwango kizuri zaidi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ombi hilo tumelipokea na tutaangalia namna ya kulifanyia kazi. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Amsabi Mrimi.

MHE. JEREMIAH M. AMSABI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana; ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne pamoja na Rais wa Awamu ya Tano ya ukamilishaji wa ujenzi wa lami kipande cha Mnata -Mugumu mpaka Arusha? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, barabara ya Nata – Mugumu kwenda Arusha ni barabara ambayo inaanzia Makutano-Sanzate – Nata – Mugumu na kuelekea Arusha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba hadi tunavyoongea mkandarasi yupo *sige* kujenga kilometra 40 kuanzia Sanzate kwenda Nata na baada ya Nata tunafuata Nata kwenda Mugumu. Kwa hiyo, Serikali ina mpango wa kuhakikisha kwamba barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha lami kadri fedha itakavyoendelea kupatikana. Ahsante. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Pallangyo swali la nyongeza.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne ambaye aliitoa mwaka 2012 ya kuijenga barabara ya Sangisi - Akeri hadi Ndorombo kwa kiwango cha lami. Ahadi hiyo aliitoa wakati wa mazishi ya aliyekuwa Mbunge wetu Marehemu Jeremiah Sumari? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja na kwa kuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Awamu ya Nne, naomba nimbakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili tutalichukua kwa uzito mkubwa na ikiwezekana baada ya kipindi hiki cha Bunge tukutane tuone kwa nini imechukua muda mrefu ili tuweze kuona namna ya kutimiza ahadi ya Kiongozi wa Taifa. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Zacharia Issaay swali la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom – Mkalama – Meatu ni barabara muhimu sana kwa wakazi wa majimbo hayo niliyoyataja.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi hii barabara huwa kila siku najiuliza haya majina yanayotajwa na kila siku inauliziwa barabara hiyo tu, maana naona na Mbunge wa nyuma yako hapo anataka kusimama aseme barabara hiyo hiyo tu. Karibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, kama ulivyo sema barabara hii ya kutoka Karatu – Mbulu – Hydom - Sibiti kuja Lalagwa – Maswa – Kolandoto ni barabara ambayo inaunganisha mikoa mingi, tayari tupo kwenye manunuzi kipande cha Mbulu – Hydom. Pia Daraja la Sibiti kama nilivyo jibu kwenye maswali mengine limeshakamili ka na tunategemea kuongeza kilometra 20 pande zote kwenye barabara hiyo. Hali kadhalika, kuanzia Kolandoto tupo kwenye mpango wa kutafuta fedha kuanza ujenzi kutokea Kolandoto kwenda Sibiti. Ahsante. (*Makofisi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijiini sasa aulize swali lake.

Na. 96

Ujenzi wa Daraja la Kalebe – Bukoba Vijijiini

MHE. JASSON S. RWEIKIZA aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa Daraja la Kalebe utaanza na kukamilika kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijiini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Daraja la Kalebe lenye urefu wa mita 32.56 lipo katika barabara ya Kyaka II – Kanazi – Kyetema yenye urefu wa kilometra 60.65. Barabara hii ni ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja la Kalebe umejumuishwa katika mradi wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kyaka II – Kanazi – Kyetema ambao unatekelezwa chini ya Mhandisi Msauri *Luptan Consult Ltd.* kwa kushirikiana na Mhandisi *Consultancy* kwa gharama ya shilingi milioni 340.035. Kazi hii imeanza tarehe 31 Disemba, 2021 na unatarajiwa kukamilika tarehe 30 Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, baada ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo pamoja na barabara hiyo. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza swali la nyongeza.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Swali la kwanza; kwa kuwa huko nyuma nimewahi kuuliza swali hili humu ndani la barabara hii na daraja hili na nikapewa majibu yanayofanana hivyo huko nyuma zaidi ya mara mbili.

Je, ni lini nitapewa majibu ambayo yanatia moyo zaidi na matumaini zaidi kuliko hayo majibu niliyopewa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa barabara hii inafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kama alivyosema Mheshimiwa Waziri na kazi hiyo inakaribia kukamilika, na kwa kuwa barabara hii na daraja hili linahudumia kata 18 kati ya kata 29 za Jimbo langu, na kwa kuwa hii pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano.

Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa na kukamilika? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kufuatilia sana hii barabara. Ametaka Serikali impe maneno ya matumaini, naomba niseme siyo tu maneno ya matumaini lakini atakubaliana nami kwamba Wakandarasi sasa hivi wapo *site* wakiwa wanafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba daraja alilolisema litatekelezwa kwanza kabla halafu wata-submit document lianzé kujengwa halafu ndiyo upembuzi na usanifu wa kina wa barabara uendelee wakati daraja hili linajengwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Rweikiza awe na imani kwamba kwamba Serikali ya Awamu ya Sita ipo kazini na wananchi wawe na matumaini kwamba walichoahidi Marais kinatekelezwa. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Oliver Semuguruka.

Na. 97

Kufanya Uchunguzi wa Ugonjwa wa Saratani – Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA K.n.y. MHE. KABULA E. SHITOBELA aliuliza:-

Je, Serikali imefikia wapi kuhusu kufanya uchunguzi ili kujua chanzo cha ugonjwa wa saratani katika Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa na ina mpango gani wa kudhibiti ongezeko la ugonjwa huo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Godwin Mollel majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mbunge wa Viti Maalum lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeshafanya utafiti wa kina nchi nzima uliosaidia kutambua kuwa Kanda ya Ziwa ni saratani zifi zinaongoza ambazo ni saratani ya kibofu cha mkojo, saratani ya mji wa uzazi wa kinamama, saratani ya damu, macho na figo. Aidha, wataalamu wamekusanya sampuli za damu za watu 7,000 ambaao hawana saratani ili kulinganisha na sampuli za damu za wenyewe saratani. Utafiti huu utasaidia kubaini chanzo cha hizo saratani. Hivyo, kwa sasa bado utafiti unaendelea na visababishi vinavyosemwa bado ni nadharia tu kutohana na shughuli za kijamii katika maeneo husika.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi sasa mpango wa kudhibiti ongezeko umejlkita katika kutoa ellmu ya afya kwa viashiria vinavyodhaniwa pamoja na kuzingatia mkakati wa kitaifa kwenye maeneo saba yaliyoainishwa ili kudhibiti viashiria vyta saratani. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu masuri ya Serikali, ninalo swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itaiwezesha hospitali zote za kanda kutoa huduma ya tiba ya kansa kwa asilimia 100?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo anahangaika na matatizo ya wananchi na akinamama wa Kagera, lakini jinsi ambavyo anashirikiana na Wabunge wa majimbo kwa kuwafuata kwenye viti vyao na kuwauliza mambo ambayo wanaweza wakafuatilia kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

pamoja. Hili linaonesha ni kwa nini umeaminika miaka iliyopita na sasa unaendelea kuaminika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, amenunua kifaa chenye thamani ya shilingi bilioni 18 ambacho ni kifaa pekee kwa Afrika Mashariki kwa sasa na viko vitano tu kwa Afrika ambacho kina uwezo wa kusaidia kupima kansa na kiko *Ocean Road* na kinazalisha mionzi ambayo ilikuwa tunaenda kuchukua Afrika Kusini. Kwa maana hiyo sasa mionzi iliyokuwa inachukuliwa Afrika Kusini hata nchi za Afrika Mashariki sasa watakuwa wanachukua hapa *Ocean Road*.

Mheshimiwa Spika, lakini hiyo haijatosha kwa Kanda ya Ziwa; kwa Kanda ya Ziwa tayari Serikali imepeleka shilingi bilioni 7.4 kwa ajili ya kuboresha miundombinu pale na kununua vifaa ili kuweza kutoa huduma pale kwa asilimla 100, *KCMCimeshapelekwa* shilingi bilioni sita kwa ajili hiyo na kwa upande wa Kanda ya Mbeya sasa hivi tukio kwenye hatua, inatakiwa ufanyike ujenzi kujenga kituo kimoja ambacho kinashughulikia kansa kwa eneo lote. Tayari michoro imeshachorwa na sasa tathmini inafanyika ili kujua sasa ni shilingi ngapi itumike hiyo kazi ianze mapema. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 98

COSTECH Kupewa Fedha za Kutosha kwa Ajili ya Programu za Vijana

MHE. JUDITH S. KAPINGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha *COSTECH* inapata fedha za kutosha kwa ajili ya kuwekeza katika *STARTUP* programu za vijana?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango wa *STARTUP* programu za vijana katika ubunifu na teknolojia kama nyenzo muhimu katika kuongeza tija na ubora katika uzalishaji wa bidhaa, utoaji wa huduma na kuzalisha ajira mpya kwa ajili ya vijana nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) inapata fedha za kutosha kwa ajili kuendeleza ubunifu na ubiasharishaji wa teknolojia ikiwemo kupitia *STARTUP* programu, mwaka 1995 Serikali ilianzisha Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia (MTUSATE).

Mheshimiwa Spika, kupitia Mfuko wa MTUSATE, kila mwaka Serikali hutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza ubunifu na matokeo ya utafiti unaofanywa nchini kwa lengo la kutatua changamoto zinazoikabili jamii. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 shilingi bilioni 3.5 zimetengewa kupitia mfuko huo. Vilevile kupitia utekelezaji wa Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Juu kwa ajili ya Mageuzi ya Kiuchumi *COSTECH* imetengewa shilingi bilioni 2.13 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake ikiwemo kujenga Mfumo wa Kielektroniki wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ambao utawezesha kusajili watafiti, wabunifu, vifaa na miradi ya utafiti na ubunifu pamoja na teknolojia zinazozalishwa hapa nchini na zinazoingia kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inashirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kuhakikisha kwamba *COSTECH*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

inawezesha miundombinu ya ukuzaji ubunifu na ubiasharishaji wa teknolojia ikiwemo uanzishaji wa *STARTUP* za ubunifu na teknolojia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Judith Kapinga, swali la nyongeza.

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante na naishukuru Serikali kwa majibu mazuri na nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, je, ni bunifu ngapi zimeweza kubiasharishwa kutokana na kupata *support* moja kwa moja na Serikali kuititia *COSTECH*?

Mheshimiwa Spika, lakini mbili, mwaka jana Serikali mlituahidi ikifika Disemba, 2021 tutaletewa Sera kuhusiana na sayansi, teknolojia na ubunifu. Sasa ningependa kupata *commitment* ya Serikali kwa sababu mwaka jana halikufanyika; sasa je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha katika mwaka huu Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu mpya inaletwa kwa sababu tuliyonayo ni ya mwaka 1996 na inahusisha sayansi na teknolojia peke yake, haina ubunifu na hivyo haiwezi kuwasaidia vijana katika kujipambanua katika masuala ya ajira ya sayansi, teknolojia na ubunifu? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba sasa kujibu kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Judith Kapinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, amezuungumzia suala la bunifu ngapi; naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kuwa kati ya bunifu 200 zilizoibuliwa kwenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mashindano yetu ya MAKISATU, jumla ya bunifu 26 zinaendelea kuendelezwa na Serikali, ili kufikia dhamira ya kubiasharishwa ili kuleta tija katika jamii. Kwa hiyo, ni bunifu hizo 26. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili amezungumzia suala la sera, naomba tukiri kwamba kulikuwa na ucheleweshaji kidogo wa sera hii yam waka 1996, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hivi sasa Wizara yangu inaendelea na mapitio ya sera hii na ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023 tutaitleta sera hiyo hapa Bungeni kwa ajili ya kupitishwa. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 99

Serikali Kuwapangia Wanafunzi wa Vyuo Maeneo ya Mafunzo kwa Vitendo

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA aliliza:-

Je, kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa mafunzo ambao utahakikisha wanafunzi wa vyuo vikuu wanapangiwa moja kwa moja maeneo ya kwenda kujifunza badala ya utaratibu wa sasa wa mwanafunzi kutafuta mwenyewe?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mitaala ya vyuo vikuu huwataka wanafunzi kukamilisha masomo kwa kufanya mafunzo kwa vitendo katika taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi. Utaratibu uliopo ni kwamba vyuo vikuu vinaainisha maeneo wanayokusudia kupeleka wanafunzi na kuomba nafasi za kufanya mazoezi kwa vitendo. Baada ya maeneo ya kufanya mazoezi kwa vitendo kupatikana, vyuo huwapatia wanafunzi barua za kuwatambulisha kwenye taasisi husika ili waweze kupokelewa.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wana uhuru pia wa kutafuta maeneo ya kufanya mafunzo kwa vitendo na kukiujlisha chuo kwa taarifa rasmi. Baada ya wanafunzi kupata nafasi katika Taasisi husika vyuo huwapa barua za utambulisho ili waweze kupokelewa na kuendelea kufanya mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa vyuo vikuu nchini kudumisha mahusiano na taasisi mbalimbali vikiwemo viwanda na kuwa na mikataba ya makubaliano ya kupeleka na kupokea wanafunzi kwenye mafunzo kwa vitendo. Nakushukuru. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa nafasi za kufanya mazoezi kwa vitendo kwa wanafunzi bado imekuwa shida sana, inakuwa kama hisani, upendeleo au kujuana kwa mara kadhaa.

Je, ni lini Serikali itaweka muongozo na kanuni ya kuelekeza taasisi za umma na za binafsi na waajiri kuweka utaratibu mzuri wa kuwapokea wanafunzi hawa bila kuhangaika sana? (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa vile majibu ya Serikali yameashiria kama hakuna tatizo kubwa kwenye zoezi hili; je, ni kwa nini Serikali isifanye utafiti wa kina wa kubaini changamoto na matatizo yanayowakumba wanafunzi hawa na kuweka utaratibu rahisi wa kupata nafasi? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba sasa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma yenyeh sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu kwenye programu hizi za mafunzo kwa vitendo na katika programu hizo tunajua kwamba tunapambana au tunakabiliana na changamoto mbalimbali.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa changamoto hizi tutaendelea kuzifanyia kazi na kuzitatu, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa vile ametoa ushauri, kwa nini tusifanye utafiti, basi naomba sasa tulichukue wazo hili twende tukafanye utafiti ili kwa pamoja kuweza kukabiliana na changamoto hizi. Nakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 100

Kuufanya Mkoa wa Morogoro Kuwa Kitovu cha Utalii

MHE. NORAH W. MZERU aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa moja ya kitovu kikuu cha utalii duniani kwa kuwa ni Mkoa wenye vyanzo vingi nya utalii?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya utalii katika Mkoa wa Morogoro, Serikali ilipandisha hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere. Sambamba na jitihada hizo, Serikali kupitia Mradi wa Kukuza Maliasili na Kuendeleza Utalii (*REGROW*), barabara zenye urefu wa takribani kilometra 996, njia za watembea kwa miguu kilometra 132.5, viwanja vya ndege saba, malango ya kuingilia wageni nane, vituo vya askari nane na vituo vya kutolea taarifa kwa wageni vitatu vitajengwa katika Hifadhi za Taifa za Mikumi, Udzungwa na Nyerere Mkoani Morogoro. Juhudi hizi zitaendelea kuchochea hali ya utalii katika Mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo katika hatua nyingine Serikali imeendelea kupandisha hadhi maeneo mbalimbali ikiwemo Hifadhi ya Wanyamapori ya Jamii ya Wami Mbiki kuwa Pori la Akiba. Vilevile kukamilika kwa reli ya mwendokasi (*SGR*) pamoja na kutumika kwa reli ya *TAZARA* kutaongeza wigo wa shughuli za utalii katika mikoa ya Morogoro na Pwani. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Norah Mzeru, swalii la nyongeza.

MHE. NORAH W. MZERU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, je, kuna mpango gani wa kuwavutia wawekezaji katika sekta ya utalii Morogoro? (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Norah Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Norah kwa kuendelea kuimarisha utalii, lakini pia kuendelea kuhamasisha katika maeneo mbalimbali ikiwemo maeneo yaliyohifadhiwa katika Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, nipende tu kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeweza kuainisha maeneo mbalimbali kwenye maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya kuwekeza na shughuli hizi za uwekezaji zinahamasishwa katika maeneo mengine mengi ambayo utalii unafanyika. Hivyo, nimtoe wasiwasi katika hifadhi ya Udzungwa, Mikumi, pamoja na Nyerere, tumetenga maeneo mahususi kwa ajili ya uwekezaji. Hivyo, tunaendelea kuwaalika wawekezaji wa ndani ya nchi na nje ya nchi waweze kufika katika maeneo hayo na kuwekeza kwa ajili ya kuongeza na kukuza utalii. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, sasa aulize swalii lake.

Na. 101

Tatizo la Mawasiliano ya Simu Kata ya Likawage

MHE. ALLY M. KASSINGE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawezesha upatikanaji wa mawasiliano ya simu katika Kata ya Likawage na vijiji vyake vya Likawage, Nainokwe na Liwiti?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa na kwa unyenyekevu kabisa naomba upokee salamu za pongezi kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Bariadi kwa wewe kuchaguliwa kwa kishindo kabisa kuwa Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote tulibaini uwepo wa changamoto ya mawasiliano ya simu katika Kata ya Likawage na vijiji vyake vyote. Hivyo, Serikali ilitangaza kata hii katika zabuni ya awamu ya tano ya mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, kata hiyo ilipata mto a huduma wa Kampuni ya Tigo iliyokamilisha ujenzi wa minara miwili mnamo mwezi Oktoba, 2021. Ujenzi wa minara hiyo umetatua tatizo la mawasiliano lilitokuwepo katika Kata ya Likawage na vijiji vyake. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Awali ya yote nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pia kwa utekelezaji wa changamoto ya mawasiliano katika Kata ya Likawage.

Mheshimiwa Spika, maswali mawili ya nyongeza; moja, kwa kuwa changamoto ya mawasiliano Kata ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Likawage imedumu kwa muda mrefu na hivyo wana Likawage wanayo furaha sana kwa ambacho Serikali imewafanya.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana kufuatana nami baada ya Bunge hili, ili kwenda kuzindua mnara huo?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, changamoto hiyo iliyopo katika Kata ya Likawage bado pia ipo katika Kata ya Kikole. Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba wanatatua changamoto ya mawasiliano katika Kata ya Kikole? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipengele cha kwanza cha swalii lake ni ombi la uzinduzi wa minara hiyo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kazi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inatekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi na sisi tuko tayari kuambatananae na kuhakikisha kwamba, mnara huo unazinduliwa ili wananchi wa eneo husika waendelee kupata huduma ya mawasiliano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala la pili ni kuhusu kata ambayo inachangamoto ya mawasiliano. Ni jukumu la Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 61(j) ambapo inatakiwa kuhakikisha kwamba tunafikisha mawasiliano kwa wananchi wote, lakini kabla ya kufanya hivyo lazima tufanye tathmini na kujiridhisha ukubwa wa tatizo na baada ya hapo tutachukua hatua ili kutatua changamoto hiyo. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, swalii la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, hali ilivyo katika Jimbo la Kilwa inafanana kabisa na hali ilivyo kwenye Jimbo la Sumve ambapo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote wakiongozana na Naibu Waziri walikuja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa minara katika Kata za Bugando, Mwandumo na Lyoma na ujenzi huo leo ni mwaka mzima haujakamilika.

Je, Wizara haioni sasa kuna umuhimu wa kuharakisha ujenzi huu ili watu wa kata hizo waanze kupata mawasiliano kama ilivyo kwenye kata zingine?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Kundo, majibu.

NAIBU WAZIRI HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA

YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kasalali, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda kwanza niongee kwamba ujenzi wa minara hii unahitaji vifaa ambayo tunaviingiza kutoka nje ya nchi na kwa sababu ya changamoto ambayo ilikuwepo ya UVIKO-19 uzalishaji wa vifaa hivi katika nchi ambazo tulikuwa tunaagiza ulipungua kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, nina uhakika kabisa, na hii sio changamoto ya Sumve kuna maeneo mengi, na Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamelalamika minara katika maeneo yao bado haijasimama kwa muda mrefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Iakini naomba nitoe taarifa kuanzia sasa mpaka mwezi wa nne tunaenda kuhakikisha minara 288 inawashwa. Hivyo, baada ya kuwashaa minara hii baadaye sasa ndio tutajua kwamba changamoto bado imebaki maeneo gani, ili tuweze kuchukua hatua. Nakushukuru sana. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 102

Hitaji la Mnara wa Mawasiliano Kata ya Mtego wa Noti - Kigoma Kusini

MHE. NASHON W. BIDYANGUZE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga mnara wa mawasiliano ya simu katika Kata ya Mtego wa Noti ili wananchi waweze kupata huduma ya mawasiliano ya simu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) ilifanya tathmini ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa kutembelea Kata ya Mtego wa Noti mnamo tarehe 19 Disemba, 2021 na kubaini kuwa kuna changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika Kata hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mtego wa Noti imeainishwa ili kuingizwa katika zabuni ijayo ya kufikisha huduma za mawasiliano ya simu inayotarajiwa kutangazwa katika mwaka huu wa fedha 2021/2022. Aidha, ujenzi wa mnara huo utaanza mara baada ya kupatikana mtoe huduma na hivyo wananchi wa kata hiyo watarajie kupata huduma za mawasiliano ya simu mara baada ya kukamilika ujenzi huo, ahsante.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze swali la nyongeza.

MHE. NASHON W. BIDYANGUZE: Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru pia kwa Serikali kutoa majibu mazuri lakini bado naomba niulize swali moja la nyongeza.

Katika Vijiji vya Ilalangulu, Chagu, Katumba na Songambele ni maeneo ambayo yanazungukwa na msitu wa Halmashauri na ambao msitu ule wakati mwingine wananchi wanapata shida ya kutekwa na hivyo kukosa mawasiliano.

Naomba Serikali itoe majibu kwamba ni lini hasa hawa wananchi nao wataweza kupata nafuu ya kupata mawasiliano kwenye vijiji vyao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema katika jibu langu la msingi na pia kwa maelekezo ya utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi Ibara 61(j) ni haki ya msingi kwa kila wananchi wanaoishi ndani ya nchi yetu kupata mawasiliano; hivyo tunaamini kabisa kwamba baada ya kufanya tathmini na kujridhisha ukubwa wa tatizo tutaenda kuchukua hatua na kuhakikisha kwamba wanafikishiwa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile katika maeneo ambayo yako pembezoni na maeneo ambayo ni ya mbuga tunaamini kwamba katika mkataba huu ambao Mheshimiwa Waziri anaenda kuusimamia ili usainiwe maeneo 90 yanaenda kupata utatuzi wa changamoto wa mawasiliano baada ya kukamilika kwa ujenzi wa minara 90.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kipindi ambacho Serikali itakuwa tayari basi tutahakikisha kwamba mawasiliano katika eneo hilo itakuwa imetatuliwa ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Zedi swal la nyongeza.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kata yangu ya Karitu ndio kata pekee ambayo bado haijapata mnara wa mawasiliano ya simu Jimboni kwangu. Zaidi ya mara mbili kata hii imekuwa kwenye orodha ya kata ambazo zinapaswa zijengewe minara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote lakini mwaka unaisha haujajengwa.

Sasa swal langu ni kwamba je, Wizara ina mpango gani au mkakati gani wa kuhakikisha kwamba kata zote zinazokuwa kwenye mpango wa kujengewa minara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote basi inajengewa kwa mwaka huo husika wa fedha?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kuhusu kata ya Karitu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge alichokisema na hili limekuwa ni tatizo kwa muda mrefu ni kwamba katika zabuni ambazo zimepita tulitangaza ujenzi wa minara katika maeneo 199 lakini watoa huduma walijitokeza katika maeneo 90. Sisi kama Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote tunatoa ruzuku, ruzuku ambayo tunayoitoa mtoa huduma anaenda kujiridhisha katika eneo ambalo anatakiwa kujenga mnara na baada ya kuona

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwamba *business case* inaonesha kabisa kwamba baada ya muda mrefu kabisa hawezি kupata faida yoyote hivyo maeneo hayo wanayakwepa.

Mheshimiwa Spika, Iakini sasa Serikali imeanzisha mazungumzo ili tuangalie namna bora ya kuhakikisha kwamba tunapotangaza maeneo haya basi maeneo yote yapate watoa huduma kulingana na *market share* ya kila mto huduma hapa nchini nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 103

Mkakati wa Kujenga Kiwanda cha Parachichi Mkoa wa Iringa

MHE. DAVID M. KIHENZILE Aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Kiwanda cha Parachichi Mkoa wa Iringa hususan Mufindi Kusini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA
Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa niaba ya Waziri Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara namba kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea na azma ya kuhamasisha ujenzi wa viwanda katika nchi yetu. Moja ya mikakati ambayo Serikali imeweka ni pamoja na kutenga maeneo katika kila Wilaya na kuweka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

miundombinu wezeshi ili kuvutia uwekezaji wa viwanda kulingana na malighafi zinazopatikana katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Mufindi, Serikali imetenga maeneo mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa viwanda ikiwemo eneo la Igowole katika Jimbo la Mufindi Kusini. Serikali inaendelea kuhamasisha wawekezaji kujenga viwanda vnavyotumia malighafi zinazopatikana Tanzania ikiwemo zao la parachichi Wilayani Mufindi, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

MHE. DAVID M. KIHENZILE: Mheshimiwa Spika, parachichi ni moja ya mazao saba ya kimkakati ambayo Serikali imeyatangaza, zao la pili kwa Mufindi Kusini ni chai.

Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu *commitment* ya Serikali katika kusaidia wakulima ambao majani yao yanamwagwa wanakosa soko na viwanda havichukui.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ziko tetesi kwamba kiwanda hicho kimeuzwa atatusaidia Mheshimiwa Naibu Waziri kama atakuwa na majibu ipi *commitment* ya Serikali juu ya maslahi ya wafanyakazi kama kweli kiwanda hicho kimeuzwa Mufindi ya Kusini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru na nimpongeze Mbunge mwenzangu kutoka Mufindi ambaye anafuatilia sana maendeleo ya wilaya hiyo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nia ya Serikali Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha tunaweka mazingira wezeshi kwa ajili ya maendeleo ya viwanda na hasa tukizingatia kuwa sekta binafsi iwe kiongozi kwa ajili ya kufikia uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, moja ya mikakati ya kukwamua maendeleo katika sekta ya viwanda ni kuhakikisha viwanda viliviyopo vinaendelea, lakini pia kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda nya parachichi; viko viwanda viwili katika mkoa wa Iringa; *Kibidula Avocado Packaging Industry* ambayo inafanyakazi vizuri, lakini pia na Kiwanda cha GBRI, Kampuni ya GBRI pale Iringa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Unilever kwa maana ya Kampuni ya Chai, sisi kama Wizara tumeshapata *notice* ya kuuzwa kwa kampuni hiyo na taarifa hizi ziliifikia Tume ya Ushindani mwaka jana mwezi Desemba kwa maana ya tarehe 17 Desemba, 2021 na hatua zinazochukuliwa kwa kampuni ambayo inauzwa huwa kwanza ni kutangaza *notice* ya siku 14 kwa wale ambao ni wadau au wanahusika katika mchakato wa kuuza. Kwa hiyo siku zile 14 ziliisha na hakukuwa na mtu ye yote mwenye maoni au malalamiko.

Mheshimiwa Spika, lakini pili sisi kama Serikali kupitia Tume ya Ushindani tunaendelea sasa kufuatilia hatua stahiki za uuuzwaji wa kampuni hiyo. Kwa ruhusa yako labda nifafanue kidogo kama utaruhusu kampuni ya Unilever ina kampuni tanzu ya Ekaterra ambayo ndiyo inasimamia sekta ya chai, sasa wanauza kwa Kampuni ya *Puchin Bidco* ambayo yenye we itachukua eneo hilo. Kwa hiyo, kwa sasa tumeshaiagiza *FCC* waendelee kufuatilia na kama kuna watu wenyе malalamiko kuhusiana na mauziano haya walete maoni au malalamiko kwenye Tume ya Ushindani.

Mheshimiwa Spika, lakini tatu kuna masuala ya maendeleo ya wafanyakazi nayo yatazingatiwa katika mchakato huo, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Shally Raymond swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, ahsante; zao la parachichi limekuweko nchini miaka nenda rudi na hata mikoa mingine likiwa ni chakula cha mbwa; hadi majuzi Serikali ilivyoanza kuona kwamba ni zao la kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatuambia nini sasa kujenga kiwanda cha kuchakata parachichi katika mkoa wa Kilimanjaro ambapo maparachichi mazuri sana yako kule Rombo, Mwika, Kahe na kwingine ambapo yanatupwa tu hadi leo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge kutoka Kilimanajro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo azma ya Serikali ni kuhakikisha tunaongeza ujenzi wa viwanda kwa kuweka mazingira wezeshi. Kilimanjaro ni moja ya maeneo ambayo yanalima kwa wingi sana parachichi hivyo basi ombi letu ni kuhakikisha na sisi kama wawekezaji tuanze kutumia fursa, kwanza tunaweka miundombinu kupitia *SIDO* changamoto kubwa tuliyonayo ni *collection centers* kutunza katika vyumba vya ubaridi matunda yale ili yaweze kuchukuliwa na wenye viwanda. Kwa hiyo kupitia *SIDO* tutaenda kuhakikisha sasa kunakuwa na ofisi katika ngazi za Halmashauri au Wilaya ili kupunguza upotevu wa mavuno ya matunda yanaposubiriwa kupelekwa kwenye viwanda ambavyo tayari viko nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Maji Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini sasa aulize swali lake.

Hitaji la Maji Kijiji cha Fundimbanga-Tunduru

MHE. HASSAN Z. KUNGU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kuwapatia maji wananchi wa Kijiji cha Fundimbanga, Kata ya Matemanga katika Jimbo la Tunduru Kaskazini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Wilaya ya Tunduru ni wastani wa asilimia 69. Katika kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Tunduru, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 inaendelea kuboresha huduma ya maji safi na salama kwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Maji Muhuvesi, Semeni, Ndaje-Mbesa kwa awamu ya pili na ukarabati wa Mradi wa Maji Njenga na Misyaje, ukarabati wa Mradi wa Maji Nalasi na Namwinyu, ujenzi wa Mradi wa Maji Masuguru, upanuzi wa Mradi wa Maji Majimaji, Chalinze, Ligoma, Makoteni na Imani, Kazamoyo na Daraja Mbili.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Matemanga ina jumla ya vijiji vinne, ambavyo ni Milonde, Changarawe, Fundimbanga na Matemanga. Katika vijiji vitatu vinapata huduma ya majisafi na salama kupitia mradi mkubwa wa maji wa Matemanga. Vilevile Kijiji cha Fundimbanga kinapata huduma ya maji kupitia visima virefu viwili vya pampu za mkono, ambavyo havitoshelezi mahitaji kwa wananchi wa kijiji hicho.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Katika kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji kwenye Kijiji cha Fundimbanga, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imekamilisha utafiti wa maji chini ya ardhi na uchimbaji wa kisima utafanyika mwezi Aprili, 2022. Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji utafanyika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Hassan Kungu, swali la nyongeza.

MHE. HASSAN Z. KUNGU: Mheshimiwa Spika, ahsante nimeridhishwa na majibu mazuri ya Serikali, lakini je, Naibu Waziri yuko tayari kuja Jimboni kwangu ili kuweza kutembelea miradi hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ombi hilo la Mheshimiwa Mbunge.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Zidadu kwa umahiri wake wa ufuatilaji wa miradi ya maji. Suala la kuja Jimboni manta hofu, nitafika. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo swali la nyongeza.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ahsante; kauli ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ni kumtua ndoo mama kichwani, lakini Tukuyu kuna shida sana ya maji, Serikali ilipanga kutoa fedha shilingi bilioni 4.5 kumaliza tatizo la maji Tukuyu mjini. Lakini mpaka sasa wamepeleka shilingi milioni 500 tu sasa akinamama wa Tukuyu hali ni mbaya sana kutafuta maji.

Sasa je, ni lini Serikali itapeleka hizo fedha kiasi cha shilingi bilioni nne ili kumaliza tatizo la maji Tukuyu mjini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mahundi majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Mbeya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli na hii si mara ya kwanza Mheshimiwa Suma Fyandomo kufuatilia na amekuwa akifuatilia kwa ushirikiano wa karibu kabisa na Mheshimiwa Mwantona na sisi Wizara ya Maji tumekaa jana, tumeshaweka kwenye mpango tunaongeza shilingi milioni 500 nyingine ili kazi ziweze kuendelea na mgao ujao tutaongeza tena shilingi milioni 500 hadi kuweza kukamilisha mradi huu muhimu kwa sababu Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan lengo ni kuona maeneo yote maji yanapatikana bombani na Tukuyu ni moja ya eneo muhimu sana na Mheshimiwa Mbunge tutafanyakazi kwa pamoja, tutaleta maji kuhakikisha wakinamama wa Tukuyu pia tunawatua ndoo kichwani.

SPIKA: Mheshimiwa Deus Sangu swali la nyongeza.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Katika Jimbo langu la Kwela Serikali ililetä fedha shilingi bilioni 2.9 kwa ajii ya mradi ndani ya kata ya Ikozi, lakini mpaka sasa mradi huo haujakamilika ni kama umetelekezwa. Nataka nijue *commitment* ya Serikali ni namna gani ambavyo watawahakikishia ndani ya muda mfupi wananchi wa kata ya Ikozi wanapata maji?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi yote ambayo tayari utekelezaji unasubiriwa ama umeanza Mheshimiwa Waziri ameshaagiza watendaji wetu mikoani wote kuhakikisha hii miradi inakamilika hivyo Mheshimiwa naomba nikutoe hofu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kazi zinakuja kufanyika mradi lazima utekelezwe. Mama Samia anasema kumtua ndoo mama kichwani siyo *option*, ni lazima. (*Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa tumalizie Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swalı lake.

Na. 105

Serikali Kuwawezesha Maafisa Ushirika Nchini

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Je, Serikali imewezesha kwa kiasi gani Maafisa Ushirika kuweza kufanya shughuli zao kwa ufanisi, ikizingatiwa kuwa kumekuwa na msukumo mkubwa sana wa kuanzisha Vyama vya Ushirika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Mavunde, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali nchini ili kujenga umoja na mshikamano katika ukuzaji uchumi wa Watanzania kuititia Ushirika. Jitihada hizo pia hufanyika sambamba na kuweka mazingira wezeshi kwa maafisa ushirika ambao wanalo jukumu la kuhamasisha uanzishwaji na uendelezwaji wa Vyama vya Ushirika. Lakini pia utoaji mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa ushirika kwa viongozi na wanachama wa Vyama vya Ushirika.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ilitenga jumla ya shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya:-

- (i) Kununua magari 13 ambayo taratibu za manunu zipo katika hatua za mwisho, pikipiki 137 zimenunuliwa ili kuwezesha ofisi za Warajisi Wasaidizi wa Mikoa 26 ya Tanzania Bara kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;
- (ii) Mafunzo ya usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini kwa Maafisa Ushirika 184 yametolewa;
- (iii) Kutoa mafunzo ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kwa maafisa ushirika 100;
- (iv) Kuunda Mfumo wa TEHAMA utakaowezesha ufuatilaji na usimamizi wa Ushirika nchini; na
- (v) Kuendelea na kazi za usimamizi na kaguzi za mara kwa mara katika Vyama vya Ushirika 9,185.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba elimu ya kutosha inatolewa kwa viongozi na wanachama wa Vyama vya Ushirika nchini. Aldha, Serikali haitasita kuwachukulia hatua kali viongozi wote wasio na uadilifu ili kuwezesha wanachama wa Ushirika wananaufaika na ushirika wao.

SPIKA: Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kazi kubwa katika kusimamia vyama vya ushirika ipo kwenye wilaya zetu.

Je, vifaa hivi vilivyozungumziwa vinaelekezwa kwenye Wilaya au Mikoa? (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Pili, Taarifa ya Shirika la Ukaguzi (*COASCO*) ya mwaka 2019/2020 inaonesha ni vyama 6,021 vilifanyiwa ukaguzi, kati ya vyama hivyo ni vyama 289 nivyo vilivyopatiwa hati safi, sawa na asilimia 4.8.

Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuwawezesha maafisa ushirika ili waweze kufanya kazi hiyo kwa ufanisi zaidi? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pikipiki hizi 137 zimeelekezwa katika Halmashauri za Wilaya na kama nilivyosema hapo awali, pamoja na hiyo pia Wizara imeona kuna umuhimu wa kuanza kuandaa bajeti ya kutenga fedha za kununua magari kwa ajili ya kusaidia zoezi la ushirika katika mikoa yetu. Kwa hiyo nimuondolee hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hii ya ushirika tunaipa thamani kubwa na tunatambua umuhimu wake katika kumuendeleza mkulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, la pili ni linalohusu kuiweshera *COASCO* kufanya ukaguzi ili kuweza kupata hali halisi ya vyama vyetu vya ushirika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti Yam waka 2021/2022 Serikali tumetenga shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunavifikia vyama vingi vya ushirika na kufanya ukaguzi. Lengo lake ni kuweza kufikia maeneo mengi zaidi kuliko ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali tumeona umuhimu na tumeendelea kuongeza katika eneo hili.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Fatma Toufiq, swalii la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa ikisisitiza uanzishwaji wa vyama vya ushirika, je, Serikali haioni kwamba umefikia wakati kuwahamasisha wananchi wa Mkoa wa Dodoma wakaanzisha ushirika ukizingatia kwamba zao la zabibu ni zao la biashara na ni zao la kimkakati?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Dodoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mazao ambayo Serikali iliyaongeza katika mazao ya kimkakati ni pamoja na zabibu. Serikali inatambua umuhimu wa zao la zabibu katika Mkoa wa Dodoma na manufaa makubwa ambayo wananchi wamekuwa wakiyapata kupitia zabibu. Hivyo, katika kuharakisha maendeleo ya zao la zabibu katika Mkoa wa Dodoma hivi sasa tayari Mrajisi ameanza na zoezi la usajili wa Vyama vya Ushirika vya Msingi 11 na ifikapo mwishoni mwa mwezi huu wataitisha mkutano wa majadiliano kupitia kamati ambayo imeundwa kwa ajili ya kuja na Chama cha Ushirika ambacho kitasimamia vyama vya msingi, lengo letu ni kuendelea kuipa thamani zabibu ya Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tayari mchakato umeanza na muda si mrefu tutakamilisha zoezi hili, na wakulima wa zabibu wa Dodoma watapata nafasi ya kuwa na chombo ambacho kitasimamia zao hili la zabibu katika Mkoa wa Dodoma.

SPIKA: Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi nitoe pongezi kwa Wizara ya Kilimo kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kufuatilia kilimo cha miwa katika Jimbo la Kilombero, na hivi karibuni Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuendelea kuboresha ushirika bado kuna baadhi ya watu wa ushirika ambao wanalamikiwa na wakulima, hususan katika Jimbo la Kilombero.

Je, Waziri ama Naibu Waziri atakuwa tayari sasa kuja Kilombero ili kufanya mkutano maalum na wakulima wa miwa na kuwasikiliza kuhusu malalamiko yao kuhusiana na ushirika?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, utayari wa kwenda Kilombero kufanya mkutano.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Abubakari na Wabunge wote wa ukanda wa Kilombero, Mtibwa pamoja na maeneo yote hayo, nitakuja mwenyewe binafsi, nitakuja kufanya mikutano na wakulima, nitafanya mikutano na viongozi wa Ushirika na makampuni ili tuweze kuyaondoa matatizo yaliyoko kwenye eneo hilo. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

MHE.BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *COASCO* ambalo linashughulika na suala la ukaguzi wa Vyama vyta Ushirika nchini limeonekana kuwa na upungufu wa *staffs* ambao kimsingi ndido wanaosimamia masuala haya ya ukaguzi. Sasa je, Serikali inasema nini kuhusiana na suala hili la kuimarisha *COASCO* ili suala zima la ukaguzi wa Vyama vyta Ushirika ikiwemo vyama vyta msingi liweze kufanyika ipasavyo?

Lakini pia nini mpango wa Serikali...

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Swali la nyongeza ni moja tu Mheshimiwa Butondo. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Butondo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tunakiri kumekuwepo na udhaifu kwenye *COASCO*. Hatua tuliyoamua kuchukua kama Wizara na mwelekeo wa Serikali kuanzia mwaka kesho *COASCO* bajeti yake ya kwenda kukagua Vyama vya Msingi na Vyama Vikuu vya Ushirika itabebwa moja kwa moja na Serikali na hawatoishi kwa kupewa fedha na Vyama vya Ushirika ambao wanakwenda kuwakagua.

Lakini la pili, sasa hivi tunafanya *capacity analysis* ili tuweze kufikia malengo ambayo tunatakiwa kuyafikia.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba ule utaratibu wa *COASCO* kwenda kukagua Chama cha Msingi ama Chama Kikuu na kuhudumiwa na chama, utaratibu huo kuanzia mwaka ujao wa fedha unakufa, bajeti yote ya ukaguzi ambayo ni ya wastani wa bilioni nne itabebwa na Wizara, nao watafanya kazi kama ambavyo tunamtenga fedha *CAG*.

SPIKA: Ahsante sana. Katibu!

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI: Uchaguzi wa Naibu Spika. (*Makofi*)

UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA

SPIKA: Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, hayo makofi nadhani yanaathiria kura za kutosha kwa Mheshimiwa Mheshimiwa Naibu Spika.

Sasa Waheshimiwa Wabunge mlishtangaziwa kwamba siku ya leo tutakuwa na uchaguzi wa Naibu Spika, na msimamizi wetu wa uchaguzi ni Katibu wa Bunge. Kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hiyo nitamwita ili atuelekeze utaratibu namna tutakavyompata Naibu Spika. Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Ahsante. Mheshimiwa Spika, baada ya kiti cha Naibu Spika kuwa wazi tulitoa taarifa kwa umma, tulipeleka taarifa kwenye vyama vya siasa vyenye sifa ya kusimamisha wagombea na tulitoa taarifa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa zote hizo tulirejea masharti ya Ibara ya 85(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 yanayoelekeza kwamba Naibu Spika atachaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge. Hivyo, vyama vya siasa vyenye sifa ya kusimamisha wagombea ni vile ambavyo vina wawakilishi humu Bungeni, yaani, Chama cha Mapinduzi, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ACT Wazalendo na Chama cha Wananchi (CUF). Aidha tulieleza kwamba mwisho wa kuleta majina ya wagombea ni tarehe 10 Februari, yaani jana, saa 10:00 jioni.

Mheshimiwa Spika, hadi kufika muda huo ni Chama Cha Mapinduzi pekee ndicho kilichokuwa kimewasilisha jina la mgombea ambaye ni Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Naibu Spika unaongozwa na utaratibu uliowekwa kwenye Kanuni ya 11 na Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni za Bunge. Kanuni ya Saba ya Nyongeza hiyo, pamoja na mambo mengine inaelekeza kwamba, endapo jina lilitowasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi ni moja, basi mgombea huyo atapigiwa kura ya ndiyo au hapana, na iwapo atapata kura nyingi za ndiyo atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ninaomba sasa nieleze utaratibu utakaotumika kwenye uchaguzi wa Naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa utaratibu uliowekwa na Bunge hili, mgombea atatakiwa kufika mbele ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge ili kujieleza, kuulizwa maswali kama yatakuwepo na kuyajibu pamoja na kuomba kura. Na baada ya hapo kila Mbunge atapewa karatasi ya kura ambayo ina jina la mgombea, na atatakiwa kupiga kura ya siri kwa kuweka alama ya vyema pembedi ya neno ndiyo au hapana na kuitumbukiza kwenye sanduku la kura, na baada ya hapo kura zitahesabiwa na matokeo yatatangazwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha kuwasilisha na ninaomba tuanze taratibu zetu. (*Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu wetu nitamuita sasa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu aje mbele yenu kwa ajili ya kujieleza na kuomba kura. (*Makof/Vigelegele*)

(Hapa Mhe. Mussa Azzan Zungu Aliingia Ukumbini)

MBUNGE FULANI: Jaza ujazwe.

SPIKA: Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu mbele yako ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ndio wapiga kura kwenye nafasi uliyogombea ya kuwa Naibu Spika, na ninakupa fursa ili uzungumze nao na kisha uwaombe kura halafu tuendelee na utaratibu. Karibu Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: *Right Honorable Dr. Tulia Ackson, Speaker of the National Assembly of Tanzania..., (Makof)*

Right Honorable Kassim Majaliwa Majaliwa, Prime Minister of the United Republic of Tanzania, Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa AG, Waheshimiwa Wabunge, Chief Whip, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wa jumba hili, nimesimama kwa unyenyekevu na kwa heshima kubwa. (Makof)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mimi ninaitwa Mussa Azzan Zungu, nimeteuliwa na Chama cha Mapinduzi ili kugombea kiti cha Naibu Spika ambacho kiko wazi.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, kazi za Bunge ambazo nimezifanya miaka yote mnazifahamu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awatie imani wote ili mnipe kura za ndiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kura za Wabunge wote. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa umemaliza maelezo?

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Ndiyo.

SPIKA: Nashukuru sana. Waheshimiwa mnaruhusiwa kumuuliza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu maswali matatu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Sioni Mbunge anayetaka kuuliza. Nimewaona wako wabunge wawili. Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali kwa mgombea.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali mgombea.

Mheshimiwa Zungu umekuwa Mbunge wa muda mrefu ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na sasa hivi unatuomba kura ili uweze kuwa Naibu Spika wa Bunge hili. Tunata tusikie kutoka kwako, nini hasa unataka kufanya ili kuliboresha Bunge letu? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, kazi za Naibu Spika zimeainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 la ambazo Wabunge wote

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tumezipitisha. Majukumu yangu yameainishwa, na mimi ninafanyakazi chini ya Mheshimiwa Spika kwa maelekezo yoyote anatakayoyatoa Mheshimiwa Spika. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Kiswaga, swali kwa mgombea.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa mgombea wa Unaibu Spika, kwanza nikupe pongozi kwa kuanza kufanya mazoezi ya kizungu ili umwakilishe vyema Spika utakapokwenda nchi za nje.

Mheshimiwa mgombea, sisi Wabunge, kama wawakilishi wa wananchi, wananchi wetu wamekuwa na matarajio makubwa sana na kile ambacho tunaweza *ku-deliver* ni kidogo kulingana na kile wanachokitarajia. Wewe ukiwa kama Naibu Spika, utatusaldiaje sisi Wabunge ili tuweze kufanya kazi zetu vizuri kule majimboni ili tuweze kusukuma hizi kazi ambazo tumeaminiwa na wananchi? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Mussa Azza Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Waheshimiwa Wabunge, katika Kanuni za Bunge Toleo la 2020 limeainisha majukumu yangu. Maelekezo yoyote yatakayotolewa na Mheshimiwa Spika katika kuboresha mahusiano ya Wabunge ndani na nje ya Bunge ndiyo nitakayoyafanya. (*Makofii*)

Niwaombe, Serikali yetu kwa kipindi hiki chini ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, kuna pesa nydingi za miradi. Wabunge lazima tujue namna ya kuisimamia miradi. Hilo nitachukua maelekezo kutoka kwa Mheshimiwa Spika, ni namna gani tutashirikiana ili tuhakikishe pesa za wananchi zinatumika ipasavyo. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Ussi Pondeza.

MHE. USSI SALUM PONDEZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ningependa kumuuliza mgombea wetu,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Bwana Zungu, pindi tukikuchagua, ile style ambayo umetuzoeshaa, ya jaza ujazwe itaendelea?

SPIKA: Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, pale ambapo Spika hatakuwepo anamwachia nafasi Naibu Spika, Naibu Spika asipokuwepo anawaachia nafasi Wenyevitii; kuendesha Bunge hili tutaendesha kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020. (*Makofii/Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nadhani tunakubaliana kwamba mgombea wetu amejitosheleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ahsante sana kwa kuyajibu maswali hayo klikamillifu, sasa unaweza kurejea kwenye kitichako. (*Makofii/Vigelegele*)

Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Katibu sasa tusaidie ili tuweze kujua Wabunge wangapi wako humu ndani ili tupate akidi, na pia igongwe kengele maeneo ya nje ya hapa ili Wabunge waweze kuingia humu ndani.

Taarifa niliyopewa mpaka sasa, na kama wataongezeka tutawataarifu. Wabunge walioko humu Bungeni ni Wabunge 280, kama wataongezeka tutawajulisha na Katibu baada ya kupata hii akidi nadhani sasa tuanze utaratibu wa kura.

Waheshimiwa Wabunge, tutafuata utaratibu wetu ule wa kawaida vijana wako tayari hapa kwa ajili ya kugawa karatasi zetu za kura ambayo kwa sababu mgombea ni mmoja kutakuwa na kura ya ndiyo au hapana halafu tutawaleta majibu hapo baadaye.

Anzeni basi kugawa karatasi au?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, zoezi sasa ni kugaiwa karatasi na makatibu, wasaidizi wa katibu watakuwa wanazunguka huko kuwapa karatasi kwa haraka.

Waheshimiwa Wabunge, masanduku haya yanaletwa hapo mbele na hayana kura hata moja wala karatasi. Wabunge ambao bado haujapata karatasi za kura, makatibu angalieni upande ambao karatasi hazijafika kuanzia kwa Mheshimiwa Kunambi hapo huo upande wote haujapata karatasi.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hamjaanza kukusanya nataka kujua kama wote tumepata karatasi, kuna Mbunge yejote ambaye hajapata karatasi mpaka sasa? Mheshimiwa Kanyasu umepata karatasi ama bado? Katibu unayepita hapo nyuma wapatie karatasi.

Haya nadhani Wabunge wote tumeshapata karatasi makatibu anzeni kukusanya karatasi zilizopigwa kura tayari.

Mheshimiwa Ester Bulaya karatasi yako ya kura. Kuna Mbunge ambaye karatasi yake hajakusanya karatasi ya kura Mbunge yoyote ambaye karatasi yake bado, makatibu zinaashiriwa kwamba zimeshakusanya leteni masanduku hapa mbele.

Chima hiyo siyo karatasi ya kura msije mkaingiza mambo mengine, Mheshimiwa Esther Matiko umempigia kura Naibu Spika? Naona umeshikilia karatasi hapo, makatibu rudisheni masanduku ya kura hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge, masanduku yote ya kura zilizopigwa yamerudi yako hapo mbele. Mheshimiwa Zungu tafadhali changua Mbunge ambaye unataka akakusaidie kuhakiki zoezi la kuhesabu kura.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru naamini meza. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana kwa imani yako kwangu na makanibu hapa, lakini na mimi acha nitume huko mwakilishi Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate akasimamie zoezi hili la kuhesabu kura. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Bilakwate unashabiriwa ili haya ma-box yaweze kutoka hapa. (*Makofii*)

Haya tafadhalii muende huku na Katibu wa Bunge ameshatangulia huko kwa ajili ya kusaidia kwenye hili zoezi.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tukisubiri matokeo ya kura hizi nilete kwenu kwanza matangazo tuliyonayo, halafu nitawaambia tutaendelea na utaratibu gani.

Kwanza nilete matangazo kwenu ya wageni mbalimbali walioko hapa Bungeni wa Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni watano wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ambao wako jukwaa la Spika amba ni familia yake kutoka Mkoani Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Pusi Munthali. (*Makofii*)

Ameongozana na Ndugu Mwinyi Maulid, yupo pia Ndugu Abdul Zungu, yupo pia Ndugu Hanan Abdul, yupo pia Ndugu Mohamed Hadi, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao wageni wengini 11 wa Mheshimiwa Zungu na hawa ni Mheshimiwa Said Ally Nassoro ambaye ni Naibu Meya wa Mtwara Mikindani, tunayepia Mheshimiwa Shaaban Musa ambaye ni Diwani *Pugu Station*, tunaye Mheshimiwa Busolo Pazi ni Diwani Buguruni, tunaye Mheshimiwa Sharick Chogole ni Diwani Kivukoni, tunaye Mheshimiwa Mariam Lulida ambaye ni Diwani Mchafukoge. Simuoni huyu pengine hajapata nafasi ya kuingia lakini yupo Ndugu Saidi Side ambaye ni Mwenyezi wa CCM Wilaya ya Ilala, yupo Ndugu Ramadhani Mkela ambaye ni kada wa CCM, yupo pia Ndugu Ally Makame ambaye ni kada wa CCM, yupo Ndugu Shadab Shongole, kada wa CCM, yupo pia Ndugu Salim Msanga ambaye ni Katibu wa Mbunge,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tunayepia Ndugu Mwamtum Ditopile ambaye ni katibu wa Mbunge, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, muwe mnajifunza naona Mheshimiwa Zungu anamakatibu wawili hapa. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, kwanza ni Wageni 52 wa Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati kutoka Bukoba Mjini Mkoani Kagera, ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya St. Joseph Kolping Sekondari wakiongozwa na Makamu Mkuu wa shule Ndugu Petrius Severis, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Hawa Chakoma ambao ni jamaa zake kutoka Kibaha, Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Ndugu Fredrick Mmari, hapa wameandika wageni wawili yupo mgeni mwingine. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo kwanza ni wageni 15 ambao ni viongozi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato Tanzania na Wachungaji wakiongozwa na Mchungaji Emmanuel Andrew, karibuni sana, sina hakika kama wameingia. (*Makofi*)

Lakini tunao wanafunzi 100 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma siwaoni humu ndani, lakini tangazo limewekwa hapa.

Tunao wageni watatu kutoka Jijini Arusha ambao wanaiongozwa na..., hawa ni wageni watatu kutoka Jijini Arusha Ndugu Rosemary Massawe, Ndugu Regina Laizer na Ndugu Florence Elius, karibuni sana, (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni tulionao Bungeni leo, lakini lipo tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (*TWPG*) anawatangazia Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote kuwa kesho tarehe 12 Februari 2022 saa nne asubuhi kutakuwa na mafunzo yatakayofanyika ukumbi wa Msekwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wabunge wote wanawake mnaombwa kuhudhuria bila kukosa. Tangazo linatoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanaweke Mheshimiwa Shally Raymond.

Wakati bado tuko kwenye matangazo hapa niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge mambo mawili kabla hatujaendelea; la kwanza ni Waheshimiwa Wabunge huwa mnasahau matakwa ya Kanuni ya 73(3); ukiingia kwa kuchelewa tazama mzungumzaji yuko upande gani, usikatize kati ya Spika na anayezungumza, kanuni zetu zinakataza na zinaweka staha ndani ya Bunge, lakini pia unakuwa unamkatiza yule anayezungumza kwa sababu anapozungumza anatazama kiti huku mbele. Kwa hiyo, wewe ukipita katikati unamfanya yale aliyokuwa anazungumza mwingine unayapoteza kidogo na wengine wanapita mbele wakiwa wamependeza sana kwa hiyo inakuwa mtihani. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, niwaombe sana mzingatie matakwa ya kanuni ukifika umechelewa tazama mzungumzaji yuko wapi? Sasa baada ya kukumbushwa kumbushwa mara kadhaa sasa mtaanza kuambiwa fulani rudi ulipotoka, sasa haitakuwa njema sana.

Jambo lingine la kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge japokuwa huwa hatulipendi kulizungumza zungumza ni la mavazi, kipimo unacho wewe lakini pia na kanuni zimetuwekea kipimo. Kabla hujaja humu Bungeni wakati ule unajiandaa wewe jiambie kama ungeitwa na Rais kuapishwa umeteuliwa jambo ndiyo unatakiwa utoke hapa ndani uelekee Chamwino ungekwenda au ungeomba uende nyumbani kwanza. (*Makofi*)

Hicho ndiyo kipimo rahisi yaani kama ungeitwa kutokea hapa Bungeni, kapigwa simu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba fulani mlete nataka nimuapishe kwa nafasi fulani, ungeomba Waziri Mkuu kwanza uende nyumbani ukabadiilishe ndiyo uende ikulu au ndiyo moja kwa moja, kama huwezi kwenda moja kwa moja basi ujue vazi hilo humu ndani haliruhusiwi. Nadhani hilo limeelewaka vizuri. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, na sisi wenyewe vipimo vingine tujivekeee, siyo lazima mtu akukumbushe kwamba nguo hii bwana unaweza kwendea sokoni, lakini siyo Bungeni, unaweza kwenda msibani, lakini siyo Bungeni. Kwa hiyo tuzingatie matakwa ya kanuni zetu.

Sasa baada ya kusema hayo kwa kutumia kanuni yetu ya 5 kwa uendeshaji bora wa shunguli za Bunge kwa sababu matokeo yetu yatatuchukua nusu saa mpaka dakika arobaini kuhesabu. Sasa kuliko tutawanyike nimeamua nitumie mamlaka niliyonayo kwenye kanuni ya 5 tutaendelea na Wenyeviti watawasilisha halafu wakimaliza matokeo yatakuwa tayari yataletwa hapa ndani tutaendelea na ratiba hiyo. (*Makof*)

Katibu!

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda,
Biashara na Mazingira kuhusu Shughuli za Kamati kwa
Mwaka 2021**

na

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo
na Maji kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021**

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimuite kwenu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara na Mazingira Mheshimiwa David Kihenzile aje awasilishe mawazo, maoni na mapendekezo ya Kamati kwa Bunge, karibu Mwenyekiti. (*Makof*)

MHE. DAVID M. KIHENZILE- MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, taarifa ya shughuli ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuanzia Januari 2021 hadi Februari, 2022.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yote hii iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne; sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili inaelezea namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022, sehemu ya tatu inaelezea maoni na mapendekezo ya Kamati na sehemu ya nne ni hitimisho la taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, muundo na majukumu ya Kamati; majukumu ya Kamati yameainishwa katika fasili ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, njia zilizotumika kutekeleza majukumu; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitumia njia mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo:-

Kwanza, kupokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji za Wizara na taasisi zilizopo chini ya usimamizi wa Kamati; taarifa hizi zilijumuisha taarifa za kawaida za utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazosisimamia.

Pili, kupokea, kuchambua, kujadili na kushauri juu ya Mikataba ya Kimataifa iliopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo ipo chini ya Wizara inazosisimamia.

Tatu, ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo; Kamati ilifanya ziara katika miradi mbalimbali kwa lengo la

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kukagua utekelezaji wa miradi hiyo na kubaini ufanisi uliopo katika utekelezaji wake.

Nne, kufanya vikao nya Kamati pamoja na wadau wa sekta ya viwanda na biashara kwa lengo la kufahamu namna wanavyoendesha shughuli zao (mafanikio na changamoto zao) kisha kuishauri Serikali kwa nia ya kuboresha.

Tano, kushiriki warsha na semina mbalimbali zilizoendeshwa na wadau wa sekta za viwanda, biashara na mazingira wa lengo la kuwajengea wajumbe uelewa juu ya sekta hizo.

Sita, kutembelea baadhi ya viwanda nchini kuona namna wanavyoendesha shughuli zao (mafanikio na changamoto zao) kisha kuishauri Serikali kwa nia ya kuboresha.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili; shughuli zilizofanywa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022 Kamati ilitekeleza majukumu yake yanayohusiana na usimamizi wa Wizara mbili; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, majukumu yaliyotekelawa na Kamati ni kama yanavyoonekana katika kurasa ya tatu ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Kamati ilitoa mapendekezo kwenye maeneo mbalimbali yanayosimamiwa na Wizara hizo.

Kamati imearifiwa juu ya utekelezaji wa mapendekezo hayo na kujiridhisha kuwa Serikali imejitahidi

kuzingatia mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, sehemu kubwa ya miradi ya kimkakati hasa ambayo inasimamiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) haijaanza kutekelezwa na kwa ilioanza haifanyi vyema hali ambayo Kamati hairidhishwi nayo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kamati imeona Serikali inahitaji kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na Wizara hizi, aidha maeneo ambayo Serikali inapaswa kuongeza nguvu kwa upande wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa maagizo yafuatayo:-

(a) Bado kuna changamoto ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya kimkakati mfano utekelezaji wa Mradi wa Matrekta ya *URSUS* unasuasua ambapo mbia katika mradi huu Kampuni ya *URSUS S.A* ya Poland ameshindwa kukamilisha utekelezaji wa mkataba wa mradi huu. Mradi ulipaswa kuwa umekamilika kufikia Juni, 2018 na matrekta 2,400 yalipaswa kuwa yamekwishaingizwa nchini, lakini ni matrekta 822 tu yalyopokelewa.

(b) Bado hatujapata tija iliyokusudiwa katika utekelezaji wa lengo la kusimamia na kufuatilia miradi ya kimkakati; kwa mfano Miradi ya Liganga na Mchuchuma, Mradi wa Magadi Soda ya Engaruka na Mradi wa Kiwanda cha Matairi cha Arusha bado hakuna jambo lillikalilikia katika miradi hiyo.

(i) Liganga na Mchuchuma; Kamati haijawahi kuridhishwa na mwenendo wa suala la mradi huu ambao haujaanza hadi muda huu ambao taarifa hii inaandaliwa. (*Makofii*)

Mara kwa mara Wizara imekuwa ikija na habari mbalimbali juu ya mradi huu. Mara nydingi ni taarifa za kujirudia rudia ambazo Kamati haioni muendelezo wake, na kutoona umakini au nia ya dharti ya Serikali katika kufanya mradi huu uanze au kuachana na mwekezaji wa Kampuni ya *Sichuan Ltd.* Katika mkuutano wa mwisho wa mwezi Februari, 2022

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

baina ya Kamati na Wizara; Wizara imeahidi jambo hili linakwenda kuisha muda si mrefu, kwa-- mwekezaji kuanza kazi au kuvunja mkataba naye.

Kamati inaishauri Serikali kuweka nguvu na jitihada kumaliza majadiliano haya ambayo yamechukua muda mrefu kumalizika, jambo ambalo linachelewesha Taifa letu kupata mapato ya kodi, ajira kwa vijana na ahueni kwa wananchi wa Wilaya ya Ludewa ambao wanahitaji kufidiwa kutokana na maeneo yao kuchukuliwa na mradi huu.

(ii) Kuhusu Kiwanda cha Matairi cha Arusha (*General Tyre*), Wizara iliamua kubadilisha matumizi ya eneo hilo yaani kuachana na suala la kiwanda hicho kufufuliwa, badala yake imeamua kufanya eneo hilo kuwa la uwekezaji ili biashara mbalimbali zianzishwe hapo na wawekezaji. Kamati hajjaridhishwa na kitendo cha Serikali kufanya maamuzi makubwa ya aina hiyo bila kushirikisha Kamati, ingawa Kamati iliishauri Wizara mara kadhaa juu ya umuhimu wa kufanya eneo hilo kuendelea kuwa kiwanda cha matairi kutokana na ukweli kwamba uhitaji wa matairi hapa nchini ni mkubwa. (*Makofi*)

Baada ya Kamati kuonesha kutoridhishwa na jambo hili, Wizara ilieleza Kamati mambo kadhaa ambayo wanaamini yanaleta ugumu wa kufufua kiwanda hicho. Kamati imeielekeza Wizara kuandaa andiko linaloonesha namna gani inadhani wazo lao jipya litakuwa na tija kuliko mradi wa awali.

(ii) Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa maagizo yafuatayo:-

(a) Uratibu katika kuzisukuma Wizara, Taasisi, Mikoa pamoja na Halmashauri zote nchini kufuutilia Vitengo vya Mazingira na kuviezeshwa kifedha kutekeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(b) Mfuko wa Taifa wenye dhamana ya usimamizi wa mazingira ulioanzishwa tangu mwaka 2007 haujaanza kufanya kazi ilivyotarajiwa. Ni rai ya Kamati kwa Serikali kuangalia namna ya kuwezeshwa kifedha ili kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi; taarifa za kina kuhusiana na miradi iliyotembelewa na Kamati, maelezo na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na maoni ya Kamati ziliwasilishwa katika Mkutano wa Tatu wa Bajeti uliofanyika mwezi Aprili, 2021.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Mpango wa Mapato na Matumizi ya mwaka 2021/2022; masuala yaliyobainika katika uchambuzi wa bajeti pamoja na maoni ya Kamati yaliwasilishwa katika Mkutano wa Nne wa Bajeti uliofanyika mwezi Aprili, 2021.

Mheshimiwa Spika, taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; katika kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022 Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo. Aidha, taarifa zilizopokelewa na Kamati, pamoja na maoni na ushauri wa Kamati ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 7 hadi 55 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu, maoni ya jumla:-

(i) Pamoja na kwamba baadhi ya majukumu mahsus ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni kuandaa, kuratibu na kupitia sera na mikakati ya sekta za viwanda, biashara na masoko; Kamati ilibaini kuwa sera zilizopo ni za muda mrefu na zimepitwa na wakati, hivyo kuna haja ya Wizara kuharakisha mchakato wa mapitio ya sera ili kuendana na kasi ya mazingira ya sasa.

(ii) Kwa kuwa Wizara hii ndiyo Wizara inayosughulika na viwanda ambavyo tunaamini vitatoa fursa kubwa ya ajira kwa Taifa letu, na kwa kuwa kwa kipindi cha nusu mwaka Kamati ilibaini ni asilimia 33.3 tu ya bajeti ya maendeleo imepokelewa. Kamati inashauri Serikali kupeleka fedha kwa Wizara hii ili iweze kutekeleza miradi ya kimkakati kama ilivyopangwa.

(iii) Kwa kuwa Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) linakabiliwa na changamoto ya ongezeko la njia zisizo rasi za kuingiza bidhaa hapa nichini, jambo linalosababisha kuongezeka kwa bidhaa hafifu sokoni; Kamati inashauri Serikali kuzisimamia kwa ukaribu mamlaka zinazohusika na udhibiti ili kuhakikisha zinashirikiana katika kufanya ukaguzi, lakini pia Serikali iangalie namna ya kupunguza gharama zilizopo ili kuweza kuwavutia wafanyabiashara kuitishaa bidhaa zao katika vituo halali.

(iv) Kamati haijawahi kuridhishwa na mwenendo wa suala la utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayosimamiwa na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kama vile Liganga na Mchuchuma ambao hadi sasa Wizara imeiarifu Kamati kuwa iko katika hatua za majadiliano na mbia, hivyo basi ni rai ya Kamati kwa Serikali kuweka msukumo katika kutekeleza miradi muhimu ya kimkakati yenye maslahi kwa Taifa.

(v) Moja ya changamoto kubwa kwa wawekezaji na wananchi ni kuchukua muda mrefu kufanya usajili wa kampuni au biashara jambo ambalo linasababisha watu wengi kukata tamaa na kupata usumbufu mkubwa. Ni rai ya Kamati kwa upande wa *BRELA* waweke muda maalum tangu mteja ameanza kuomba kufungua kampuni au biashara hadi anakamilisha na vilevile kuweka maafisa wa kutosha wa kuwasaidia wawekezaji na wananchi katika kutoa elimu ya usajili wa biashara au kampuni zao. Aidha, Serikali inapaswa kurekebisha mifumo ya kidigitali ya *BRELA* na kuhuisha taarifa zinazowekwa kwenye mtandao huo mara kwa mara ili kuboresha na kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa huduma kwa wateja.

(vi) Ili Kulinda uwekezaji wa viwanda vya ndani, Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio na maboresho, kupunguza kodi na tozo mbalimbali zinazohusiana na uzalishaji wa viwandani ili kuviezeshesha viwanda kushindana katika soko tukizingatia tumeingia katika Soko la Afrika – AfCFTA.

(vii) Pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na Baraza la Mazingira (*NEMC*) katika kukuza uelewa wa masuala ya mazingira bado kumekuwa na uelewa mdogo wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake kwa wawekezaji na wananchi kwa ujumla. Hivyo, ni rai ya Kamati kwa Serikali kuititia *NEMC* kuongeza kasi ya kuelimisha wananchi na wadau mbalimbali juu ya athari na umuhimu wa uhifadhi wa mazingira.

(viii) Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kwa wadau wa sekta ya mazingira juu ya upatikanaji wa Cheti cha Tathmini ya Athari za Mazingira –*TAM (Environment Impact Assessment (EIA))* hali ambayo inasababisha wawekezaji wengi kukwama kutekeleza miradi yao kwa wakati, Kamati inaishauri Serikali kushughulia changamoto zinazoikwamisha *NEMC* kutekeleza jukumu hili kwa haraka kwa kuwaongezea Fedha na watumishi wa ukaguzi wa mazingira.

(ix) Kwa kuwa kumekuwa na changamoto ya kutokuwa na bei elekezi ya upatinakanaji wa cheti na kibali cha *EIA*; Kamati inaishauri Serikali kuititia *NEMC* iwe inatoa elimu ya ziada kwa wawekezaji juu ya bei elekezi ya gharama ya Tathmini ya Athari ya Mazingira kuendana na mradi unaokusudiwa ambapo wafafanue kwa uwazi kabisa aina fulani ya mradi, gharama zinakadirisha kuanzia kiasi fulani hadi fulani kwa lengo la kusaidia wananchi kutotozwa gharama zaidi na baadhi ya washauri elekezi wasio waadilifu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati; sekta ya uwekezaji, viwanda na biashara; maoni na mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia ukubwa wa hoja, athari za matokeo yatakayotokana na hoja husika, kujirudia

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa hoja na hatua zinazostahili kuchukuliwa kushughulikia hoja husika.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kushuhudia juhudimbalimbali za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zinazolenga kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na nchi mbalimbali zinazotaka kufanya biashara na Tanzania. Kamati inapongeza na kuunga mkono juhudimbalimbali za Serikali ambazo zimelenga kuimarisha sekta za viwanda, biashara na uwekezaji na hatimaye kuweka mazingira mazuri ya kufanya Biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni mapendekezo ya Kamati:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya kimkakati kwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara: -

Kwa kuwa kuna changamoto ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati iliyochini ya Wizara hii kuitia taasisi zake ama kwa kutoanza au kutokamiliaka kwa miradi;

Na kwa kuwa mkwamo huo wa utekelezaji wa miradi unaleta hasara kwa Serikali na kuchelewesha maendeleo ya nchi katika ukusanyaji kodi, ajira na uchagizaji wa uchumi wa jamii zinazozunguka miradi hiyo.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba miradi yote ya kimkakati inayotekelizwa na Shirika la *NDC* ipewe msukumo katika utekelezaji wake. Mfano Mradi wa Liganga na Mchuchuma majadiliano yanayoendelea baina ya Serikali na mbia (*Kampuni ya Sichuan Ltd*) yamechukua muda mrefu kumalizika, hivyo Serikali inapaswa kumaliza majadiliano hayo ili mradi sasa uanze kutekelezwa na wananchi wawezekunufaika na uwepo wa rasilimali hizi katika maeneo yao. Aidha, kwa maeneo ambayo wananchi ardhi zao zilitwaliwa kupisha utekelezaji wa miradi, Serikali inapaswa kuwalipa fidia bila kusubiri miradi husika kuanza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo kwa sasa havifanyi kazi:-

Kwa kuwa Kamati imefafanua kuhusu dosari za ubinafsishaji na uendelezaji wa viwanda vilivyobinafsishwa nchini;

Na kwa kuwa dosari hizo zimesababisha kutokuendelezwa kwa viwanda na hata kutokuwepo na tija kwa vile vichache vinavyofanya kazi;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali kuweka malengo ya kutafuta wawekezaji wenye nia ya dhati na uwezo katika kuendeleza viwanda hivyo.

(b) Kwa viwanda vitakavyobinafsishwa tena Serikali ifanye tathmini ya kina yenye kuwa na tija kwa Taifa. Aidha, viwanda vitavyobinafsishwa kwa njia ya ubia Serikali iingie mikataba yenye tija na yenye kuipa nguvu ya maamuzi katika ubia huo.

Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo ya nje ya Nchi (*EPZA*): -

Kwa kuwa *EPZA* inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha, jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu yake ya kisheria ya kumiliki ardhi na kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda;

Na kwa kuwa *EPZA* inatwaa maeneo mengi karibu nchi nzima na rasilimali za kuyaendeleza maeneo hayo ni chache;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali kupitia Mamlaka ya *EPZ* kuhamasisha sekta binafsi kushiriki kuwekeza katika kuyaendeleza maeneo ya *EPZA* kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuyajengea miundombinu wezeshi na kuyaweka tayari kwa ajili ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, utendaji na ufanisi wa kiwanda cha viuwadudu cha *Tanzania Biotec Products Limited (TBPL)*:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*) imejenga kiwanda cha kuzalisha viuadudu vya kuua viluwiluvi wa mbu wanaoeneza ugonjwa wa Malaria.

Na kwa kuwa lengo la kuanzishwa kwa kiwanda hiki ilikuwa ni kutokomeza Malaria nchini na kiwanda hiki kimejengwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100, hata hivyo, hadi sasa kiwanda hiki kimesimamisha uzalishaji wa viuwadudu kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo uchakavu wa mitambo, ukosefu wa wateja, ukosefu wa fedha

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia: -

(a) Serikali iwe na utayari wa kutoa msukumo kwa Wizara za Afya na TAMISEMI ambao ndiyo wateja wakubwa wa bidhaa zinazozalishwa viuwadudu kuweza kununua bidhaa hizi;

(b) Serikali kuchukua hatua za kufanya matengenezo katika mitambo ya uzalishaji kama inavyohitajika kitaalamu ili sasa uzalishaji uweze kuendelea;

(c) Serikali kufanya mapitio ya mikataba iliyosainiwa baina ya Serikali ya Tanzania na *Labiofam*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utendaji wa *One Stop Center*: -

Kwa kuwa wawekezaji nchini wamekua wakipata changamoto ya kufanya usajili, kupata majibu na kupata huduma katika eneo moja;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na kwa kuwa changamoto hiyo imesababisha wawekezaji kupata usumbufu usio wa lazima na kuzunguka ofisi mbalimbali za Serikali bila kupata ufumbuzi wa masuala yao kwa wakati;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali iweke wataalam wenye uwezo wa kufanya maamuzi katika vituo hivi ili wawekezaji wanapofika nchini waweze kupata huduma zote kwa wakati mmoja.

(b) Serikali ikamilishe mifumo ya huduma kwa njia ya mtandao ambayo imekwishaianza, yaani mfumo wa utoaji huduma unounganisha taasisi za *TRA*, *BRELA*, Idara ya Uhamiaji, *NIDA* na kadhalika. Vilevile mfumo wa uondoshaji wa kontena bandarini, mifumo ambayo kwa sasa imefikia 50% ya utengenezwaji.

(c) *TIC* katika tovuti yake iweke mahitaji yote yanayohitajika kufuatwa na nyaraka zinazohitajika ili muwekezaji afahamu kabisa nini anapaswa kuwa nacho na ni wapi ataanza na kumalizia.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mazingira; mazingira ni suala mtambuka, ili kuleta maendeleo endelevu suala la uhifadhi wa mazingira halina budi kupewa kipaumbele kwani kwa kiasi kikubwa ufanisi wa miradi yetu ya maendeleo inategemea uimara wa mazingira. Kuna haja ya Serikali yetu kuongeza umakini na kuongeza juhudhi katika kusimamia masuala ya uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika kuhakikisha inaisaidia Serikali katika masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira inashauri mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira: -

Kwa kuwa moja ya changamoto katika kuhifadhi mazingira ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ongezeko la joto, mafuriko ya mara kwa mara na ukame; usimamizi wa taka zitokanazo na vifaa vyta umeme; viumbi vamizi; usimamizi wa kemikali na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi;

Na kwa kuwa Halmashauri zetu zina Maafisa Mazingira lakini weledi na mchango wa maafisa hawa katika kusimamia masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira hauridhishi

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali kuwahamishia kiutawala maafisa mazingira katika Wizara yenye dhamana ya mazingira ili waweze kutoa mrejesho wa utekelezaji wa majukumu yao moja kwa moja kwa Wizara hiyo. Aidha, Serikali inapotaka kuajiri maafisa wa kushughulikia mazingira waangalie wenye taaluma ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendeshaji wa shughuli za Mfuko wa Mazingira:-

Kwa kuwa mfuko wa uendeshaji wa shughuli za mazingira ulianzishwa kwa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kwa lengo la kuwezesha shughuli za usimamizi wa mazingira nchini kufanya kwa ufanisi

Na kwa kuwa changamoto ya mfuko huu ni uhaba wa fedha, jambo linalosababisha kushindwa kuendelea na utekelezaji wa majukumu yake;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali itafute vyanzo vyta mapato ili kuwezesha mfuko huu kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne; hitimisho; napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika, kwa ushirikiano unaoutoa kwa Kamati yetu wakati wote. Aidha, nikupongeze kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa Bunge letu tukufu, tunakuombea afya njema na utumishi uliotukuka katika kutekeleza majukumu yako. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, vilevile shukrani za dhati ziende kwa Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia vyema shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge, kwa ushirikiano wake kwangu wakati wote. Aidha, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kujadili na kuchambua taarifa mbalimbali zilizowasilishwa katika Kamati na hatimaye kuwasilisha maoni na mapendekezo kuhusu shughuli zilizoteklezwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka 2021/2022. Naomba orodha yao yote iingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati naomba pia nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dkt. Ashatu Kijaji, Mbunge; Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Mbunge, Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira; Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Mbunge; na Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira - Mheshimiwa Khamis H. Khamis, Mbunge, pamoja na Makatibu Wakuu na watendaji wa Wizara zote pamoja na taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hizo kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kwa kipindi chote hiki.

Mheshimiwa Spika, vilevile, naomba nimshukuru Katibu wa Bunge - Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati, pamoja na yeye, nawashukuru Makatibu wa Kamati - Ndugu Felister Mgonja, Ndugu Nyamwanja Chipanda pamoja na Msaidizi wa Kamati - Ndugu Modesta Kipiko kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUANZIA JANUARI, 2021 HADI FEBRUARI, 2022 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020, Naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne (4); Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya Pili inaelezea namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022, Sehemu ya Tatu inaelezea Maoni na Mapendekezo ya Kamati na Sehemu ya Nne ni Hitimisho la taarifa hii.

1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Fasili ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira imepewa majukumu yafuatayo:

- (i) Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira;
- (ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara hizo;

(iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

1.2 Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitumia njia mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake kama ifuatavyo:-

(i) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji za Wizara na taasisi zilizopo chini ya usimamizi wa Kamati; Taarifa hizi zilijumuisha taarifa za kawaida za utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia;

(ii) Kupokea, kuchambua, kujadili na kushauri juu ya Mikataba ya Kimataifa iliyopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo ipo chini ya Wizara inazozisimamia;

(iii) Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; Kamati ilifanya ziara katika miradi mbalimbali kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi hiyo na kubaini ufanisi uliopo katika utekelezaji wake;

(iv) Kufanya Vikao vya pamoja na wadau wa Sekta ya Viwanda na Biashara kwa lengo la kufahamu namna wanavyoendesha shughuli zao (mafanikio na changamoto zao) kisha kuishauri Serikali kwa nia ya kuboresha;

(v) Kushiriki warsha na semina mbalimbali zilizoendeshwa na wadau wa Sekta za Viwanda, Biashara na Mazingira wa lengo la kuwajengea wajumbe uelewa juu ya sekta hizo; na

(vi) Kutembelea baadhi ya Viwanda nchini kuona namna wanavyoendesha shughuli zao (mafanikio na changamoto zao) kisha kuishauri Serikali kwa nia ya kuboresha.

SEHEMU YA PILI

2.0 SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022 Kamati ilitekeleza majukumu yake yanayohusiana na usimamizi wa Wizara mbili (2); Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na Taasisi zilizopo chini ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, Majukumu yaliyotekelawa na Kamati ni pamoja;

- i. Mafunzo ya kuzifahamu wizara hizi mbili pamoja na taasisi zilizopo chini yake; kupokea taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zake;
- ii. Ugaguzi wa Miradi ya Maendeleo; kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa Mwaka wa Fedha ulioishia (2020/2021) pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka unaoendelea (2021/2022);
- iii. Kuchambua na kushauri juu ya Mikataba ya Kimataifa iliyopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo ipo chini ya Wizara inazozisimamia;
- iv. Vikao na wadau wa Sekta za Viwanda, Biashara na Mazingira pamoja na ziara za kuwatembelea wadau hao kwa lengo la kusikiliza maoni yao; na kushiriki warsha na Semina za kujenga uelewa kwa Wajumbe.

2.1 Taarifa ya Utekelezaji wa mapendekezo ya kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilitoa mapendekezo kwenye maeneo mbalimbali yanayosimamiwa na Wizara hizo.

Kamati imearifiwa juu ya utekelezaji wa mapendekezo hayo na kujiridhisha kuwa, Serikali imejitahidi kuzingatia

mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, Sehemu kubwa ya miradi ya kimkakati hasa ambayo inasimamiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) haijaanza kutekelezwa na kwa ilioanza haifanyi vema hali ambayo kamati hairidhishwi nayo.

Hivyo basi, Kamati imeona Serikali inahitaji kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na Wizara hizi, Aidha maeneo ambayo Serikali inapaswa kuongeza nguvu ni pamoja na:-

i) **Kwa upande wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa maagizo yafuatayo:-

a) Bado kuna changamoto ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya kimkakati mfano Utekelezaji wa Mradi wa Matrekti ya URSUS unasuasua ambapo Mbia katika mradi huu Kampuni ya URSUS S.A ya Poland ameshindwa kukamilisha utekelezaji wa Mkataba wa mradi huu. Mradi ulipaswa kuwa umekamilika kufikia Juni, 2018 na matrekti 2400 yalipaswa kuwa yamekwishaingizwa nchini lakini ni matrekti 822 tu yaliyopokelewa;

b) Bado hatujapata tija illyokusudiwa katika utekelezaji wa lengo la kusimamia na kufuatilia Miradi ya Kimkakati. Mfano miradi ya **Liganga na Mchuchuma, Mradi wa Magadi Soda ya Engaruka, na Mradi wa Kiwanda cha Matairi cha Arusha** bado hakuna jambo liliokamilika katika miradi hiyo.

i) **Liganga na Mchuchuma.**

Kamati hajjawahi kuridhishwa na mwenendo wa suala la mradi huu ambao haujaanza hadi muda huu ambao taarifa hii inaandaliwa. Mara kwa mara Wizara imekua ikija na habari mbalimbali juu ya mradi huu. Mara nyangi ni taarifa za kujirudia rudia ambazo kamati haioni muendelezo wake, na kutoona umakini au nia ya dhati ya Serikali katika kufanya mradi huu uanze au kuachana na mwekezaji wa kampuni ya Sichuan Ltd. Katika m kutano wa mwisho wa mwezi Februari 2022, baina ya Kamati na Wizara. Wizara imeahidi Jambo hili

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

linakwenda kuisha muda si mrefu, kwa-- mwekezaji kuanza kazi au kuvunja mkataba naye. Kamati inaishauri Serikali kuweka nguvu na jitihada kumaliza majadiliano haya ambayo yamechukua muda mrefu kumalizika. Jambo ambalo linachelewesha taifa letu kupata mapato ya kodi, ajira kwa vijana na ahueni kwa wananchi wa wilaya ya Ludewa ambaao wanahitajni kufidiwa kutokana na maeneo yao kuchukuliwa na mradi huu.

ii) Kuhusu Kiwanda cha matairi cha Arusha (General Tyre), Wizara iliamua kubadilisha matumizi ya eneo hilo yani kuachana na suala la Kiwanda hicho kufufuliwa, badala yake imeamua kufanya eneo hilo kuwa la uwekezaji ili biashara mbalimbali zianzishwe hapo na wawekezaji. Kamati hajjaridhishwa na kitendo cha Serikali kufanya maamuzi makubwa ya aina hiyo bila kushirikisha kamati, ingawa kamati illishauri wizara mara kadhaa juu ya umuhimu wa kufanya eneo hilo kuendelea kuwa kiwanda cha matairi kutokana na ukweli kwamba uhitaji wa matairi hapa nchini ni mkubwa. Baada ya kamati kuonesha kutoridhishwa na jambo hili, wizara ilieleza kamati mambo kadhaa ambayo wanaamini yanaleta ugumu wa kufufua kiwanda hicho. Kamati imeielekeza wizara kuandaa andiko linalo onesha namna gani inadhani *wazo lao jipya litakua na tija kuliko mradi wa awali*.

iii) **Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira**, Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa maagizo yafuatayo:-

a) Uratibu katika kuzisukuma Wizara, Taasisi, Mikoa pamoja na Halmashauri zote nchini kufuatilia vitengo vya Mazingira na kuviwezesha kifedha kutekeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

b) Mfuko wa Taifa wenye dhamana ya usimamizi wa Mazingira *ulioanzishwa tangu mwaka 2007 haujaanza kufanya kazi ilivyotarajiwa. Ni Rai ya Kamati kwa Serikali kuangalia namna ya kuvezeshwa kifedha ili kuanza kufanya kazi.*

2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa lengo la kubaini ufanisi uliopo katika utekelezaji wa miradi hiyo kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni, 2020. Katika kipindi cha tarehe 12 hadi 17 mwezi Machi, 2021 Kamati ilitembelea miradi mitatu (3) inayotekelizwa na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Miradi hiyo ni Mradi wa Mchuchuma *Coal* (**Mradi Namba 3171 Fungu 44**), Mradi wa Liganga *Vanadium Titanium* (**Mradi Namba 3161 Fungu 44**) pamoja na **Mradi Na. 6260 – Institutional Support** ambao unahusu kuzijengea uwezo taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Taasisi zilizotembelewa na Kamati ni pamoja na EPZA- Bagamoyo na Benjamina Mkapa illyopo Ubungo External, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO) liliopo Msasani jijini Dar es Salaam na eneo la Uwekezaji (TAMCO-Kibaha Industrial Park) liliopo chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC).

Mheshimiwa Spika, Taarifa za kina kuhusiana na miradi iliyotembelewa na Kamati, maelezo na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na maoni ya Kamati ziliwasilishwa katika mkutano wa tatu wa Bajeti uliofanyika mwezi Aprili, 2021.

2.3 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Mpango wa Mapato na Matumizi ya Mwaka 2021/2022;

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Kamati za Bunge za Kisikta hufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara zinazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoishia pamoja na kufanya ulinganisho wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata. Hivyo basi, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

pamoja na Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya makamu wa Rais-Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Aidha, Masuala yaliyobainika katika uchambuzi pamoja na maoni ya Kamati yaliwasilishwa katika Mkutano wa nne wa Bajeti uliofanyika mwezi Aprili, 2021.

2.4 Taarifa mbalimbali za Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Taasisi zilizo chini yake

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Januari 2021 hadi Februari, 2022, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo. Taarifa zilizopokelewa na Kamati ni kama zifuatavyo:-

a) Kupokea na Kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu muundo na majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Aidha, Kamati ilieleza kuhusu baadhi ya majukumu mahsusii ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ni pamoja na Kuandaa, kuratibu na kupitia sera na mikakati ya sekta za Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa Mafanikio makuu ya Sekta ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha Mwaka 2015-2020 na kubaini kuongezeka kwa Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kutoka **aslilimia 7.9** mwaka 2015 hadi **aslilimia 8.5** mwaka 2020; Ongezeko la Ujenzi wa Viwanda Vipya 8,477 ambavyo vimeanzishwa kati ya mwaka 2015 hadi 2019. Aidha, Wizara ilieleza kuhusu utekelezaji wa Blueprint unaolenga kuboresha mazingira ya kufanya biashara ambaa umelenga kuondoa Tozo Kero, Ada zinazojirudia na Kurahisisha Majukumu ya Taasisi za Udhibiti; na kuendeleza kukamilisha taratibu za utekelezaji wa miradi ya Kimkakati iliopo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini changamoto zinazoikabili Wizara katika kutekeleza majukumu yake ambazo ni upungufu wa Rasilimali watu na fedha kulingana na ukubwa wa majukumu ya Wizara; Maeneo ya Uwekezaji yenye kukosa miundombinu ya msingi na saidizi jambo linalopelekea baadhi ya wawekezaji kushindwa kuwekeza nchini; viwanda vya ndani kukosa ulinzi dhidi ya Bidhaa zinazoingia kutoka nje; kuwa na Sera zilizopitwa na wakati jambo linalopelekea kutoendena na mazingira ya sasa ya Biashara.

Mheshimiwa Spika, kutatua changamoto ya mwitikio mdogo wa Sekta nyingine katika utekelezaji wa Blueprint, Kamati inaishauri Serikali kuzisimamia Wizara zote kuhakikisha zinatekeleza maelekezo ya Blueprint kama yalivyoelekezwa katika Sekta yake. Sambamba na hilo Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ianzishe kitengo kitakachofuatilia kila Sekta kuona utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka chombo kimoja cha Usimamizi wa tozo zote ili taasisi au shirika lolote likitaka kuanzisha, kufuta au kuongeza tozo yoyote ni lazima wapitie katika Mamlaka hiyo na ikiwezekana tozo zote ziliipwe kwa pamoja na Serikali isisitize malipo kwa njia ya mtandao (*online*). Lengo ni kutatua changamoto ya uwepo wa tozo nyingi ambazo zinaonekana kuwa kikwazo katika mazingira ya kufanyia biashara;

Mheshimiwa Spika, Sera nyingi zinazosimamia uendeshaji wa Sekta za Viwanda na Biashara zimepitwa na wakati na haziendani na uhalisia wa mazingira ya sasa. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha na kukamilisha mapitio ya Sera hizo na kupata sera mpya; (mabadiliko yafanyike kulingana na rejea inayofanywa na kuendana na wakati);

Mheshimiwa Spika, Katika kuanzisha Sera ya *Local Content*, Kamati inaishauri Serikali kusimamia kwa makini namna mwekezaji wa ndani (local partner) anavyopatikana na pia waweke vigezo vya kuweza kupima uwezo wa mwekezaji wa ndani juu ya utekelezaji wa uwekezaji husika ili kuondoa hatari ya kuja kushindwa kutekeleza mkataba mbeleni;

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie namna kuvilinda viwanda na bidhaa zetu kwa kuweka uwiano wa kodi kwa bidhaa zinazoingia ili kuhakikisha bidhaa za ndani zinaweza kushindana katika soko. Sambamba na hilo kwenye miradi ya Umma iweke ulazima wa kutumia bidhaa za ndani ili tuweze kulinda viwanda vyetu; na

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza katika kufanya utafiti wa soko mara kwa mara kwa lengo la kubaini mahitaji ya soko na kuhamasisha wafanyabiashara wetu wa ndani kuzalisha kulingana na mahitaji ya soko.

b) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Majukumu ya Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo ya nje ya Nchi (EPZA);

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa hii na kuelezwu kuhusu msingi wa uanzishwaji wa Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo ya nje ya Nchi (EPZA).

Mheshimiwa Spika, malengo ya kisera ya EPZA ni pamoja na Kuongeza na kuendeleza kukuza mauzo ya bidhaa za viwandani katika masoko ya nje; Kukuza sekta ya viwanda ili kuongeza ajira za viwandani; Kuendeleza uhawilishaji wa teknolojia za uzalishaji viwandani, sambamba na kufundisha stadi husika kwa Watanzania; na Kuhamasisha usindikaji na uchakataji wa malighafi zinazozalishwa Nchini ili kuongeza thamani.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya EPZA Kamati ilibaini changamoto zifuatazo; Uhaba wa rasilimali fedha jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu yake ya kisheria ya kumiliki ardhi na kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda; kukosekana kwa uelewa wa pamoja na mtazamo unaofanana baina ya Mamlaka za Serikali katika kuwezesha/ kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Mamlaka ya EPZ hususani katika kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji hasa

miundombinu (Ardhi, Umeme, Maji); na upungufu wa rasilimali watu zenyé Ustadi na Maarifa yanayohitajika viwandani.

Mheshimiwa Spika, EPZA inatwaa maeneo mengi karibu Nchi nzima na rasilimali za kuyaendeleza maeneo hayo ni chache, hivyo kubaki na maeneo ambayo hayana faida kwa Mamlaka, Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka ya EPZ kuhamasishe Sekta binafsi kushiriki kuwekeza katika kuyaendeleza maeneo ya EPZA kwa kuyajengea miundombinu wezeshi na kuyaweka tayari kwa ajili ya Uwekezaji;

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri Serikali kupitia SEZ zihamasishe zaidi wawekezaji wa ndani kushiriki kuwekeza katika maeneo hayo. Aidha, Serikali izisimamie Mamlaka zingine za Serikali kutoa ushirikiano kwa EPZA pamoja na wawekezaji wanaowekeza chini ya maeneo hayo;

c) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Majukumu ya Shirika la Viwango Tanzania - TBS.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa juu ya msingi wa uanzishwaji wa TBS ambapo kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Sura Na. 130, TBS inapewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa viwango nchini (The Bureau shall be the custodian and overseer of observance of standards in Tanzania). Madhumuni ya kuanzishwa kwa TBS ni pamoja na kuratibu uandaaji wa viwango vya kitaifa katika sekta mbalimbali; na Kudhibiti usalama na ubora wa bidhaa zinazozalishwa au kuingizwa nchini; na udhibiti wa usalama wa chakula na vipodozi. Lengo likiwa ni kulinda afya na usalama wa walaji na mazingira ili kuchangia jitihada za Serikali kupanua soko la bidhaa zetu na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini Changamoto zinazoikabili TBS ambazo ni pamoja na;

- Ongezeko la njia zisizo rasmi za kuingiza bidhaa hapa Nchini jambo linalopelekea kuongezeka kwa bidhaa hafifu sokoni;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Upungufu wa Wataalamu wa Matengenezo ya Vifaa vyatia Maabara jambo linalopelekea kuchelewa kwa matengenezo ya vifaa, hivyo kuchangia kukwamisha shughuli za uchunguzi wa sampuli; Kutokuwepo kwa Bodi ya Wakurugenzi jambo linalopelekea kukwamisha baadhi ya maamuzi ambayo yanahitaji Baraka za Bodi.

- Ushirikiano mdogo/hafifu baina ya Taasisi za Ukaguzi zilizopo katika Vituo vya Mipakani pamoja na gharama kubwa za ukaguzi, vinasababisha baadhi ya wafanyabishara kuamua kutumia njia za panya kuingiza bidhaa zao na kupelekeea uwepo wa bidhaa hafifu sokoni. Kamati inaishauri Serikali kuzisimamia kwa ukaribu Mamlaka hizo kuhakikisha zinashirikiana katika kufanya ukaguzi, lakini pia Serikali iangalie namna ya kupunguza gharama zilizopo ili kuweza kuwavutia wafanyabiashara kuitisha bidhaa zao katika vituo halali;

Mheshimiwa Spika, Kwa lengo la kuongeza nguvu katika zoezi la ukaguzi hususani huko wilayani, Kamati inaishauri Serikali kuititia Shirika la Viwango *TBS* kuwatumia Maafisa Biashara waliopo katika Halmashauri zetu kwa kuwapatia elimu kuhusu viwango na usimamizi wa Viwango katika bidhaa pamoja na kuhakikisha bidhaa zilizopo masokoni zimekaguliwa na ziko katika ubora unaostahili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuititia Wizara ya Viwanda na Biashara kusimamia Shirika la Viwango (*TBS*) pamoja na Tume ya Ushindani (FCC) kuhakikisha wanafanya kazi kwa ushirikiano katika kuhakikisha bidhaa zilizopo sokoni zinakidhi viwango lakini pia ni halali na zinaleta ushindani wa usawa sokoni; na

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza Mpango wa Serikali wa kuhamishia ukaguzi wa Magari baada ya Kuingia nchini, Kamati inashauri kuwa Serikali itoe elimu kwa jamii juu ya jambo hili lakini pia ifanye uhamasishaji kwa wananchi wawewe kutumia mawakala/makampuni ya uagizaji magari yaliyopo hapa nchini, kwa lengo la kupunguza hatari ya kuletewa magari mabovu, kwakuwa mawakala hawa tayari wana mikataba na Nchi na watakuwa makini kwakuwa

watajua kwamba gharama zitaangukia kwao kama gari itafika ikiwa na changamoto.

d) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Majukumu ya Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara – BRELA.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu Majukumu ya Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara – BRELA.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini changamoto zinazoikabili BRELA ambazo ni ni upungufu wa maafisa wenyе jukumu la kusaini leseni ('Assistant Registrars') hali inayopelekeea ucheleweshaji wa sajili mbalimbali hususani za Makampuni na Majina ya Biashara hivyo kupelekeea malalamiko kuwa makubwa; uelewa mdogo wa wateja juu ya matumizi ya TEHAMA hususani katika maeneo ya vijijini na wilayani; na uelewa mdogo wa wafanyabiashara juu ya Sheria zizosimamiwa na taasisi hiyo:

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kutokuwepo kwa Sera ya Taifa ya Miliki Ubunifu jambo linalopelekeea kuchelewa kupata Sheria ya Miliki Ubunifu inayoendana na mazingira ya sasa; na kuchelewa kwa mapitio ya Sheria ya Taifa ya Leseni za Viwanda jambo linalopelekeea kuendelea kutumia Sheria iliyopitwa na wakati na haiendani na mazingira ya sasa ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto wanazozipata wananchi na wavekezaji wakati wanapotaka kusajili ikiwemo kuchukua muda mrefu hadi kusajili kampuni/biashara, jambo ambalo linapelekeea watu wengi wanaotaka kusajili kampuni kukata tamaa. Kamati inashauri BRELA waweke muda maalum (timeline) tangu mteja ameanza kuomba kufungua kampuni/biashara hadi anakamilisha, ili kuweza kujua wangapi wameweza kufungua kampuni na kwa muda gani na walishindwa kufungua na sababu zilizopelekeea kushindwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kurekebisha Mifumo ya kidigitali ya BRELA na kuhuisha taarifa zinazowekwa kwenye mtandao huo mara kwa mara, ili kuboresha na kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa huduma kwa wateja. Hii imetokana na malalamiko ya wateja wengi juu ya ukosefu wa huduma kwa wakati ikiwemo huduma zinazopatikana kwa njia ya Mtandao;

Mheshimiwa Spika, Kutoptaka na huduma isiyoridhisha inayotolewa na BRELA inayopelekea wateja wengi kukata tamaa kufungua kampuni na wawekezaji kutoka nje, kuondoka bila ya kuwekeza nchini. Kamati inaishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kuititia BRELA kutoa elimu kwa wafanyakazi wa Ofisi hiyo na kuongeza ufuutiliaji wa ufanisi wa wafanyakazi ikiwemo kuwawekea malengo ya kufikia na kuwapa motisha mbalimbali ambazo zitawaongezea ari ya kufanya kazi kwa ufasaha na weledi. Aldha, BRELA ifanye uchambuzi wa kutosha wa upekuza wa wawekezaji kutoka nje kuhakikisha uwezo upo wa kutekeleza.

e) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Majukumu ya Tume ya Ushindani (FCC).

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilipokea taarifa kuhusu Majukumu ya Tume ya Ushindani (FCC).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa majukumu ya FCC ambayo ni pamoja na Kusimamia ushindani katika uchumi wa soko nchini; kushughulikia makubaliano ya makampuni yaliyo kinyume cha sheria ya ushindani; kuchunguza na kuchukua hatua za kisheria kwa makampuni au mtu anayetumia vibaya nguvu ya soko; kufanya upembuzi yakinfu kwa makampuni yanayoleta maombi ya kutaka kuungana; na kuchunguza na kuchukua hatua kwa makampuni yaliyoungana bila kufuata taratibu za Sheria ya Ushindani.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili FCC ni pamoja na uhaba wa wafanyakazi kulingana na mahitaji halisi ya taasisi; mapungufu katika sheria ya ushindani ambayo ni

sheria ya Mwaka 2003 na katika utekelezaji wa sheria hiyo yamebainika baadhi ya masuala yanayohitaji kufanyiwa marekebisho na mchakato wa marekebisho umechukua muda mrefu na haujakamilika; na vyanzo vya mapato visivyo vya uhakika ambavyo yanategemea faini, ada na michango kutoka mamlaka za udhibiti ambazo pia ni wadau ambao kesi zao zinaweza kupelekwa mbele ya FCC (mfano; EWURA, LATRA n.k).

Mheshimiwa Spika, upungufu wa wafanyakazi uliopo FCC unaopelekea kuchelewesha utoaji wa huduma na kukwamisha shughuli mbalimbali zinazotakiwa kutekelezwa na shirika. Kamati inaishauri Serikali kutoa vibali vya kuajiri mapema iwezekanavyo kwa FCC ili kuondokana na upungufu uliopo katika shirika hilo na kuongeza ufanisi katika kusimamia na kulinda biashara nchini;

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri FCC kupunguza muda unaotumika kuchunguza na kutolea maamuzi maombi ya miungano ya makampuni (merger). Suala la miungano ya makampuni lifanyike kwa wakati na kwa ufanisi ili kutofifisha ushindani na kuua biashara nchini; na

Mheshimiwa Spika, Uzamani wa Sera na Sheria ya FCC unapelekea Shirika kutoendana na kasi ya mabadiliko ya kiushindani ya kibashara yanayotokea Duniani. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mapitio ya Sera na kuleta Bungeni mapendekezo ya marekebisho ya sheria ili kuweza kuboresha utendaji wa Shirika na kuimarisha ushindani wa kibashara nchini.

f) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Mkakati wa Serikali wa kurudisha Viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo kwa sasa havifanyi kazi:**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya Wizara iliyoelezea mkakati wa Serikali katika kushughulikia viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo kwa sasa havifanyi kazi. Taarifa ya Wizara ilieleza kuwa Katika kipindi cha Agosti, 2017 hadi Aprili, 2019, ufuatiliaji na tathmini ulifanyika kwa viwanda 156

na shirika moja (1) na kubaini kuwa viwanda 88 vinafanya kazi, viwanda 48 pamoja na shirika 1 vina changamoto, viwanda 20 havitafaa kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa baadhi ya changamoto zilizopelekea baadhi ya viwanda kutokufanya kazi ambazo ni wawekezaji kutokuwa na uwezo wa kifedha (mtaji) na kitaalam kuvientesha kwa tija; na baadhi ya wawekezaji kukiuka masharti ya mkataba wa mauzo. Aidha, viwanda 48 vyenye changamoto vimokusudiwa kurejeshwa Serekalini kwa malengo ya kutafuta wawekezaji mahiri katika kuendeleza viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa viwanda 20 kati ya vile vilivyokuwa changamoto vimefanikiwa kurejeshwa Serikalini na mpango wa kuvibinafsisha tena unaandaliwa. Baadhi ya Viwanda vilivyorejeshwa Serikalini na vinatarajiwu kubinafsishwa tena ni pamoja na Kiwanda cha Kutengeneza Vipuri cha Mang'ula; Kiwanda cha Ngozi Mwanza; Kiwanda cha Kusindika Mbegu za Mafuta (MOPROCO); Manawa Ginneries Co. Ltd; Musoma Textile Mills; TLD – Utegi (Mara); Nachingwea Cashewnut Processing Factory.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji juu ya Kiwanda cha URAFIKI na kujulisha kuwa, kiwanda hichi kilibinafsishwa kwa njia ya ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Changzhou State Owned Textile Assets Operations Company. Kiwanda hiki kimekuwa na changamoto nyingi ikiwemo kukosekana kwa mtaji wa kutosha kuendesha kiwanda na teknolojia duni iliyopitwa na wakati, hivyo kusababisha kusimama uzalishaji kuanzia Disemba, 2017 baada ya kuijendesha kwa hasara kwa takribani miaka 22 mfululizo. Kwa sasa majadiliano yanaendelea katika ya Serikali mbili ya Tanzania na China ili mbia mwenza aondoke na Serikali ya Tanzania iweze kumiliki kiwanda hiki kwa asilimia 100 na hatimaye kujipanga kwa lengo la kukirejesha kiwanda hiki kufanya uzalishaji tena.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako inaishauri Serikali kufanya jitihada za makusudi ili mchakato wa kufufua kiwanda cha URAFIKI ukamilike na kianze kufanya kazi ili tuache kulipa

mishahara ambayo kwa sasa haizalishi. Aidha, turudishe bidhaa za Urafiki sokoni kwa kuwa sasa wafanyabiashara wasio waaminifu wamekuwa wakitumia jina la urafiki kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa kabla ya kufanya ubinafsishaji mpya ifanyike tathimini ya kina kubaini ni kwa nini awali tuliamua kufanya ubinafsishaji, na kwanini viwanda husika vilishindwa kuendelezwa ili tutumie taarifa hizo kujipanga ili tusijerudia makosa; Aidha, Tuzingatие maslahi mapana ya Taifa kwa Mikataba itakayoingiwa wakati ubinafsishwaji mpya utakapofanyika, msisitizo hasa uwekwe katika kutafuta wawekezaji na apewe mtu mwenye uwezo wa kukiendeleza kiwanda;

g) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utendaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)

Mheshimiwa Spika, NDC inajukumu la Kusaidia ushiriki wa wananchi wengi katika shughuli za kiuchumi; hii ikiwa ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa miundombinu na kubuni mifumo ya kisasa inayokubalika kwa uendeshaji wa biashara.

Mheshimiwa Spika, miradi inayosimamiwa **NDC** ni pamoja na Mradi wa Mchuchuma na Liganga, Mradi wa Magadi Soda wa Engaruka, uendeshaji wa Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools Manufacturing Company (KMTC), Mradi wa Kiwanda cha Kuunganisha Matrekt aina ya URSUS, uwekezaji katika Kampuni ya ETC Cargo Limited, Mradi wa Makaa ya Mawe wa Ngaka, Mradi wa chuma ghafi wa Maganga Matitu na makaa ya mawe, Kiwanda cha Viuwadudu cha Tanzania Biotech Products Limited (TBPL), Mradi wa maeneo ya Viwanda(Eneo la TAMCO – Kibaha);

Mheshimiwa Spika, Kamati yako inaishauri Serikali ifanye mapitio ya mikataba yote ya Ubia ambayo iliingiwa na NDC kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali kama nchi kutonufaika na miradi hiyo, mfano Mradi wa Makaa ya Mawe ya Ngaka; Aidha, Majadiliano yanayoendelea kuhusiana na

miradi hii ya kimkakati inayotekelizwa na NDC itafutiwe ufumbuzi wa haraka ili iweze kuleta tija kwa Taifa.

h) Kupokea na kujadili Taarifa kuhusu Maudhui ya Mwongozo wa Mageuzi ya Udhibiti ili kurahisisha Mazingira ya kufanya Biashara nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*).

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilielezwa kuhusu Mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara nchini (Blueprint for regulatory reforms to improve the business environment for Tanzania) ambalo ni andiko maalumu liloandaliwa kwa lengo la kuweka misingi endelevu ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini. Andiko hili limefanua changamoto mbalimbali zilizokuwa zikilalamikiwa kukwamisha biashara nchini pamoja na mapendekezo ya ufumbuzi wake;

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilielezwa juu utekelezaji wa Blueprint ambao ulianza tarehe 1 Julai, 2019, Blueprinti iliangalia maeneo ya kuboresha hasa sheria, kanuni, mifumo ya kietroniki, na taratibu kwenye mamlaka za udhibiti zote; pia inalenga kupunguza, kufuta au kurekebisha leseni, tozo na faini zenye kukinzana; Kuondoa muingiliano kwenye mamlaka za udhibiti; Kuboresha mifumo ya kaguzi kwenye mamlaka; na Kujenga uwezo mamlaka za udhibiti na Taasisi za Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, ni miaka miwili na nusu toka utekelezaji wa Blueprint umeanza lakini tija iliyopatikana sio ya kuridhisha. Kamati inaona kuna haja ya kuboresha vipengele vifuatavyo ili kupata tija inayokusudiwa;-

➤ Tujiwekee *Benchmark* ya kujipima kwa kuangalia ni nchi gani ina mazingira mazuri ya biashara ndani ya EAC, SADC, Africa na Dunia na kujilinganisha pale tulipofika. Kwa kufanya hivyo, tutafahamu mapungufu yetu na hivyo kuyaboresha kwa nia ya kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara lakini pia itatuwezesha kushindana sokoni. Aidha, Serikali ijivekee vigezo vyake vya kujipima kuhusu mazingira mazuri

ya ufanyaji biashara nchini na isimamie vigezo hivyo kuhakikisha vinatekelezwa;

- Tutumie mifumo ya kielektroniki katika taratibu zote za udhibiti kuanzia kupata vibali, malipo ya tozo na faini mbalimbali ili kupunguza urasimu na mianya ya rushwa;
- Wakati wakuandaa sheria, kanuni, faini tozo mbalimbali tuangalie washindani wetu hususani majirani zetu ili tuisitofautiane nao sana ili kuwalinda wazalishaji wa ndani kuweza kushindana katika soko hasa kupindi hiki tunapoenda kuridhia Mkataba wa AfCFTA;
- Mamlaka za Udhibiti zijiyelekeze katika mlengo wa Udhibiti na si utafutaji wa mapato, jambo hili litaboresha mahusiano katika Serikali na Sekta ya Biashara;
- Serikali ije na mkakati maalumu wa kudhibiti biashara za mitandaoni (online business) kwa lengo la kuboresha na kikuza sekta hii pamoja na kujipatia mapato lakini pia kuwalinda wanunuzi juu ya utapeli unaofanyika katika biashara za mitandaoni; na
- Mchakato wa kutunga Sheria ya Kuwezesha Mazingira ya Biashara (Business facilitation Act) ukamilike ili kurahisisha utekelezaji wa Blueprint.

i) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Uendeshaji wa Shughuli za Kituo cha zana za Kilimo na Tecnolijia Vijijini – CAMARTEC na Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo – TEMDO;**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa kuhusu Uendeshaji wa Shughuli za Kituo cha zana za Kilimo na Tecnolijia Vijijini – CAMARTEC na Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo – TEMDO;

Mheshimiwa Spika, Kituo cha zana za Kilimo na Tecnolijia Vijijini – CAMARTEC kilianzishwa kwa malengo ya kukuza matumizi ya zana za kilimo na teknolojia sahihi ili kuongeza uzalishaji katika kilimo na kuboresha hali ya maisha ya wananchi vijijini.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilielezwa kuhusu majukumu ya CAMARTEC ambayo ni pamoja na kufanya Utafiti na Maendeleo unaozingatia mahitaji ya wadau; kutoa mafunzo na Uhawilishaji wa Teknolojia; na Majaribio ya Zana za Kilimo na Teknolojia sahihi za vijijini. Aidha, Changamoto za CAMARTEC ni pamoja na Ufinyu wa bajeti ya kituo na mara nyingine fedha hizo kutopelekwa; uhaba wa watumishi hususani wataalamu wa fani ya uhandisi; na Uhaba wa vifaa na eneo la majaribio jambo linalokwamisha kufanya majaribio ya zana zinazozalishwa.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya TEMDO ni pamoja na Kutafiti, kubuni, kuendeleza na kuunda mitambo, mashine na vifaa pamoja na teknolojia mbalimbali na kuhamasisha utengenezaji wake kibiashara na matumizi yake katika shughuli za uzalishaji mali ili kukuza uchumi; kutoa huduma za kihandisi kwenye viwanda vidogo, vyakati na vikubwa kwa lengo la kuongeza ufanisi, matumizi bora ya rasilimali, ubora wa bidhaa na uwezo wa ushindani; na Kutoa mafunzo kwa wahandisi na mafundi mchundo wanaofanya kazi viwandani na Taasisi zingine ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea changamoto zinazolikabili Shirika ambazo ni pamoja na ufinyu wa bajeti na wakati mwingine hazipelekwi; uhaba wa wafanyakazi hususani wahandisi na mafundi mchundo; Sheria ya kuanzishwa kwa Taasisi (Establishment Act) kutokuwa na kanuni zake (*Regulations*), hivyo kuifanya Taasisi kushindwa kutekeleza baadhi ya majukumu bila mwingiliano;

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona haja ya kuziweka pamoja taasisi tatu za Utafiti ambazo ni TEMDO, CAMARTEC na TIRDO kwa kuwa majukumu yake yanashabihiyana kwa namna moja ama nyingine. Pamoja na kuziunganisha wagawiwe majukumu kuanzia ngazi ya kutoa huduma ya kihandisi, kufanya utafiti, ubunifu, uzalishaji wa prototype na mwisho kiwepo kitengo maalumu kwa ajili ya kujitangaza na kutafuta muwekezaji wa kufanya uzalishaji kwa ajili ya biashara.

Muunganiko huu utatatua changamoto ya ufinyu wa rasilimali watu na fedha ambazo kwa sasa ilizikabili taasisi zote hizi;

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri mara baada ya kuziunganisha taasisi hizi, Serikali iandae mpango wa kuiwezesha taasisi hiyo kwa kuipatia teknolojia itakayowezesha kuendana na kasi ya teknolojia duniani ili waweze kupata mashine zinazoendana na mazingira ya sasa na hatimaye kuweza kushindana sokoni; na

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya Sukari na kutoa fursa kwa wazalishaji wadogo wadogo kuzalisha Sukari, jambo hili litatatua changamoto ya baadhi wa wakulima kukosa soko la miwa. TEMDO imetusaidia kusanifu mitambo midogo ya kutengeneza sukari kwa *low scale*, Serikali itafute muwekezaji atakaenunua *prototype* hii na kuzialisha kwa ajili ya biashara ili iwafikie wakulima wadogo wa miwa, hii itasidia kutatua changamoto ya upungufu wa Sukari nchini lakini pia itaongeza ajira.

j) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utendaji wa Baraza la Ushindani (FCT);

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya Utendaji wa Baraza la Ushindani (FCT) ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani Namba 8 ya Mwaka 2003 (Fair Competition Act, No. 8/2003). Baraza lina jukumu la kupokea, kusikiliza na kuamua kesi za rufaa za ushindani wa kibiashara na udhibiti wa soko zitokanazo na maamuzi ya Tume ya Ushindani pamoja na Mamlaka za Udhibiti ambazo ni EWURA, TCAA, TCRA, LATRA na PURA. Aidha, Baraza linajukumu la kusikiliza rufaa zitokanazo na masuala ya ushindani wa kibiashara na udhibiti wa Soko, pia, Baraza hupokea, husikiliza na kutolea maamuzi rufaa zitokanazo na bidhaa bandia kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Alama za Bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto zinazoikabili Baraza katika utekelezaji wa majukumu yake ambazo ni pamoja na kutokuwa na rasilimali fedha ya kutosha kuweza kushughulikia jambo linalokwamisha

utekelezaji wa majukumu ya Baraza ikiwepo kushindwa kuboresha mifumo ya usajili; uzamini wa Sheria ya Baraza jambo ambalo linakwamisha majukumu ya Baraza ikiwepo sheria ya viwango vya uchangiaji wa fedha kutoka Mamlaka za udhibiti na Serikali kwa ajili ya kuendesha shughuli za Baraza havijainishwa katika Sheria hivyo, kupelekea Wachangiaji kutowajibika katika kuchangia viwango vinavyokidhi mahitaji katika Bajeti ya Baraza; na Kanuni za Baraza zinazotumika kuendesha Mashauri ni za mwaka 2012. Ni wazi kwamba kutokana na mabadiliko ya wakati zinahitaji kufanyiwa maboresho.

Mheshimiwa Spika, Wadau wanaochangia katika bajeti ya FCT na wao ni mionganoni mwa wanaoweza kushitakiwa katika Baraza hilo. Kuna haja ya Sheria ya FCT kufanyiwa mabadiliko na bajeti ya Baraza ikawa inatoka Serikalini kama ilivyo kwa Taasisi nyingine za Serikali. Ni wazi kuwa FCT haltekelezi majukumu yake kwa ukubwa unaotarajiwa kuna haja ya kufanya maboresho ya Sheria na Kanuni za uendeshaji wa shughuli za Baraza ili kuliweka katika nafasi nzuri ya utekelezaji wa majukumu yake; na

Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi ambacho Serikali inaendelea kutafakari mapendekezo ya kubadili Sheria na Bajeti ya FCT ili iwe inatolewa na Serikali badala ya kuchangiwa na wadau, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Taasisi zilizoelekezwa kisheria kuchangia Bajeti ya FCT zinapeleka pesa hizo tena kwa kiwango kilichopangwa. Aidha, kwa kuwa SUMATRA ni moja ya Taasisi iliyopashwa kuchangia bajeti ya FCT na kwa sasa imegawanyika kuwa TASAC na LATRA lakini ni Taasisi ya LATRA tu ndio inachangia, Kamati inaishauri Serikali kuwa TASAC nao wachangie bajeti ya FCT.

k) Kupokea na kujadili maoni ya Wadau wa Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Blueprint na maoni yao juu ya namna bora ya kuboresha mazingira ya kufanya Biashara na Uwekezaji nchini;

Mheshimiwa Spika, katika kikao hiki Kamati ilipokea maoni ya Wadau kutoka Taasisi tatu (3) ambazo ni Shirikisho la Wenyeviwanda Tanzania – CTI, TCCIA na TANEXA ambao

kama Wawakilishi wa Wadau wahusika wanazozisimamia walipata fursa ya kuwasilisha maoni yao juu ya Utekelezaji wa Blueprint lakinia pia maoni yao juu ya maeneo ya kufanyiwa maboresho ili lengo hasa la kuwa na Blueprint litimie.

Wadau walieleza mambo mbalimbali ambayo yaliyofanyiwa kazi kutohana na utekelezaji wa Blueprint pamoja na juhudini mbalimbali za Serikali na kupongeza. Mambo hayo ni pamoja na: -

- Kupungua kwa baadhi ya tozo ambapo jumla ya tozo 60 zilifutwa;
- Muunganiko wa baadhi ya Mamlaka za Udhibiti ambapo inapunguza urasimu wa jambo moja kutekelezwa na Taasisi zaidi ya moja;
- Vikao vya majadiliano kati ya Serikali na Wadau wa Sekta ya Viwanda na Biashara kwa lengo la kusikiliza changamoto mbalimbali zinazokabili sekta hizo;
- Ushirikiswaji wa Wadau katika majadiliano ya uandaaji wa Ajenda za kitaifa, Sera pamoja na mikakati mbalimbali ya kitaifa; na
- Kutumia bidhaa za ndani katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kitaifa.

Aidha, Wadau waliwasilisha changamoto ambazo wangependa zifanyiwe kazi kwa lengo la kuboresha mazingira ya Biashara nchini, changamoto hizo ni pamoja na: -

- a) Mabadiliko ya mara kwa mara ya *Fiscal Policy* jambo linalopelekea Wawekezaji kupata changamoto katika kupanga Bajeti zao za muda mrefu;
- b) Mamlaka za Udhibiti bado ni nyingi na ushirikiano wao ni hafifu jambo linalopelekea usumbufu kwa Wadau na ucheleweshaji wa baadhi ya maamuzi;

- c) Ukubwa wa gharama za ETS jambo linaloongeza gharama za uzalishaji;
- d) Nishati ya umeme siyo wa uhakika jambo linaloathiri uzalishaji viwandani;
- e) Hakuna Sera inayotabirika/kueleweka inayosimamia shughuli za kilimo hususani uuzaji wa mazao ya kilimo jambo linalopelekea kila Mwenye Mamlaka kwa eneo lake anajipangia taratibu zake ikiwepo tozo, namna ya uuzaji wa mazao na kuna muda baadhi ya maamuzi huwa hayana faida sana kwa Mkulima;
- f) Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kutotambua vyeti au makubaliano ya kimazingira yanayotolewa na Mamlaka nyingine za Sekta, mfano cheti cha *Environmental Protection Plan* (EPP) cheti kinachotolewa na Wizara ya Madini;
- g) Serikali kusitisha utaratibu wa kutoa *Export Credit Guarantee Scheme* pamoja na *SME Guarantee Scheme* ambayo ilikuwa inawasaidia Exporters kusafirisha bidhaa zao kwa wakati;
- h) Upatikanaji wa Vifungashio jambo linalopelekea baadhi ya bidhaa zetu kushindwa kushindana katika soko la nje na muda mwagine bidhaa zinapata soko lakini mzalishaji anashindwa kuzalisha kwa kiwango kinachohitajika kwa wakati kutokana na kukosa vifungashio;
- i) Uchelewaji wa kupata *scanner report* kwa ajili ya makasha yanayosafirishwa nje ya Nchi jambo linalopelekea baadhi ya mizigo kuachwa na meli na hivyo kushindwa kumfikia muhusika kwa wakati na pia huongeza gharama sababu utalazimika kulipia *storage*;
- j) Bidhaa ya Korosho kulazimika kupakiwa katika Bandari ya Mtwara wakati hakuna meli kubwa inayoenda katika bandari hiyo lakini pia bandari hiyo haina makasha yakutosha;

k) Uchache wa vyumba vyaa baridi (*Cold rooms*) katika Viwanja vyaa Ndege pamoja na Bandari kunatunyima fursa ya kuuza nje bidhaa kama matunda na mbogamboga kwa wingi; na

l) Sheria ya Madini kuwataka Wachimba madini kulipia asilimia 16 ya *possession* hii inawaumiza Wachimbaji wa chokaa ambayo yenyewe si kama madini mengine yenyewe hutumika kama malighafi.

Mheshimiwa Spika, lengo la kikao hiki ilikuwa kuiwezesha Kamati kupata undani wa utekelezaji wa Blueprint na mazingira ya ujumla ya kufanya biashara. Kamati inaishauri Serikali kuwa na Kalenda ya kodi kwa kipindi cha miaka mitatu mitatu na ndani ya muda huo kusiwe na mabadiliko ya kikodi jambo litakalotoa fursa kwa wawekezaji kupanga mipango yao ya fedha ya muda mrefu;

i) Usafirishaji wa mazao ya kilimo umekuwa na vikwazo sana wakati upatikanaji wa soko bado ni changamoto. Kamati inaishauri Serikali kupunguza vikwazo katika usafirishaji wa mazao ya kilimo ambapo mazao ya Biashara yaruhusiwe kusafirishwa popote ndani ya nchi;

ii) Kwa lengo la kuwawezesha wazalishaji wa ndani kushiriki katika masoko ya kikanda hasa hili soko la Afrika AfCFTA, Kamati inaishauri Serikali kuoanisha (*harmonization*) viwango na taratibu mbalimbali zinazosimamia viwanda ziendane na washindani wetu katika soko ili tuweze kushindana;

iii) Mkataba na SICPA juu ya Stempu za Kodi za Kielektroniki – ETS unaelekea kuisha, Kamati inaishauri Serikali kufanya marejeo ya mkataba huu kwa lengo la kupunguza gharama ya stampu hizo ambazo kiuhalisia ziko juu na kwa baadhi ya bidhaa inaonekana kuwa kubwa kuliko hata kodi inayoingia Serikalini;

iv) Kutokana na changamoto ya uhaba wa makasha pamoja meli kubwa za mizigo kushindwa kufika katika Bandari ya Mtwara, Kamati inaishauri Serikali kutoa fursa kwa mteja

kuchagua Bandari anayoona ni rahisi kwake kutumia isiwe lazima kutumia Bandari ya Mtwara. Pia, ili kuweka matumizi endelevu ya Bandari ya Mtwara, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwa pamoja na Mradi wa Liganga na Mchuchuma pamoja na *Standard Guarge* ili bidhaa mbalimbali ziweze kupelekwa katika Bandari hiyo;

v) Tutambue mazao ya Biashara na utaratibu wa upatikanaji wa leseni ya usafirishaji wa mazao ya Biashara kwa ndani na nje ya nchi uwe unaratibiwa na Wizara moja ambayo ni Wizara ya Viwanda na Biashara;

vi) Katika kuhamasisha uwekezaji tutoe vivutio maalumu kwa muwekezaji atakaekuja kuwekeza kiwanda cha kuzalisha vifungashio ili kuwawezesha wazalishaji wetu wa ndani kuvipata kwa urahisi vikiwa na ubora unaotakiwa na hatimaye kuzifanya na muonekano mzuri (*presentable*) sokoni;

vii) Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira liwe na wepesi na utayari wa kuoanisha masharti ya Sheria ya Mazingira na vyeti vyta kimazingira yanayotolewa na Mamlaka nyingine za Sekta, mfano cheti cha *Environmental Protection Plan* (EPP).

I) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utendaji wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE);

Mhesimiwa Spika, Kamati yako ilipokea taarifa kuhusu Utendaji wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE);

Mhesimiwa Spika, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 31 ya Mwaka 1965, lengo likiwa ni kuanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Biashara Nchini ili kuziba pengo lililokuwepo la wataalamu wa masuala ya biashara na viwandani. Majukumu ya msingi ya CBE ni kutoa mafunzo ya elimu katika fani za biashara, Kufanya tafiti katika

fani za biashara, na Kutoa ushauri wa kitaalam katika fani za biashara.

Mheshimiwa Spika, katika utendaji wa CBE wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ambayo ni uwepo wa mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo wakati uwezo wa mapato ni mdogo; na wanafunzi kuchelewa kulipa ada hivyo kuchelewesha/ kukwamisha baadhi ya shughuli za chuo hususani miradi ya maendeleo na wakati mwingine kusababisha hela hizo kuvuka kuingia mwaka mwingine wa fedha.

Mheshimiwa Spika, CBE ilianzishwa kwa lengo mahsus i la kuziba pengo lililokuwepo la wataalamu wa masuala ya biashara na viwandani. Lakini Kamati ilibaini kuwa pengo hilo bado linaonekana hususani kwa wataalamu wa viwanda bado hawatoshi na Kamati katika ziara zake imeshuhudia wenyewe viwanda wakilalamikia ukosefu wa wataalamu wenyewe fani ya viwandani. Kamati inasisitiza Serikali kushirikiana na CBE kuhakikisha wanafunzi wengi zaidi kujunga na kozi zinazohusiana na masuala ya Viwandani. Aidha, **CBE iongeze kasi ya kujitangaza na ijieleze kikamilifu juu ya entry na exit level zake jambo ambalo litaongeza sifa ya CBE na hadhi yake inayostahili;**

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaishauri CBE kianzishe kitengo cha maendeleo na utafiti na kuwahamasisha wakufunzi wa chuo kufanya tafiti kwa kuwapatia zawadi au kuwatambua wanaofanya vizuri katika utafiti kwa lengo la kuwaongezea ari ya kufanya tafiti. Aidha, Tafiti hizi zitangazwe ili ziweze kutumika kwa maendeleo ya nchi kwa ujumla; na

Mheshimiwa Spika, Chuo cha CBE Dodoma kinatazamia kujenga Hostel/maeneo ya Medeli hali ya kuwa mpango yao ni kufanya CBE mjini kuwa na programu za masomo ya jioni na *post graduate* ambao wahitaji wengi ni wafanyakazi ambao hawahitaji kukaa hostel. Kwakuwa CBE Dodoma ina mpango wa kujenga chuo katika eneo jingine nje ya mji na kwa kutambua ufinyu wa Rasilimali fedha kwa CBE, Kamati inaishauri CBE kuelekeza nguvu zote katika eneo hilo jipya

nje ya mji, badala ya kuendelea kujenga kwa vipande vipande. Ujenzi wa CBE nje ya mji utasaidia wanafunzi kupata eneo litakalo kidhi mahitaji yao yote hususani hostel na kuwaepusha kuishi mitaani.

m) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Programu ya KAIZEN

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilipokea taarifa kuhusu Programu ya KAIZEN. Kamati ilielezwa kuwa Programu ya KAIZEN ni falsafa ya uongezaji endelevu wa ubora na tija kwa njia ya kushirikisha watumishi na uongozi katika kampuni husika kwa lengo la kuleta mabadiliko chanya katika uwajibikaji kwenye kampuni au kiwandani na katika mlolongo mzima wa uzalishaji ili kuhimili ushindani. KAIZEN inatekelzwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na JICA, SIDO na CBE na mradi huu unakusudia kuendeleza Sekta ya viwanda kwa kuimarisha ubora na tija ili kuwezesha viwanda vilivyopo na vile vitakavyoanzishwa viwe na ukiasi endelevu kwa kuhakikisha kuna matumizi sahihi ya rasilimali.

Mheshimiwa Spika, KAIZEN ilianza kutekelezwa nchini mwaka 2013 na baadhi ya changamoto zinazoikabili KAIZEN ni pamoja kasi ndogo ya kuenea kwa falsafa ya KAIZEN kwenye sekta ya viwanda nchini na hii inatokana na ukosefu wa bajeti ya kutosha kuweza kutembelea viwanda ili kutoa elimu kwa wafanyakazi na wamilliki wa viwanda, ukosefu wa wakufunzi wa kutosha ili kwenda sambamba na viwanda vilivyopo nchini hali hii hukwamisha kasi ya kueneza kwa falsafa ya KAIZENI.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Wizara kuongeza kasi katika kutekeleza Programu ya KAIZENI ili waweze kuviflikia viwanda vingi, kwani kipindi cha kuanzia 2015 hadi 2020 Programu ya KAIZENI imeweza kuhudumia viwanda 135 tu na mradi unaelekea kuisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutafuta namna ya kuingiza Programu ya KAIZEN katika Sekta ya Kilimo kwa lengo la kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa viwango

vinavyotakiwa ili viwanda vyetu viweze kupata malighafi zenyе ubora na kwa kiwango kinachohitajika; Aidha, Katika kufundisha wakufunzi wa Programu ya KAIZEN Maafisa Biashara wa Halmashauri wahuishishwe ili waweze kusaidia, kwa wingi wao itakuwa rahisi kusambaza/kuitangaza programu hii.

n) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa Chuma wa Liganga na Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma pamoja na Mpango wa Serikali wa Kufufua Kiwanda cha Matairini cha General Tyre

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hii kamati ilielezwa kuhusu historia ya Mradi wa Chuma wa Liganga na Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma ambapo Miradi ya chuma cha Liganga na makaa ya mawe ya Mchuchuma ipo katika Wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe. Makaa ya mawe ya Mchuchuma yaligunduliwa mwaka 1860 wakati chuma cha Liganga kiligunduliwa mwaka 1898. Tokea kipindi hicho pamekuwepo na tafiti nyingi pamoja na juhudi mbalimbali za kuanzisha kiwanda cha chuma bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, Makaa ya mawe yatakayopatikana yatatumika kwa ajili ya kuzalisha nishati ya umeme wa uhakika kwa ajili ya matumizi ya viwanda na majumbani. Vile vile, makaa yenye ubora wa juu yatatumika katika kuchenjua chuma katika mradi wa Liganga na kama chanzo cha nishati viwandani. Kwa upande mwingine, Chuma kitakachopatikana Liganga kitakuwa ni msingi wa maendeleo ya viwanda vya mitambo na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na dhamira ya nchi yetu kujenga uchumi wa viwanda, tunahitaji kiasi kikubwa cha chuma kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, hata hivyo **Kamati inasikitishwa na namna ambavyo Serikali inalishughulika jambo hili kwani Timu ya watalaam iliundwa mwaka 2007 na watalaam kutoka Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Kazi, Wizara ya Uchukuzi, STAMICO, TANESCO, NDC na Ofisi ya**

Mwanasheria Mkoo wa Serikali hadi leo hakuna hatua zilizofikiwa katika kumaliza majadiliano haya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kiwanda cha matairi cha *General tyre* kamati yako inaona ipo haja ya Serikali kufanya tathmini tena kuhusu kubadili matumizi ya kiwanda hiki ili kuona tija ya mabadiliko hayo.

o) Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na taasisi zake kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2021)

Mheshimiwa Spika Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni Wizara mpya ambayo inaendeshwa kwa Bajeti za Fungu 11, 44 na 60 zilizopitishwa mwaka 2021/2022 chini ya Ofisi ya Waziri Mkoo – Uwekezaji (Fungu 11) na Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44 na 60). Kamati illelezwa kuwa Bajeti zake ni jumla ya Shilingi **112,718,672,000.00** ambapo Fungu 11 ni Shilingi **7,048,213,000.00**, Fungu 44 ni Shilingi **81,398,833,000.00** na Fungu 60 ni Shilingi **24,271,626,000.00**. Hadi mwezi Desemba, 2021, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi **37,568,546,480.67** sawa na asilimia **33.33** ya jumla ya Bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia na kujadili taarifa ya bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai - Desemba 2021) iliyowasilishwa, Kamati imebaini kuwa wizara ina vipaumbele vingi hali inayochangia miradi mingi iliyoibuliwa kutotekelezwa kwa wakati na mingine kutotekelezwa kabisa, Sera hazipo na kama zipo ni za muda mrefu ambazo zimepitwa na wakati, na kiasi kidogo cha bajeti kimetolewa mpaka sasa ambapo ni **asilimia 33.33 tu**.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Wizara hii ndiyo wizara inayoshughulika na viwanda ambavyo tunaamini vitatoa fursa kubwa ya ajira kwa Taifa letu, Kamati inashauri Wizara hii ipewe bajeti ya kutosha na kwa wakati

Mheshimiwa Spika, Aidha, kuwa miradi mingi ya kimkakati inachukua muda mrefu kutekelezwa, Kamati inashauri,

kuwepo na vipaumbele vichache ambavyo vinaweza kutekelezwa kwa wakati. Kwa upande wa Sera zinapotungwa Kamati ni mdau wa wizara hii, hivyo wajumbe washirikishwe kikamilifu ili kutoa maoni kabla Sera haijaanza kutumika.

p) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuhusu utendaji na ufanisi wa kiwanda cha viuwadudu cha Tanzania Biotec Products Limited (TBPL);

Mheshimiwa Spika, Katika kikao hiki kamati yako ilielezwa kuwa, Serikali kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imejenga kiwanda cha kuzalisha viuadudu nya kuua viluwiluwi wa mbu wanaoeneza ugonjwa wa malaria. Ugonjwa wa Malaria unaoongoza kwa kusababisha vifo vingi hapa nchini. Kiwanda hiki kimejengwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimla 100; kwa kutumia teknolojia kutoka nchini Cuba ambapo kampuni ya Labiofam S.A ilipewa jukumu la kujenga na kukabidhi kiwanda hicho kwa Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa ujenzi wa kiwanda Turnkey Agreement kati ya NDC na LABIOFAM ulisainiwa tarehe 29 Aprili, 2010. Masuala makubwa kuhusu majukumu ya LABIOFAM yalikuwa ni kujenga kiwanda kwa utaratibu wa 'Turnkey' kwa miezi 19 ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Kitanzania kabla ya kuanza kazi na hatimaye kuikabidhi NDC kiwanda kinachozalisha viuadudu.

Mheshimiwa Spika, Masuala makubwa kwa upande wa NDC yalikuwa ni kuilipa LABIOFAM gharama za ujenzi wa kiwanda kiasi cha Dola za Kimarekani **22,307,688.20** kwa kuanzia na malipo ya awali (advance payment) ya 75% ya kiasi hicho. Pia NDC ilikuwa na jukumu la kutoa eneo la mradi, kuweka miundombinu ya maji safi na taka, umeme na barabara pamoja na kusimamia ujenzi wa kiwanda na kuajiri wafanyakazi wa kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mradi huu kuwa na lengo zuri kamati yako ilielezwa kuwa bado uzalishaji katika kiwanda hiki ni kwa kiasi kidogo na hakizalishi kwa sasa kwa sababu

kuna changamoto kubwa ya hitilafu za mitambo ya kiwanda ambapo mitambo mingi ya kiwanda haipo katika hali nzuri ikiwemo mfumo wa *air condition* ambao ni mbovu sana na vifaa vyake vingi vimeharibika.

Mheshimiwa Spika, kuna wasiwasi mkubwa kwamba endapo mikoa itaanza kuagiza viuadudu, kiwanda kinaweza kushindwa kuzalisha kukidhi mahitaji. Mitambo ya kiwanda imekua haifanyiwi matengenezo kama inavyohitajika Kitaalamu kutokana na ukosefu wa fedha za kugharamia matengenezo na vipuri. Pia mitambo mingi imepungua ufanisi wake kutokana na kutokutumika ipasavyo. Hitilafu katika mitambo inatokana na menejimenti ya kiwanda kushindwa kuheshimu mikataba iliyosainiwa baina ya Labiofam na wauzaji wa mitambo hiyo toka China.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupokea taarifa ya mradi huu na kufanya majadiliano na wizara Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Serikali iwe na utayari wa kutoa msukumo kwa wizara ya Afya na Tamisemi ambao ndiyo wateja wakubwa wa bidhaa zinazozalishwa (viuwadudu). Aidha, Serikali ihakikishe kiwanda hiki kinaendelezwa ili kufikia malengo yake na dhamira ya Serikali ya kutokomeza malaria inafikiwa.
 - b) Serikali itafute wawekezaji binafsi PPP wenyewe nia ya kuwekeza na kuendeleza kiwanda hichi.
 - c) Hatahivyo, mkataba wa kiwanda hichi ufaniyiwe mapitio kwani asilimia 6 ya faida inayotozwa na mbia ni kubwa sana.
- q) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa Mradi wa NEDF.**

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipokea na kujadili taarifa kuhusu Mfuko wa kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (National Entrepreneurship Development Fund - NEDF), mfuko huu ulianzishwa mwaka 1994 kwa Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kamati yako ilielezwa kuwa Madhumuni ya Mfuko huo ni kutoa mikopo kwa wenyewe Viwanda Vidogo na Wajasiriamali Wadogo Tanzania Bara, kwa lengo la kuanzisha na kuendeleza miradi yao katika sekta zifuatazo:

- a) Sekta ya uzalishaji:** Sekta hiyo inahusika na Viwanda Vidogo, Kilimo, Usindikaji wa Vyakula (matunda na mboga), Ufugaji, Uvuvi na Madini;
- b) Sekta ya biashara:** Sekta hiyo inahusika na uuzaaji wa bidhaa za Vyakula, Vinywaji na Maduka ya bidhaa mchanganyiko; na
- c) Sekta Nyinginezo:** Ambazo ni Afya (maduka ya dawa baridi), huduma za Uchapishaji, Ujenzi, Utalii na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu unaendeshwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kuititia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Mfuko unasimamiwa na kuratibiwa na Kamati ya Kitaifa (National Coordination Committee - NCC), na Mwenyekiti wake ni Katibu Mkuu, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Wajumbe Saba (7) kutoka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Sheria na Katiba, Ofisi ya Waziri Mkuu, "National Microfinance Bank Plc" (NMB), "Tanzania Chamber of Commerce, Industries and Agriculture" (TCCIA) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi cha Miaka 27 (Mwaka wa Fedha 1994/1995 hadi 2020/2021) jumla ya Shilingi 6,648,886,000 zilitolewa na Serikali kuititia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ili kukuza Mfuko wa NEDF. Hata hivyo, kutokana na uwekezaji (*Recapitalization*) unaotokana na riba za makusanyo ya mikopo hadi kufikia Septemba, 2021 mtaji wa Mfuko umekua na kufikia Shilingi 9,765,670,054.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na SIDO katika usimamizi wa mradi huu, Kamati inashauri Serikali iendelee kutafuta Fedha zaidi ili mfuko uwezo kuwafikia

wananchi wengi zaidi hasa wa vijjini ambao ndio wazalishaji wakubwa. Aidha, Serikali kupitia SIDO wajitahidi kupunguza riba ya mikopo ambayo ni asilimia 18 hadi 22 inayotolewa kwa wajasiriamali na iangalie upya vigezo vyta kutoa mikopo ili vijana wengi wanaomaliza masomo yao waweze kutambuliwa na kupewa mikopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ione uwezekano wa SIDO kupitia wataalamu wake kubuni vyanzo mbadala vyta kupata Fedha kama vile kuandaa maandiko mbalimbali yanayohusu ubunifu na uendelezaji wa vipaji mbalimbali ili waweze kuwa na mfuko ambao utawezesha kupata fedha kutoka mashirika mbalimbali duniani kama vile *Global Innovation Fund*.

2.5 Kupokea na Kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira na Taasisi zilizo Chini yake;

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira inasimamia na kushauri kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu masuala ya Usimamizi wa Mazingira. Katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022 ilipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii. Taarifa hizo ni kama ifuatavyo:

a) Kupokea Maelezo ya Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu Majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira ambapo ilielezwa kuhusu majukumu ya ofisi hii ambayo ni Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera zinazohusiana na masuala ya uhifadhi wa mazingira; Kuratibu shughuli za ulinzi wa Mazingira na kusimamia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004; Kuhamasisha uchumi, uzalishaji na uwekezaji unaozingatia Mazingira endelevu. Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ni mratibu wa masuala yote yanayohusu Mazingira lakini watekelezaji wa kuu ni Mamlaka ya Serikali za mitaa kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 .

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa changamoto zinazoikabili Ofisi hii katika kutekeleza majukumu ya Usimamizi wa Mazingira ambazo ni pamoja na Mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ongezeko la joto, mafuriko ya mara kwa mara na ukame; Usimamizi wa taka zitokanazo na vifaa vya umeme; Viumbe vamizi; Usimamizi wa kemikali na Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi;

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zetu zina Maafisa mazingira lakini weledi na mchangno wa maafisa hawa katika kusimamia masuala ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira hauridhishi. Kamati inaishauri Serikali kuwahamishia maafisa mazingira au kuwataka waripoti moja kwa moja katika Wizara yenye dhamana ya Mazingira. Aidha, wanapotaka kuajiri maafisa wa kushughulikia mazingira waangalie wenyewe taaluma ya mazingira;

Mheshimiwa Spika, Jitihada ziongezwe katika utoaji elimu na uhamasishaji kuanzia katika ngazi ya chini kabisa ya familia juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira na athari tunazoweza patikana kutokana na uharibifu wa mazingira. Jambo hili liende sambamba na elimu ya kutenganisha taka katika ngazi ya familia ili kurahisisha uchakataji wa taka hizo (handling);

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa kampeni za upandaji miti hasa Kampeni ya upandaji wa Miti milioni 1.5 katika kila Halmashauri, Serikali ilete mpango wa ufuatiliaji wa miti hii baada ya kuipanda ili kuhakikisha imekua na lengo/kusudio hasa la kampeni limefanikiwa

Mheshimiwa Spika, Serikali ilieleza kuwa kuna ongezeko la kina cha bahari jambo linalopelekea baadhi ya Visiwa kuwa katika hatari ya kupotea. Kamati inaishauri Serikali kuongeza jitihada katika kulinda mazingira ya bahari na maeneo yanayozunguka visiwa hivyo ili kuepukana na hatari ya kupotea kwa visiwa hivyo;

Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto ya ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa na kuni, Kamati inaishauri Serikali

kuhamasisha uzalishaji wa mkaa mbadala pamoja na kuongeza matumizi ya gesi na umeme. Mpango huu uende sambamba na upunguzaji wa bei za gesi na umeme ili kuwawezesha wananchi wa kawaida waweze kumudu gharama za nishati hizo. Vile vile uhamasishaji ufanyike kwa ajili upandaji wa miti maalum ya kutengenezea mkaa, ili kurahisisha upatikanaji wa magogo kwa ajili ya kutengenezea mkaa na wahusika wafundishwe uvunaji endelevu wa mkaa.

b) Kupokea Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu Majukumu ya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira – *NEMC*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili kuhusu majukumu ya Baraza la Taifa la uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*). Ambapo kwa mujibu wa kifungu Na. 20 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) linapewa jukumu la kusimamia hifadhi ya Mazingira nchini ili kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali kwa ajili ya ustawi wa maisha bora ya wananchi wa Tanzania. Majukumu mengine ya baraza ni pamoja na Kufanya mapitio na kutoa mapendekezo ili kuwezesha kupitishwa kwa taarifa/ripoti za TAM; kuainisha miradi au programu zinazohitaji kufanyiwa ukaguzi na ufuatillaji (Audit and Monitoring); kuhimiza na kuhakikisha usimamizi na uzingatiaji wa viwango vyta taifa katika utekelezaji wa sheria;

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uelewa mdogo wa wadau na Wananchi kuhusu Sheria ya Mazingira; upungufu na Migongano katika Baadhi ya Sheria; NEMC kutokuwepo kwenye mikoa yote ya Tanzania; Malalamiko ya Wadau kuhusu gharama kubwa za Tozo za Mazingira; Mapungufu kwenye kanuni ya ada na tozo za Mazingira ya Mwaka 2019 ambapo kuna baadhi ya miradi hajabainishwa katika kanuni hizo; Upungufu wa Watumishi; Ucheleweshaji

wa vibali vya Mazingira; Uwekezaji katika Maeneo ambayo hayakutengwa na kufanyiwa Tathmini ya Athari ya Mazingira;

Mheshimiwa Spika, Sekta nyingine hazina Miongozo ya Tathimini za Athari kwa Mazingira wakati Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 imeelekeza sekta zote kuwa na miongozo yake. Kamati inaishauri Serikali kuzifua tililia sekta zote na kuhakikisha zinatekeleza jambo hili kwa kuwa uwepo wa miongozo hii utasaidia kuainisha masuala katika kila sekta ili kurahisisha utekelezaji wa masuala yanayohusu tathimini ya athari kwa mazingira;

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira linadhamana kubwa ya kusimamia na kuratibu shughuli za usimamizi wa mazingira lakini kuna baadhi ya maamuzi ni lazima yafanywe na Waziri mwenye dhamana. Kamati inaishauri NEMC wapewe mamlaka kamili, badala ya kuwa Baraza iwe Mamlaka ya Taifa ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira, hatua hii itaipa mamlaka kamili ya kusimamia masuala ya Mazingira na kutoa maamuzi na pia tutampunguzia Waziri majukumu;

Mheshimiwa Spika, Katika kupambana na changamoto ya usimamizi wa takataka ngumu nchini, Kamati inaishauri Serikali kuwahamasisha Sekta Binafsi kuwekezaji katika miradi ya kuchakata takataka na kutengeneza mkaa, umeme na bidhaa nyingine. Jambo hili liende sambamba na kuelimisha jamii mpaka katika ngazi ya familia namna ya kutenganisha takataka za majumbani;

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Halmashauri kuainisha maeneo ya Uwekezaji husasani maeneo ya viwanda, pia iandaliwe kanzidata (*Database*) ya maeneo hayo na wawekezaji pindi wanapojoitokeza waelezwe juu ya maeneo hayo, jambo hili litapunguza changamoto ya kuwekeza mahala pasipo sahihi lakini pia itahifadhi mazingira yetu;

c) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa ajili ya kuijengea uelewa Kamati kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilipata fursa ya kupokea taarifa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi ni mabadiliko ya kudumu na muda mrefu katika mifumo ya hali ya hewa na uso wa Dunia yanayotokana na ongezeko la gesijoto zinazosababishwa na shughuli za maendeleo ya binadamu. Nchini Tanzania uwiano wa uzalishaji wa gesijoto kisekta ni Kilimo, Misitu, na Mabadiliko ya matumizi ya ardhi asilimia **93.2**, Nishati asilimia **3.8**, taka asilimia **1.5** na viwanda **0.5**.

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko ya tabianchi husababisha athari kwa mazingira, jamii na uchumi. Baadhi ya athari hasi za mabadiliko ya tabianchi ambazo zimekwishaonekana ni pamoja na kuongezeka kwa ukame na mafuriko; kuenea na kusambaa kwa haraka kwa magonjwa ya kuambukiza; kuyeyuka kwa barafu katika vilele vya milima mirefu; kuongezeka kwa ujazo wa maji ya bahari, hivyo kusababisha kupanda kwa kina cha maji na kufunika visiwa na kuingia kwa maji chumvi katika maeneo ya mwambao; kupotea kwa baadhi ya viumbe hai na biaoanuwai; kuharibika kwa mifumo ya ikolojia; Kupanda kwa hali ya joto na baridi katika baadhi ya maeneo; na kuongezeka kwa matukio ya vimbunga vikali.

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko ya tabianchi husababisha athari kwa mazingira, jamii na uchumi. Baadhi ya athari hasi za mabadiliko ya tabianchi kwa ujumla wake ni pamoja na kuongezeka kwa ukame na mafuriko; kuyeyuka kwa barafu katika vilele vya milima mirefu; kuongezeka kwa ujazo wa maji ya bahari, hivyo kusababisha kupanda kwa kina cha maji na kufunika visiwa na kuingia kwa maji chumvi katika maeneo ya mwambao; Kupotea kwa baadhi ya viumbe hai na biaoanuwai; Kuharibika kwa mifumo ya ikolojia; kupanda kwa hali ya joto na baridi katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, Jitihada mbalimbali ya Kitaifa na kimataifa zimefanyika kwa ajili ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, jitihada hizo zinakumbana na changamoto zifuatazo, Uelewa mdogo kwa wadau kuhusu changamoto za mabadiliko ya tabianchi na fursa zilizopo; Ukosefu wa fedha za kutosha – Mabadiliko ya tabianchi yameathiri sekta nydingi na mahitaji ni makubwa sana kwa sasa ukilinganisha na kasi ya upatikanaji wa fedha. Uandaaji wa miradi unachukua muda mrefu kwa fedha kupatikana na kuanza utekelezaji; kuongezeka kwa athari zitokanazo na tatizo la mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ukame, mafuriko, kuenea kwa magonjwa ya malaria, kuongezeka kwa kina cha maji ya Bahari yanayotishia kumeza visiwa vidogovidogo; na Kukosekana kwa fedha za kutosha kufanya utafiti katika maeneo na sekta nydingi kunasababisha mipango ya utekelezaji inayoandaliwa kuwa – *Reactive* badala ya *pro-active*.

Mheshimiwa Spika, kuna NGOs zinazopokea fedha za wafadhili kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uhifadhi wa Mazingira lakini mchango wa NGOs hizo bado hauonekani. Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudu katika kuzitafuta NGO's zote nchini zinazopokea fedha za uhifadhi wa mazingira kwa lengo la kuzitambua na kuzifuatilia kuhakikisha fedha wanazopewa zinatekeleza lengo lililokusudiwa;

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa kuongeza kasi ya utoaji elimu juu ya umuhimu wa kuhifadhi na kutunza mazingira yetu pamoja na athari zinazoweza kutokea kama hatukuyahifadhi kwa lengo la kubadili mitizamo ya watu wetu kifikira, kwa sasa watu wengi wakiambiwa kutunza mazingira wanajua ni kufagia tu;

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi mwanachama wa Mikataba mbalimbali ya Mabadiliko ya Tabia nchi, na sisi ni moja kati ya nchi zinazofanya vizuri katika kutunza misitu hivyo kupunguza hewa ukaa, tutumie mwanya huu kuandika maandiko mengi zaidi yatakayotuwezesha kupata fedha za kutekeleza miradi ya Uhifadhi wa Mazingira;

d) Kupokea na kujadii Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu matumizi salama ya Bioteknolojia ya kisasa katika Mazingira

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuhusu matumizi salama ya Bioteknolojia. Aidha, Bioteknolojia ni aina ya teknolojia inayohusisha mifumo hai au sehemu ya viumbe hai katika kuboresha uzalishaji wenyewe tija kulingana na malengo ya uzalishaji uliokusudiwa. Teknolojia hii inawezesha uhamishaji wa vinasaba vya uhai kutoka kiumbe kimoja kwenda kiumbe kingine kisichohusiana nacho kiuzazi. Kwa mfano vinasaba vya kustahimili ukame katika bacteria vinaweza kuhamishiwa kwenye zao la mhindi ili kufanya zao la mahindi liwe na tabia ya kustahimili ukame;

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Bioteknolojia ya kisasa inamanufaa/faida mbalimbali mfano katika sekta ya kilimo huongeza mavuno, Uwezo wa kustahimili magonjwa, Uwezo wa kustahimili wadudu waharibifu, kuongeza virutubisho lishe kwa wingi pamoja na Uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa upande wa sekta ya Afya bioteknolojia ya kisasa ina faida ya Kutengeneza dawa na chanjo, Kubaini viini na vimelea vya magonjwa na Kubaini vihatarishi vya magonjwa;

Mheshimiwa Spika, Pamoja na faida zake bado Bioteknolojia ya Kisasa ina athari zake ambazo kwa upande wa mazingira ni Uchavushaji wa mazao yasiyohusika, Madhara kwa viumbe ambavyo havikukusudiwa, madhara kwa bioanuai na uoto wa asili; kwa upande wa kilimo ni pamoja na kujitokeza kwa magugu sugu, kuibuka kwa visumbufu sugu vya mazao, na Uwezekano wa mbegu kuwa ghali kwa vile teknolojia hii ni għali.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kuelimishwa juu ya matumizi hayo, kamati iliona Serikali inapaswa kuangalia namna ambayo wanaweza kuanza kutumia GMO's kwa hatua ambapo wanaweza anza na mazao ya kibiashara mfano Pamba na Katani kisha kadiri muda unavyokwenda tutafanya maamuzi ya namna ya kuendelea kwani

kuendelea kutumia njia za asili katika kilimo cha biashara hatutaweza kushindana katika la Dunia;

Mheshimiwa Spika, hatuna mpango usimamizi wa uingizaji wa bidhaa zinazotokana na GMOs, mfano bidhaa za *pringos* zinasadidiika kuwa zinatokana na mmea wa GMO. Kamati inaishauri Serikali kutambua uwepo wa bidhaa za aina hiyo katika soko letu lakini pia tuandae mkakati madhubuti wa kuweza kutambua bidhaa hizo na kuzidhibiti kuhakikisha zinapata vibali kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kama Sheria inavyoolekeza.

e) Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuhusu Mkakati ya kukabiliana na viumbe vamizi Nchini;

Mheshimiwa Spika, Katika kikao hiki, kamati ilielezwa kuhusu Mkakati ya kukabiliana na viumbe vamizi Nchini. Viumbe Vamizi ni Kiumbe chochote kigeni katika mazingira ambacho uwepo wake huleta madhara kwa mazingira, uchumi, baionuai, afya ya jamii, mifugo na mimea. Chanzo cha Viumbe vamizi ni Shughuli za kibinadamu ambazo huwaleta viumbe maeneo mapya, shughuli hizo ni pamoja na majaribio ya mazao ya kilimo, misitu na mifugo; mizunguko ya mifugo toka eneo moja na jingine; mabadiliko ya tabianchi; viumbe kubadili tabia kukabiliana na mabadiliko yeyote; maendeleo ya mifumo ya usafiri duniani (mf. Safari za meli); na Mifumo ya asili kama Upepo.

Mheshimiwa Spika, Tafiti zinaonesha kuna aina 220 za Viumbe Vamizi nchini wa jamii ya mimea, wanyama na wadudu. Athari za viumbe hawa zinajitokeza zaidi katika sekta za Maliasili na Utalii, kilimo, Afya, uvuvi na mifugo. Madhara hayo ni pamoja na kupungua kwa bionuai na kuharibu vyanzo vya maji; kiuchumi hupunguza uzalishaji kilimo na kuathiri shughuli za utalii; kiafya na jamii husababisha kueneza magonjwa na kupunguza uzalishaji chakula;

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ina Mkakati na Mpango kazi wa kitaifa wa usimamizi viumbe

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Vamizi Nchini, lengo la mkakati huo ni kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania, mifumo ya kiikolojia na rasilimali za nchi ziko salama dhidi ya madhara hasi ya viumbe vamizi. Mkakati huo pia unalengwa kuimarisha udhibiti wa njia za uingiaji na kuenea kwa viumbe vamizi; Kupunguza madhara yatokanayo na viumbe vamizi, Kuimarisha uwezo wa Taifa katika kusimamia na kufanya tafiti katika masuala ya viumbe vamizi; Kuendelea kutoa elimu na kujenga uwezo wa jamii na wadau; Kupitia na kuhuisha masuala ya viumbe vamizi kwenye Sera, Sheria, Kanuni na Mikakati ya kisekta; na Kuimarisha ushirikiano na uratibu katika usimamizi na udhibiti wa viumbe vamizi nchini.

Mheshimiwa Spika, Kuna baadhi ya viumbe vamizi ambayo athari zake katika mazingira zimekwishaonekana na zinaenea kwa kasi sana mfano gugu karoti ambalo limeathiri mifugo na mdudu kantangaze ambao wameathiri shughuli za kilimo, Kamati inashari zichukuliwe hatua za haraka katika kuteketeza viumbe hivi;

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuzielekeza Wizara/mamlaka kuweka ushirikiano katika kudhibiti au kutokomeza Viumbe vamizi, mfano Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira washirikiane kutokomeza kiumbe vamizi wanaoathiri sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, magugu maji ni moja ya kiumbe vamizi ambalo tumelishuhudia limeenea katika maziwa hususani ziwa Victoria ambapo huathiri makazi na mzalia ya samaki, lakini gugu maji hili linaweza kutumika kama chakula cha mifugo na wenzetu nchi jirani zinazizunguka ziwa Victoria linatoa vivali vya kuvuna gugumaji kwa ajili ya mifugo lakini sisi tunakataza. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kutoa vibali na kutafuta namna nzuri ya kusimamia uvunaji huo kuhakikisha halisambazwi kwenye vyanzo vingine vya maji.

f) Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuhusu Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya maji;

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina eneo la Ardhi lenye ukubwa wa hekta milioni 94.5 ambapo kati ya eneo hilo hekta milioni 89 ni za Ardhi na eneo linalosalia ni eneo la maji. Tanzania inakabiliwa na changamoto za uharibifu wa mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji unaosababishwa na shughuli za binadamu zisizo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Changamoto zilizopelekea Serikali kuanzisha mkakati huu ni pamoja na kilimo kisicho endelevu katika maeneo ya vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kwenye vilele na miteremko ya safu za milima; ufugaji wa mifugo mingi inayozidi uwezo wa malisho na ufugaji wa kuhamahama na makundi makubwa ya mifugo; uharibifu unaosababishwa na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni, mkaa na shughuli za ujenzi; matukio ya mara kwa mara ya uchomaji moto misitu; na uchimbaji wa madini usioendelevu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua zilizoripotiwa kuchukuliwa na Serikali katika kutatua changamoto hizo ni pamoja na Kuondoa wafugaji na wakulima waliovamia mabonde, maeneo ya vyanzo vya maji na hifadhi kwa kushirikisha makundi yote; Kudhibiti na kusimamia uhamaji wa mifugo kutoka eneo moja kwenda jingine; Kubainisha vyanzo vya maji, kuvilinda na kuanzisha kanzi data ya vyanzo vya maji na hali ya mazingira yake; Kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa katika kaya na maeneo ya mikusanyiko mikubwa ya watu kama shule, magareza, kambi za jeshi na vituo vya afya na hospitali; Kudhibiti matukio ya uchomaji moto wa misitu na nyika; na Kuzuia shughuli za uchimbaji holela mchanga kokoto na mawe kwa ajili ya ujenzi;

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na muingiliano wa maamuzi yanaotolewa na mamlaka mbalimbali ambazo zote kwa namna moja ama nyingine zinahusika Katika kulinda vyanzo vya maji, **Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya**

kuziunganisha mamlaka zote husika (mfano mamlaka za Bonde, TFS na Sheria ya Mazingira) ili ziweze kufanyakazi kwa pamoa ili tuweze kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali hizi; na

Mheshimiwa Spika, kwakuwa, uelewa wa jamii juu ya masuala ya uhifadhi wa mazingira bado ni mdogo, **Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utoaji elimu na kuhakikisha wanawafikia watu wengi zaidi.** Aidha, ubunifu utumike watu wafuatwe kwa kuangalia makundi yao na aina ya shughuli wanazofanya na kupewa elimu stahiki juu ya utunzaji wa mazingira kuhusianisha na shughuli wanazofanya;

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ambayo yanalindwa na Sheria ya Mita 60 ambapo mengine yanaruhusu shughuli za kijamii kufanyika na mengine hayaruhusi shughuli za jamii kufanyika, kwa maeneo ambayo Serikali haitaruhusu kabisa kufanyika kwa shughuli ndani ya mita 60 kutoka chanzo cha maji, Serikali itenye bajeti ya kuyatunza maeneo hayo ili kuyaepusha kuwa vichaka vitakavyoweza hifadhi wahalifu au wanyama wakali kama nyoka.

g) Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Uendeshaji wa shughuli za Mfuko wa Mazingira;

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu ulianzishwa kuititia kifungu cha 213 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya Mwaka 2004. Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kuisaidia wizara yenye dhamana ya kusimamia masuala ya mazingira kutafuta fedha kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kutekeleza shughuli za usimamizi wa mazingira baada ya kubaini changamoto nyingi za mazingira na kuona bajeti ya Usimamizi wa Mazingira haitoshi.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoukabili Mfuko ni pamoa na uhaba wa fedha jambo linalopelekea kushindwa kuendelea na utekelezaji wa Majukumu wa mfuko; Changamoto ya kisheria ambapo Sheria Mazingira inamtambua Mkurugenzi wa Mazingira kuwa Afisa Masuhuli

wa Mfuko wakati yeye ni msimamizi wa moja kwa moja wa Sheria ya Mazingira italeta mgongano wa maslahi; Sheria hajatamka bayana wajibu wa Waziri mwenye dhamana ya Mazingira kutoa miongozo ya kisera kwa Bodi ya Mfuko jambo linaloweza kupelekea masuala ya kisera kutokupewa uzito wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu ya Mfuko ambao utazingatia maelekezo ya Bodi.

Mheshimiwa Spika, changamoto za kisheria zimepelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake kwakuwa Mfuko umeshindwa kusajiliwa na Msajili wa Hazina. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha kwa haraka mchakato wa kuhuwishwa Sheria ya Mazingira ili kukidhi matakwa yote yanayohitajika ili kukamilisha muundo wa mfuko huu na kuuwezesha kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa;

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto ya kuuweka Mfuko wa Mazingira kama taasisi inayojitegemea lakini pia Serikali imejielekeza katika kupunguza wingi wa taasisi, Kamati inashauri Serikali kuuweka Mfuko wa Mazingira chini ya Taasisi ya NEMC;

Mheshimiwa Spika, Katika kutafuta vyanzo vya mapato vya mfuko wa mazingira Serikali isijielekeze katika kuanzisha chanzo kipywa cha tozo au kuongeza kodi ambao tayari zimeonekena kuelmewa mfano tozo iliyopo katika mafuta (petrol na disel).

Mheshimiwa Spika, Vyanzo vya mapato vipatikane kutoka katika shughuli ambazo moja kwa moja zinahusika na mazingira mfano tozo ya uvunaji wa misitu asilimia chache iingie kwenye Mfuko wa Mazingira. Aidha, Serikali ihushe Sekta Binafsi katika kuchangia kwenye shughuli za utunzaji wa Mazingira.

h) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Kampeni Kabambe ya Uhifadhi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa hiyo changamoto za uharibifu wa mazingira nchini zimeendelea kujitokeza,

baadhi ya changamoto hizo ni Uharibifu wa ardhi ambapo asilimia 16 ya ardhi ya nchi imeharibika na asilimia 61 iko hatarini kuharibiwa; Uharibifu na ufyekaji wa misitu ambao 469,420 za misitu hufyekwa kila mwaka; Ongezeko la athari za mabadiliko ya tabianchi; na Uharibifu wa mifumo ikolojia ya majini.

Mheshimiwa Spika, maeneo mahsusni ya Kampeni Kabambe kwa mwaka 2021-2022 ambayo ni maeneo yaliyoonekana kuwa changamoto zaidi ni pamoja na Usimamizi wa taka na usafi wa mazingira; Uzalishaji endelevu viwandani; Udhibiti wa viumbe vamizi; Matumizi ya nishati mbadala; Mabadiliko ya tabianchi; Upandaji na utunzaji wa miti; Uchimbaji endelevu wa madini; Kilimo na ufgajji endelevu; Uvuuvi endelevu; na Hifadhi ya vyanzo vya maji na matumizi endelevu ya rasilimali za maji.

Mheshimiwa Spika, Shughuli za binadamu kwa kiasi kikubwa zinahuzisha matumizi ya rasilimali tulizonazo ikiwepo misiti na vyanzo vya maji, tuzielimishe jamii juu ya matumizi endelevu rasilimali hizi badala ya kuweka makatazo/vikwazo katika kutumia rasilimali hizo. Mfano watu wafundishwe juu ya uvunaji endelevu wa mkaa badala ya kukataza au kutozwa kodi kubwa ya mkaa. Pia, jamii zielimishwe juu ya matumizi sahihi ya maeneo ya kandokando ya maji, yani Sheria ya Mita 60 na Kanuni za kutumia maeneo ya ndani ya Mita 60 kutoka kingo za maji ziwekwe wazi na jamii ielimishwe;

Mheshimiwa Spika, Tozo ya Rais kwa halmashauri zinazofanya vizuri katika kampeni za upandaji miti ilitolewa kwa mara ya mwisho 2014, Tuzo hii irudishwe kwakuwa ilikuwa ikitoa motisha kwa Halmashauri pia ilikuwa inataja Halmashauri zilizofanya vibaya pia hivyo zilikuwa zikiongeza juhud;

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze nguvu na kazi katika kutoa elimu ya Uhifadhi wa Mazingira na elimu hii ijielekeze katika kubadili mitazamo ya jamii juu ya umuhimu wa kutunza mazingira na athari zitokanazo iwapo mazingira hayatahifadhiwa. Aidha, tuanzishe mitaala maalumu ya Elimu ya masuala ya uhifadhi wa mazingira kuanzi katika ngazi ya

Shule ya Msingi kwa lengo la kuvijenga vizazi vyetu juu ya umuhimu wa Kuhifadhi mazingira;

Mheshimiwa Spika, Serikali irudishe utaratibu uliokuwa unafanyika awali wa kutoa ruzuku kwa wadau wanaojitolea kushiriki jitihada za kutunza na kuhifadhi mazingira, mfano wadau wanaofanya “Agrofarming” watambuliwe na kupewa tuzo. Utaratibu huu ulikuwa unahamasisha jamii kushiriki katika harakati mbalimbali ambazo zinalenga kutunza na kuhifadhi mazingira;

i) Kupokea na kujadili taarifa ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira – NEMC kuhusu uratibu wa Tafiti za Mazingira, uainishaji wa Changamoto za Mazingira na Kuandaa Miradi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004 inatoa fursa kwa NEMC ya kufanya tafiti za mazingira, katika maeneo mbalimbali yakiwemo maeneo lindwa na nyeti kwa lengo la kutambua changamoto za kimazingira kwenye maeneo mbalimbali na namna ya kuzitatu. Tafiti hizi pia hutumika kuhuishwa masuala ya mazingira katika mipango ya maendeleo; kufikia lengo la uchumi wa kati unaojengwa na viwanda na usimamizi madhubuti wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya changamoto za kimazingira zenyet kuhitaji ufumbuzi ni pamoja na uharibifu wa ardhi; uharibifu misitu; upotea kwa makazi ya viumbe-pori na bioanuai; kupungua kwa ubora wa mifumo ya maji; Uchafuzi wa mazingira hasa katika maeneo ya mijini; Mabadiliko ya Tabia Nchi; Mimea Vamizi; na Taka Hatarishi kwa mfano takaa za kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa tafiti za mazingira ni pamoja na baadhi ya sekta kutotoa kipaumbele kwa masuala ya mazingira au kuwa na mawazo kuwa uhifadhi wa mazingira unakinanza na maendeleo jambo linalopelekea baadhi ya wadau kusita kushiriki kikamilifu kwenye tafiti za mazingira kwa hofu ya

kudhihirika kwa mambo yao yasiyozingatia sheria; uwezo mdogo kifedha na rasilimali watu katika kufanya tafiti;

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Mazingira 1997 ni nyenzo kuu inayotumika katika kutekeleza shughuli za usimamizi wa mazingira lakini kwa sasa Sera inayotumika ni ya mwaka 1997 ina umri takribani wa miaka 25 ambapo kuna mabadiliko na changamoto nyingi za kimazingira zimejitokeza na Sera hii haizitambui. yamekamilika na imepata Baraka ya Baraza la Mawaziri. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka mchakato wa kupata Sera mpya maana Sera hiyo inategemewa sana ili kufanya mchakato wa maboresho ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 kwa kuwa kuna baadhi ya mambo yamekwama utekelezaji wake kwa kuwa yalikuwa na changamoto za kisheria ikiwepo Mfuko wa Taifa wa Mazingira;

Aidha, Sera mpya na Sheria itakapoboreshwu izitambue Taasisi ya TFS, TANAPA na Ngorongoro *conservation area* kama wanufaika wakubwa wa mazingira, waelekezwe kuchangia walau kwa asilimia chache katika Mfuko wa Taifa wa Mazingira ili kuendeleza shughuli za usimamizi wa mazingira;

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye *Mapping* ya Nchi nzima kuainisha maeneo yenye changamoto za kimazingira na yale ambayo kutokana na shughuli zinazofanyika yanaweza kuathirika baadae hatua ambayo itatoa picha ya jitihada zinazohitajika na kuwezesha kujipanga;

Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto ya upungufu wa Rasilimali watu kwa NEMC, Kamati inaishauri NEMC kuwatumia Maafisa Mazingira ambao wapo katika kila Halmashauri ili waweze kuwasaidia kusimamia masuala ya mazingira katika maeneo yao kwa kuzingatia mahitaji ya NEMC.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri kuwa Serikali ianzishe vituo vya Mazingira katika ngazi ya kijiji ili waweze kuifikia jamii kwa urahisi na kuwapa elimu stahiki kutokana na aina ya

uharibifu wanaoufanya, ukaribu huu utazifanya jamii kuwa vinara wa utunzaji wa mazingira bila kusukumwa. Aidha, itolewe elimu ya kutosha kwa wadau mbalimbali wa mazingira juu ya uwepo wa *Green Climate Fund* ili waweze kuzipata fedha hizo na kuongeza kasi katika kutekeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira; na

Mheshimiwa Spika, kemikali ya zebaki inayotumiwa na wachimbaji wadogo katika kuchenjua Dhahabu inauzwa kwa kificho/magendo, Kamati inaishauri Serikali kuwatafuta waingizaji wa zebaki nchini na kuwaweka wazi ni nani na nani wenye vibali vya kuuza hiyo zebaki na zile za magendo zikazuiliwa hatua ambayo tutaweza kudhibiti matumizi yake;

j) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Mwongozo wa Usimamizi wa Usafishaji Mito katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na mikakati ya Serikali katika kuainisha maeneo ya Uchimbaji mchanga Nchini.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Muongozo wa Usafishaji Mito katika Jiji la Dar es Salaam ulianzishwa kwa lengo la kupunguza madhara yanayoweza kutokana na uchimbaji holela wa mchanga katika mito ya Dar es Salaam. Madhara yanayotazamiwa ni pamoja na mmomonyoko wa kingo za mito, mafuriko, uharibifu wa miundo mbinu, mali na hata uhai wa watu na viumbe hai wengine.

Mheshimiwa Spika, malengo na madhumuni ya Mwongozo huu ni kuelekeza aina ya mfumo (*Framework*) wa usafishaji wa mito kwa kuondoa mchanga jinsi utakavyofanyika ili mazingira yaendelee kuwa salama na kuhakikisha tope na taka ngumu zinazohitaji kuondolewa unafanyika kitaalam ili kuepuka mafuriko na kingo za mito kuharibiwa; kuzitambua shughuli za usafishaji wa mito kama ajira na kuziratibu kwa utaratibu unaofaa ambao unaleta manufaa ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mwongozo umebainisha wadau wanaohusika katika shughuli hii na kuwagawia majukumu yao, wadau hao ni NEMC, Mamlaka ya Bonde la Wami na

Ruvu, Tume ya Madini, TANROAD, TARURA, TRC na Sekretarieti ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya changamoto zinazojitokeza wakati wa kusimamia utekelezaji wa Mwongozo huu ni uelewa mdogo wa jamii juu ya maana na umuhimu wa kusafisha mito, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Usimamizi na Uhifadhi wa vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla; wakandarasi na vikundi kukosa uaminifu na kughushi nyaraka ili kujiongezea kipato; baadhi ya Kamati za Mazingira na Serikali za Mitaa kutokuwajibika ipasavyo katika kusimamia ufanisi wa usafishaji wa mito kwa mujibu wa mikataba na maelekezo ya Kikosi Kazi; na baadhi ya wakandarasi na vikundi kutofuata taratibu na maelekezo ya kimkataba na matokeo yake wanaharibu mazingira na kuzuka kwa migogoro kati yao na jamii;

Mheshimiwa Spika, Mwongozo huu ni wa mwaka 2019 na unatumia Dar es Salaam kama eneo la mfano. Kwa kuwa umeshatekelezwa kwa miaka miwili sasa, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mwongozo wa Nchi nzima na kuanza utekelezaji katika maeneo mengine tuisubiri mpaka na yenye yakaathirika zaidi;

Mheshimiwa Spika, Kwa sasa Jiji la Dar es Salaam lina Dampo la kisasa moja tu ambapo ni changamoto kwa takataka za Jiji zima kuweza kufikishwa katika dampo hilo jambo linalopelekea baadhi ya Wananchi waliokaribu na mito kutupa takakata katika mito. Kamati inaisisitiza Serikali kuja na mkakati wa kujenga madampo kulingana na ukubwa wa Jiji la Dar es Salaam na wingi wa watu. Jambo hili liende sambamba na uhamasishaji wa uwekezaji viwanda vya kuchakata taka;

Mheshimiwa Spika, Suala la wasafisha mito kulipia kibali cha kusafisha na kibali cha madini yaweza kuwa changamoto inayopelekea kasi ya kusafisha mito kuwa ndogo. Mfano mto Msimbazi una urefu wa kilomita 18.32 lakini ni km 1.07 tu ndio zimesafisha na Mto Mbezi una km 10.40 lakini ni km 5.36 ndio zimesafisha. Kamati inaishauri Serikali kupunguza aina

moja ya tozo hasa hii ya madini kwa kuwa watu wale wameshawekwa katika kundi la Wasafishaji na sio Wachimba mchanga;

Mheshimiwa Spika, Serikali izihimize Halmashauri kuainisha na kutenga maeneo kwa ajili ya uchimbaji wa madini ujenzi (mchanga, kokoto, kifusi na mawe) ili kulinda mazingira na kusaidia maendeleo;

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 inaruhusu kufanyika kwa shughuli ambazo sio za kudumu katika eneo la ndani ya Mita 60 kutoka kingo ya vyanzo vya maji, lakini kuna baadhi ya Watendaji wa Serikali katika ngazi za Vijiji hawana elimu hii na wamekuwa wakiwakataza na kuwafanya vurugu mpaka hata kuharibu mazao ya Wananchi wanapoyakuta ndani ya Mita 60. Kamati inaishauri Serikali kuwaelimisha Watendaji wa ngazi ya Vijiji juu ya Sheria hii; na

Mheshimiwa Spika, Ili kupunguza wingi wa maji yanayoingia katika mito na muda mwagine kusababisha mafuriko, Kamati inaishauri Serikali kuwaelimisha jamii juu ya uvunaji wa maji ya mvua na kwa Taasisi za Serikali iwe ni lazima katika ujenzi kuweka miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua.

k) Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuhusu mchakato wa tathmini ya athari ya mazingira (EIA), majukumu ya NEMC katika kutekeleza kanuni ya Tathmini ya Athari ya Mazingira (EIA) pamoja na gharama za EIA.

Mheshimiwa Spika, Tathimini ya Athari ya Mazingira - TMA (Environmental Impact Assessment - EIA) ni tathimini inayofanywa kwa lengo la kuhakikisha maamuzi ya kutekeleza na utekelezaji wa mradi au shughuli fulani haina athari katika mazingira. EIA hufanyika kwa lengo la kuweka mifumo bora ya kulinda mazingira ikiwa ni pamoja na kupunguza kiwango cha taka zitakazozalishwa, kutoa kipaumbele kwa jamii kutokana na mradi unaoanzishwa, kuainisha athari zilizopo na madhara yanayoweza kujitiokeza

kutokana na mradi unaoenda kutekelezwa, kutoa maamuzi sahihi kuhusu utekelezaji wa mradi, kulinda afya ya jamii na kuhakikisha usalama wa wafanyakazi;

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Athari za Mazingira ni hatua muhimu sana inayotakiwa kufuatwa kabla ya mradi wowote kuanza utekelezaji wake lakini kumekuwa na malalamiko mengi ya wawekezaji kuwa EIA inawachelewesha kwa kuwa huchukua muda mrefu. Kamati inaishauri kuangalia na kutatua changamoto zinazoikwamisha NEMC kutekeleza jukumu hili kwa haraka ikiwepo kuwaongezea watumishi (wataalamu ukaguzi);

Mheshimiwa Spika, NEMC pekee haitaweza kufanya ufuutiliaji wa utekelezaji wa masharti ya cheti cha EIA katika miradi iliyofanyiwa EIA, kwa lengo la kupata ufanisi katika hilo, Kamati inaishauri NEMC kuwatumia Maafisa Wakaguzi wa Halmashauri kwa kuwapatia mafunzo stahiki ili waweze kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo yao na kutoa ripoti kwa miradi yenye changamoto ili NEMC iweze kufika na kuchukua hatua;

I) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira (OMR-M) kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2021)

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira imekabidhiwa majukumu ya kitaifa ya kuratibu mambo yote ya Muungano na Ushirikiano kati ya SMT na SMZ katika mambo yasiyo ya Muungano, pamoja na kusimamia hifadhi ya Mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya Bajeti ya nusu mwaka kwa wizara hii na kubaini kuwa hadi kufikia Disemba, 2021 Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) ilipokea jumla ya Shilingi **3,588,905,642.53** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia **59.9** ya bajeti iliyotengwa. Fedha za maendeleo zilizotolewa ni Shilingi **2,629,475,402.90** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia **88** ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

kati ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kiasi cha Shilingi **345,474,999.84** ni kwa ajili ya Mishahara ya Idara ya Mazingira; Shilingi 2,055,873,366.00 ni mishahara ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC); na Shilingi **1,187,557,276.69** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC) kwa Idara ya Mazingira. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa Fedha za miradi ya maendeleo kwa **asilimia 88. Ni Rai ya Kamati kwa Wizara kusimamamia miradi iliopangwa kutekelezwa kwa ufanisi.**

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio kuna changamoto ambazo wanakabiliiana nazo

a) Uelewa mdogo wadau na Wananchi kuhusu Sheria ya Mazingira Pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na Baraza katika kukuza uelewa wa masuala ya mazingira, bado kumekuwa na uelewa mdogo wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake kwa wawekezaji, wataalamu elekezi na jamii kwa ujumla.

b) Upungufu wa Watumishi

Idadi ndogo ya watumishi wenyewe taaluma ya mazingira na fani mahususi katika kusimamia baadhi ya miradi kwenye sekta husika. Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Baraza lina upungufu wa watumishi wapatao **137** ikilinganishwa na watumishi **203** walipo kwa sasa, ili kukamilisha idadi ya watumishi **340** wanaohitajika.

m) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu Usimamizi wa mazingira katika Sekta ya Mafuta na Gesi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata maelezo ya Wizara juu ya uanzishwaji wa Shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi nchini Tanzania ambazo zilianza toka mwaka 1952. Aidha, Ugunduzi wa kwanza wa gesi asilia nchini ulifanyika mwaka 1974 katika maeneo ya kisiwa cha Songo Songo mkoani Lindi chini ya kampuni ya **Azienda Generale Italiana Petroli (AGIP)** kwa kushirikiana na **American Oil Company (AMOCO)**

Mheshimiwa Spika, kiasi cha gesi asilia kilichogundulika nchini katika maeneo ya nchi kavu (onshore) na baharini (offshore) hadi kuflikia Februari 2020, ni futi za ujazo **Trillioni 57.54**.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya mafuta na gesi ni Nyenzo muhimu sana katika muendeleo wa jamii na uchumi wa Taifa kwa ujumla. Gesi asilia imeleta ufanisi katika uzalishaji viwandani kwa kuwa nishati ya uhakika kama inavyotumika katika kiwanda cha Twiga Cement, Dar es Salaam na Dangote, Mtwara. Gesi asilia ni nishati safi kulinganisha na nishati zingine kama vile makaa ya mawe, mafuta lakini ipo changamoto ya umwagaji wa mafuta machafu(*oil chafu*) hivyo ni Rai ya Kamati kwa Serikali kuweka mpango mkakati wa kimazingira kwa kufanya tathmini na kutoa ufanuzi kwa wananchi juu ya athari ya *oil chafu* na namna ya kuzihifadhi bila kuathiri mazingira.

n) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Tathmini ya Mazingira kimkakati (SEA);

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilijengewa uelewa kuhusu Mwongozo wa Taifa wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati (SEA) ambao una Madhumuni yafuatayo;

a) kutoa mwongozo juu ya hatua za kufuata unapofanya TMK. Miongozo hii inawezesha watumiaji kutekeleza sheria ya Mazingira na Kanuni zake kwenye TMK,

b) Miongozo itatumika kwenye Sera, Miswada, Kanuni, Mikakati, Mipango, Programu na miradi yote ambayo ni ndani ya mawanda ya Kanuni za EMA na TMK.

Mheshimiwa Spika, Kwa muhtasari, madhumuni ya TMK ni kuhakikisha kwamba masuala ya mazingira yanafafanuliwa na yanajitokeza katika kufanya maamuzi ya kimkakati katika kusaidia maendeleo ya kimazingira na kijamii na endelevu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira pia inakabiliana na Changamoto mbalimbali ambazo ni;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- a) Uelewa mdogo wa faida ya kufanya TMK kwa maendeleo endelevu
- b) Ukosefu wa fedha za kufanya TMK hasa kwa Wizara na Taasisi za Serikali
- c) Baadhi ya TMK zinafanya kwa matakwa ya wadau wa Maendeleo
- d) Kuto kamili kwa baadhi ya TMK zilizowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, ni Rai ya Kamati kwa Wizara hii kuweka mpango madhubuti wa kuelemisha wanachi juu ya Sera, Sheria na Kanuni za Mazingira. Aidha, kwa changamoto zilizoripotiwa zote zipatiwe ufumbuzi wake.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI YA JUMLA

1. Pamoja na kwamba baadhi ya majukumu mahsusini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni kuandaa, kuratibu na kupitia sera na mikakati ya sekta za Viwanda, Biashara na Masoko; Kamati ilibaini kuwa Sera zilizopo ni za muda mrefu na zimepitwa na wakati hivyo kuna haja ya Wizara kuharakisha mchakato wa mapitio ya Sera ili kuendana na kasi ya mazingira ya sasa.
2. Kwa kuwa Wizara hii ndiyo wizara inayoshughulika na viwanda ambavyo tunaamini vitatoa fursa kubwa ya ajira kwa Taifa letu, Na kwakuwa kwa kipindi cha nusu mwaka Kamati ilibaini ni **asilimia 33.3** tu ya bajeti ya maendeleo imepokelewa. **Kamati inashauri Serikali kupeleka Fedha kwa Wizara hii ili iweze kutekeleza miradi ya kimkakati kama ilivyopangwa.**
3. Kwakuwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linakabiliwa na changamoto ya ongezeko la njia zisizo rasmi za kuingiza bidhaa hapa nchini jambo linalopelekea kuongezeka kwa bidhaa hafifu sokoni; **Kamati inaishauri Serikali kuzisimamia**

kwa ukaribu Mamlaka zinazohusika na udhibiti ili kuhakikisha zinashirikiana katika kufanya ukaguzi, lakini pia Serikali iangalie namna ya kupunguza gharama zilizopo ili kuweza kuwavutia wafanyabiashara kuitisha bidhaa zao katika vituo halali;

4. Kamati haijawahi kuridhishwa na mwenendo wa suala la utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayosimamiwa na wizara ya uwekezaji, Viwanda na Biashara, kama vile Liganga na Mchuchuma ambao hadi sasa, Wizara imeiarifu Kamati kuwa iko katika hatua za majadiliano na mbia, **Hivyo basi ni Rai ya kamati kwa Serikali kuweka msukumo katika kutekeleza miradi muhimu ya kimkakati yenye maslahi kwa Taifa.**

5. Moja ya changamoto kubwa kwa wawekezaji na wananchi ni kuchukua muda mrefu kufanya usajili wa kampuni/biashara jambo ambalo llinapelekea watu wengi kukata tamaa na kupata usumbufu mkubwa;

Ni Rai ya Kamati kwa upande wa BRELA waweke muda maalum tangu mteja ameanza kuomba kufungua kampuni/ biashara hadi anakamilisha na vilevile kuweka maafisa wa kutosha wa kuwasaidia wawekezaji na wananchi katika kutoa elimu ya usajili wa biashara/kampuni zao. Aidha, Serikali inapaswa kurekebisha mifumo ya kidigitali ya BRELA na kuhuisha taarifa zinazowekwa kwenye mtandao huo mara kwa mara ili kuboresha na kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa huduma kwa wateja.

6. Ili Kulinda uwekezaji wa viwanda vya ndani, Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio na maboresho (kupunguza) kodi na tozo mbalimbali zinazohusiana na uzalishaji wa Viwandani ili kuviiwezesha viwanda kushindana katika soko tukizingatia tumeingia katika Soko la Afrika – AfCFTA;

7. Pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na Baraza la Mazingira (NEMC) katika kukuza uelewa wa masuala ya mazingira bado kumekuwa na uelewa mdogo wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake kwa wawekezaji na wananchi kwa ujumla hivyo ni **Rai ya Kamati kwa Serikali**

kupitia NEMC kuongeza kasi ya kuelimisha wananchi na wadau mbalimbali juu ya athari na umuhimu wa uhifadhi wa Mazingira.

8. Kwakuwa kumekuwa na malalamiko mengi kwa wadau wa sekta ya mazingira juu ya upatikanaji wa cheti cha tathmini ya Athari za Mazingira -TAM (Environment Impact Assessment (EIA)) hali ambayo inapelekea wawekezaji wengi kukwama kutekeleza miradi yao kwa wakati, **Kamati inaishauri Serikali kushughulia changamoto zinazoikwamisha NEMC kutekeleza jukumu hili kwa haraka kwa kuwaongezea Fedha na watumishi(wataalamu) wa ukaguzi wa Mazingira;**

9. Kwakuwa kumekuwa na changamoto ya kutokuwa na bei elekezi ya upatinakanaji wa cheti na kibali cha EIA; Kamati inaishauri Serikali kupitia NEMC iwe inatoa elimu ya ziada kwa wawekezaji juu ya bei elekezi ya gharama ya Tathmini ya Athari ya Mazingira kuendana na mradi unaokusudiwa ambapo wafafanue kwa uwazi kabisa aina fulani ya mradi, gharama zinakadirwa kuanzia kiasi fulani hadi fulani kwa lengo la kusaidia Wananchi kutotozwa gharama zaidi na baadhi ya Washauri elekezi wasio waadilifu;

3.1 Mapendekezo ya Kamati

3.2 Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia ukubwa wa hoja, athari za matokeo yatakayotokana na hoja husika, kujirudia kwa hoja na hatua zinazostahili kuchukuliwa kushughulikia hoja husika.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kushuhudia juhudi mbalimbali za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazolenga kuboresha mazingira ya Kufanya biashara nchini ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na nchi mbalimbali zinazotaka kufanya biashara na Tanzania. Kamati inapongeza na kuunga mkono juhudi mbalimbali za Serikali ambazo zimeleenga kuimarisha Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji na hatimaye kuweka mazingira mazuri ya kufanya Biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni mapendekezo ya Kamati;

3.2.1 Utekelezaji wa miradi ya kimkakati kwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

KWA KUWA, kuna changamoto ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ilio chini ya Wizara hii kuititia taasisi zake ama kwa kutoanza au kutokamiliika kwa miradi;

NA KWA KUWA, Mkwamo huo wa utekelezaji wa miradi, unaleta hasara kwa Serikali na kuchelewesha maendeleo ya nchi katika ukusanyaji kodi, ajira na uchagizaji wa uchumi wa jamii zinazozunguka miradi hiyo.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

Kwa miradi yote ya kimkakati inayotekelzeza na Shirika la NDC, ipewe msukumo katika utekelezaji wake. Mfano; Mradi wa Liganga na Mchuchuma majadiliano yanayoendelea baina ya Serikali na mbia (kampuni ya Sichuan Ltd) yamechukua muda mrefu kumalizika hivyo Serikali inapaswa kumaliza majadiliano hayo ili mradi sasa uanze kutekelezwa na wananchi waweze kunufaika na uwepo wa rasilimali hizi katika maeneo yao. Aidha, kwa maeneo ambayo wananchi ardhi zao zilitwaliwa kupisha utekelezaji wa miradi, Serikali inapaswa kuwalipa fidia bila kusubiri miradi husika kuanza.

3.2.2 Utekelezaji wa Mradi wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo kwasasa havifanyi kazi

KWA KUWA, Kamati imefafanua kuhusu dosari za ubinafsishaji na uendelezaji wa viwanda vilivyobinafsishwa nchini;

NA KWA KUWA, Dosari hizo zimesababisha kutokuendelezwa kwa viwanda na hata kutokuwepo na tija kwa vile vichache vinavyofanya kazi

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

(c) Serikali kuweka malengo ya kutafuta wawekezaji wenye nia ya dhati na uwezo katika kuendeleza viwanda hivyo.

(d) Kwa viwanda vitakavyobinafishwa tena Serikali ifanye tathmini ya kina yenye kuwa na tija kwa Taifa. Aidha, viwanda vitavyobinafishwa kwa njia ya ubia Serikali iingie mikataba yenye tija na yenye kuipa nguvu ya maamuzi katika ubia huo.

3.2.3 Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo ya nje ya Nchi (EPZA);

KWAKUWA, EPZA inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu yake ya kisheria ya kumiilki ardhi na kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda;

NA KWAKUWA, EPZA inatwaa maeneo mengi karibu nchi nzima na rasilimali za kuyaendeleza maeneo hayo ni chache;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba; Serikali kupitia Mamlaka ya EPZ kuhamasisha Sekta binafsi kushiriki kuwekeza katika kuyaendeleza maeneo ya EPZA kwa kuyajengea miundombinu wezeshi na kuyaweka tayari kwa ajili ya Uwekezaji;

3.2.4 Utendaji na ufanisi wa kiwanda cha viuwadudu cha Tanzania Biotec Products Limited (TBPL);

KWA KUWA, Serikali kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imejenga kiwanda cha kuzalisha viuadudu vyta kuua viluwiluvi wa mbu wanaoeneza ugonjwa wa malaria.

NA KWAKUWA, lengo la kuanzishwa kwa kiwanda hiki ilikua ni kutokomeza malaria nchini na kiwanda hiki kimejengwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100, hatahivyo, hadi sasa kiwanda hiki kimesimamisha uzalishaji wa viuwadudu kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo uchakavu wa mitambo, ukosefu wa wateja, ukosefu wa fedha n.k

KWAHIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali iwe na utayari wa kutoa msukumo kwa wizara ya Afya na Tamisemi ambao ndiyo wateja wakubwa wa bidhaa zinazozalishwa (viuwadudu) kuweza kununua bidhaa hizi;

- b) Serikali kuchukua hatua za kufanya matengenezo katika mitambo ya uzalishaji kama inavyohitajika Kitaalamu ili sasa uzalishaji uweze kuendelea;
- c) Serikali kufanya mapitio ya mikataba iliyosainiwa baina ya Serikali ya Tanzania na Labiofam.

3.2.5 Utendaji wa *One Stop Center*,

KWA KUWA, Wawekezaji nchini wamekua wakipata changamoto ya kufanya usajili, kupata majibu na kupata huduma katika eneo moja;

NA KWAKUWA, Changamoto hiyo imepelekea wawekezaji kupata usumbufu usio wa lazima na kuzunguka ofisi mbalimbali za Serikali bila kupata ufumbuzi wa masuala yao kwa wakati;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

(d) Serikali iweke wataalamu wenye uwezo wa kufanya maamuzi katika vituo hivi ili wawekezaji wanapofika nchini waweze kupata huduma zote kwa wakati mmoja.

(e) Serikali ikamilishe mifumo ya huduma kwa njia ya mtandao ambayo imekwishaianza. Yani mfumo wa utoaji huduma unounganisha taasisi za TRA BRELA, Idara ya Uhamiaji, NIDA n.k., vilevile mfumo wa uondoshaji wa kontena bandarini, mifumo ambayo kwasasa imefikia 50% ya utengenezwaji.

(f) TIC katika tovuti yake iweke mahitaji yote yanayohitajika kufuatwa na nyaraka zinazohitajika ili muwekezaji afahamu kabisa nini anapaswa kuwa nacho na ni wapi ataanza na kumalizia.

3.3 Usimamizi wa Mazingira

Mheshimiwa Spika, Mazingira ni suala mtambuka, ili kuleta maendeleo endelevu suala la uhifadhi wa mazingira halina budi kupewa kipaumbele kwani kwa kiasi kikubwa ufanisi wa

miradi yetu ya maendeleo inategemea uimara wa mazingira. Kuna haja ya Serikali yetu kuongeza umakini na kuongeza juhudhi katika kusimamia masuala ya uhifazi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika kuhakikisha inaisaidia Serikali katika masuala ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira inashauri mambo yafuatayo:-

3.3.1 Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

KWAKUWA, moja ya changamoto katika kuhifadhi Mazingira ni pamoja na Mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ongezeko la joto, mafuriko ya mara kwa mara na ukame; Usimamizi wa taka zitokanazo na vifaa vya umeme; Viumbe vamizi; Usimamizi wa kemikali na Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi;

NA KWAKUWA, Halmashauri zetu zina Maafisa mazingira lakini weledi na mchango wa maafisa hawa katika kusimamia masuala ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira hauridhishi.

KWAHIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba; Serikali kuwahamishia kiutawala maafisa mazingira katika Wizara yenye dhamana ya Mazingira ili waweze kutoa mrejesho wa utekelezaji wa majukumu yao moja kwa moja kwa wizara hiyo. Aidha, Serikali inapotaka kuajiri maafisa wa kushughulikia mazingira waangalie wenye taaluma ya mazingira.

3.3.2 Uendeshaji wa Shughuli za Mfuko wa Mazingira;

KWAKUWA, mfuko wa uendeshaji wa shughuli za Mazingira ulianzishwa kwa sheria ya mazingira (EMA 2004) kwa lengo la kuwezesha shughuli za usimamizi wa mazingira nchini kufanyika kwa ufanisi.

NA KWAKUWA, changamoto ya Mfuko huu ni uhaba wa fedha jambo linalopelekea kushindwa kuendelea na utekelezaji wa Majukumu yake;

KWAHIYO BASI Bunge linaazimia kwamba; Serikali itafute vyanzo vya mapato ili kuwezesha mfuko huu kutimiza majukumu yake.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe Mhe. Tulia Ackson (Spika) kwa ushirikiano unaoutoa kwa Kamati yetu wakati wote. Aidha, nikupongeze kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa Bunge letu tukufu, tunakuombea afya njema na utumishi uliotukuka katika kutekeleza majukumu yako.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu. Vilevile shukrani ziende kwa Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kujadili na kuchambua Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa katika Kamati na hatimaye kuwasilisha maoni na mapendekezo kuhusu Shughuli zilizotekelzwa na Kamati kwa kipindi cha mwaka 2021/2022. Aidha, Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard).

- i) Mhe. David Mwakiposa Kihenzile, Mb - **Mwenyekiti**
- ii) Mhe. Eric James Shigongo, Mb - **M/Mwenyekiti**
- iii) Mhe. Usonge Hamad Juma, Mb
- iv) Mhe. Martha Nehemia Gwau, Mb
- v) Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
- vi) Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
- vii) Mhe. Lucy John Sabu, Mb

- viii) Mhe. Hawa Chakoma Mchafu, Mb
- ix) Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb
- x) Mhe. Hajji Makame Mlenge, Mb
- xi) Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb
- xii) Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mb
- xiii) Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb
- xiv) Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb
- xv) Mhe. Maryam Omar Said, Mb
- xvi) Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb
- xvii) Mhe. Zulfa Mmaka Omary, Mb
- xviii) Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb
- xix) Mhe. Nancy Hassan Nyarusi, Mb
- xx) Mhe. Salim Hassan Turky Toufiq, Mb
- xxi) Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb
- xxii) Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
- xxiii) Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb
- xxiv) Mhe. Dkt. James Kimea Alfred, Mb
- xxv) Mhe. Daudi Silanga Njalu, Mb
- xxvi) Mhe. Irene Alex Ndyamkama, Mb

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Kamati naomba pia nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Dkt Ashatu K. Kijaji, Mb, Mhe. Dkt. Suleiman Said Jafo, Mb Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Exoud Silaoneka Kigahe, Mb, na Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira Mhe. Khamis H. Khamis Mb, pamoja na Makatibu Wakuu na watendaji wa Wizara zote pamoja na Taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hizo kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kwa kipindi chote hiki.

Vile vile, naomba nimshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Mwihambi(ndc), kwa ushirikiano ambao amekuwa akitoa kwa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athumanı Hussein, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha na uchumi, Ndg. Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati, Ndg. Felister Mgonja, Ndg. Nyamwanja Chipanda pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Modesta Kipiko kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

4.1 Hoja

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

David Mwakiposa Kihenzile (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIR

11 FEBRUARI, 2022

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati. Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge; tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, utangulizi; kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022.

Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kujitoa kwao na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake kwa wakati.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, taarifa ninayowasilisha imegawanyika katika sehemu kuu nne zifuatazo: -

- (a) Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelzwa;
- (b) Sehemu ya pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;
- (c) Sehemu ya tatu inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na,
- (d) Sehemu ya nne ni hitimisho la taarifa.

Mheshimiwa Spika, muundo na majukumu ya Kamati; majukumu ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji yameainishwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Nyongeza ya Nane. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilitumia njia mbalimbali kama zilivyoainishwa kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

Moja; kutembelea na kukagua utekekelezaji wa miradi ya maendeleo; kushughulighia Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula; kupokea na kujadili taarifa 25 za utekelezaji za Wizara ambapo taarifa kumi ziliwasilishwa na Wizara ya Kilimo na taasisi zilizo chini ya Wizara; taarifa tisa kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na taasisi zilizo chini yake na taarifa sita kutoka Wizara ya Maji kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake Kamati pia ilipokea na kujadili Taarifa sita kutoka Wizara mbalimbali na sekta binafsi ambazo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

shughuli zake zinachangia mnyororo wa thamani kwa mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvubi nazo ni:-

(a) Wizara ya Fedha na Mipango; kuhusu Taarifa ya Utendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo yaani *TADB*.

(b) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; kuhusu mpango mkakati wa kuimarishe uchukuzi na usafirishaji wa mazao ya bustani kwa lengo la kufikia masoko ya kimataifa.

(c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine yaani *SUA*; kiliwasilisha taarifa kuhusu changamoto za sekta za kilimo, mifugo na uvubi na mapendekezo ya utatuzi wa changamoto hizo kwa ajili kuongeza tija katika mnyororo mzima wa uzalishaji.

(d) Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi; kiliwasilisha Taarifa kuhusu hatua za kuchukua ili kuujenga upya ushirika kwa lengo la kuongeza tija kwenye kilimo kwa kuwawezesha wana ushirika kushiriki kikamilifu kwenye mnyororo mzima wa thamani.

(e) Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania; iliwasilisha Taarifa kuhusu mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kuboresha upatikanaji wa uhaba wa masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvubi.

Mheshimiwa Spika, ziara ya kutembelea mashamba ya bustani mkoani Arusha na Moshi; kutokana na kukua na fursa iliyopo kwenye biashara ya bustani mwezi Agosti, 2021 Kamati ilifanya ziara ya kikazi Mkoani Arusha na Kilimanjaro kwa ajili kujielimisha kuhusu shughuli za kilimo cha bustani nchini. Pamoja na kutathmini utekelezaji wa Sera ya *PP* na kukagua utekelezaji wa programu ya kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya pili ambayo inatekelezwa na sekta kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo Kamati ilibaini kuwa Tanzania ni moja kati ya nchi 20 duniani zinazozalisha kwa wingi mazao ya bustani na hivyo kupelekea tasnia ya

mazao ya bustani kukua kwa kasi ambapo inakadiriwa kukua kwa asilimia saba kwa mwaka. Inatoa ajira za moja kwa moja kwa takribani milioni 6.5 na kuchangia fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo Kamati ilibaini hapa nchini Tanzania tasnia ya bustani haijafanya vizuri licha ya fursa iliyopo kutokana na ya changamoto zifuatazo: -

- (i) Gharama kubwa za uzalishaji zinazowakabili wawekezaji;
- (ii) Matumizi duni ya teknolojia za kisasa zinazofaa kwa kilimo;
- (iii) Gharama kubwa za usafirishaji;
- (iv) Tozo na kodi nyingi za Serikali;
- (v) Ukosefu wa ndege za kusafirishia mizigo;
- (vi) Uchache wa gati za kupakia na kupakua mizigo katika bandari zetu;
- (vii) Uelewa mdogo wa wataalamu kutoka mamlaka mbalimbali za Serikali kuhusu umuhimu wa kuhudumia bidhaa zinazoharibika haraka yaani *perishable goods*;
- (viii) Kushindwa kutumia kikamilifu fursa ya masoko ya kimataifa na hivyo kupelekea wafanyabiashara kutoka nchi za nje kununua mazao ya bustani kutoka kwenye mashamba ya wakulima, kisha kuyaweka kwenye vifungashio vinavyoonesha bidhaa hizo zimezalishwa kwenye nchi zao;
- (ix) Kukosekana kwa teknolojia za kisasa kama miundombinu ya umwagiliaji, huduma za maabara za kisasa, na kupima udongo; na
- (x) Kukosekana kwa wataalamu wa kutosha wa huduma za ugani.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kufanya kazi changamoto zilizopo. Pia Kamati inaipongeza *TAHA* kwa jitihada zao katika tasnia ya kilimo cha bustani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Taarifa za utekelezaji kwa bajeti hizi za sekta inazosimamia. Uchambuzi uliofanywa na Kamati ulibaini kuwa kwa ujumla utolewaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo hususan sekta za uzalishajji ambazo ni kilimo, mifugo na uvuvi si wa kuridhisha na hauna tija kwa sekta hizi. Hii inathibitishwa na takwimu zilizotolewa na wizara husika kuhusu kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi mwezi Disemba kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Kilimo - Fungu 43 ilikuwa imepokea fedha za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 42.7 na fedha za maendeleo za nje ni asilimia 4.2;

(ii) Tume ya Umwagiliaji – Fungu 05 ilikuwa imepokea fedha za maendeleo za ndani ambazo ni sawa na asilimia moja na hakuna fedha yoyote ya maendeleo kutoka nje iliypokelewa;

(iii) Tume ya Ushirika – Fungu 24 haikutengewa fedha yoyote ya kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na ukomo wa bajeti;

(iv) Sekta ya Mifugo – Fungu 99 ilikuwa imepokea fedha za maendeleo za ndani yenye asilimia 5.1 na hakuna fedha za nje zilizotolewa; na

(v) Sekta ya Uvuvi – Fungu 64 ilikuwa imepokea fedha za maendeleo za ndani ambazo ni asilimia 12.6 na hakuna fedha ya maendeleo kutoka nje iliyyotengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya maji, Kamati imeridhishwa na upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo, kwani hadi mwezi Disemba Wizara ya Maji ilikuwa imepokea asilimia 50 ya fedha ya kutekeleza miradi

ya maendeleo kutoka Mfuko wa Maji; na asilimia 56 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa sekta zinazotoa huduma kwa jamii kama maji hazitegemei bajeti inayotengwa na Serikali ambayo ina ukomo badala yake Serikali imetafuta vyanzo mahsusи въя fedha na kuziwekeea uzio fedha zinazopatikana kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati sehemu ya pili; matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye shughuli zilizotekelizwa na Kamati yameelelwа kwa kina kwenye Taarifa ya Kamati, hata hivyo napenda kuainisha mambo mahsusи yaliyobainishwa ambayo ni pamoja na:-

- (i) Bajeti ndogo zinazotengwa na kutolewa;
- (ii) Ukosefu wa viwanda въя kuzalisha mbolea hali ilipelekeea Serikali kutumia fedha nyingi kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi;
- (iii) Kilimo cha kutegemеа mvua ambacho kimekuwa siyo cha uhakika kutokana na mabadiliko ya tabianchi na hivyo kupungua kwa uzalishaji na tija hivyo kuwakatisha tamaa wakulima;
- (iv) Ukosefu wa watumishi sahihi na ya zana bora za kilimo, ambapo takribani asilimia 54 ya wakulima nchini wanaendelea kutumia jembe la mkono kama njia kuu ya uzalishaji badala ya kutumia zana bora za kilimo;
- (v) Changamoto zinazoikabili tasnia ya ushirika nchini. Tasnia ya ushirika inakabiliwa na changamoto kadhaa, nyingi zikiwa zinatokana na mapungufu katika utekelezaji na baadhi zikiwa na zinatokana na mapungufu katika sera na sheria za ushirika. Baadhi ya changamoto hizo zimefafanuliwa kwenye Taarifa ya Kamati;
- (vi) Uwepo wa wingi wa athari za magonjwa ya mifugo na hivyo kupelekeea madhara yafuatayo; kuathirika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa biashara ya nyama kimataifa na hivyo kulikosesha Taifa fedha za kigeni; kuligharimu Taifa fedha nyingi kununua dawa kwa ajili ya matibabu ya wanyama, magonjwa ya mifugo kuchangia magonjwa ya binadamu kwa takriban asilimia 60 na namba nyingine zimeorodheshwa kwenye taarifa ya Kamati.

(vii) Uwezo mdogo wa nchi yetu kuzalisha, na kusambaza mbegu bora za mazao, mifugo na vifaranga vyatamaki kwa wakulima, wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa licha ya uwepo wa Kampuni kubwa ya kuzalisha ng'ombe wa nyama kwa sababu ya kukosa fedha za kufanya uwekezaji imepelekea *NARCO* kushindwa kuzalisha na kusambaza mbegu bora za mifugo wa nyama kwa wafugaji na kupelekea wafugaji wenye uwezo wa kifedha kutafuta mbegu bora kutoka nchi Jirani kwa mfano Kenya, Zambia na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali imejielekeza kuongeza uwekezaji na uzalishaji mkubwa wa viumbi maji yaani ufugaji wa samaki kwa kutumia fursa iliyopo katika rasilimali za maji zilizopo katika bahari, maziwa, mabwawa, mito na mabonde oevu. Hata hivyo Kamati imebaini uzalishaji wa vifaranga bora bado uko chini kutokana na changamoto kadhaa ikiwa pamoja uhaba wa zana na pembejeo, huduma hafifu za ugani na uwekezaji mdogo unaotokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mbegu bora za mazao ya kilimo, ukosefu wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati umeathiri utendaji kazi wa Wakala wa Mbegu za Kilimo ambao wakati mwingine wanashindwa kuzalisha mbegu kwa wakati ili kuendana na kalenda na misimu ya mazao

Mheshimiwa Spika, upungufu wa vyakula, malisho na rasilimali maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo; tathmini

iliyofanywa na Serikali imeonesha kwa kipindi cha kuanzia mwezi Septemba, 2021 hadi Januari 2022 kukosekana kwa malisho ya mifugo kuliko sababishwa na ukame kumepelekeea madhara kenyet tsnia ya mifugo kama vifo vya mifugo, kupungua kwa thamani ya mifugo kutokana na kudhoofika, kuongezeka kwa magonjwa, kukauka kwa vyanzo vya maji, migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhikutokana na wafugaji kuhangaika kutafuta maji na malisho, biashara ya mifugo hai kwenye minada mbalimbali imepungua kutokana na wafugaji wengi kuhama maeneo yao ya asili kwenda kutafuta malisho ya maji sehemu za mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya kuchinja mifugo na kuchakata nyama vimeathirika kwa kupungua kwa mifugo inayopelekwa viwandani. Bei ya nyama kwenye mabucha zimepanda kutoka wastani wa shilingi 6,000 hadi shilingi 7,500 kwa kilo ya nyama ya mchanganyiko na kutoka shilingi 8,000 hadi shilingi 12,000 kwa kilo ya nyama ya steki kutokana na kupungua kwa ng'ombe wanaouzwa minadani kwa ajili ya kuchinjwa hivyo tunafikiria watu watapata utapiamlo kwa kukosekana kwa protini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viwanda vya kusindika maziwa kushindwa kuzalishwa kulingana na mahitaji na hivyo Taifa kulazimika kutumia fedha za kigeni kuagiza maziwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuperomoka kwa ufanisi na usimamizi wa tsnia ya ugani ni changamoto kubwa kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kukosekana kwa mfumo unaosababishwa na wizara za kisekta ndio chanzo cha kuperomoka kwa ufanisi wa tsnia ya ugani.

Mheshimiwa Spika, changamoto katika shughuli za utafiti; tafiti katika kilimo, ufugaji na uvuvi hufanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo yaani *TARI*, taasisi pia kwa mifugo yaani *TALRI*, Taasisi pia kwa Samaki yaani *TAFIR*/kwa kushirikiana na vyuo vikuu mbalimbali.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, changamoto inayozikabili taasisi za utafiti ni bajeti ndogo inayotengwa na Serikali kutotosheleza mahitaji na hivyo taasisi za utafiti kulazimika kutegemea fedha za utafiti kutoka kwa wadau wa maendeleo, hatua hii imepelekea baadhi ya tafiti kufanyika nje ya matakwa ya nchi yetu na kufuata matakwa ya wafadhili na hivyo kutotatua matatizo halisi yanayoikabili sekta ya kilimo, ufugaji.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maji nchini na changamoto zinazoikabili maji; katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati imebaini kasi ya uharibifu wa vyanzo vya maji kutokana na ongezeko la idadi ya watu pamoja na mabadiliko ya tabia nchi inayoashiria kupungua kwa kiasi cha maji kwenye vyanzo vya maji vilivyopo. Licha ya changamoto zilizopo uchambuzi wa Kamati umebaidi kuwa huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama imeendelea kuimarika nchini kwani idadi ya wananchi wanaopata maji safi na salama imeongezeka na kufikia asilimia 70 kwa upande wa vijiji na asilimia 84 kwa upande wa mijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Kamati ilibaini baadhi ya changamoto zinazoikabili Wizara ya Maji kwenye utaratibu na usimamizi wa sekta ya maji kama zilivyoainishwa kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia Wizara ya Maji shilingi bilioni 90.2 ambazo ni fedha za mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19 ambazo zinalenga kuchochaea ukuaji wa sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, semina na mafunzo; katika Kipindi cha Januari 2021 hadi Januari 2022, Kamati ilipatiwa semina na mafunzo mbalimbali kwa ajili ya kuwapatia maarifa kama

inavyoelezwa kwenye vitabu vyetu vy a kwenye vishkwambi vyenu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu, mapendekezo ya Kamati; kuimarisha mfumo wa usimamizi wa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi; kwa kuwa kukosekana kwa Naibu Katibu Mkuu - TAMISEMI anayesimamia sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi katika ngazi za Serikali za Mitaa kumepelekea kukosekana kwa mfumo bora wa usimamizi na kusababisha sekta hizi kutofanya vizuri kama inavyotarajiwa. Hivyo basi, Bunge inashauri Serikali irudishe nafasi ya Naibu Katibu Mkuu - TAMISEMI atakayeratibu masuala yote ya sekta za uzalishaji za kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kutengeneza ajira kwa vijana kupitia sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuongeza uwekezaji kwenye sekta hizi; kwa kuwa llani ya Chama cha Mapinduzi imedhamiria kutengeneza ajira zisizopungua milioni nane ifikapo mwaka 2025 kwa kuielekeza Serikali kuchochaea ukuaji wa uchumi hususani katika sekta ya viwanda vinavyotumia malighafi za kilimo, mifugo, na uvuvi; na kwa kuzingatia ukweli kwamba sekta hizi ndio sekta zinazoajiri Watanzania walio wengi, Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kutambua hilo zimeandaa mipango mikakati yenye lengo la kuleta mageuzi kwenye sekta husika kwa kuongeza tija na kutengeneza ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mipango mikakati iliyopo inahitaji uwekezaji mkubwa amba ni vigumu kutekeleza mipango hiyo kupitia bajeti ya Serikali ambayo inatengwa kidogo na mara nyingi ina ukomo wa bajeti. Hivyo basi, Bunge linashauri kwamba:-

(a) Serikali ione umuhimu wa kuongeza utengaji wa upatikanaji wa fedha za bajeti kwa ajili ya kuwezesha sekta hizi za uzalishaji kutekeleza mipango mikakati iliyojiwekeea.

(b) Serikali kwa kutumia njia za kidiplomasia iwahimize wadau wa maendeleo na sekta binafsi kusaidia kugharamia miradi ya maendeleo kupitia bajeti nje ya mfumo wa Serikali.

(c) Serikali itafute vyanzo mahsus kwa ajili ya kuziwezesha sekta hizi za uzalishaji, pesa itakapopatikana iwekewe uzio. Aidha, ione umuhimu wa kutoa dhamana kwa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili ziweze kukopa mikopo yenye riba nafuu kwani tathmini ya Kamati imeonyesha kila shilingi moja inayowekezwa kwenye sekta hizi inaweza kupata faida kati ya shilingi mbili hadi mbili na nusu.

Mheshimiwa Spika, kuongeza uzalishaji wenyе tija kwa kutumia teknolojia na ubunifu wa kisasa pamoja na matumizi ya mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakulima wengi nchini ni wakulima wadogo ambao wameendelea kutegemea zana duni za kilimo, mbegu zisizo na ubora, uhaba wa maafisa ugani na ukosefu wa taarifa sahihi kuhusu afya ya udongo pamoja na kilimo cha kutegemea mvua kumepelekea uzalishaji mdogo usio na tija.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Bunge linashauri kwamba Serikali iiwezeshe kifedha Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji kwani kwa sasa mfuko huu unategemea tozo zinazotokana na *scheme* za umwagiliaji. Serikali iiwezeshe ASA kibajeti ili iweze kuendelea kuendeleza shughuli za uzalishaji wa mbegu bora na kutoa elimu, kwa wakulima kuhusu umuhimu wa kutumia teknolojia na mbinu za kisasa katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imebainika kuwa kwa muda mrefu sasa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi zimeendelea kuwa na changmoto nyingi ambazo kwa kiasi kikubwa zimeendelea kusababisha ufinyu wa tija hasa kwa wakulima wadogo ikiwa ni pamoja na ufinyu wa huduma za ugani, huduma za bima, upatikanaji wa pembejeo na mbinu duni za uzalishaji, sambamba na changamoto za miundombinu duni za uzalishaji, usafirishaji, uchakataji na masoko. Pamoja na mambo mengine changamoto hizi zinazifanya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi zionekane hatarishi na hivyo, kutopewa kipaumbele na wawekezaji

ikiwa ni pamoja na kukosa huduma muhimu za fedha na mitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ni Taasisi ya Maendeleo na kwa mujibu wa miongozo ya Benki Kuu, *TIB* hairuhusiwi kupokea amana za muda mfupi ambazo ni chache; na zinazopatikana zinakuwa ni gharama kubwa ambazo wakulima wadogo hawawezi kumudu gharama hizo; na ili *TADB* iweze kutimiza malengo ya uanzishwaji wake Benki inategemea, mikopo ya masharti nafuu ili kuweza kuijendeleza.

Hivyo basi, Bunge linashauri kwamba Serikali iongeze mitaji *TADB* ili kukuza uwezo wa benki wa kuzihudumia sekta za kilimo, mifugo na uvuvi na kuwa na mchango madhubuti katika ukuaji wa sekta hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali isaidie upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kutoka taasisi mbalimbali zinazotoa mikopo yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kuimarisha zana ya ushirika nchini; kwa kuwa imebainika kuwa pamoja na mambo mengine sera ya ushirika ya mwaka 2002 na Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013 na Sheria ya Shirika la Ukagazi, Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) ya mwaka 2005 imekuwa kikwazo kwa ushirika kufanya vizuri.

Hivyo basi, Bunge linashauri kwamba Serikali ilete Bungeni mchakato wa marekebisho ya Sera ya Ushirika ya mwaka 2002, Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013 na Sheria ya Shirika la Ukagazi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka uzalishaji na usafirishaji wa mauzo ya mazao ya bustani; Serikali iangalie matatizo yaliyopo na iweze kuyatatua. Kuimarisha upatikanaji wa malisho na rasilimali ya maji na afya ya mifugo. Pia Serikali iangalie kuongeza fedha kwenye tasnia hii ya mifugo kusudi iweze kuimarika.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kuhusu kuimarisha tasnia ya ukuzaji viumbe maji pia Serikali iangalie jinsi ya kuongeza fedha, jinsi ya kuongeza tasnia ya ukuzaji viumbe kwa sababu watu wengi sasa hivi wanakula samaki na samaki, ni protini ambayo inasagika kwa urahisi kwenye mwili wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, kuendeleza kuimarisha huduma ya maji na usafi wa mazingira kuangaliwe kutoharibika kwa vyanzo vya maji. Kwa hiyo, Serikali iweze kuangalia kutoharibika kwenye vyanzo vya maji na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, usimamizi endelevu wa miradi mbalimbali nchini, ukuzaji vipaji na ubunifu wa mafundi mchundo; imeonekana kuwa vyuo vingi sasa hivi vinajibadilisha vinakuwa vyuo vikuu ukichukua vyuo ambavyo vilikuwa ni vya *Technical College* kwa mfano kama Vyuo vya *Tanga Technical* na vyuo vingine; Kamati inashauri kuwa viendelee kutoa elimu iliyokuwa inatoa badala ya kubadilika kuwa vya kutoa mambo ya vyuo vikuu.

Hivyo basi, Bunge linashauri kwamba Baraza la Taifa Elimu ya Ufundi Tanzania (*NACTE*) kutathmini maboresho yaliyofanyika, ili kuona umuhimu wa kurudisha malengo yaliyoanzishwa vyuo vya ufundi kama *Mbeya Technical, Dar es Salaam Technical, Arusha Technical* na Chuo cha Maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa mipango ya pamoja ya muda mrefu ya Serikali; hivyo basi, Bunge linashauri kwamba Serikali ione umuhimu wa kurudisha Tume ya Taifa ya Mipango na kufanya kuwa taasisi inayojitegea chini ya Ofisi ya Rais na kuiwezesha kifedha pamoja na kuipatia wataalam wa kutosha ili iweze kuendelea na kazi yake ya kupanga mipango ilivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; naomba kuchukua nafasi hii kwanza kabisa kuwapongeza Mawaziri wote ambao wapo kwenye taasisi hii ya mifugo pamoja, bila ya kumsahau na Profesa Adolf Mkenda ambaye alikuwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe ambaye ni Waziri wa Kilimo, Waziri

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jumaa Aweso pamoja na Naibu Mawaziri wote ambao wako kwenye tasnia hii ya Kilimo, Mifugo na Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu wote kwenye tasnia hii ya mifugo, kilimo na maji. Pia naomba nitumie nafasi hii kutambua mchango wa wadau wote ambao tulikuwa nao, Chuo Kikuu cha Kilimo - *SUA*, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Benki ya Maendeleo ya Kilimo, *Agriculture Council Tanzania*, Mamlaka ya Kiwanja cha Ndege, *Tanzania Private Sector*, *Tanzania Horticultural Association*, *Research, Community and Organizational Development Associates*, *Tanzania Private Sector Foundation*, *Agricultural Sector Policy and Institutional Reforms Strengthens Agricultural Non-State Actors*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwashukuru wajumbe wa kamati, ambao wamefanya kazi nzuri na majina yao naomba yaonekane kwenye *Hansard* kama yalivyo.

Mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kukushukuru wewe mwenyewe na kumshukuru Mheshimiwa Zungu, ambaye naamini atakuwa Naibu Spika ingawaje kura hazijahesabika, Sekretarieti yote ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ya Bunge Ndugu Athumanii Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi Ndugu Mswige Bisile na Ndugu Gerald Magili, Makatibu wa Kamati Ndugu Rachel Nyega na Ndugu Eunice Shirima na Msaidizi wa Kamati Ndugu Mohamed Kizingiti kwa umakini na ueledi wao katika kufanikisha kazi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja; baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekeliza na kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu shughuli ilizotekeliza kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Januari 2022 pamoja

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KWA KIPINDI CHA JANUARI 2021 HADI JANUARI 2022 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli zilizotekelizwa na Kamati, kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Januari 2022. Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kujitoa kwao na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake kwa wakati na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta ikiwemo Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji zina wajibu wa kuwasilisha Taarifa za Mwaka za shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelizwa na Kamati kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Januari 2022 na imegawanyika katika Sehemu Kuu Nne zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa Maelezo ya Jumla kuhusu Majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelizwa;

b) Sehemu ya Pili inahusu Uchambuzi na Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati;

c) **Sehemu ya Tatu** inabainisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati; na,

d) **Sehemu ya Nne** ni Hitimisho la Taarifa.

1.2 Muundo na Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(b) ikisomwa pamoja na kifungu cha 5 (7) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta, ambayo, imepewa jukumu la kusimamia Wizara Tatu ambazo ni: -

- a) Wizara ya Maji;
- b) Wizara ya Kilimo; na
- c) Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, majukumu ya Kamati hii ni: -

- i) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
- ii) Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekewa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na
- iv) Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu unaofanywa na Wizara hizo.

1.3 Njia na mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 96 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati za Kudumu za Bunge ni Mawakala wa Bunge na hivyo

hutekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge. Kamati za Kudumu za Bunge huliwakilisha Bunge katika kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zenyewe kukidhi matakwa ya Katiba na huku ikiongozwa na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Njia hizo ni: -

- i) Vikao vya Uchambuzi wa Bajeti za Serikali kwa Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020;
- ii) Vikao vya kushughulikia Miswada ya Sheria kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) pamoja na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge;
- iii) Kupokea maoni ya Wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge;
- iv) Ziara za kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ili kujiridhisha kuhusu hatua za utekelezaji na ufanisi wake, kwa kulinganisha kiasi cha fedha kilichotengwa na kupokelewa na Wizara/ Taasisi husika;
- v) Kupokea na kujadili Taarifa mbalimbali za Utendaji wa Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge; na
- vi) Kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kujenga uwezo na kubadilishana uzoefu na Taasisi mbalimbali za Serikali na Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi.

1.4 Shughuli zilizotekelawa

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji imetekeliza shughuli zifuatazo: -

1.4.1 Kutembelea na Kukagua Utekekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inayozitaka Kamati za Bunge za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati hii ilitembelea na kukagua Miradi mbalimbali ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Maji iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya Pili ya taarifa hii.

1.4.2 Kuridhia Mikataba ya Kimataifa

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 ikisomwa pamoja na Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotaka Mikataba ya Kimataifa ambayo kwa masharti yake inahitaji kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Kwa madhumuni ya utekelezaji wa jukumu hilo, katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Januari, 2022, Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilishughulikia Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (*East African Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary (SPS) Measures*).

Mheshimiwa Spika, azimio hili pamoja na mambo mengine lilikusudia kukuza na kuimarisha biashara ya chakula na mazao ya kilimo mionganoni mwa nchi wanachama, kuimarisha

uratibu wa masuala ya viwango vya afya ya mimea, usalama wa wanyama na chakula kwa kuwa na mwongozo wa pamoja ndani ya Jumuiya kuhusu masuala hayo na kutoa fursa ya pamoja katika Kanda ya kujilinda dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea na wanyama.

1.4.3 Kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kifungu cha 6(2)(a) na(b) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(d) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi cha Januari 2021 hadi Januari, 2022, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilipokea na kujadili Taarifa **Ishirini na Tano (25)** za Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zake, ambapo, Taarifa Kumi (10) ziliwasilishwa na Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Taarifa Tisa (9) kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Taasisi zilizo chini yake na Taarifa Sita (6) kutoka Wizara ya Maji, kama ifuatavyo:-

i) **Taarifa Kumi (10) kutoka Wizara ya Kilimo na Taasisi zake kuhusu:** -

- a) Muundo na Majukumu ya Wizara ya Kilimo;
- b) Utekelezaji wa Programu ya kuendeleza Kilimo Awamu ya Pili – ASDP 11;
- c) Muundo na Majukumu ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), mafanikio na changamoto katika kutafiti, kusimamia, kuhamasisha na kuratibu shughuli za utafiti wa kilimo Tanzania Bara;
- d) Hatua zilizochukuliwa na Serikali/Wizara kushughulikia malalamiko ya Wakulima kutokana na kukosekana kwa vipimo stahiki katika biashara ya mazao ya kilimo;
- e) Hatua zilizochukuliwa na Serikali/Wizara kuimarisha upatikanaji wa mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu pamoja upatikanaji wa viuatilifu kwa mazao ya pamba na korosho;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- f) Mafanikio na Changamoto katika kushughulikia dharura ya uvamizi wa nzige wa jangwani Kaskazini mwa Tanzania katika mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro;
 - g) Mafanikio na Changamoto kwenye ununuzi wa mahindi na mchele na upatikanaji wa uhakika wa masoko ya mazao mengine;
 - h) Shughuli za Utafiti wa Kilimo zinazotekelizwa na Vituo vya Utafiti wa Kilimo nchini;
 - i) Usimamizi na Usalama wa Chakula Nchini; na
 - j) Mpango Mkakati wa Wizara ya Kilimo kuelekea Tija na Mageuzi ya Sekta ya Kilimo.
- ii) **Taarifa Tisa (9) kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu: -**
- a) Muundo na Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi;
 - b) Mpango Mkakati wa Kuimarisha Sekta ya Mifugo;
 - c) Mpango Mkakati wa Kuimarisha Sekta ya Uvuvi;
 - d) Muundo na Majukumu ya Bodi ya Nyama, mafanikio na changamoto tangu kuanzishwa kwake;
 - e) Muundo na Majukumu ya Bodi ya Maziwa, mafanikio na changamoto tangu kuanzishwa kwake;
 - f) Mwongozo wa utoaji chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo kwa mfumo wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi;
 - g) Utilewaji wa Huduma za Chanjo ya Mifugo nchini na utekelezaji wake;
 - h) Mpango wa kuimarisha Uchumi wa Buluu (*Blue Economy*) kwa kuongeza uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu na eneo la uchumi wa bahari; na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

i) Taarifa ya Utendaji wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kuendeleza na kueneza ufugaji bora wa ng'ombe wa nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje kwa kutumia mbinu za ufugaji wa kisasa.

iii) Taarifa Sita (6) kutoka Wizara ya Maji kuhusu: -

- a) Muundo na Majukumu ya Wizara ya Maji;
- b) Muundo na Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji;
- c) Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Mabonde nchini;
- d) Sheria ya Rasilimali za Maji nchini;
- e) Mipango Mikakati iliyopo ya kutumia maji ya Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa kwa manufaa ya wananchi waishio jirani na maziwa hayo; na
- f) Taarifa ya Chuo cha Maji kuhusu Mkakati wa kuandaa Wataalam wa kusimamia miradi ya maji ili kuifanya miradi ya maji kuwa endelevu.

iv) Taarifa sita (6) kutoka Wizara mbalimbali na Sekta Binafsi ambazo shughuli zake zinachangia mnyororo wa thamani kwa mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kama ifuatavyo: -

a) Wizara ya Fedha na Mipango

Taarifa ya Utendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*Tanzania Agriculture Development Bank -TADB*);

Taarifa kuhusu ushiriki wa TADB katika kuendeleza kilimo chenye tija kwa kuwapatia mikopo wakulima. Mafanikio na changamoto za utoaji mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima.

b) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi – Sekta ya Uchukuzi

✓ Taarifa kuhusu Mpango Mkakati wa kuimarisha Uchukuzi na Usafirishaji wa mazao ya kilimo yatokanayo na maua,

matunda, mbogamboga na viungo kwa lengo la kufikia masoko ya kimataifa; na

✓ Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro Taarifa kuhusu Mkakati wa kuimarissha usafirishaji wa mizigo itokanayo na mazao ya Bustani kwa njia ya anga katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (*Kilimanjaro International Airport - KIA*).

c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

✓ **Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (Sokoine University of Agriculrure - SUA);**

Taarifa kuhusu Changamoto za sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi na mapendekezo ya utatuzi wa changamoto zilizobainika ili kuongeza tija katika mnyororo mzima wa uzalishaji; na

✓ **Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (Moshi Co- Operative University - MoCU);**

Taarifa kuhusu hatua za kuchukua ili kuujenga upya ushirika kwa lengo la kuongeza tija kwenye kilimo kwa kuwawezesha wana ushirika kuhusika katika mnyororo mzima wa thamani.

d)Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (*Tanzania Private Sector Foundation - TPSF*)

Taarifa kuhusu mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kuboresha upatikanaji wa uhakika wa masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

1.4.4 Ziara ya kutembelea mashamba ya Bustani na baadhi ya wawekezaji (Wadau) wanaofanya shughuli za uzalishaji wa maua na mboga mboga mkoani Arusha na Kilimanjaro;

Mheshimiwa Spika, kutoptera na kukua na fursa iliyopo kwenye biashara ya maua, matunda, mbogamboga na viungo ulipa kibali Kamati ifanye ziara ya kikazi Mkoani Arusha na Kilimanjaro kwa ajili kujielimisha kuhusu shughuli za kilimo cha bustani nchini.

Mheshimiwa Spika, ziara hiyo ilifanyika kuanzia tarehe 13- 14 Agosti, 2021 kwa ufadhilli wa Shirika lisilo la Kiserikali la *Tanzania Horticulture Association* (TAHA) kwa ajili ya kupokea taarifa ya shughuli za Asasi hii ambayo ni Asasi kilele inayoshughulikia uendelezaji wa kilimo cha mazao ya bustani nchini. Aidha, Kamati ilitaka kufahamu changamoto zinazoikabili sekta ndogo ya bustani na kufanya sekta hii kushindwa kushiriki kikamilifu kufikia fursa iliyopo kwenye masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo Kamati ilibaini kuwa Tasnia ya mazao ya bustani ni sekta ndogo ya kilimo inayokuwa kwa kasi ambapo inakadiriwa kukua kwa **asilimia 7** kwa mwaka, huku kilimo kwa ujumla wake kikukua kwa **asilimia 3-4** kwa mwaka. Kuendelea kukua kwa kasi kwa tasnia hii, kumepelekea kuajiri wakulima na watu wanojishughulisha na shughuli za mnyororo wa thamani wa mazao ya mboga mboga, matunda na viungo kufikia **millioni 6.5**.

Mheshimiwa Spika, vilevile Tasnia hii ni moja ya sekta inayochangia fedha nyngi za kigeni kwenye kilimo, ambapo mchango wa sekta hiyo kwa mwaka 2019 ilikuwa **asilimia 38** ya fedha zote zinazotokana na mazao ya kilimo. Aidha, takwimu za Shirika la Chakula Duniani – *Food Agriculture Organization* (FAO) zinazotolewa na taasisi yake ya *Food and Agriculture Data* (FAOSTAT) zinaonyesha kuwa **Tanzania ni moja kati ya nchi 20 duniani zinazozalisha kwa wingi mazao ya bustani**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nafasi ya Tanzania katika uzalishaji wa mazao ya bustani duniani, ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo, hata hivyo bado nchi yetu hajafanya vizuri kufikia na kufaidika na masoko ya kimataifa kama ambavyo nchi za Ethiopia na Kenya zilivyofanikiwa. Takwimu zifuatazo zinaonyesha ulinganisho wa uzalishaji wa mazao ya bustani kwa nchi za Tanzania, Kenya na Ethiopia.

Jedwali Na. 1: Ulinganisho wa uzalishaji wa mazao ya bustani kwa nchi za Tanzania, Kenya na Ethiopia

NCHI	UKUBWA WA ARDHI -SQ MLES	MATUMIZI YA HEKA	UZALISHAJI KWA TANI
KENYA	224,081	2,800	160,000
ETHIOPIA	426,373	1,450	52,000
TANZANIA	364,945	120	7,000

CHANZO: Taarifa ya TAHA kwenye Ziara ya Kamati mkoani Arusha na Kilimanjaro Agosti, 2021

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini uzalishaji wa mazao ya bustani kwa nchi yetu uko chini kutohana na sababu mbalimbali ikiwemo kufungwa kwa muda mrefu kwa mashamba makubwa yaliyokuwa yanazalisha bidhaa hizo. Hali hii imepelekea kampuni nyingi zilizokuwa zinashughulika na bidhaa za bustani kufunga shughuli zao na au kuzalisha chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, kufungwa kwa mashamba hayo kumeisababishia Serikali hasara zifuatazo: -

- i) Kupungua kwa mapato ya Serikali yatokanayo na fedha za kigeni katika kilimo kiasi cha **\$ 42,450,000**;
- ii) Kamapuni zilizofunga biashara kushindwa kulipa mkopo kiasi cha **shilingi 88.8 bilioni** zilizotolewa na Benki ya Uwekezaji Tanzania (*Tanzania Investment Bank TIB*); na
- iii) Tafiti zinaonyesha tangu kufungwa kwa kampuni hizo kuanzia mwaka 2012- 2020 **ajira 4,010** zimepotea.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini pia kuwa, nchi zilizofanikiwa kwenye uzalishaji wa mazao ya bustani zimefanya uwekezaji mkubwa kwenye mikakati ya masoko, mikopo yenyeye riba nafuu kwa wakulima wadogo, matumizi ya teknolojia za kisasa, pamoja na uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu ya usafirishaji kama bandari na usafiri wa anga na huduma bora za ugani ikiwa ni pamoja na upimaji wa afya ya udongo na huduma za vifaa vyataga kisasa

kwa ajili ya maabara. Hatua hizi zimepelekea kuuza kwa wingi mazao hayo nje ya nchi kama inavyoonekana kwenye takwimu zifuatazo: -

Ulinganisho wa Uuzaji wa Mazao ya Bustani Nje ya Nchi kwa Mwaka:

- Kenya – Maua – US\$ 800,000 Mboga Mboga na Matunda – US\$ 2.5 bilioni
- Ethiopia – US\$ 794 Milioni
- Misri – US\$ 2.5 bilioni
- Israel – US\$ 6-8 bilioni
- Tanzania – US\$ 700 millioni

Mhesimiwa Spika, nchini Tanzania tasnia ya bustani inakabiliwa na changamoto mbalimbali, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na: -

- i) Gharama kubwa za uzalishaji zinazowakabili wawekezaji;
- ii) Matumizi duni ya teknolojia za kisasa zinazofaa kwa kilimo;
- iii) Gharama kubwa za usafirishaji;
- iv) Tozo na kodi nyingi za Serikali;
- v) Ukosefu wa ndege za kusafirishia mizigo;
- vi) Uchache wa gati za kupakia na kupakua mizigo katika bandari zetu. Kwa mfano: **Kenya kuna gati 21, Tanzania ina gati 12;**
- vii) Uelewa mdogo wa wataalamu kutoka mamlaka mbalimbali za Serikali kuhusu umuhimu wa kuhudumia bidhaa zinazoharibika haraka (*perishable goods*);
- viii) Kushindwa kutumia kikamilifu fursa ya masoko ya kimataifa na hivyo kupelekea wafanyabiashara kutoka nje ya nchi kununua mazao ya bustani kutoka kwenye mashamba ya wakulima, kisha kuyaweka kwenye vifungashio vinavyoonyesha bidhaa hizo zimezalishwa kwenye nchi zao.

- ix) Kukosekana kwa teknolojia za kisasa kama miundombinu ya umwagiliaji, huduma za maabara za kisasa, na kupima udongo; na
- x) Kukosekana kwa wataalamu wa kutosha wa huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, licha ya changamoto hizo, Kamati inatambua na inaipongeza Serikali kwa kuondoa baadhi ya kodi na tozo za usafiri zilizokuwa zinachangia kuzorota kwa ukuaji wa tasnia hii, kuongezeka kwa bajeti ya kuratibu shughuli za mazao ya bustani kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na kuboresha huduma ya usafiri wa anga kwenye viwanja vya Ndege vya kimkakati vya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro na Uwanja wa Ndege wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maboresho yaliyofanyika kwenye viwanja hivi, Kamati imebaini maboresho hayo hayajawa na manufaa tarajiwa kutokana na ongezeko la ghamama za usafirishaji linalosababishwa na kukosekana kwa uwiano mzuri wa mizigo (*cargo imbalance*) inayotoka na kuingia nchini; kiwango cha mizigo inayoingia nchini ni kidogo ikilinganishwa na kiwango cha mizigo inayotoka nchini kuelekea nje ya nchi. Hali hii hupelekea ndege inapokuja tupu, kulazimika kuongeza bei ya mizigo ili kufidia ghamama za kuja nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo kwa Serikali, Kamati pia inaipongeza TAHA kwa kusaidia kufungua masoko ya mazao ya bustani duniani ambapo hadi sasa yamepatikana masoko nchini India, Afrika Kusini na Pakistan.

1.4.5 Uchambuzi wa Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(2) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza

ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za sekta inazosimamia ambazo zinajumuisha mafungu yafuatayo: -

- ✓ Wizara ya Kilimo - Fungu 43;
- ✓ Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - Fungu 05;
- ✓ Tume ya Maendeleo ya Ushirika - Fungu 24;
- ✓ Wizara ya Maji Fungu 49; na
- ✓ Wizara ya Mifugo na Uvuvi – Sekta ya Mifugo Fungu 99; na
- ✓ Sekta ya Uvuvi Fungu 64.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ulitazama ulinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika kwa kipindi cha nusu mwaka hadi kufikia mwezi Disemba, 2021 kwa lengo la kutathmini mafanikio yaliyofikiwa katika kutekeleza malengo yaliyowekwa kwenye sekta husika pamoja na kusaidia kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ili kuweza kutoa ushauri wenye tija katika kuimarisha sekta zinazosimamiwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati ulibaini kuwa, kwa ujumla utolewaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo hususan sekta za uzalishaji ambazo ni kilimo, mifugo na uvuvi si wa kuridhisha na hauna tija sekta hizi. Hii inathibitishwa na takwimu zilizotolewa na Wizara husika kuhusu kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi mwezi Disemba kama ifuatavyo: -

- ✓ Wizara ya Kilimo - Fungu 43 ilikuwa imepokea fedha za maendeleo za ndani **shilingi 35,092,042,238** ambazo ni sawa na **asilimia 42.7** na fedha za maendeleo za nje **shilingi 3,789,267,202** sawa na **asilimia 4.2**;
- ✓ Tume ya Umwagiliaji – Fungu 05 ilikuwa imepokea fedha za maendeleo za ndani **shilingi 349,620,000** ambazo ni sawa na **asilimia 1.0** na hakuna fedha yoyote ya maendeleo kutoka nje iliypokelewa;

- ✓ Tume ya Ushirika – Fungu 24 haikutengewa fedha yoyote ya kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na ukomo wa bajeti;
- ✓ Sekta ya Mifugo – Fungu 99 ilikuwa imepokea fedha za maendeleo za ndani **shilingi 3,217,386,250** ambazo ni sawa na **Asilimia 5.1** na Hakuna fedha za nje zilizotolewa na
- ✓ Sekta ya Uvuvi – Fungu 64 ilikuwa imepokea fedha za maendeleo za ndani **shilingi 15,236,392,642** ambazo ni sawa na **Asilimia 12.6** na hakuna fedha ya maendeleo kutoka nje iliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya huduma ya maji kupitia Wizara ya Maji – Fungu 49 ilikuwa imepokea **shilingi 87,999,810,828.08** sawa na **asilimia 50** kutoka **Mfuko wa Maji**, shillingi **95,880,019,380.18** sawa na **asilimia 56** kutoka **Mfuko Mkuu wa Serikali** na **shilingi 210,899,753,650.78** sawa na **asilimia 70**. Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa sekta zinazotoa huduma kwa jamii kama maji hazitegemei bajeti inayotengwa na Serikali ambayo ina ukomo badala yake Serikali imetafuta vyanzo mahsusvi vyatengeneza na kuziwekea uzio fedha zinazopatikana kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyokusudiwa.

1.4.6 Mahitaji ya Bajeti katika Sekta ya Mifugo

Mheshimiwa Spika, kutokana na athari za ukame zilizoathiri sekta ya mifugo Kamati ilitaka kufahamu ili mahitaji halisi ya Bajeti kwa sekta hii. Kamati ilichambua Mpango Mkakati wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kubaini kuwa Ili kuendeleza sekta ya mifugo, maeneo saba ya kimkakati yanatakiwa kutengewa fedha kwa kipindi cha miaka mitano (2022/23 - 2026/27) ambayo yanahitaji jumla ya shilingi **1,949,671,644,815** kama ifuatavyo: -

(i) Kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo – shilingi **104,943,611,999**;

(ii) Kuimarisha huduma za maji, malisho na vyakula vyatengeneza na kuziwekea uzio fedha zinazopatikana kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyokusudiwa – shilingi **879,393,000,000**;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (iii) Kuimarisha afya ya mifugo – shilingi **774,087,400,000**
- (iv) Kuboresha huduma za ugani- shilingi **43,786,320,030**;
- (v) Kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo ya Taaluma za; Mifugo – shilingi **61,711,812,786**
- (vi) Kuwezesha Uongezaji Thamani Mazao ya Mifugo – shilingi **30,218,000,000**; na
- (vii) Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa – shilingi **55,531,500,000**.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mahitahi haya ya **shilingi 1,949,671,644,000** ni sawa na wastani wa **shilingi 389,934,328,000** kwa mwaka ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 kiasi cha **shilingi 16,400,000,000** sawa na **asilimia 4** ya mahitaji alisi.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelawa na Kamati kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Januari 2022, naomba sasa nitoe Taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, masuala yatakayotolewa taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa ni changamoto ambazo zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara na Taasisi zake pamoja na Sekta Binafsi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, hivyo kuleta tija kwa Taifa.

2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyobainishwa na Kamati kama ifuatavyo: -

2.2.1 Yatokanayo na Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali

i) Changamoto ya Mfumo wa Ugharamiaji Sekta ya Kilimo ambayo inajumuisha kilimo vipando, mifugo na uvuvi

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sekta hizi zimeendelea kutegemea bajeti kuu inayotengwa na Serikali ambayo huwa ni kidogo na hivyo kutotoshelaza kutekeleza vipaumbele vya sekta husika, aidha kwa muda mrefu kiasi kinachotengwa huwa hakitolewi kwa wakati. Mbali ya fedha zinazotengwa kuwa hazitoshi, kwa miaka mingi kiasi kinachotolewa huwa chini ya tengeo. Aidha, katika ngazi ya Serikali za Mitaa ni Halmashauri chache sana hutenga fedha kwa ajili ya kuimarishe sekta hizi licha ya kunufaika na tozo na kodi zitokanazo na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

ii) Upatikanaji wa Mbolea kwa Wakati na kwa Bei Nafuu

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tija ya mazao ya kilimo inategemea matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora, viuatifu na mbolea. Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini takribani **asilimia 90** ya mbolea za viwandani zinazotumika nchini huagizwa kutoka nje ya nchi hali hii imesababisha wakulima kupata mbolea na viuatifu kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa msimu wa mwaka 2021/2022 bei za mbolea zimepanda katika soko la dunia kulikochangiwa na uwepo wa UVIKO 19 na kupelekea baadhi ya viwanda vya uzalishaji wa mbolea kusimamisha uzalishaji na vingine kupunguza uzalishaji na nchi wazalishaji wa mbolea kusitisha uuzaaji wa mbolea nje ya nchi zao ili kutosheleza mahitaji yao na hivyo kuchangia bei za mbolea ndani ya nchi kuongezeka maradufu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hiyo ya bei juu ya mbolea, bado wakulima wengi nchini wanakabiliwa na changamoto ya mbolea kupatikana wakati msimu wa kupandia ukiwa umemalizika kutokana na muda mrefu

unaotumika kutoa mbolea bandarini. Vilevile uwepo wa matumizi ya mbolea yasiyo sahihi pamoja na kutumia mbolea na viuatilifu bila kujua mahitaji ya udongo kumepelekeea tija ndogo kwenye kilimo.

iii) Kilimo cha Kutegemea Mvua

Mheshimiwa Spika, wakulima wengi wa nchi yetu ni wakulima wadogo ambao wameendelea kutegemea kilimo cha mvua ambacho hakina uhakika. Kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi kumepelelea uhaba wa mvua na mvua zisizotabirika kumnesababisha kupunguza uzalishaji na tija hivyo kuwakatisha tamaa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, ipo haja ya kupunguza utegemezi wa kilimo cha mvua kuweka mikakati maradufu ya uvunaji na utunzaji wa maji na kuongeza mkazo kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia maziwa, bahari, mito, chemichemi ikiwemo mabonde mengi yanayotiririsha maji kwa wingi hasa wakati wa mvua.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa pamoja na umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji, hakuna mradi mkubwa wa kimkakati unaotekelezwa ili kuongeza tija kwenye kilimo badala yake Serikali imekuwa ikitenga fedha kidogo kwa ajili ya kujenga na kukarabati skimu za umwagiliaji.

iv) Ukosefu wa Matumizi Sahihi ya Zana Bora za Kilimo

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonyesha **asilimia 54** ya wakulima nchini wanaendelea kutumia jembe la mkoно kama njia kuu ya uzalishaji badala ya kutumia zana bora za kilimo. Hali hii imesababishwa na kukosekana kwa mipango madhubuti ya kitaifa ya kuendeleza matumizi ya zana bora za kilimo yakiwemo matrekta pamoja na kukosekana kwa mipango ya kujenga au kufufua viwanda vya kuzalisha zana za kilimo.

v) Changamoto zinazokabili Tasnia ya Ushirika Nchini

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya vyama vya ushirika nchini yanawezwa kupimwa kwa kuangalia idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika. Vyama vya ushirika

nchini vinamiliki viwanda vikubwa, vyta kati na vidogo vidogo vipatavyo 171. Kati ya hivyo, viwanda 145 vinafanya kazi. Aidha, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa hadi hivi sasa, hakuna Asasi iliyofanikiwa kuwa na viwanda vingi katika sekta mbalimbali kama ushirika, hakuna Asasi shirkishi zilizo katika uzalishaji, uchakataji na utafutaji masoko na kuuza kwa kiwango cha vyama vyta ushirika nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini ushirika ndio njia sahihi ya kumkomboa mkulima kutoka kwenye unyonyaji, kupitia vyama vyta ushirika ni rahisi kupata mitaji kwa njia ya mikopo kutoka Taasis za fedha hivyo mchango wa ushirika ni mkubwa katika kuwaendeleza wanachama wake, kutengeneza fursa za ajira na kuchangia katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa ushirika kwa maendeleo ya wanachama na Taifa kwa ujumla Tasnia ya Ushirika inakabiliwa na changamoto kadhaa, nyangi zikiwa zinatokana na mapungufu katika utekelezaji na baadhi zikiwa zinatokana na mapungufu katika Sera na Sheria za Ushirika. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatazo: -

- a) Wanachama wengi wa vyama vyta ushirika, wakiwemo Viongozi, Watendaji wa Vyama husika na Wasimamizi wa vyama vyta ushirika wakiwemo Maafisa Ushirika kutokuwa na weledi pamoja na uelewa wa maadili na misingi ya ushirika;
- b) Wigo wa ushirika kutopanuka kwa haraka kuingia katika maeneo mapya ili kuendana na mipango ya maendeleo ya kiuchumi ya Taifa kama vile uanzishwaji wa viwanda na miradi mbalimbali mikubwa ili kuwawezesha wanaushirika kuhusika katika mnyororo mzima wa thamani – kuanzia ununuzi na usambazaji wa pamoja wa pembejeo; uzalishaji wa mali ghafi (*raw materials*); uhifadhi (*warehousing*), uchakataji katika viwanda vyta ushirika, ufungashaji na uuzaaji katika maduka makubwa ya walaji na ya jumla ya ushirika (*cooperative supermarkets/stores*);
- c) Kutokuwepo na mfumo wa kisheria unaomwezesha Mrajis wa Vyama vyta ushirika kuhusika moja kwa moja katika

usimamizi wa makampuni yanavyomilikiwa na Vyama vy'a Ushirika na hivyo kusababisha viwanda vingi vinavyomilikiwa na vyama vy'a ushirika kukosa taaluma ya usimamizi na kuwa katika hatari ya kufilisika;

- d) Kukosekana kwa mfumo imara wa masoko ya mazao ya vyama vy'a ushirika unaowezesha vyama vikuu vy'a ushirika kuhusika katika kusimamia mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani katika mazao kunakochangia kuongeza gharama wa wanachama;
- e) Kukosekana kwa vigezo na mfumo sahihi wa upatikanaji wa Watendaji na Wajumbe wa Bodi za Vyama vy'a Ushirika kwa kuzingatia ukubwa wa biashara wanayofanya na mchepuo husika; na
- f) Kukosekana kwa ulazima wa elimu na mafunzo ya ushirika kwa Wanachama, Watendaji, Wajumbe wa Bodi za Vyama vy'a Ushirika pamoja na na Taasisi zinazohusika na ushirika.

vi) Uwepo wa Wingi wa Athari za Magonjwa ya Mifugo

Mheshimiwa Spika, huduma za Afya ya Mifugo ni muhimu katika kuhakikisha kuwa mifugo inayozalishwa inakidhi viwango kulingana na mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Ili kufikia lengo hilo, mifugo inapaswa kukingwa dhidi ya magonjwa yanayoweza kusababisha vifo vy'a mifugo, kuhatarisha afya ya jamii na kuhatarisha usalama wa biashara na kuongeza gharama kwa wazalishaji wa mifugo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini uwepo wa wingi wa athari za magonjwa ya mifugo unatokana na uwepo wa mfumo hafifu kitaifa wa kuchunguza, kutambua na kuzuia au kudhibiti magonjwa. Hali hii imepelekea mifugo mingi inayozalishwa nchini hukabiliwa na magonjwa na hivyo kupelekea madhara yafuatayo: -

- a) Kuathirika kwa biashara ya nyama kimataifa na hivyo kulikosesha Taifa fedha za kigeni kutokana na kushindwa kuza nyama katika baadhi ya masoko ya kimataifa;

- b) Kulighalimu Taifa fedha nyingi kununua dawa kwa ajili ya matibabu ya wanyama; kwa mfano Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Sotoka ya Mbuzi na Kondoo na Mdondo yanaigharimu nchi **Shilingi Bilioni 101.8** kwa mwaka; na
- c) Magonjwa ya mifugo huchangia magonjwa ya binadamu kwa takriban **asilimia 60** na kuligharimu taifa fedha nyingi kwa ajili ya kununua vifaa tiba na dawa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini licha ya umuhimu wa afya ya mifugo kwa mifugo yenyewe, binadamu na kwa biashara, udhibiti wa magonjwa ya mifugo unakabiliwa na changamoto mbalimbali, zifuatazo ni baadhi ya changamoto hizo: -

- a) Upungufu wa **majosho 8,525** na uchakavu wa majosho yaliyopo kwa ajili ya kuogesha mifugo;
- b) Upungufu wa vituo vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo;
- c) Bei kubwa ya dawa za kuogesha mifugo na viuatilifu vya mifugo;
- d) Upungufu wa madaktari wa mifugo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- e) Maeneo mengi ya nchi kuzungukwa na mapori ya hifadhi na wanyama pori hivyo kuleta changamoto katika kudhibiti baadhi ya magonjwa ya mifugo kama vile ugonjwa wa miguu na midomo na ugonjwa wa ndorobo;
- f) Baadhi ya chanjo na dawa kutozalishwa nchini hivyo kulazimika kutumia fedha nyingi za kigeni kuingiza chanjo na dawa kutoka nje ya nchi; na
- g) Elimu duni ya ufugaji bora kwa wafugaji ikiwemo kutozingatia ratiba za chanjo na matibabu kwa mifugo.

vii) Uwezo Mdogo wa Nchi Yetu Kuzalisha, na Kusambaza Mbegu Bora za Mazao, Mifugo na Samaki kwa Wakulima, Wafugaji na Wavuvi

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa licha ya uwepo wa Kampuni kubwa ya kuzalisha ng'ombe wa nyama kwa sababu ya kukosa fedha za kufanya uwekezaji imepelekea Kamapuni ya Ranchi za Taifa (*National Ranching Company Limited - NARCO*) kushindwa kuzalisha na kusambaza mbegu bora za mifugo wa nyama kwa wafugaji na kupelekea wafugaji wenye uwezo wa kifedha kutafuta mbegu bora kutoka nchi jirani za Kenya, Zambia na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali imejielekeza kuongeza uwekezaji na uzalishaji mkubwa wa viumbe maji (ufugaji wa samaki) kwa kutumia fursa iliyopo katika rasilimali za maji zilizopo katika Bahari, Maziwa, Mabwawa, mito na mabonde oevu (*Aquaculture*). Hata hivyo Kamati imebaini uzalishaji wa vifarnga bora bado uko chini kutokana na changamoto kadhaa ikiwa pamoja uhaba wa zana na pembejeo, huduma hafifu za ugani na uwekezaji mdogo unaotokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mbegu bora za mazao ya kilimo, ukosefu wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati umeathiri utendaji kazi wa Wakala wa Mbegu za Kilimo (*Agricultural Seed Agency -ASA*), na hivyo kushindwa kutekeleza ipasavyo kazi ya uzalishaji wa mbegu kwa wakati hasa ikizingatiwa uzalishaji wa mbegu hutegemea msimu wa mvua, kalenda na misimu ya mazao.

Mheshimiwa Spika, hali hii imepelekea mashamba yanayotumiwa na ASA kuzalisha mbegu, kushindwa kuzalisha kwa tija kwa sababu ya kutegemea mvua badala ya uzalishaji mbegu kwa kutumia umwagiliaji, kushindwa kufanya ukarabati wa miundombinu ambayo ni uchakavu na kushindwa kufufua mashamba ya mbegu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sababu hizi zimepelekeea nchi yetu kutumia fedha nyingi za kigeni kuagiza mbegu kutoka nchi za nje ambapo **asilimia 60** ya mbegu zinazotumika nchi huagizwa kutoka nje na huuzwa kwa gharama kubwa ambayo wakulima wengi hawamudu.

viii) **Upungufu wa Vyakula, Malisho na Rasilimali Maji kwa Ajili ya Kunyweshea Mifugo;**

Mheshimiwa Spika, uhaba wa maji na malisho unasababisha vifo via mifugo na uzalishaji wa mifugo isiyo na ubora kulingana na mahitaji ya soko hususan viwanda nya kusindika nyama na masoko ya kimataifa. Aidha, tija ya mifugo katika utoaji wa maziwa upungua hususan wakati wa kiangazi na hivyo kukwamisha usindikaji wa maziwa viwandani.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa malisho ya mifugo kullkosababishwa na ukame ambapo tathimini iliyofanywa na Serikali inaonyesha kwa kipindi cha kuanzia mwezi Septemba, 2021 hadi Januari 2022 athari zitokanazo na ukame zimepelekeea madhara kwenye tasnia ya mifugo kama ifuatavyo: -

- a) Vifo via mifugo takribani **306,358** ambavyo vinajumuisha **ng'ombe 157,695, mbuzi 48,290, kondoo 94,230, punda 6,135** na **ngamia 8**;
- b) Kupungua kwa thamani ya mifugo kutokana na kudhoofika;
- c) Kuongezeka kwa magonjwa yaenezwayo na kupe kunakosababishwa na ukosefu wa maji kwenye majosho na wafugaji wengi kwenda mbali na majosho kutafuta malisho na maji;
- d) Kukauka kwa vyanzo via maji kwa mifugo hususani mabwawa, malambo, visima, mito na madimbwi;
- e) Migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi kutokana na wafugaji kuhangaika kutafuta maji na malisho;

- f) Biashara ya mifugo hai kwenye minada mbalimbali imepungua kutokana na wafugaji wengi kuhama maeneo yao ya asili kwenda kutafuta malisho na maji sehemu za mbali. Hali hii imesababisha bei ya ng'ombe bora kwenye minada kupanda kutoka **shilingi 1,400,000** hadi shilingi **1,900,000** kwa ng'ombe mmoja;
- g) Viwanda vya kuchinja mifugo na kuchakata nyama vimeathirika kwa kupungua kwa mifugo inayopelekwa viwandani. Mfano kiwanda cha *Tan Choice* cha Kibaha kilisimamisha kuchinja ng'ombe tangu mwezi Oktoba, 2021 kutokana na uhaba wa ng'ombe wenye ubora stahiki kwa ajili ya nyama ya kuuza nje ya nchi;
- h) Bei ya nyama kwenye mabucha zimepanda kutoka wastani wa shilingi 6,000 hadi shilingi 7,500 kwa kilo ya nyama ya mchanganyiko na kutoka shilingi 8,000 hadi shilingi 12,000 kwa kilo ya nyama ya steki kutokana na kupungua kwa ng'ombe wanaouzwa minadani kwa ajili ya kuchinjwa; na
- i) Kwa upande wa viwanda vya kusindika maziwa kushindwa kuzalisha kulingana na mahitaji na hivyo Taifa kulazimika kutumia fedha za kigeni kuagiza maziwa kutoka nje ya nchi.

ix) Kuporomoka kwa Ufanisi na Usimamizi hafifu wa Tasnia ya Ugani

Mheshimiwa Spika, kuporomoka kwa Ufanisi na Usimamizi hafifu wa Tasnia ya Ugani ni changamoto kubwa kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kukosekana kwa mfumo unaosimamiwa na Wizara za kisekta ndio chanzo cha kuporomoka kwa ufanisi wa tasnia ya ugani licha ya Wizara za kisekta kuwa na Kurugenzi ya Mafunzo na Ugani.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa mfumo unaosimamiwa na Wizara za kisekta ulianza mwaka 2000 baada ya Serikali kuzingatia Utekelezaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Sheria ya Serikali za Mitaa ambapo Mfumo wa Ugatuzi wa Madaraka ulianza kutumika

kwa kuwezesha wananchi kuwa chachu ya kuibua Mipango ya Maendeleo badala ya kupangiwa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali Mfumo wa Ugatuzi wa Madaraka umechangia kukosekana kwa mfumo bora wa usimamizi wa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi hasa kwa maafisa ugani kutokana na Wizara za kisekta kushindwa kuainisha mafunzo yanayotakiwa kisekta na kushindwa kuwachukulia hatua za kinidhamu pindi inapohitajika kufanya hivyo. Aidha, uadilifu wa mfumo wa usimamizi wa sekta na Watumishi umechangiwa na kutokuwepo kwa mfumo bora wa kiunganishi katika ngazi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zimepelekea kwa muda mrefu sasa Huduma ya Ugani kukabiliwa na upungufu mkubwa wa Maafisa Ugani katika ngazi ya Kijiji, Kata na Halmashauri za Wilaya. Pia, wagani wachache walioipo wanakabiliwa na upungufu wa vitendea kazi ikiwemo vyombo vyaya usafiri na mafunzo rejea ya mara kwa mara ili kuwawezesha kutoa huduma ya ugani wa kilimo, mifugo na uvuvi kulingana na mabadiliko ya kiteknolojia na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, Kamati inaipongeza Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kutenga fedha kwa ajili ya kununua pikikipi na simu janja kama vitendea kazi kwa ajili ya kuwasaidia wagani kuwafikia wakulima kwa urahisi na kurahisisha mawasiliano na wakulima.

x) **Changamoto katika shughuli za Utafiti**

Mheshimiwa Spika, tafiti katika kilimo, ufugaji na uvuvi hufanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (*Tanzania Agricultural Research Institute –TARI*), Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (*Tanzania Livestock Research Institute –TALRI*), Taasisi ya Utafiti wa Samaki (*Tanzania Fisheries Research Institute – TAFIRI*) kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu Mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza kazi nzuri inayofanywa na Taasisi za Utafiti nchini kulingana na kile walichowea kutokana na bajeti ndogo wanayotengewa ambapo tafiti nydingi zinazohusu mbegu bora za mazao, aina bora za malisho ya mifugo na samaki na namna bora ya uzalishaji wa mazao ya mifugo zimefanyika na matokeo yamepatikana. Hata hivyo, matokeo ya tafiti hizi hayajawafikia na hayatumiwi na walengwa kutokana na kutokuwepo kwa mfumo imara wa usambazaji wa matokeo ya utafiti kutoka kwa watafiti kwenda kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto nydingine inayozikabili Taasisi za Utafiti ni utegemezi wa fedha za utafiti kutoka kwa wadau wa maendeleo hatua hii imepelekea baadhi ya tafiti kufanyika nje ya matakwa ya nchi yetu na kufuata matakwa ya wafadhili na hivyo kutotatua matatizo halisi yanayozikabili sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini matokea ya utafiti yamekuwa yakiwanufaisha wazalishaji wengi wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi hata hivyo, wanaufaika wengi hawachangii chochote kwenye gharama za utafiti isipokuwa kwa mazao ambayo yanasmamiwa na Bodi za Mazao kama Kahawa, Chai, Pamba na Korosho ambapo asilimia kidogo ya mauzo ya kila kilo hupelekwa kusaidia shughuli za utafiti, hatua ambayo imeongeza ufanisi kwa mazao hayo.

xi) Utekelezaji wa Miradi ya Maji Nchini na Changamoto zinazoikabili Sekta ya Maji

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati imebaini kasi ya uharibifu wa vyanzo vyta maji kutokana na ongezeko la idadi ya watu pamoja na mabadiliko ya tabia nchi inaashiria kupungua kwa kiasi cha maji kwenye vyanzo vyta maji vilivyopo. Tafiti zinaonyesha hadi mwaka 2019, mahitaji ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile majumbani, umwagiliaji, viwanda na mazingira ni wastani wa **mita za ujazo milioni 47,444** kwa mwaka kati ya **mita za ujazo milioni 125,274** kwa mwaka zilizopo. Vilevile, makadirio yameonesha kuwa mahitaji ya

maji yataongezeka kufikia wastani wa **mita za ujazo bilioni 80.2** kwa mwaka ifikapo mwaka 2035.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha nchi yetu haifiki kwenye uhaba wa maji (*water stress*) hatua madhubuti za usimamizi, uendelezaji na matumizi sahihi ya rasilimali za maji zinahitajika kuchukuliwa ili kuiepusha nchi yetu kufikia kwenye hali ya uhaba wa maji. Kwa muktadha huu, Serikali haina budi kuendeleza kwa vitendo mikakati ya kutunza na kuendeleza rasilimali za maji ili kukabiliana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini pia nchi yetu ina vyanzo vingi vya maji vinavyojumuisha maji shirikishi kutoka ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa, Natron, Chala na Jipe pamoja na Mito ya Kagera, Mara, Malagarasi, Momba, Mwiruzi, Umba, Ruvuma na Songwe. Katika vyanzo hivyo, inakadiliwa kuwa kuna takribani **asilimia 43.3** ya rasilimali zote za maji za Tanzania. Idadi hiyo ya vyanzo vya maji inaifanya **Tanzania kuwa nchi pekee Barani Afrika yenye Mabonde mengi ya maji shirikishi**.

Mheshimiwa Spika, licha ya rasilimali nyingi ya maji iliyopo nchini, na jitihada kubwa inayofanywa na Serikali kwenye sekta hii, bado wananchi wanakabiliwa na ukosefu wa huduma ya maji safi na salama na kulazimika kutumia muda mwingi kwenda kutafuta maji safi umbali mrefu. Aidha, mifugo mingi inaendelea kupoteza maisha kutoptana na ukame na pia Serikali kutotekeleza mipango iliyopo ya kuvuna na kuhifadhi maji pindi yanapokuwa mengi wakati wa masika.

Mheshimiwa Spika, vile vile nchi yetu ni sehemu ya mabonde matatu makubwa ya maji katika Bara la Afrika, ambayo ni Bonde la Mto Nile unaoanza Ziwa Victoria na kumwaga maji katika Bahari ya Mediterania, Bonde la Mto Zambezi unajumuisha maji kutoka Ziwa Nyasa na kumwaga maji Bahari ya Hindi, na Bonde la Mto Kongo unaoanza Ziwa Tanganyika na kumwaga maji Bahari ya Atlantiki.

Mheshimiwa Spika, ili kunufaika na kuondokana na migogoro inayoweza kutokea kupitia matumizi ya maji shirikishi Kamati

inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Maji na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutumia njia za kidiplomasia wakati wote ili kuweza kunufaika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Serikali kuhusu miradi inayotekelawa kwa kupitia maji ya Ziwa Victoria kwa lengo la kuwanufaisha wananchi wanaoishi jirani na ziwa hilo. Kamati imeridhishwa na miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa kwani kwa kiasi kikubwa wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya maji safi, salama na ya kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria, Kamati ilitaka kufahamu mipango ya Serikali katika kuhakikisha wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya kandokando ya maziwa makuu ya Tanganyika na Nyasa nao wanapata huduma ya maji safi na salama ili kuondokana na changamoto ya ukosefu wa maji unaowakabili.

Mheshimiwa Spika, napenda kulialifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imeridhishwa na kazi nzuri inayofanywa na Serikali kwa kubuni na kutekeleza miradi ya maji inayoendelea katika ziwa Tanganyika na Nyasa. Kamati inaamini kukamilika kwa miradi hiyo kutaboresha mazingira ya upatikanaji maji safi na salama kwa kupunguza usumbufu kwa baadhi ya wananchi kutembea Kilomita nyingi kutoka sehemu moja kwenda nyingine ili kufuata maji safi na salama kwa matumizi ya nyumbani na huduma za kijamii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi iliyoanza kutekelezwa na mipango mizuri iliopo ya kutumia vyanzo vya maji vya maziwa makuu, Kamati imebani changamoto mbalimbali zinazokwamisha utekelezaji wa miradi inayotumia vyanzo vya maziwa makuu. Changamoto hizo ni pamoja na uhitaji wa uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa miundombinu ya maji, gharama kubwa za uendeshaji zinazotokana na miradi hiyo kutumia mifumo ya kusukuma maji kwa mashine (*pump*)

pamoja na gharama za mitambo ya kusafisha maji inayohitaji fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa pamoja na changamoto hizo huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama imeendelea kuimarika nchini kwani idadi ya wananchi wanaopata maji maji safi na salama imeongezeka na kufikia **asilimia 70** kwa upande wa vijiji na **asilimia 84** kwa upande wa mijini. Mafanikio haya yametokana na hatua nzuri za uratibu na usimamizi, mapato yanayotokana na ufanisi wa Mfuko wa Taifa wa Maji pamoja na utaratibu wa kutumia *Force Account*. Hatua hizi zimewezesha miradi mingi kutekelezwa kwa kutumia wakandarasi wa ndani, kukamilika kwa wakati na kuokoa nusu ya ghrama kwa kila mradi uliotekelizwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini baadhi ya changamoto zinazoikabili Wizara ya Maji, kwenye uratibu na usimamizi wa sekta ya maji kuwa ni pamoja na: -

- i) Uharibifu wa Vyanzo vya Maji na Uchafuzi wa Rasilimali za Maji zinazoendelea kupungua kutoptokana na mwenendo wa ongezeko la mahitaji linalotokana na ongezeko la watu, uharibifu na uchafuzi wa vyanzo vya maji na mazingira na mabadiliko ya tabianchi;
- ii) Miundombinu hafifu ya maji taka majumbani, hotelini na viwandani kumepelekea utirilishaji wa maji taka ambayo hayajatibiwa na kuingia kwenye maji hususan maji ya mito na maziwa na kusababisha uchavuzi ambao ni hatari kwa mtumiaji wa maji hayo;
- iii) Shughuli za kilimo katika vyanzo vya maji (*Upsteram*). Shughuli hizi zimekuwa zikichangia kukauka kwa vyanzo vya maji hususan mito na chemichemi. Vilevile, mabwawa yamekuwa yakijaa tope zinazosababishwa na shughuli za kilimo pale mvua zinaponyesha na kutiririsha maji yenye tope (*sedments*);

iv) Ukataji miti kiholela katika vyanzo vya maji. Hali hii imekuwa ikisababisha vyanzo vya maji kukauka na hivyo kuongeza kasi ya kupungua kwa maji nchini; na

v) Shughuli za uchimbaji madini. Kuwepo kwa mabwawa ya tope sumu (*Tailling Storage Facility*) kwenye migodi mbalimbali kimekuwa ni chanzo kimojawapo cha uchafuzi wa maji juu na chini ya ardhi kwa kutirisha maji yenyе sumu kwenye vyanzo vya maji.

2.2.2 Uchambuzi wa Azimio la Bunge

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa taarifa, Kamati ilichambua na kujadili Azimio la Bunge lililohusu Bunge kuridhia Itifaki ya Jumuia ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (*East African Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary - (SPS) Measures*) lilliochambuliwa na kujadiliwa na Kamati na hatimaye kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, uchambuzi wa Kamati ulibaini uwepo wa mapungufu ya mifumo ya usimamizi na uwezo mdogo wa Taasisi mbalimbali nchini zinazohusika afya ya mimea, usalama wa chakula na wanyama hivyo Kamati ilishauri kuandaa Mpango Kazi utakaoainisha namna ambavyo Serikali itachuka hatua stahiki kuimarisha Taasisi husika ili ziendane na mabadiliko ya wakati na kukamata fursa zinazoambatana na azimio hilli.

2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mnamo mwezi Machi, 2021, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilifanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo minne (4) inayotekelzwa katika Manispaa ya Morogoro. Miradi iliyokaguliwa ni pamoja na: -

2.2.3.1 Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji Mkoani Morogoro

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikagua mradi wa Ujenzi na ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji unaotekelzwa na Wizara

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji wenyewe lengo la kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ya mpunga, Mahindi, Vitunguu na Nyanya.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhidhishwa kwa kiasi kikubwa na ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji ambapo umewezesha tija kuongezeka kwenye uzalishaji wa Mpunga kutoka tani 1.8 kwa hekta hadi tani 5.0 – 8.0 kwa hekta, Mahindi kutoka tani 1.5 hadi tani **3.7- 5** kwa hekta, Vitunguu kutoka wastani wa tani 13 hadi 26 kwa hekta na Nyanya kutoka wastani wa tani 5 hadi 18 kwa hekta.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umeonyesha sekta ya umwagiliaji endapo itawezeshwa kikamilifu ina fursa kubwa ya kuchangia pato la Taifa na kuhakikisha usalama wa chakula kutokana na uwepo wa ardhi, maji na masoko ya uhakika. Pamoja na fursa kubwa ilyopo kwenye killmo cha umwagiliaji, Kamati imebaini bado nchi yetu hajatumia vizuri fursa hii kutokana na bajeti ndogo inayotengwa pamoja na mtiririko hafifu wa fedha za maendeleo zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo.

Jedwali Na. 2: Mtiririko afifu wa fedha za maendeleo katika kutekeleza miradi ya umwagiliaji nchini

Na	Mwaka	Fedha za Ndani			Fedha za Nje		
		Zilizoidhinishwa	Zilizolewa	Asilimia	Zilizoidhinishwa	Zilizolewa	Asilimia
1	2014/2015	15,000,000,000	0	0%	18,933,020,000	10,659,134,612.50	56%
2	2015/2016	6,000,000,000	0	0%	47,394,574,000	5,131,032,895.00	11%
3	2016/2017	6,000,000,000	2,239,980,000	37%	29,369,529,428	1,101,177,000.00	4%
4	2017/2018	5,600,000,000	1,539,468,298	27%	14,503,412,150	2,468,524,644.66	17%
5	2018/2019	6,000,000,000	0	0%	19,820,458,000	5,365,635,000.00	27%
6	2019/2020	3,000,000,000	950,926,062	32%	29,501,462,613	11,672,553,342.78	40%
		41,600,000,000	4,730,374,360	11%	159,522,456,191	36,298,057,494.94	23%

Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Kilimo kwa Kamati iliyotolewa Tarehe 12 Machi, 2021 kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilikagua mradi wa kuongeza uzalishaji wa mpunga- *Expanded Rice Production Project* ambao ulilenga ujenzi wa maghala matano (5). Kamati iliridhidhishwa na ujenzi wa maghala hayo ambayo yamekamilika na kusaidia kuongeza kipato cha wakulima, utoshelevu wa chakula nchini, kupunguza mfumuko wa bei wa chakula na kupunguza umaskini wa chakula.

2.2.3.2 Miradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Morogoro

Mheshimiwa Spika, mradi wa kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Morogoro inatekelezwa na Wizara ya Maji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) ambayo inahudumia Manispaa ya Morogoro, Mji wa Kilosa na Mji wa Mikumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati illikagua ujenzi wa tanki kubwa la **maji la lita 2,000,000** ambao ulilenga kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi katika maeneo ya viwandani, Kihonda na SGR- Morogoro uliokuwa unatekelezwa kupitia *Force Account* na kukamilika kwa gharama ya **shilingi milioni mia sita (600 Milioni)**, ikilinganishwa na gharama za Mkandarasi ambazo zilikuwa **shilingi bilioni moja na milioni mia mbili (1.2 Bilioni)**.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati imejionea na imeridhishwa na ujenzi wa mradi huu na inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mradi huu kwa muda mfupi (miezi kumi na mbili) na kwa gharama nafuu ambapo Serikali imeokoa **asilimia 50** ya gharama za mradi, fedha ambazo zitatumika kutekeleza miradi mingine katika Manispaa ya Morogoro na kupunguza usumbufu kwa Wananchi wa Manispaa hiyo kutembea umbali mrefu kufuata maji.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Bwawa la Mindu, ambalo ndicho chanzo kikuu cha Maji kwa Manispaa ya Morogoro ambacho kinachangia takribani **asilimia 75** ya maji yote yanayozalishwa hivi sasa. Kamati ilishuhudia jinsi ambavyo Bwawa la Mindu limejaa

tope, Aidha, kujaa tope huku kumepelekea bwawa hili kupoteza uwezo wake kwa takribani **asilimia 40**. Changamoto hii inaweza kukabiliwa kwa kuondoa tope (*dredging*), kuongeza tuta kwa takribani mita 2.5 pamoja na kuzuia shughuli za binadamu zinazoendelea katika uwanda wa juu wa bwawa hilo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kamati ilibaini pamoja na Morogoro kubarikiwa mito mingi inayotiririka maji takribani mwaka mzima, Manispaa ya Morogoro bado ina uhaba wa maji kutokana na uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na mito hiyo kuvamiwa na kusababisha ugumu wa zoezi la uratibu wa maji yanayotakiwa kufika kwenye makingio ya maji kwa ajili ya wananchi wa mijini. Hali hii imesababishwa na uhaba wa fedha unaoikabili MOROWASA na hivyo kushindwa kulinda vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, MOROWASA pia inakabiliwa na uhaba wa fedha za uwekezaji na hivyo kushindwa kukarabati miundombinu chakavu ambayo inapelekea upotevu mkubwa wa maji (*Non Reveue Water*) ambao unafikia **asilimia 40** na hivyo kuongeza gharama za uendeshaji ambazo zinawaathiri wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilibaini huduma ya majitaka inayotolewa na Mamlaka ya Majisafi Morogoro bado haijatekelezwa kwa ufanisi ili kuendana na kasi ya ukuaji wa Manispaa kwani mpaka sasa ni **aslimia 6.3** tu ya wakazi wa Manispaa ndio wameunganishwa kwenye huduma ya majitaka. Hali ya utoaji wa huduma ya maji taka sio tu iko chini kwa Manispaa ya Morogoro pekee, bali kwa Majiji, Miji Mikuu na Manispaa nyingi nchini.

2.2.3.3 Ziara ya Kutembelea Makao Makuu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo (*Agriculrural Seed Agency- ASA*)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Taifa wa Mbegu za Kilimo ulianzishwa kwa lengo la uzalishaji na uendelezaji wa mbegu za kilimo ili kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kuongeza uzalishaji wa mbegu bora zinazofaa kwa kilimo. Kamati ilifanya ziara katika Makao Makuu ya Ofisi za ASA ili

kubaini changamoto zinazoikabili Taasisi hii na kupelekeea uhaba wa mbegu na kuligharimu Taifa fedha nydingi kuagizwa mbegu kutoka nje ya nchi ambazo huuzwa kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini ASA inakabiliwa na changamoto mbalimbali, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na: -

- i) Ukosefu wa fedha za maendeleo na kupelekeea ASA kushindwa kufanya ukarabati wa miundombinu ambayo ni chakavu na kushindwa kufufua mashamba ya mbegu ya Serikali;
- ii) Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kutopatikana kwa wakati na hivyo kuathiri kazi ya uzalishaji wa mbegu ili kuendana na misimu ya kilimo na hivyo kupelekeea mashamba mengi kushindwa kuzalisha kwa tija kwa sababu ya kutegemea mvua badala ya uzalishaji mbegu kwa kutumia umwagiliaji;
- iii) Ukosefu wa Hifadhi ya Mbegu ya Taifa (*Strategic Seed Reserve*) ambapo kwa kawaida nchi inatakiwa kuwa na hifadhi ya mbegu kwa ajili ya kuhifadhi mbegu bora zinazozalishwa na wakala ili kuwa na akiba kama tahadhari iwapo janga lolote linapotokea nchini; na
- iv) Uvamizi wa mashamba ya ASA kwa ajili ya shughuli za kibinadamu kama makazi, shughuli za kilimo pamoja na malisho kwa ajili ya mifugo, hali ambayo husababishwa na Ufinyu wa bajeti na kupelekeea ASA kushindwa kulinda mashamba ya mbegu kama sheria inavyoolekeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukaguzi wa Miradi, Kamati ilipokea na kujadili taarifa Mkakati wa Wakala wa Mbegu katika uzalishaji wa Mbegu za alizeti ambapo ilibainika kuwa Serikali kupitia ASA imeandaa mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za alizeti kufikia Tani 5,000 ifikapo mwaka 2023. Mkakati wa ASA ni kuongeza uzalisha kwa kutumia hekta 2,500 kupitia kilimo cha umwagiliaji Serikali imeanza

kuwekeza miundombinu ya umwagiliaji katika baadhi ya mashamba yake ili kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini mahitaji ya ndani ya mafuta ya kula ni **Tani 570,000**, utekelezaji wa kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za alizeti ukienda sambamba na utumiaji wa teknolojia ya mbegu bora za alizeti utawawezesha wakulima kulima **hekta 625,000** zitakozosalisha kiasi cha **Tani 625,000** za alizeti ghafi ambapo baada ya kuchakatwa itatoa kiasi cha **Tani 262,500** za mafuta ya alizeti.

Aidha, utafiti unaonyesha kuwa endapo uhamasishaji wa matumizi ya mbegu bora za alizeti utafanyika nchi nzima matumizi yataongezeka na kufikia **asilimia 43**. Na kwamba **asilimia 57** iliyobaki itaweza kuzalishwa kwa kutumia mbegu za kawalda ambapo inakadiriwa uzalishaji wa mafuta utakuwa ni **Tani 356,250** na kufanya jumla ya uzalishaji wa mafuta ya alizeti kufikia **Tani 618,750** sawa na ziada ya **Tani 48,750** ya mahitaji. Kamati imeridhishwa na mipango iliyobainishwa kwenye mkakati huu na inaamini utekelezaji wake utasaidia kupunguza/kuondoa kabisa uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia, ilipokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Wakala wa Mbegu kuhusu Mpango wa Bajeti wa kutumia kiasi cha **Tshs 51,486,502,900** kwa ajili ya kuzalisha kiasi cha **Tani 5,000** katika **hekta 2,500** kwa kutumia umwagiliaji ambapo uzalishaji utafanyika kwa misimu miwili (2) kwa mwaka .

Mheshimiwa Spika, Mpango huu pamoja na mambo mengine unalenga kupunguza uhaba wa mafuta ya kula na kupunguza kiasi kikubwa cha fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi pamoja na kushusha bei ya bidhaa hiyo. Vilevile Mpango huu utawezesha kuongeza pato la mkulima na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mpango huu una tija na manufaa kwa Taifa kwani unalenga kuhakikisha nchi

inajitosheleza katika mahitaji ya mbegu na kulipunguzia Taifa gharama za kuagiza mbegu bora kutoka nje ya nchi, Kamati inaishauri Serikali katika mwaka wa Fedha 2022/2023 kuitengea ASA fedha hizo kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Mpango huu.

2.2.3.4 Ziara ya Kukagua Kituo cha Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji Kingolwira – Morogoro

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabia nchi na kuongezeka kwa matumizi ya samaki kutokana na umuhimu wake kwenye afya ya binadamu imepelekea upungufu wa samaki na mazalia yake, hatua hii iliilazimu Serikali kuanzia miaka ya 70 kuweka mkazo kwenye ufugaji wa samaki. Ili ufugaji wa samaki ufanikiwe ni muhimu kuimarisha upatikanaji wa vifanga na huduma za ugani hususan mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea kituo hiki ili kukagua thamani ya fedha iliyotumika kufanya ukarabati, upanuzi ujenzi wa jengo la kitotoleshi na kibanda cha mlinzi kwa ajili ya ukuzaji viumbe maji ili kuongeza wigo wa utoaji huduma za ugani na uzalishaji vifaranga vyta samaki. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Kituo cha Kingolwira, kilitengewa kiasi cha **shilingi 262,360,200.00** kwa ajili ya shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na ujenzi na ukarabati uliofanyika kwa kuwa unalenga kuboresha mazingira ya kazi, kuongeza uzalishaji wa vifaranga na kuimarisha ulinzi wa kituo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongozi hizo, Kamati ilishangazwa na taarifa kuwa Kituo cha Kilongolwira ndio kituo kikubwa cha Taifa cha uzalishaji wa vifaranga huku kikikabiliwa na changamoto ya uchakavu wa majengo, upungufu wa mabwawa ya kufugia samaki, vyombo vyta usafiri na upungufu wa maji ambaa ndio nguzo muhimu katika ufugaji wa samaki.

2.2.4 Semina na Mafunzo

Mheshimiwa Spika, katika Kipindi cha Januari 2021 hadi Januari 2022, Kamati ilipatiwa Semina na Mafunzo kutoka Wizara mbalimbali, Taasisi za Serikali na Sekta binafsi ambazo shughuli zao kwa namna moja au nyingine zinaingiliana na shughuli za kuongeza mnyororo wa thamani kwenye mazao ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na sekta ya maji kwa ajili ya kujengea Kamati uelewa.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya mafunzo yaliyotolewa pamoja na Wizara/Taasisi zilizotoa mafunzo hayo kwa Kamati yamefafanuliwa kwa kina kama ifuatavyo: -

i) **Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (Livestock Training Agency - LITA)**

Mheshimiwa Spika, katika semina hii Kamati ilijifunza majukumu ya LITA ambayo ni pamoja na kuandaa wataalamu (Maafisa Ugani) kwa ajili ya kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji, kuandaa wataalamu kwa ajili ya kufanya kazi kwenye viwanda vinavyosindika mazao yatokanayo na mifugo pamoja na kuzalisha na kutunza rasilimali za mifugo na malisho bora kwa ajili ya kufundishia na kuhudumia jamii ya wafugaji ili kuwa na ufugaji wenye tija.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu huo, Kamati ilibaini LITA inakabiliwa na upungufu na uchakavu wa miundombinu kama madarasa, maktaba na maabara za kufundishia, upungufu wa wakufunzi, ukosefu wa fedha za maendeleo pamoja na kukosekana kwa mikopo ya Serikali na hivyo wanafunzi kushindwa kuhitimu mafunzo kwa kukosa ada.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi zimepelekea upungufu wa maafisa ugani kutoka **Maafisa ugani 17,400** wanaohitajika hadi **3,600 waliopo sasa** hali inayofanya Wafugaji kushindwa kupata elimu ya ufugaji wa kisasa na hatimae kuendelea kufuga kiasili na hivyo mifugo kukosa tija inayohitajika katika soko la ndani na la kimataifa.

ii) **Soko la Bidhaa Tanzania** (*Tanzania Mercantile Exchange - TMX*);

Mheshimiwa Spika, semina kuhusu umuhimu wa soko la bidhaa za kilimo iliandaliwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa lengo la kuiwezesha Kamati kufahamu soko la bidhaa za kilimo linavyofanyika kwa kutumia mfumo wa kielektoniki. Wajumbe walifahamu kuwa wanunuzi wengi wa ndani na nje ya nchi ununua bidhaa kwa njia ya mtandao na hivyo kuwezesha wanunuzi wa bidhaa kufanya manunuzi popote walipo pasipo kulazimika kufika kwenye soko la bidhaa au nchini.

Mheshimiwa Spika, soko la kimtandao linaaminika duniani katika kuweka mpangilio na uwazi katika soko kwa kuwa na utaratibu unaopunguza athari za bei, unaoleta usawa wa bei na kuunganisha moja kwa moja muuzaji na mnunuzi.

Vilevile, taarifa ya Serikali ilieleza kuwa, manufaa yanayopatikana kutokana na Mfumo wa Soko la Bidhaa ni pamoja na: -

- a) Kupanua wigo wa soko la mazao ya wakulima;
- b) Upatikanaji wa malighafi kwa bei zenyе ushindani na uwazi;
- c) Wakulima kuzalisha zaidi na kuongeza ubora wa mazao;
- d) Mauzo ya mazao kuweza kufanyika kwa wakati mmoja kwa nchi nzima na hivyo kuondoa utofauti mkubwa wa bei kwa maeneo;
- e) Kupunguza hasara kwa wakulima inayotokana na kuuza mazao kabla ya kuvuna;
- f) Kupunguza hasara kwa wanunuzi;
- g) Kuimarika kwa takwimu ya mazao yanayouzwa na kununliwa nchini; na
- h) Kurahisisha na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na manufaa hayo ya Soko la Bidhaa, bado mfumo huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

- a) Uelewa mdogo mionganoni mwa wadau kuhusu namna Soko la Bidhaa linavyofanya kazi;
- b) Uzalishaji mdogo kwa baadhi ya mazao;
- c) Ukosefu wa bidhaa zenyenye viwango na ubora wa kimataifa;
- d) Baadhi ya sheria zilizoanzisha Bodii za Mazao, kuzipa Bodii hizo mamlaka ya kuendesha na kusimamia minada;
- e) Uhaba wa ghala zinazokidhi viwango vya kuhifadhia mazao kwa muda mrefu huku yakibaki na ubora unahohitajika; na
- f) Upinzani toka kwa wachuuzi na watu wengine wanaonufaika na mifumo holela iliyopo ya uuzaaji mazao wakihofia kupungua kwa faida au kuondolewa kabisa katika mfumo wa mauzo ya mazao.

iii) **Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (Tanzania Agricultural Development Bank - TADB)**

Mheshimiwa Spika, semina kuhusu Majukumu ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania iliandaliwa na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuiwezesha Kamati kufahamu majukumu ya benki hiyo, mafanikio na changamoto na namna benki hiyo inavyosaidia upatikanaji wa mikopo katika kuhakikisha ukuaji wa sekta ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe walielewa kuwa, TADB ilianzishwa na kupewa jukumu la kuwa benki ya kitaifa ya maendeleo ya kilimo nchini inayojidesha kibia shara na kwa kuzingatia utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya kilimo nchini.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Hivyo riba ya mikopo itolewayo na TADB haina tofauti sana na benki nydingine za biashara. Baadhi ya majukumu makuu ya benki ni pamoja na: -

- a) Kuchagiza utoaji wa mikopo katika sekta ya kilimo na mifugo ili kuchangia katika ukuaji wa sekta hizo;
- b) Kuongoza, kama benki ya kitaifa ya maendeleo ya kilimo, katika kutengeneza mikakati na programu za kujenga uwezo wa kutoa huduma za fedha zinazolenga kuendeleza minyororo ya thamani ya mazao ya kilimo na mifugo;
- c) Kuchangia katika utekelezaji wa programu ya mageuzi ya sekta ya fedha (*Government's Second-Generation Financial Sector Reforms*) na kuendeleza kilimo nchini Tanzania kwa kuzingatia malengo ya kitaifa yaliyoainishwa na mipango mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo (Vision 2025), Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano (FYDPs), Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo (ASDS), na Programu za Maendeleo ya Kilimo (ASDPs);
- d) Kuchagiza utoaji wa huduma za fedha kwa sekta ya kilimo kwa kutoa mikopo ya muda mfupi, muda wa kati, na muda mrefu kwa kupitia benki za biashara, benki za jamii (*community banks*), vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS), na taasisi ndogo-ndogo za fedha (MFIs) zinazotoa mikopo katika sekta ya kilimo; na
- e) Kujenga uwezo wa taasisi zinazotoa huduma za fedha kwa sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na benki za biashara, benki za jamii, vikundi vya kuweka na kukopa (SACCOS), vyama vya msingi na vyama vya ushirika, vikundi vya wakulima wadogo wadogo, makampuni madogo yanayojishughulisha na kilimo nakadhalika.

iv) Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB)

Mheshimiwa Spika, semina kuhusu mfumo wa Stakabadhi Ghalani iliandaliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na ilihusu kuwaelimisha Wajumbe namna mfumo wa stakabadhi

ghalani unavyofanya kazi. Taarifa ya Serikali ilieleza kuwa, mfumo huu unausika na aina ya biashara ambayo bidhaa zinahifadhiwa ndani ya maghala yenye leseni na mamiliki wa bidhaa anapewa risiti zinazothibitisha kuwa hati ya bidhaa zilizowekwa kuwa ni za umiliki mahususi, thamani, aina, idadi na ubora (daraja).

Mheshimiwa Spika, baadhi ya faida za mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni pamoja na kumuwezesha mkulima kuhifadhi mazao yake bila usumbufu huku akisubiri kuuza mazao yake kwa bei nzuri, biashara huweza kufanyika baadae na bila ya kulazimika kuhamisha bidhaa husika kutoka kwenye ghalenye leseni, kurahisisha upatikanaji wa mkopo kwa kupunguza mashaka katika biashara ya kilimo, kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna, kuongeza ubora wa mazao na kuvutia uwekezaji mkubwa katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, madhumuni makuu ya kuanzisha Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni kukuza juhudini za Serikali kufanya kuwa rasmi mifumo ya masoko iliyopo kwa lengo la kupunguza vipingamizi mbalimbali vinavyopelekea uzalishaji usio na tija na utafutaji masoko kwa mazao ya kilimo. Vipingamizi hivyo ni pamoja na hasara baada ya kuvuna, kiwango cha chini cha ubora, mabadiliko ya mara kwa mara ya bei, ukosefu wa taarifa za soko za kuaminika na uhaba wa fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida zilizolezwa hapo juu na dhamira ya Serikali kuanzisha mfumo huu mwaka 2005, Kamati imebaini bado Mfumo wa Stakabadhi za Ghala haufanyi vizuri kutokana na changamoto zifuatazo: -

- a) Uelewa mdogo kuhusu Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unavyofanyakazi;
- b) Uhaba wa ghalanibora za kuhifadhia mazao;
- c) Vyama vya Msingi kukosa elimu na vifaa vya uhakiki wa ubora kabla ya kuingiza ghalani;

- d) Kukosekana/ uwepo wa vifungashio duni na visivyo na ubora unaohitajika;
- e) Kukosekana kwa vipimo sahihi kama mizani; na
- f) Uhaba wa Fedha na vitendea kazi.

v) **Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (Cereals and Other Produce Board of Tanzania - CPB)**

Mheshimiwa Spika, semina kuhusu Muundo na Majukumu ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, mafanikio na changamoto iliandaliwa na Wizara ya Kilimo ambapo ilielezwa kuwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kimsingi imechukua majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na lililokuwa Shirika la Usagaji la Taifa – *National Milling Corporation*- NMC. Na kwamba majukumu ya CPB ni pamoja na kufanya biashara ya nafaka na mazao mengine, kuongeza thamani ya nafaka na mazao mengine na kushirikiana na wadau wengine katika uendelezaji wa nafaka na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2018 CPB ilipoanza kutekeleza majukumu yake, imefanikiwa pamoja na mambo mengine: -

- a) Kujenga vinu vipyta, vihenge na maghala ya kuhifadhiya mazao katika kanda nne;
- b) Kujenge kiwanda cha kusaga na kukoboa mahindi, kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti, kiwanda cha kusindika korosho na ujenzi wa kiwanda cha kukoboa mpunga;
- c) Kurejesha na kufuatilia mali zilizokuwa zinamilikiwa na NMC;
- d) Kuhamasisha na kusajili wakulima 81,480 wanaomiliki ekari 75,802.2 katika Wilaya za Nanyumbu, Newala, Tandahimba na Mtwara vijiji kwa lengo la kuuza mhogo mkavu nchini China ifikapo mwaka 2025; na

e) Kutafuta masoko ya mazao ya wakulima nchi za nje, ambapo hadi sasa masoko ya maharage ya soya yamepatikana nchini Rwanda, Mchele nchini Zimbambwe na Visiwa vya Comoro. Aidha vituo vya kusambaza bidhaa za CPB vimefunguliwa mjini Nairobi, Mombasa, DRC na Juba.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu hayo, CPB imefanikiwa kuongeza uwezo wa kuchakata mazao kutoka **tani 15,000 mwaka 2018** hadi **kufikia tani 146, 400 za sasa** hatua iliyosaidia kuongezeka kwa mtaji kutoka **shilingi bilioni 2** hadi **shilingi bilioni 20** za sasa. Kwa kutambua mafanikio haya, Serikali imetoa kibali kwa CPB kukopa kwenye benki za biashara hatua iliyosaidia CPB kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kutoka **tani 2,200** kwa mwaka hadi tani **200,000**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua kazi nzuri inayofanywa na CPB na kuipatia kibali. Kamati ina amini mkopo utakaopatikana utaiongezea CPB uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja kuwajengea Watumishi ujuzi wa biashara na kufanya ukarabati wa majengo na mitambo chakavu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, CPB inakabiliwa na changamoto za Watumishi kukosa ujuzi wa kibashara, uchakavu wa majengo na mitambo iliyokuwa ya NMC na ukosefu wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kutunza mazao baada ya kuvuna na hivyo kupelekea mazao kukosa ubora unaohitajika ndani na nje ya nchi.

vi) **Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (National Food Reserve Agency - NRFA)**

Mheshimiwa Spika, Cemina kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka iliandaliwa na Wizara ya Kilimo kwa lengo la kuwaelewesha Wajumbe majukumu ya NFRA ambayo ni pamoja na kununua na kuhifadhi chakula kwa ajili ya kukabiliana na upungufu na majanga mbalimbali na uhakika wa nchi kuwa na usalama wa chakula ambapo jukumu hili ili liweze kutekelezwa kwa ufanisi linategemea uwezo wa NFRA kuhifadhi nafaka.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali ilionyesha kuwa, uwezo mdogo wa kuhifadhi pamoja na uchakavu wa miundombinu ya uhifadhi ulipelekea NFRA kuwa na **maghala 34** yenye uwezo wa kuhifadhi **tani 251,000** zinazotosheleza mahitaji ya dharura ya kitaifa ya miezi miwili tu.

Kwa kutambua uwezo huu mdogo, Serikali kupitia Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) uliutaka Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuongeza uwezo wa kuhifadhi chakula kitakachotosheleza mahitaji ya dharura ya kitaifa angalau kwa miezi minne kutoka **Tani 251,000 hadi Tani 501,000** kupitia Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa katika mikoa nane ya Ruvuma, Njombe, Songwe, Rukwa, Katavi, Shinyanga, Manyara na Dodoma kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Poland kwa gharama ya **dola za kimarekani milioni 55**.

Pamoja na kwamba maendeleo ya utekelezaji wa mradi ni ya kuridhisha, hata hivyo mradi unakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

a) Mmoja wa wakandarasi kuvunja mkataba baada ya kukataliwa madai yafuatayo: -

- ✓ Kuomba kuongezewa miezi kumi na mbili kutoka kwenye ongezeko la awali ambalo lilikuwa linaisha Desemba, 2020 kinyume na mkataba;
- ✓ Kuomba kuongezewa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni kumi na mbili kinyume na makubaliano ya mkataba; na
- ✓ Kuomba kupewa kiasi chote cha fedha ambacho kilitengwa katika muda wa matazamio kinyume cha mkataba.

b) Kuchelewa kwa upatikanaji wa vibali vyta ajira za mafundi sanifu wa kuendesha vihenge mara mradi utakapokamilika; na

c) Kuchelewa kwa upatikanaji wa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kutoka Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa mradi huu kwa Taifa, na kwa sababu changamoto zilizoainishwa katika kipengele (a) na (b) ziko ndani ya Serikali, Kamati inaitaka Serikali kushughulikia changamoto hizo mapema iwezekanavyo.

vii) **Baraza la Kilimo Tanzania (Agricultural Council of Tanzania - ACT)**

Mheshimiwa Spika, semina kuhusu umuhimu wa kuendeleza Tasnia ya Alizeti kwa ajili ya kuwezesha Taifa kujitosheleza kwa mafuta ya kula iliandaliwa na Balaza la Kilimo Tanzania.

Mafunzo haya yaliwajengea uwezo Wajumbe kwenye maeneo muhimu yafuatayo: -

a) Mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni katika ya **600,000- 700,000 MT** kwa mwaka, ifikapo mwaka 2025 inakadiriwa mahitaji ya mafuta ya kula yataongezeka na kufikia **750,000 – 800,000 MT** kwa mwaka;

b) Uwezo wa uzalishaji wa ndani wa mafuta ya kula ni **290,000 MT** kwa Mwaka katika ya hizo **247,000 MT** sawa na **asilimia 85** huzalishwa kutokana na alizeti;

c) Pungufu ya mafuta ya kula ambayo ni sawa na **asilimia 55** huagizwa kutoka nje ya nchi na kuigharimu Serikali takribani **Dola za Marekani milioni 300** kwa mwaka;

d) Pamoja na matumizi duni ya teknolojia na upatikanaji usio wa uhakika wa mbegu bora, ukosefu wa viwanda vyenye teknolojia ya kisasa ya kusindika mafuta ya kula, takwimu zinaonyesha Tanzania ni nchi ya pili kuzalisha mafuta ya kula ya alizeti kwa wingi baada ya Afrika Kusini; na

e) Mahitaji ya mafuta ya kula ya alizeti yameongezeka kutokana na umuhimu wake kwa afya hivyo kuiweka nchi

yetu kwenye fursa ya kuzalisha kwa wingi kwa matumizi ya ndani na ziada kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na fursa iliyopo kwenye tasnia ya alizeti, Kamati inaishauri Serikali:

- a) Kuhamasisha mikataba ya uzalishaji, usindikaji na masoko ambapo wasindikaji wakubwa au wananzi wakubwa wanaingia mikataba ya ulimaji (*contract farming*) na wakulima (mtu binafsi, vikundi au vyama vya msingi) na mikataba hiyo inatakiwa kulindwa na sheria;
- b) Wasindikaji wakubwa kuingia mikataba na wasindikaji wadogo (*contract processing*) ambaye anaweza kuwa mtu binafsi, kikundi cha wakulima au AMCOSS ambapo msindikaji mdogo anaweza kusindika na kupata mafuta ghafi na kuyauza kwa msindikaji mkubwa ili kusafishwa kwa viwango vya soko na;
- c) Serikali kuweka mazingira wezeshi na kuhamasisha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa viwanda vya kusindika mafuta ya kula.

viii) **Chuo cha Taifa cha maji**

Mheshimiwa Spika, semina kuhusu Mkakati wa Chuo cha Maji katika kuandaa wataalamu wa kusimamia miradi ya maji iliandaliwa na Wizara ya Maji na illenga kuelimisha Kamati majukumu ya Chuo na umuhimu wake katika kuandaa mafundi mchundo ili kuwezesha miradi ya maji kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo ya kuanzishwa Chuo cha Maji mwaka 1974 ilikuwa ni kutoa mafunzo yaliyolenga katika uzalishaji wa wataalamu wa maji (*Middle Level Human Capital*) ikiwa ni jitihada za Serikali katika kuhakikisha kuwa sekta ya Maji inakuwa na wataalam sahihi, wakutosha na wenye weledi na umahiri unaohitajika kukwamua changamoto za sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwake Chuo cha Taifa cha Maji kimefanikiwa kuzalisha wataalamu wa Maji ambapo Inakadiriwa karibu ya **asilimia 70** ya wataalamu (*Technicians & Engineers*) wa maji nchini wametokana na chuo cha maji kwa njia moja au nyine na bado chuo kimeendelea kuaminika kitaifa na kimataifa. Aidha, Chuo cha Maji katika Mwaka wa Fedha 2020/ 2021 kimefanikiwa kuanzisha Program Mpya za Mafunzo ambazo zitatoa Shahada ya kwanza katika *Engineering Hydrology*, Shahada ya kwanza katika *Hydrogeology and Water Well Drilling*, Shahada ya kwanza katika *Sanitation Engineering*, Shahada ya kwanza katika *Community Development in Water and Sanitation* na Stashahada ya *Sanitation Engineering*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha Chuo cha Taifa cha Maji kinabaki kwenye jukumu la msingi la kuanzishwa kwake kwa kuzalisha mafundi mchundo, kwani uzoefu unaonyesha vyuo kama Mbeya *Technical*, Dar *Technical* na Arusha *Technical* vilivyokuwa vinazalisha mafundi mchundo vilibadilika na kuanza kutoa mafunzo ya vyuo vikuu kutohana na mifumo ya mishahara ambayo ilipekea wahandisi kulipwa mishahara mikubwa kuliko mafundi matokea yake kumekuwa na uhaba mkubwa wa mafundi mchundo nchini.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAPENDEKEZO YA KAMATI

3.1 Kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, kukosekana kwa NAIBU KATIBU MKUU- TAMISEMI anayesimamia sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika ngazi za Serikali za Mitaa kumepelekea kukosekana kwa mfumo bora wa usimamizi na kusababisha sekta hizi kutofanya vizuri kama inavyotarajiwa,

NA KWA KUWA, imethibitika uwepo wa Naibu Katibu Mkuu (Elimu) na Naibu Katibu Mkuu (Afya) – TAMISEMI umesaidia sekta za Elimu na Afya kupata msimamizi na msemaji wa sekta hizi chini ya Katibu Mkuu – TAMISEMI kumeonyesha mafanikio makubwa kwa sekta hizi,

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba,

i) Serikali irudishe nafasi ya Naibu Katibu Mkuu – TAMISEMI atakeye ratibu masuala yote ya sekta za uzalishaji za kilimo, mifugo na uvuvi.

ii) ili kuimarisha usimamizi wa Watumishi walioko katika Sektetarieti za Mikoa na Halmashauri, Wizara za kisekta kwa kushirikiana na TAMISEMI na Ofisi ya Rais Manejimenti ya Utumishi na Utawala Bora ziandae andiko litakalotumika kufanya Marekebisho ya Kanuni za Sheria ya Utumishi za mwaka 2003 ili kuweka vipengele vitakavyoruhusu Makatibu Wakuu wa Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi kuwa mihimili mshiriki wa Mamlaka ya ajira, upangaji wa safu ya Watumishi, Upimaji wa maadili na ufanisi wa kazi na masuala ya nidhamu. Kamati inaamini kwa kufanya hivi, kutawezesha, Wizara za kisekta kupanga safu za Watumishi na kushughulikia masuala ya nidhamu na hivyo kuwezesha uwepo wa usimamizi bora wa Watumishi ndani ya Mfumo wa Ugatuzi.

3.2 Kutengeneza ajira kwa vijana kupitia sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kuongeza uwekezaji kwenye sekta hizi

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, Chama Tawala kimezamiria kutengeneza ajira zisizopungua **8,000,000 (milioni nane)** ifikapo mwaka 2025 kwa kuielekeza Serikali kuchochea ukuaji wa uchumi, hususan katika sekta ya viwanda vinavyotumia malighafi za kilimo, mifugo, na uvuvi. Na kwa kuzingatia ukweli kwamba sekta hizi ndio sekta zinazoajiri Watanzania walio wenjei, Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kutambua hilo zimeandaa mipango mikakati yenye lengo la kuleta mageuzi kwenye sekta husika kwa kuongeza tija na kutengeneza ajira,

NA KWA KUWA, Mipango Mikakati iliyopo inahitaji uwekezaji mkubwa ambao ni vigumu kutekeleza mipango hiyo kuitia Bajeti ya Serikali ambayo inatengwa kidogo na mara nyingi ina ukomo wa bajeti,

HIVYO BASI Bunge linashauri kwamba,

- a) Serikali ione umuhimu wa kuongeza utengaji na upatikanaji wa fedha za bajeti kwa ajili ya kuwezesha sekta hizi za uzalishaji kutekeleza Mipango Mikakati iliyojiwekea;
- b) Serikali kwa kutumia njia za kidiplomasia iwaimize wadau wa maendeleo na sekta binafsi kusaidia kugharamia miradi ya maendeleo kuptia bajeti nje ya mfumo wa Serikali (Off Budget); na
- c) Serikali itafute vyanzo mahusus kwa ajili ya kuziwezesha sekta hizi za uzalishaji, pesa itakayopatikana iwekewe uzio. Aidha, ione umuhimu wa kutoa dhamana kwa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili ziweze kukopa mikopo yenye riba nafuu kwani tahimini ya Kamati imeonyesha kila shilingi moja itakayowekezwa kwenye sekta hizi inaweza kupata faida kati ya shilingi mbili hadi mbili na nusu.

3.3 Kuongeza uzalishaji wenye tija kwa kutumia teknolojia na ubunifu wa kisasa pamoja na matumizi ya mbegu bora

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, wakulima wengi nchini ni wakulima wadogo ambao wameendelea kutegemea zana duni za kilimo, mbegu zisizo na ubora, uhaba wa maafisa ugani na ukosefu wa taarifa sahihi kuhusu afya ya udongo pamoja na kilimo cha kutegemea mvua kumepelekea uzalishaji mdogo usio na tija;

NA KWA KUWA, mafanikio ya uwekezaji uliofanywa kuitia ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji, kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora za mazao ya kilimo, matumizi sahihi ya teknolojia na uwezeshaji wa vitendea kazi kwa Maafisa ugani kumeonyesha mafanikiao katika kilimo;

HIVYO BASI Bunge linashauri kwamba,

- ✓ Serikali iuwezeshe Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji kwani kwa sasa mfuko huu unategemea tozo zinazotokana na skimu za umwagiliaji ambazo si nyingi kiasi cha kuweza kutunisha mfuko huu ili uweze kutekeleza Mpango kabambe wa kuachana na kilimo cha kutegemea mvua;
- ✓ Kuiwezesha ASA kibajeti ili iweze kuendeleza shughuli za ugunduzi na uzalishaji wa mbegu bora ikiwa ni pamoja na kujenga ghala kwa ajili ya matumizi ya hifadhi mbegu ya kitaifa ili kuwa na uhakika wa usalama wa mbegu na usalama wa Taifa kwa ujumla; na
- ✓ Kuwezesha wakulima kutumia teknolojia na mbinu za kisasa pamoja.

**3.4 Kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania
(*Tanzania Agricultural Development Bank - TADB*)**

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, imebainika kuwa kwa muda mrefu sasa, sekta za kilimo mifugo na uvuvi zimeendelea kuwa na changamoto nyingi ambazo kwa kiasi kikubwa zimeendelea kusababisha ufinyu wa tija hasa kwa wakulima wadogo ikiwa ni pamoja na ufinyu wa huduma za ugani, huduma za bima, upatikanaji wa pembejeo na mbinu duni za uzalishaji sambamba na changamoto za miundombinu duni ya uzalishaji, usafirishaji, uchakataji wa mazao na masoko. Pamoja na mambo mengine, changamoto hizi zinazifanya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi zionekane hararishi na hivyo kutopewa kipaumbele na wawekezaji ikiwa ni pamoja na kukosa huduma muhimu za fedha na mitaji,

NA KWA KUWA, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ni Taasisi ya Maendeleo na kwa mujibu wa miongozo ya Benki Kuu, TADB haiuruhusiwi kupokea amana (*deposits*) za muda mfupi (chini ya miaka miwili) ambazo ni chache na zinazopatikana zinakuwa ni gharama kubwa ambazo wakulima wadogo hawawezi kumudu gharama hizo na ili TADB iweze kutimiza malengo ya uanzishwaji wake, benki

inategemea mikopo ya masharti nafuu (*concessional loans*) ili kuweza kujiedesha,

HIVYO BASI Bunge linashauri kwamba,

a) Serikali iiongezee mtaji TADB ili kukuza uwezo wa benki wa kuzihudumia sekta za kilimo, mifugo na uvuvi na kuwa na mchango madhubuti katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III). Kuongezwa kwa mtaji kutaifanya TADB kutatua changamoto ya kushindwa kutoa mikopo kwa miradi mikubwa yenyе mahitaji ya fedha yanayozidi ukomo wa mikopo kwa mteja mmoja yaani '*Single Borrowers' Limit*' ambayo kwa sasa ni **shilingi 15.0 billion**.

b) Serikali isaidie upatikanaji wa mikopo yenyе masharti nafuu kutoka taasisi mbalimbali zinazotoa mikopo yenyе riba nafuu ikiwemo kuridhia mkopo kutoka taasisi ya *French Development Agency (FDA)* kwa kuweka saini wa mkatiba wa mkopo wa gharama nafuu kwa TADB; na

c) Serikali iipatie TADB jukumu la kusimamia fedha za maendeleo zinazoelekezwa kwenye sekta ya kilimo ili kuongeza ufanisi na urejeshwaji pale inapohitajika. Aidha, Kamati inapendekeza fedha hizi zijumuishe fedha za mifuko ikiwemo Mfuko wa Umwagiliaji (*Irrigation Development Fund*) na Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo SMEs (*SME Credit Guarantee Scheme- SCGS*) kwa kuzingatia uzoefu wa TADB katika usimamizi wa mifuko yenyе malengo maalum kutokana na TADB kudhihirisha uwezo mkubwa katika uratibu wa mifuko ya aina hiyo; na

3.5 Mapendekezo ya Kuimarisha Dhana ya Ushirika Nchini

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, historia inathibitisha hakuna Asasi iliyowahi kumiliki au inayomiliki viwanda vikubwa, vya kati na vidogo vidogo katika sekta mbalimbali kama Ushirika, hakuna Asasi shirkishi zilizo katika uzalishaji, uchakataji na utafutaji masoko na kuuza kwa kufikia mafanikio yaliyofikiwa na kiwango cha Vyama vya Ushirika.

Mafanikio ya vyama vyaa ushirika kufanya vizuri hadi kufikia uwezo wa kumiliki viwanda vikubwa, vyaa kati na vidogo Ushirika ni ushirikiano wa hiari wa wanachama unaolenga katika kukidhi mahitaji yao ya kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni na unaomilikiwa na kuendeshwa na wanachama hao kidemokrasia ndani ya taasisi yao ya kibiashara,

NA KWA KWU, imebainika kuwa pamoja na mambo mengine Sera ya Ushirika ya mwaka 2002 na Sheria ya Vyama vyaa Ushirika ya mwaka 2013, na Sheria ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vyaa Ushirika (COASCO) ya mwaka 2005 vimekuwa vikwazo kwa ushirika kufanya vizuri.

HIVYO BASI Bunge linashauri kwamba,

Serikali ilete Bungeni mchakato wa marekebisho ya Sera ya Ushirika ya mwaka 2002 na Sheria ya Vyama vyaa Ushirika ya mwaka 2013, na Sheria ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vyaa Ushirika (COASCO) ya mwaka 2005 kwa kuangalia upya maeneo yafuatayo: -

- a)Vigezo na mifumo ya upatikanaji wa watendaji na Wajumbe wa Bodi za Vyama vyaa Ushirika na Taasisi zinazohusika na uendeshaji na usimamizi wa vyama;
- b) Kuongeza wigo mfumo wa vyama vyaa ushirika ili viweze kushiriki katika uanzishwaji wa viwanda na miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushiriki katika mnyororo wa thamani;
- c) Kuongeza kipengele kitakachompa Mrajis uwezo wa kusimamia au kushauri uendeshaji wa miradi ya pamoja hasa kampuni ambazo vyama vyaa ushirika vina hisa kubwa ili kuzuia matumizi mabaya ya rasilimali;
- d) Kuelekeza ulazima wa elimu na mafunzo endelevu ya ushirika kwa wanachama, watendaji na wajumbe wa bodi za vyama vyaa ushirika na taasisi zinazohusika na ushirika. Aidha, kuna haja ya kuweka na kutekeleza mfumo wa kuandaa manejimenti za vyama vyaa ushirika na taasisi za usimamizi (*Unified Cooperative Management Services*

System) ili kuhakikisha vyama hivyo vinaendeshwa na kusimamiwa na watendaji wenyewe utaalamu wa ushirika;

e) Kuimarishe mfumo wa ukaguzi na kuboresha mfumo wa utekelezaji wa taarifa za ukaguzi pamoja na

f) Wizara kuharakisha mchakato wa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Ushirika.

3.6 Kuongeza Uzalishaji na Usafirishaji wa Mauzo ya Mazao ya Bustani

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, imebainika kuwa, kilimo cha bustani ni moja ya tasnia za kilimo inayokuwa kwa kasi hapa nchini na kuifanya Tanzania kuwa moja kati ya nchi 20 duniani zinazozalisha mazao ya mboga mboga, maua, matunda na viungo kwa wingi na kipelekea kuchangia fedha nyingi za kigeni kwenye pato la Taifa, kuajiri vijana na wanawake wengi. Hata hivyo tasnia hii inakabiliwa na changamoto ya gharama kubwa za usafiri, ukosefu wa vituo vyta kuchakata na kuhifadhi mazao ya bustani na kufungwa kwa muda mrefu kwa mashamba yaliyokuwa yanatumika kuzalisha mazao hayo mkoani Arusha kumesababisha tasnia hii kutofanya vizuri licha ya eneo kubwa na hali ya hewa nzuri inayofaa kwa kilimo ikilinganishwa na nchi zingine;

NA KWA KUWA, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye viwanja vyta ndege vyta kimataifa vyta Julius Nyerere, Kilimnjiaro na Songwe ili kuhamasisha ndege za mizigo za kimataifa kusafirisha bidhaa hizo kwa haraka na kwa gharama nafuu hata hivyo, bado uwekezaji huo haujaleta tija iliyotarajiwa kutokana na kukosekana kwa mkakati wa kuwezesha ndege zinazofuata bidhaa hizo kuwa na mizigo ya kuleta nchini ili kupunguza gharama za kufidia kuja tupu.

HIVYO BASI Bunge linashauri kwamba,

Serikali itekeleze yafuatayo: -

a) Kuanzisha Mamlaka ya kusimamia mazao ya bustani (*Horticulture Development Authority*) ambayo itaratibu

masuala yote ya mazao ya bustani na kuwa kiungo muhimu kati ya Serikali na Sekta binafsi na hivyo kuwezesha sekta hii kuchangia zaidi katika kukuza uchumi, pato la Taifa na ajira;

b) Kushughulikia changamaoto zilizopelekea mashamba ya mazao ya bustani yaliyoko mkoani Arusha kufungwa ikiwa ni pamoja na kutafuta wawekezaji wengine;

c) Serikali iandae Mpango Mkakati wa ujenzi wa vituo vyatukusanya mazao (*collection centres*) na *park houses* na kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Mkakati huo;

d) Wizara ya Kilimo ihakikisha inashirikiana na Mamlaka za viwanja vyatukusanya mazao (*collection centres*) na *park houses* na kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Mkakati huo;

e) Wizara ya Kilimo kwa kutumia Maafisa Ugani iendelee kutoa elimu kuhusu mbinu bora za kilimo ili kuwasaidia wakulima kuzifikia fursa zilizopo za kuuza mazao hayo ndani na nje ya nchi.

3.7 Kuimarisha Upatikanaji wa Malisho na Rasilimali maji kwa ajili na Afya ya Mifugo

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, kukosekana kwa huduma muhimu kwa wafugaji kama chanjo kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mifugo, upungufu wa nyanda za malisho na malisho duni kwa ajili ya chakula cha mifugo na ukosefu wa maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo na hivyo kuathiri sekta ya ufügaji na kupelekeea mifugo mingi kupoteza maisha , kushuka kwa uzalishaji wa nyama yenye ubora na uhaba wa maziwa hali hii imesababisha viwanda vyatukusanya mazao ya mifugo kushindwa kuzalisha kwa tija na hivyo kuongeza umaskini wa kipato kwa wafugaji.

NA KWA KUWA, athari hizi zinatokana na bajeti ndogo ya maendeleo inayotengwa na kutolewa kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya maji (mabwawa/malambo na visima virefu) kwa ajili ya kukabiliana na athari za ukame pamoja na Serikali kushindwa kuendeleza maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho.

HIVYO BASI Bunge linashauri kwamba,

- a) Serikali itoe fedha za Bajeti ya Maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuendeleza sekta ya mifugo ikiwa ni pamoja na kujenga malambo, kuimarisha mashamba ya malisho na kutoa ruzuku kusaidia chanjo ya mifugo;
- b) Serikali iandae utaratibu maalum utakaotumika kwa mifugo kutumia Ranchi za Taifa wakati wa ukame; na
- c) Serikali iruhusu wafugaji kutumia maeneo ya '*baffer zone*' za Hifadhi za Taifa wakati wa ukame kama ambavyo nchi jirani zinafanya.

3.8 Kuimarisha Tasnia ya Ukuzaji Viumbe Maji

Mheshimiwa Spika.

KWA KUWA, mahitaji ya samaki ulimwenguni yameendelea kuongezeka kutohana na umuhimu wake kwenye lishe na afya ya binadamu imepelekea mazao ya samaki kuvuliwa kwa wingi na hivyo kusababisha kuendelea kupungua kwa samaki na mazalia yake na kupelekea Taifa kushindwa kujitosheleza kwa mahitaji ya samaki na hivyo kulazimika kuingiza samaki kutoka nje ya nchi,

NA KWA KUWA, ukuzaji viumbe maji kwenye vizimba, mabwawa, na maziwa unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya samaki na kukabiliana na upungufu wa samaki uliopo, ili kuwa na uhakika wa chakula na lishe. Vilevile, ufugaji wa samaki ni biashara kubwa duniani ambayo ikitumika vizuri itasaidia kukuza uchumi na ustawi wananchi pamoja na kutoa ajira kwa vijana,

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba,

a) Serikali ifanye jitihada za makusudi kwa ajili ya kuongeza uwekezaji na uzalishaji mkubwa wa viumbi maji (ufugaji wa samaki) kwa kutumia fursa iliyopo katika rasilimali za maji zilizopo katika Bahari, Maziwa, Mabwawa, mito na mabonde oevu (*Aquaculture*).

b) Kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa samaki na vyakula nya samaki;

c) Kuimarisha huduma za ugani kwa kuwapatia maafisa ugani utaalamu wa ukuzaji wa viumbi maji kwani wananchi wamehamasika kufuga samaki kwenye vizimba lakini hakuna wataalamu wa kutosha kuwasaidia mbinu bora za ufugaji.

**3.9 Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya athari za Uviko 19
Mheshimiwa Spika,**

KWA KUWA, fedha maalum za Mpango wa Maendelo kwa Ustawi Taifa na Mapambano dhidi ya athari za UVICO 19 Sh. trillioni 1.3 zimeelekezwa kusaidia huduma za jamii na mafanikio ya fedha hizo tumeyaona,

NA KWA KUWA, sekta za uzalishaji za Kilimo, Mifugo na Uvuvi zimeathirika pia na athari za maradhi haya; ambapo kwa upande wa sekta ya kilimo (mazao) kumekuwa na ongezeko kubwa la bei ya mbolea, sekta ya uvuvi imeathirika kutokana na meli za uvuvi wa bahahari kuu kuounguza safari zake kutokana na janga la kovid 19 na sekta ya mifugo kuititia viwanda nya kusindika na kuchakata kushindwa kusafirisha nyama nchi za nje na hivyo kushuka kwa mapato yatokanayo na fedha za kigeni.

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba, Serikali iangalie uwezekano wa kuzipatia sekta hizi kiasi cha fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya athari za Uviko 19 ili ziweze kusaidia kupunguza madhara yalioambatana na maradhi haya

3.10 Kuendelea kuimarisha Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, maji ni msingi wa uhai wa binadamu na injini ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Upatikanaji wa uhakika wa huduma ya majisafi na salama na usafi wa mazingira huchangia katika kuzuia magonjwa na hivyo kuimarisha na kuboresha maisha ya wananchi,

NA KWA KUWA, mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la idadi ya watu pamoja na shughuli za binadamu kumepelekeea kasi ya uharibifu wa vyanzo vya maji na kuashiria kupungua kwa kiasi cha maji kwenye vyanzo vya maji vilivyopo nchini,

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba,

a) Serikali katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 itenye bajeti na kuanza kutekeleza miradi ya ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda, Farkwa na Ndembera kwa lengo la kuimarisha uwezo wa nchi kuhifadhi maji;

b) Kushirikiana na sekta binafsi kuweka mfumo wa kuvuna maji ya mvua katika maeneo yote nchini, ili kuhakikisha kuwa maji ya mvua hayapotei bure na badala yake yanahifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu, kilimo cha umwagiliaji na kunyweshea wanyama;

c) Kukamilisha miradi mikubwa ya maji inayoendelea nchini kote na kuhakikisha vijiji vyote vilivyopo kando kando ya miradi hiyo mikubwa vinanufaika na miradi inayopita kwenye vijiji vyao;

d) Kuanza kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi;

e) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya maji pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji; na

f) Kuendelea kujenga na kuimarisha huduma ya majitaka ambayo ufanisi wake bado ni wa kiwango cha chini.

3.11 Usimamizi Endelevu wa Miradi mbalimbali nchini kwa ukuzaji vipaji, ubunifu na funndi

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA, imebainika vyuo vingi nya ufundi vilivyokuwa vikizalisha mafundi mchundo viliachana na malengo ya kuanzishwa kwake na kuwa Vyuo Vikuu kwa sababu ya tofauti ya mfumo wa mishahara kati ya waandishi (*graduate*) na mafundi mchundo (*technician*), ambapo *graduate* anaanza kazi na mshahara mkubwa kuliko *technician* mwenye uzoefu wa muda mrefu kazini,

NA KWA KUWA, vyuo nya ufundi vilivyoanzishwa chini ya Wizara mama kwa lengo la kusaldia sekta husika, vikisha kuwa vyuo vikuu vinatoka kwenye usimamizi wa Wizara mama na kuwa chini ya Wizara ya Elimu. Mfumo huu wa kubadilisha mahitaji ya vyuo umeua ufundi nchini na kupelekeea miradi mingi ya maendeleo kukosa usimamizi endelevu licha ya miradi hiyo kujengwa kwa gharama kubwa,

HIVYO BASI Bunge linashauri kwamba,

a) Balaza la Taifa la Elimu ya Ufundti Tanzania (*The National Council for a Technical Education - NACTE*) kutathimi maboresho yaliyofanyika ili kuona umuhimu wa kurudisha malengo yaliyoanzisha vyuo nya ufundi kama Mbeya *Technical*, Dar *Technichenical*, Arusha *Technical* na Chuo cha Maji n.k; na

b) Ofisi ya Rais Manejimenti ya Utumishi kupitia Idara ya Bodii ya Mishahara ma ishirikiane kwa karibu zaidi na Wizara ya Elimu na Balaza la Taifa la Elimu ya Ufundti ili kutahimini upya upangaji wa madaraja na ngazi za mishahara kulingana na elimu na uzoefu kazini na aina ya kazi kwa lengo la kuhakikisha kila mwajiriwa analipwa ujira wake kwa kadri inavyofaa na kustahilli.

3.12 Utekelezaji wa Mipango ya Pamoja ya Muda Mrefu ya Serikali

Mheshimiwa Spika,

KWA KUWA; katika utekelezaji wa mjukumu yake, Kamati imebaini kuwa kwa kuwa nchi yetu bado changa kiuchumi inahitaji kuwa na Tume ya Taifa ya Mipango, kwa sababu kukosekana kwa Tume hii kumepelekea kukosekana kwa uratibu mzuri na uendelevu wa miradi inayoibuliwa na sekta husika kutokana na yanapotokea mabadiliko ya uongozi kila kiongozi kuanza kutekeleza upya mipango mingine na mipango ya Taifa kukosa ufanisi,

NA KWA KUWA, uzoefu unaonyesha huko nyuma nchi yetu iliwahi kuwa na Tume ya Taifa ya Mipango ambapo sekta zote zililazimika kupeleka mipango yake kwenye Tume na kusaldia upangajji na utekelzaji wa bajeti ya nchi kuelekezwa kwenye mipango iliyowekwa na Tume;

HIVYO BASI, Bunge linashauri kwamba,

Serikali ione umuhimu wa kurudisha Tume ya Taifa ya Mipango na kuifanya kuwa Taasisi inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais na kuiwezesha kifedha pamoja na kuipatia wataalamu wa kutosha ili iweze kupanga mipango madhibuti ya maendeleo ya nchi kwa niaba ya Serikali.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wetu mpewda Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia Wizara ya Maji Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO – 19 kiasi cha **Shilingi 139,354,573,798.37** sawa na **asilimia 10.6** ya fedha zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) takriban **Shilingi Triliioni 1.31.**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa namna ya kipekee napenda kukupongeza Mhe. Dr Tulia Akson (Mb) kwa

kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nawashukuru Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano mlioipatia Kamati kwa kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri wote na Watendaji Wakuu wote wa Wizara na Taasisi ambazo Kamati inazisimamia kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka Mmoja Uliopita. Shukrani za Pekee ziwaendee aliyekuwa Waziri wa Kilimo Prof. Aldoph Mkenda, Waziri wa Kilimo, Mhe.Ndg. Hussein Bashe, (Mb), Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Antony Mavunde (Mb) Naibu Waziri Wizara ya Maji Mhe.Mhandisi MaryPrisca Mahundi (Mb), na Naibu Waziri Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdallah Ulega, (Mb).

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji Wakuu wote wa Wizara hizi kwa ushirikiano wao mkubwa waliooutoa wakati walipohitajika kufika mbele ya Kamati kwa ajili ya kujibu hoja mbalimbali zilizohitaji majibu ya Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya Kilimo, Mlfugo, Uvuvi na Maji.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kutambua mchango wa Wadau na Taasisi ambazo zimeshirikiana na Kamati wakati wa kutekeleza Majukumu katika kipindi cha Januari 2021 hadi Januari 2022.

Kwa uchache naomba kuwataja Wadau wafuatao: -

- a) Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA);
- b) Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU);
- c) Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB);
- d) Agricultural Concil of Tanzania(*ACT*);
- e) Mamlaka ya Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro (*KADCO*);
- f) *Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)*;
- g) *Tanznia Horticultural Association (TAHA)*;
- h) *Research, Community and Organizational Development Associates (RECODA)*;
- i) *Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)*;

- j) *Agricultural Sector Policy and Institutional Reform Strengthening* (ASPIRES); na
- K) *Agriculture Non – State Actors Forum* (ANSAF)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kufanya kazi nzuri na kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati ya kuisimamia na kuishauri Serikali. **Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD) kama ifuatavyo:** -

1. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb – **Makamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb- Mjumbe
5. Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Kakurwa Ali, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Charles John Mwijage, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Furaha Ntengo Matondo Mb - Mjumbe
8. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Mohamed Suleiman Omar, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Benaya Liuka Kapringa,, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Michael Mwita Kembaki , Mb - Mjumbe
12. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Prof. SHukrani Elisha Manya, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb – Mjumbe
22. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb – Mjumbe
23. Mhe. Dkt. Rita Enespher Kabati, Mb – Mjumbe
24. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb – Mjumbe
25. Mhe. Yahya Ali Khamis, Mb – Mjumbe
26. Mhe. Christopher Ole Sendeka, Mb - Mjumbe
27. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb - Mjumbe

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretariati yote ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, chini ya Uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Muhambi Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Msigwe Bisile na Ndg. Gerald Magili, Makatibu wa Kamati Ndg. Rachel Nyega na Ndg. Eunike Shirima na Msaidizi wa Kamati Ndugu Mohamed Kizingiti, kwa umakini na weledi wao katika kufanikisha kazi za Kamati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina Shughuli zilizotekelezwa na Kamati, Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa shughuli hizo, Maoni na Mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu shughuli ilizozitekeleza kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Januari, 2022 pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Dkt.Christine Gabriel Ishengoma, Mb
**MWENYEKITI - KAMATI YA KUDUMU
YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**

11 FEBRUARI, 2022

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mwenyekiti kwa maoni na mapendekezo hayo yaliyotolewa hapa.

MATOKEO YA UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na utaratibu wetu nimepata hapa matokeo kwa hiyo, ngoja niyatangaze kwanza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, tumefanya uchaguzi wa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kama nilivyokuwa nimesema wakati tukianza zoezi la kupiga kura kulikuwa na Wabunge 280, baadaye wakaongezeka wakati wa zoezi la kupiga kura baada ya kuwa wameshapigwa kengele huko nje wakafika idadi ya 301. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kura zilizopigwa ni kura 301, kura zilizoharibika ni kura mbili, halafu katika fomu hii kwa sababu tulikuwa na mgombe mmoja Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu idadi ya kura zilizosema ndiyo ni kura 296. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kura 296 na idadi ya kura zilizosema hapana ni kura tatu, asilimia ya hizo kura 296 kati ya kura 301 ni asilimia 98.33. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, fomu hii imesainiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate na pia Katibu wetu wa Bunge ambaye ndiye alikuwa msimamizi wa uchaguzi huu. Kwa hiyo, kwa sababu tuna zoezi linaendelea hapa mbele, tuwe na utulivu kidogo. Katibu!

NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:

KIAPO CHA NAIBU SPIKA

SPIKA: Kiapo cha Naibu Spika, nimuite Mheshimiwa Zungu ajongee hapa mbele kwa ajili ya kiapo.

Mhe. Mussa Azzan Zungu

*Hapa (Mhe. Mussa A. Zungu – Naibu Spika) Aliapa Kiapo
cha Naibu Spika*

SPIKA: Haya ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Sasa Mheshimiwa Zungu badala ya kuelekea kwenye kitu chake, atakuja hapa kuanza kazi mara moja. (*Makofi/Vigelegelgele*)

Sawa sasa kabla Mheshimiwa Naibu Spika hajaja kunipokea kazi hii, nichukue nafasi hii kwa niaba yenu wote Waheshimiwa Wabunge kumpongeza sana, sana, sana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa ushindi wa kishindo wa kuwa msaidizi wangu kwa maana ya Naibu Spika. Nampongeza kwa sababu kwa kweli yale makofi yaliyokuwa yanapigwa wakati akija hapa mbele, yameonekana dhahiri kwenye kura nyingi sana mlizompa. Inaonesha namna ambavyo mmemkubali lakini pia mmekubali awe msaidizi wangu. Kwa hiyo na mimi pia nawashukuru sana kwa kura nyingi mlizompa Mheshimiwa Zungu. (*Makofi/Vigelegele*)

Atapata fursa ya kuwashukuru atakapokuja hapa ye ye mwenyewe, lakini wakati anajiandaa kuja kumalizia shughuli za siku ya leo, nilete matangazo kwenu ambayo hatukutangaza wakati ule.

Kwanza, ni tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira anawakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote siku ya kesho kwenda kwenye uzinduzi wa sera mpya ya mazingira ya mwaka 2021. Zoezi hili litafanyika saa 2.30 asubuhi viwanja vya *Nyerere Square*. Kwa hiyo, mnakaribishwa sana muende hapo bila kukosa. Anawaomba sana, sana msikose.

Lakini tangazo lingine mtakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii iandae semina kwa ajili ya Wabunge, kwa ajili ya jambo lile la taarifa za kule Ngorongoro ili tupate uelewa wa pamoja. Semina hii itakuwa siku ya kesho kuanzia saa 4.00 asubuhi Ukumbi wa Msekwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria kwa sababu mtajifunza mengi kuhusu yale yaliyokuwa, yanajadiliwa hapa ndani hata wale amba hamjapata fursa ya kufika huko. Kwa hiyo, mnaombwa sana kufanya hivyo na kwa sababu nilishatangaza tangazo la wanawake nadhani kuhusu eneo la kufanya mkutano watafanya makubaliano. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Baada ya kusema hayo sasa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu anakuja kunipokea. (*Makofi*)

Hapa (Mhe. Mussa A. Zungu – Naibu Spika) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kuwashukuru, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu mwiningi wa rehema, namshukuru Mwenyekiti wangu wa Chama cha Mapinduzi Taifa Rais wetu Mama Samia. (*Makofi*)

Nawashukuru Wajumbe wa Kamati Kuu, nawashukuru Wajumbe wa *Caucus* ya CCM na nashukuru *august house* hii, Wabunge wote ambao wamenipa *support* ya kutosha. Kazi sio ndogo ya uchaguzi, niwaahidi kushirikiana na ninyi kufanya kazi na ninyi, kuleta mustakabali mkubwa kujenga Taifa letu. (*Makofi*)

Uchaguzi wa mwaka 2025 *is just around the corner*. Siasa zikishatoka kwenye uchaguzi zinarudi Bungeni na Bungeni ni kushirikiana na miradi ya Serikali, kuhakikisha fedha inazotoa Serikali zinasimamiwa vizuri kwenye Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Niwapongeze Wabunge wote walioshiriki kwenye kujenga madarasa na kuweka heshima kubwa sana ya Taifa letu, kuwaingiza watoto 15,000 kwa mpigo kwenye kidato cha kwanza. Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri iliyofanywa na Mawaziri wako. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye na ye ye alikwenda kusaidiana na Mheshimiwa Rais kutafuta fedha. (*Makofi*)

Kwa hiyo, baada ya hapa sasa ni jaza ujazwe, tunakaa. Katibu! (*Makofi/Kicheko*)

Kwa dakika tano, tano tunaanza na Profesa Sospeter Muhongo jiandae Cecil Mwambe, jiandae Shukurani Manya.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikupatie pongezi nydingi sana na nikutakie kila la kheri kwenye nafasi yako ya Naibu Spika.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nichukue *point* moja tu ya kusisitiza kutoka kwenye Kamati yetu ya Kilimo. Kamati imetoa mapendekezo mazuri mno na yameandikwa vizuri mno, kwa dakika tano hizi naongelea kitu kimoja tu na ni kuishauri Serikali irudishe tena Tume ya Mipango na nitatoa sababu hapa kwa nini Tume ya Mipango ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Tume ya Mipango (*Planning Commission*) ipo chini ya Wizara ya Fedha ndiyo maana inaitwa Wizara ya Fedha na Mipango, lakini inakuwa ni kama Idara, sasa kama ni Idara ndani ya Wizara haina mtizamo wa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano wa Mkoa wa Mara kwa nini Tume ya Taifa inahitajika. Mkoa wa Mara viwanja vya ndege kuna kiwanja cha Musoma Mjini, mimi nimezaliwa pale Mjini, kiwanja nimekikuta wanakikarabati sasa hivi, kabla ya Baba wa Taifa hajastaafu kuna eneo limetengwa kabisa Nyasurura, Musoma Vijijini ilikuwa itengenezwe *airport* kubwa ambayo ingehudumia hata sehemu zingine za Afrika Mashariki na nje, kwenye Ilani ya Uchaguzi kiwanja hicho kimo, juzi sisi tumekabidhi Bodi ya Viwanja kwamba jamani chukueni kiwanja mjenge.

Kwa hiyo, Musoma Mjini tuna kiwanja, toka enzi ya Mwalimu tumekuwa na kiwanja kingine kikubwa, nadhani mmesikia Serengeti Mugumu na wao wanataka kuwana kiwanja, sasa kipi ni bora katika hivi vitatu ndani ya Mkoa mmoja?

Mheshimiwa Naibu Spika, inamaanisha tunaopanga hatuna picha kubwa ya Kitaifa. Unachukua Mkoa jirani wa Simiyu na wenyewe wanataka kiwanja, Mwanza kuna kiwanja, ndiyo maana *Planning Commission* ingekuwepo vitu kama hivi vingeliweza kushughulikiwa kwenye picha kubwa ya kitaifa umuhimu wa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa pili ni ujenzi wa barabara; tumeshauri *TANROADS*, huu mpangilio wa sasa wa kilometra tano/tano, Waheshimiwa Wabunge kila mtu ana

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

furaha ana mradi wa barabara lakini kila mtu ajiulize utaisha lini? Mimi nina barabara ya kilometra 92 karibu kilometra 100, wamepewa kilomita tano, kwa hiyo muda mfupi kabisa kama pesa zinatakiwa kutoka ni miaka 20, lakini *Planning Commission* ingekuwepo ingeona ni barabara zipi ambazo ni muhimu kiuchumi badala ya kujenga kilometra tano/tano labda wangkuwa wanajenga angalau kilometra hamsini kwa mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni mambo ya umwagiliaji; tunaongea kila mbunge hapa ana *scheme* yake lakini uwezo wetu wa kifedha hatuwezi kuwa na *irrigation scheme* kila Mkoa, kila Wilaya, hatuna ubavu huo wa fedha. Kwa hiyo, *Planning Commission* ingekaa ikaona ni yupi na wapi tuwekeze zaidi tuweze kuanzisha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo, ukija kwenye ujenzi wa mambo ya vyuo vya *VETA*, kama nini Mbunge wa Musoma Vijijiini sihitaji *VETA* ya kufundisha watu kutengeneza magari, ninahitaji *VETA* ya watu wa mifugo, kilimo na uvuvi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshiiwa Profesa Muhongo.

MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja muda ungepatikana ningewaeleza zaidi. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mwambe, ajiandae Shukrani Manya.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nikupongeze kama mchangiaji aliyejita, na nimekuwa mtu wa pili kupata nafasi ya kuchangia toka uwe Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo ninataka nikukumbushe wewe mwenyewe kwa sababu tulikuwa kwenye Kamati moja na ulihudhuria kikao.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kumetokea malalamiko mengi sana kwenye suala la *inflation*. Nitatoa mfano mfupi nasi kwenye Kamati tulijadili, kwa mfano sasa hivi tumekuwa tukiongea kuhusu *inflation* kwenye nondo, kwenye sementi na vifaa vingine vya ujenzi. *Examination gloves* zimepanda kutoka shilingi 5,000 mpaka shilingi 18,000; *paracetamol tablets* kichupa chenye kukaa dawa 1,000 kimepanda kutoka shilingi 7,000 mpaka shilingi 22,000; *Vitamin B Complex* imepanda kutoka shilingi 5,000 mpaka shilingi 32,000. Naomba karatasi hizi nimpatie Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu yupo hapa meza yako impatie ili waweweze kufanya kazi waone namna ya kuwasaidia wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninataka niliseme hapa leo ni suala kubwa sana ambalo Kamati ya Viwanda na Biashara pia kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti tulileta pamoja mbele ya Mheshimiwa Spika aliyepita illkuwa ni suala la *ETS*. Kwa masikitiko makubwa sana na kwa kutaka kuwasaidia Watanzania na sisi wenyewe kama Bunge, Bunge lako limedharauliwa nasi kama Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara hatujaridhika, Serikali iliendelea mbele, wameingia mkataba na Kampuni ya *SICPA* tofauti na ushauri uliotolewa kwenye Kamati zile na hivi sasa wananchi wamekuwa kwenye sintofahamu kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za uendeshaji wa kampuni hii unazifahamu, katika akili ya kawaida kabisa kwa mfano, wakati huo walikuwa wanatoza mvinyo dola 20, sawa na shilingi 47,700 hata hivyo wanasema wamepunguza kutoka hiyo na sasa hivi wanatoza shilingi 42,000 wao ndiyo wanaliita punguzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna kampuni ambazo zinaweza zikatoa huduma hiyo hiyo kwa shilingi mbili kwa maana ya dola sawa na shilingi 4,600 ndiyo maana ninakiomba Kiti chako kitoe maelekezo mahsus kabisila ili tuweze kukaa sisi kama Wabunge tujadili jambo hili katika hatua ya dharura, tuweze kuwasaidia wananchi. Haiwezekani mtu mwenye akili ya kawaida aache kupata huduma kwa shilingi 4,600 ang'ang'anie kwenda kupata

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

huduma ya shilingi 42,000; nini tunaficha nyuma ya mkataba wa *SICPA* na *TRA* na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, karatasi ninazo hapa naomba na wewe uzipitie uone kama ninachokisema ni halali na kama hiki ninachokisema ninasingizia nitaomba Bunge lako liniwajibishe kwa sababu tunataka kuwasaidia wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya kuwa na kampuni hii ilikuwa ni kutaka kuisaidia Serikali kufanya mahesabu ili *TRA* waweze kutoza kodi stahiki, lakini matokeo yake mzigo huu wote unahamishiwa kwa wanunuzi. Hakuna kitu chochote kinachopatikana kwa Serikali. Nilitoa mfano hapa Bungeni nikasema katika shilingi kumi ambayo inatozwa na mkandarasi anayefanya kazi ya kuhesabu, lakini mkandarasi huyu anailipa Serikali shillingi moja na senti nane kiasi kingine chote cha pesa kinachobakia kinakwenda kwake mwenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba uelekeze, Bunge hili linadharauliwa sasa hivi, Kamati yetu ya Viwanda na Biashara imedhauriwa kwa sababu tulitoa ushauri mzuri kwa Serikali hata hivyo *TRA* wameendelea kuingia mkataba huu, tunataka tufahamu kama Kamati ni nani yupo nyuma ya mkataba *SICPA* na *TRA*. Kwa nini tuwapelekee wananchi mzigo mkubwa badala ya kuacha hili jambo likafanyika kama ambavyo Bunge tulishauri. Akili ya kawaida kabisa haiwezi kukubali; unakataa shilingi 4,600 unakimbilia shilingi 42,000 kwa manufaa ya nani? Nchi hii haipati shilingi moja kwa mkataba huu zaidi ya kodi inayotozwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, walichokifanya sasa hivi wametumia ujanja karatasi zipo hapa za *TRA*, wameacha kutoza kwa dola wame-*convert* zile pesa kwa shilingi halafu zinakwenda bado kutozwa na gharama hizi wale waendeshaji wanazileta tena kwa mlaji ambaye ni mwananchi wa kawaida na ndiyo sababu sasa bidhaa nyingi zinaweza kupata bei kwa sababu mwisho wa siku tozo hizi zinarudi kule. Sukari imepanda bei, chai kwa maana ya *juice*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

imepanda bei, soda zimepanda bei huko mtaani kwa sababu kubwa hizi na wenyewe walikuwa wakizileta kila mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeanza kuongea hili jambo kwa muda mrefu sana nataka sasa nitoe na mimi unisaidie kabisa, kuona kwa nini Serikali inataka kutuficha, nani yupo nyuma ya mkataba wa *SICPA* na *TRA*, kwa nini gharama hizi kubwa tunakwenda kuwahamishia wananchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba karatasi hizi zikufikie hapo, busara ikuongoze, uende kutusaidia na tunakuomba uje kwenye Kamati yetu ikikupendeza tutakueleza mengi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hiyo. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Shukran Manya, ajiandae Mheshimiwa Ezra Chiwelesa.

MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kushika wadhifa huo na nikutakie kila la kheri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji napenda kujikita katika hoja ambayo inazungumzia dhana ya muunganiko pamoja na mwendelezo katika utoaji huduma ili kukuza uchumi. Luga rahisi ni *connectivity and linkages*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ndogo hiyo ya kilimo ya mazao ya bustani, maua, mbogamboga pamoja na matunda; kwanza ni sekta ambayo inakua kwa kasi, imeonekana ikikua kwa asilimia saba kulinganisha na kilimo chote kwa ujumla kikukua kwa asilimia nne, pia kinachotoa ajira nyingi kwa Watanzania na sasa inakadiriwa kwamba *at least* Watanzania milioni 6.5 katika mnyororo mzima wanashughulika na sekta hiyo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuweka mkazo kwamba sekta hii ndogo ya maua, mbogamboga pamoja na matunda ni sekta ambayo ni *logistic sensitive*. Ninasema hivi kwa sababu tunahitaji usafirishaji kutoka kwa wazalishaji lakini je, ni wote katika mnyororo ule wanajua kwamba tuna-deal na *perishable goods*? Je, askari wetu barabarani wanajua kwamba hili ni kontena la maparachichi ambayo yanapaswa yafikie soko mapema? Je, tunapofika kwenye *ports* kuna *handling facilities* ambazo zitasaidia kutoza mapema kwa ajili ya bidhaa hizi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unagundua kwamba kama hii ni *emerging market* kwa sasa, lakini je, watu wote katika mnyororo mzima unaotaka tutoe kutoka uzalishaji kufikisha bidhaa yetu sokoni ikiwa katika hali njema wana ufahamu huo? Je, pale Mamlaka ya Bandari tutachukua siku chache kullko msafirishaji wa *copper* kwa sababu hizi ni *perishable goods*? Je, ufahamu huo upo? Je, kuna *facilities* za ku-handle kwa sababu hiki ni kitu ambacho kinahitaji uharaka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tunahitaji kuwa na *connectivity* katika sekta hii kwa sababu tusipofanya hivyo tutagundua kwamba tija yake inaweza isionekane mapema na ndiyo maana huenda hata takwimu za nini tunapeleka nje ya nchi kutoka kwenye hii sekta ndogo imesababishwa na kutokuwa na *facilities*, lakini wakati mwingine pia kutokuwa na wadau wote kuhusishwa ili tuweze kufikia malengo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo ninapenda kuiomba Serikali pamoja na Wizara husika kwamba tunapokuwa na kitu ambacho ni *emerging market* kama hii hapa ili tuweze kupata tija maana yake ni kwamba lazima tuwahusishe wadau wote wanaohusika, kwanza kuwapa elimu hiyo, lakini pia kuwapa tahadhari kwamba hebu tusifanye yale mazoea, maana yake ni kwamba tusije tukawa tunachelewesha bidhaa zetu hatimaye zikaoza au zikaharibika ubora kwa sababu tu watu fulani anadhani kwamba anapaswa kwenda kama ambavyo nafanya bidhaa nyingine.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii mara nyinge imetokea katika bandari zetu, lakini pia katika *airports* zetu japo ni kweli kwamba kuna *improvement* sana kuwepo na *standard cold rooms* katika *airport* zetu kwa ajili hiyo, nadhani kwamba bado kunahitaji kuwa na *sensitivity* juu ya jambo hili ili tuweze kupata tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu naelewa dakika zangu siyo nyingi niliamua niongelee jambo hili tu kwamba hebu sasa Serikali kwa maana ya Wizara ya Kilimo ijue kwamba wateja wake ni wengi sana, iwape elimu, iwape msukumo ili kwa pamoja kusiwe na vikwazo katika kufikia soko ambalo tunalihitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuliweka mkazo juu ya yale mashamba ya Arusha ambayo hayafanyi kazi kwa sasa, Serikali ifikie kuleta suluhisho la jambo hilo ili tuweze kupata tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Sasa nimuite *Engineer Ezra*, ajiandae Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi nichukue nafasi hii kukupongeza sawa na watangulizi waliopita kwa nafasi hii muhimu na nyeti katika Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nijikite kwenye suala la Liganga na Mchuchuma maana ni jambo ambalo limekuwa kizunguzungu kwenye Kamati yetu, tunaona tangu tumeingia ni hadithi zimekuwa nyingi, sasa nikasema nijaribu kufanya utafiti wangu kidogo ili njue ni nini kinakwamisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi ya kimkakati ambayo imetajwa katika mpango wetu wa mwaka huu 2021/2022 ambao uliwasilishwa mwezi Machi, 2021 mionganoni mwa miradi muhimu ambayo ilitajwa ilikuwa ni mradi wa Liganga

na Mchuchuma, lakini mpaka leo ni miezi sita imepita, tunategemea kupokea mpango mwingine mwezi wa Machi mwaka huu lakini ninachosema ni kwamba hatuna kilichofanyika mpaka sasa, siyo pesa ni hadithi tu vitu vyote vimebaki kama vilivyokuwa vimewasilishwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tujaribu kujikita kuona tatizo ni nini, maana huu mgodi umeongelewa kwa muda mrefu na ni mgodi wenyewe manufaa sana katika nchi hii lakini hakuna ambacho kinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuangalia hii kampuni ya Sichuan Hongda ambayo ndiyo mkandarasi, nimejaribu kufuatilia nikajua hawa watu wanachokwama ni nini. Katika ripoti ambayo tumepewa na *NDC* inaonekana hata teknolojia yenyewe ya kuchenjua madini haya kwa sababu madini ya chuma yapo na *vanadium*, yapo na *titanium*, teknolojia yenyewe kaja nayo huyu Mkandarasi ambaye tumepewa. Kwa hiyo kwa upande mkubwa hata Taifa hatukuwa tumejiandaa kwa sababu hatukujua hata uchenjuaji hata hiyo *process itafanyika* vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuangalia zaidi, huyu Sichuan Hongda anachokifanya ana-deal/na *Zinc, Zinc Oxide products* ana-deal/na mbolea na vitu vingine, *he has never done any product on ferrous metal* kabisa! Anavyo-deal/navyo ni *non-ferrous metal*, ambapo tutakuta *titanium*, tutakuta na *vanadium* lakini chuma ambayo ndiyo *product* hakuna *profile* inayoonesha kwamba huyu mtu amefanya. Sasa huenda anashindwa kuendelea na huu mradi kwa sababu uwezo hana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ambao ninataka tuende nao, *process hii as a chemistry process* ambayo ni ya kawaida kabisa maana kuna *study* zimefanyika, wenzetu *South Africa* wanachimba chuma, Egypt wanachimba chuma, Libya wanachimba chuma, hizi ni nchi ambazo tumekuwa na ushirikiano nazo mkubwa, tungeweza hata kwenda kujifunza tukajua mtu huyu tunayemkabidhi mradi ana uwezo au hana uwezo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijaribu kuangalia, mradi wa bilioni tatu *investment* kwa mwaka mmoja tunategemea tupate bilioni 1.736; kwa hiyo mwaka wa pili ile *investment* yote ya bilioni 3 itakuwa imerudi kwa sababu tutakuwa na 3.4 bilion, lakini mradi huu umekwama. Ungekuwa ni mradi mtu anauweza huyu mtu angeshakuja kuufanya, jambo ambalo inabidi tujiulize ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, China ndiyo nchi inayoongoza kwa *production* ya *steel*/hana duniani, mtu huyu anatoka China, je, kama kuna ucheleweshaji kama sehemu ya hujuma ili huu mradi usiendelee wao waendelee kufanya biashara hii? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali, kwanza kwa sababu ya muda inabidi niende haraka haraka, huu mradi *contract* yake kwanza iwe *terminated*, huyu mtu hawezo na ameshindwa kufanya hii, kwa sababu hata uwezo wa vitu anavyovifanya hauendani na chuma ambayo tumeitafuta wenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine tumeona upande wa *TPDC*, tumeona na sehemu nydingine wanapeleka vijana wao kusoma, leo tuna watalaan wa gesi hapa, tuna watalaan wa petroli hapa, lakini tunapokuja kwenye chuma hata tukiwaliza watu ile *content* yenyewe ya hii chuma ya Liganga na Mchuchuma kuna nini? Chuma ni asilimia ngapi, hiki ni asilimia ngapi, mtachenjua vipi? Wanakuambia yule mwekezaji ndiye anayekuja kuangalia njia ya kuchenjua. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inawezekana Serikali ijikite kuwezesha vijana wa Kitanzania sawa na tulivyowekeza kwenye petroli, sawa na tulivyowekeza kwenye gesi, tuwekeza kwa vijana wa Kitanzania wakasome *material specifically* kwa ajili ya *material*, wakirudi hapa watakuwa wanajua hata hizo *process* za uchenjuaji ni *chemistry* ya *form two*, lakini watu wetu hawajawezeshwa! Kama hawajawezeshwa huyu mtu anatupiga chenga kila siku, kwa hiyo kwa sababu ya muda ninapenda niishie hapo na

ninaunga mkono hoja kwamba huyu mtu aondolewe tutafute mwekezaji mwingine ambaye atalisaidia Taifa. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, ajiandae Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa na Wabunge kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hongera sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye utekelezaji wa bajeti ambao umefanyika katika Wizara zetu tatu tunazozisimamia kuanzia mwezi Julai hadi Disemba mwaka huu wa fedha. Nianze kwa kuipongeza Serikali na Wizara ya Maji kwa kazi nzuri ambazo zinaendelea katika Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunakubaliana kama Wabunge kwamba Wizara ya Maji inafanya kazi nzuri na kuna miradi ya kutosha kabisa kwa kila Mbunge katika kila Jimbo, miradi inayogharamiwa na Serikali Kuu, Mfuko wa Maji na zile hela ambazo Mama yetu Rais Samia ametoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano katika pongezi zangu hizi kwamba kwenye bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Maji Serikali ilikuwa imetenga shilingi 646,630,000,000 na katika pesa hizi Serikali imeshapeleka shilingi 413,950,671,097.95 ambayo ni sawa na asilimia 61. Kutokana na hili Mheshimiwa Juma Aweso na timu yake wanang'ara, wameendelea kung'ara kusema ukweli. Kwa hiyo, tunaipongea Serikali kwa kazi nzuri na kwa jinsi wanavyoisapoti hii Wizara ambayo tunaisimamia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeona kwamba kama Kamati kuna changamoto kwenye hii Wizara kidogo na ninaomba muichukulie seriously Waziri na watendaji wako, kwamba kwenye manunuzi kila kitu kinafanyika makao makuu na hizi Mamlaka za Maji na RUWASA kuna saa wanakwama kwamba, vifaa havifiki kwa wakati. Kwa hiyo,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ni maoni yetu kama Kamati kwamba, hili lifanyiwe marekebisho ili ununuzi uende haraka na Waziri aendelee kuchapa kazi kama ambavyo anachapa pamoja na watendaji wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Wizara hizi kama Wizara, viongozi wa Wizara hizi wanajitahidi sana kutekeleza miradi mbalimbali, lakini wana changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa fedha kama ilivyokuwa kwa Wizara ya Maji; kwa mfano, katika bajeti ya maendeleo Tume ya Umwagiliaji imepangiwa shilingi bilioni 35 kama pesa za ndani na shilingi bilioni 11.5 kama pesa za maendeleo kwa pesa kutoka nje, lakini hadi mwezi Disemba, 2021 Tume hii ilikuwa imepokea shilingi milioni 349 tu ambayo ni 1% tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tuko *serious* tunakubaliana kwamba, Wabunge wote huku kila aliyekuwa anasimama alikuwa anasema kilimo, maji, umwagiliaji, lakini kweli kwa hii *trend* ya kutoa 1% kwa miezi sita tutafika kweli? Tutatekeleza vile vitu ambavyo tulikuwa tume-*plan* na tumewaahidi watu kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hapa tunaona kuna tatizo na tunaiomba Serikali iiangalie hii Wizara kwa jicho la huruma na wawape pesa, ili watengeneze miradi ya maji na mambo yaendeleee.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya uvuvi mambo ni yaleyale katika pesa za maendeleo zilizotengwa ambazo ni shilingi bilioni 99 wameshapokea shilingi bilioni tatu tu ambayo ni sawa na 5.1% katika sekta ya uvuvi. Katika sekta ya mifugo walitengewa shilingi bilioni 16.8 na wameshapokea shilingi 2.4 ambayo ni sawa na 14.6%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hizi sekta ambazo zinaajiri wakulima wengi, wafugaji na wavuvi, sidhani kama tunazitendea haki. Kwa hiyo, ni mawazo ya kamati kwamba, pesa zilizopelekwa kutekeleza miradi ya aina mbalimbali ni ndogo na tukumbuke Rais alivyokuja kufungua Bunge letu,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutuhutubia hapa, alitoa ahadi kwamba, sekta hizi za uzalishaji kilimo, mifugo na uvuvi zitapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tutii lile agizo la Rais ili tufike mbele, bila hivyo ninaona tunakwenda ambako siko, tutahukumiwa na wale wapigakura.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme tu naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kunti; baada ya Mheshimiwa Kunti, Mheshimiwa Maryam Omar Said.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye hizi Kamati zetu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunakubaliana kwamba bila kilimo sisi sote humu tusingekuwepo ndani, kwa sababu tunakula chakula ili tuweze kupata afya bora na akili timamu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, kumbe cheo kimebadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye mtiririko wa utoaji fedha kwa Wizara ya Kilimo, Wizara ya Kilimo bado iko chini, Wizara ya Kilimo bado inaendelea kusahaulika, Wizara ya Kilimo bado imetupwa kabisa huko mafichoni ilhali hii Wizara hii ndio tunayoitegemea Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania zaidi ya 65% ndio wanapata ajira kuititia Wizara hii. Inatalisha na inatoa ajira, lakini Wizara hii ndio inayohangaika wakulima wake ambaa ni zaidi ya 80% huko vijijini watafute mbegu wenyewe, watafute pembejeo za kilimo wenyewe, mvua wanategemea ya Mwenyezi Mungu, kilimo cha kudra ya Mwenyezi Mungu, lakini Wizara hii Serikali haijawahi kuonesha nia na dhamira ya dhati ya kuisaidia ili tuweze kuliokoa Taifa letu. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Mfuko wa Pembejeo wa Taifa; Mfuko huu pamoja na Benki ya Kilimo, nianze na Mfuko wa Pembejeo wa Taifa; mfuko huu wa pembejeo wa Taifa tulitegemea Serikali itoe feedha za maendeleo kwenye Wizara ili huu Mfuko wa Pembejeo wa Taifa waweze kupatiwa fedha ili wakulima wetu wadogo wadogo kule chini waweze kupata zana za kilimo na waweze kulima kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wizara imekuwa ikinyimwa fedha na mfuko huu umeendelea kukosa fedha, matokeo yake mfuko uko pale, watumishi wako pale, hakuna kazi yoyote wanayoifanya; wanaamka asubuhi wanakuja wanasaini, wanapumzika wanasubiri muda ufile warudi majumbani kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali inaona kilimo hakina tija kwenye Taifa hili niombe tuifute hii Wizara ili wakulima wa nchi hii tuendelee kulima kwa namna tunavyoweza kuliko kuwa na Wizara ambayo haina msaada kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Kilimo; benki hii tumeendelea kuipigia kelele humu ndani, kila siku *storyni* zile zile, maneno ni yale yale na imebadilika sasa mmebakisha kufukiza kila siku mnatubadilishia Wakurugenzi; sasa huyu Mkurugenzi haujampatia fedha, unamfukuza, ultaka afanye nini? Si amekaa tu, fedha hakuna, atamkopesha nini huyo mkulima? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niiombe sana Serikali; kama kweli tuna nia na dhamira ya dhati ya kuinua kilimo cha Taifa hili na kujenga uchumi wa nchi hii, twendeni tukaongeze fedha kwenye Wizara ya Kilimo ili tuweze kuleta tija katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji; Wizara ya Maji angalau safari hii imepata mkongojo imesogea, lakini changamoto kubwa iliyoko Wizara ya Maji ni miradi mikubwa ya kimkakati.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nikiwa nje huko sijaingia kwenye jengo hili kulikuwa na mradi unaitwa Mradi wa Bwawa la Kidunda, una zaidi ya miaka 20 leo Bwawa la Kidunda halijakamilika. Sasa sijui shida ni nini kwa Serikali kwenda kutekeleza miradi hii mikubwa ambayo ina tija kubwa kwa Taifa letu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa natamani sana, tunaitaka Serikali na tumeendelea kuwashauri Wizara pamoja na Serikali, kwa maana ya Wizara ya Fedha, watusaidie hii mikataba wanayoingia na wafadhili kama wanaona haiwezekani hao wafadhili waliokuja wawaondoe watafute wafadhili wengine ili miradi iweze kutekelezeka. Napata hofu sana, Mkoa wa Dodoma leo tuna Mradi wa Farkwa, sasa hivi una zaidi ya miaka sita tunakwenda was aba, tumelipa fidia, lakini suala ni lini tunaanza ujenzi wa Bwawa la Farkwa? *Story*, kwa hiyo, tukakwenda humu ndani, watakuja, watakuja, watakuja; bado hatujakamilisha mazungumzo, bado watu sijui wanafanya nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno yamekuwa ni mengi kuliko utekelezaji na uchukuaji wa maamuzi. Serikali tunaiomba iwe inafanya haraka kwenye suala zima la uchukuaji wa maamuzi ili kupunguza muda wa kuendelea kupoteza mud ana kutokutekeleza miradi hii kwa wakati. Nakushukuru, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Maryam Omar said.

MHE. MARYAM OMAR SAID: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwanza kwa kupata nafasi hii niweze kuchangia hoja zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi moja kwa moja nitakwenda kwenye miradi ya maendeleo ambayo bado ni changamoto kubwa kwa miradi yetu kusuasua na kuchukua muda mrefu na kwa upande huo nitakwenda moja kwa moja

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwenye miradi ya Muungano ambapo nitazungumzia Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi uliopo Kaskazini A, Unguja.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mradi ulianza mwaka 2018 na tulitegemea mwaka 2022 mnamo mwezi wa saba tuwe tayari tumekamilisha mradi huu, lakini mpaka sasa huu ni mwezi wa pili tuna miezi mitatu tu mbele tuwe tumemamaliza. Mpaka sasa katika eneo lile kinachoonekana ni nyasi tu, hakuna chochote kinachoendelea, jambo ambalo ni changamoto kubwa, hivi Serikali hebu tujitathmini kwa nini tunakwama? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuseme labda ni wawekezaji wetu, kama hawana uwezo si lazima tumng'ng'anie mtu mmoja, wawekezaji ni bora tutangaze kwa *tenderkwa* watu wengi, halafu tumuangalie ni nani mwenye uwezo kuweza kukiendesha kitu na likafikia kwa wakati. Hatupati tija, tunawazuia wananchi maeneo kwa maeleo kuwa tunafanya kitu fulani. Inafikia muda, muda unamalizika; mwananchi alikuwa akilima pale halimi tena anakaa nyumbani, anakufa njaa, hatumlipi mafao yoyote na bado tunakaa na lile eneo hatulitumii kwa kazi yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani Serikali ni muda sasa wa kukaa chini tukatafakari tunapokwama na tukaendelea na miradi yetu jamani. Haya mambo ya kila siku miradi yetu kuwa wimbo wa Taifa humu ndani si sahihi. Wimbo wa Taifa ndio kila siku ni ule ule haubadiliki, mpango kila unapopita ukija miradi ni ile ile, mpango mwingine ukija miradi ni ileile, sio sawa, si haki hii, Serikali kaeni chini tutatue tujue kwamba, tukiendesha mradi hata kama ni mmoja sawa. Sekta tunamaliza muda wetu lakini tunajua kitu hiki kimefikia hapa. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitoa mfano, Liganga na Mchuchuma ni mwaka wa ngapi? Toka enzi za mababu zetu, wamekuja wazazi wetu, tumekuja sisi, watakuja watoto wetu bado tunaonesha tu mlima uko pale, faida yake ni ipi kwetu sisi? Wote tuliozauwia kwamba shughuli zote pale zisiendelee, tumemaanisha nini kama Serikali? (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtatukosesha kura zetu tusirudi humu ndani, Mbunge akitoka huko anaahidi kwamba, ndani ya miaka yangu mitano nitahakikisha jambo hili limemalizika, tunamaliza miaka mitano hakuna chochote, tunarudi kwenda kusema nini kwa wananchi? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tulifikirie hili, tusaidiane ifikie mahali tufanye jambo moja lioneckane kwamba tumefanya hiki kuliko kwamba, kila mahali, kila mahali, tunaacha mapengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye Kiwanda cha Viuadudu; nimesikia hapa taarifa ya Mwenyekiti, ameelezea Kiwanda cha viuadudu, lengo kilipoanzishwa kile kiwanda; kilianzishwa kwa madhumuni ya kumaliza malaria nchini kwetu. Leo hapa kumeelezewa nchi takribani saba hizi zinachukua dawa kutoka kwenye kiwanda chetu hiki, lakini Tanzania bado, kitu ambacho kwa tathmini ya mwisho huku walisema kwamba zilinunuliwa lita 560,308 tena ziliponunuliwa hizo wameweka msisitizo ni kwa maelekezo ya Rais wa Awamu ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tujiangalie, malaria nchini kwetu bado ni tatizo tena ni tatizo sugu. Sisi kule Zanzibar tulikuwa na mradi wa kupigiwa dawa majumbani kila miezi mitatu, ikaja mpaka sehemu igundulike na malaria ndio inakuja kambi tunapigiwa dawa, ikafikia muda tukaambiya mradi umeisha, sawa, malaria imerudi tena upya. Kama tukishirikiana hii ni nchi moja, kwa nini tusitumie rasilimali zetu zilizomo ndani na tukamaliza malaria? Hiki kiwanda kimeelekea kabisa madhumuni yake ni kumaliza malaria Tanzania, tunakwama wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ni zetu, pesa ni zilezile za Serikali, hivi kwa nini tusizoshawishi hizo Halmashauri kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum wakanunua hizi dawa na tukamaliza malaria nchini, lakini pia kiwanda kikawa kina-survive vizuri? (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Deo Mwanyika, ajiandae Mheshimiwa Charles Mwijage.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie suala la Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni la muda mrefu na kama ripoti ya Kamati ilivyooneshwa hatujaridhishwa kabisa Wanakamati na taarifa tunazozipata kuhusu mwelekeo na muendelezo wa mradi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu tunachoambiya ni kwamba uko kwenye majadiliano. Majadiliano haya ambayo hayaishi tunashindwa kuelewa ni majadiliano gani. Tuna uhakika kabisa wataalam wetu wana uwezo wa kufanya majadiliano na tumewaamini na tuna hakika pengine wanapigania maslahi makubwa ya nchi yetu ili tupate mkataba mzuri, lakini miaka 11 toka mkataba umesainiwa mpaka leo hatujaweza kukamilisha jambo hili? Hivi hatujui na hatuoni umuhimu wa chuma katika maendeleo ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kusema wote tunafahamu majadiliano siku zote sio lazima ushinde kila kitu, lakini majadiliano yanataka *compromise*, ufile mahali ukubaliane na hasa kama unajua lengo lako ni nini. Sasa sisi tunaelewa chuma tunahitaji, tunaelewa mradi huu ni mkubwa, mradi huu utabadili maisha ya watu, mradi huu tunaouita mradi wa kielelezo, mradi huu tunauita upo katika mpango wa kwanza ulioishia 2021, upo kwenye mpango wa pili unaoishia 2026, upo kwenye kila bajeti ya kila mwaka, upo kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM. Ndugu zangu, hivi tunataka nini? Tunafahamu kabisa kwamba tunapoteza kwa kutoendelea na uwekezaji kwenye mradi huu mkubwa. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kupendeza; nafahamu Waheshimiwa Wabunge kwamba Kamati yetu inajaribu ku-*negotiate* ili tupate *better terms*, lakini nitoe ushauri hebu wajaribu kuangalia maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua *approach* ikiwa ni kuangalia *negotiations* kama kama kihasibu, unaangalia tu faida kwamba, tutapata faida, hatupati mpaka mwisho unapiga hesabu unasema hapa hatupati faida, nadhani hiyo *approach* sio nzuri. Waende na *approach* ya kiuchumi ya kuangalia *multiplier effect* kwenye mradi huu; mradi huu ajira 5,000 za moja kwa moja, mradi huu ajira 33,000 ambazo hazitakuwa moja kwa moja. Ndani ya mradi huu...

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

T A R I F A

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango mzuri sana wa Mheshimiwa Mbunge, Mradi huu wa Liganga na Mchuchuma, sio tu kwamba utasaidia kuzalisha chuma ambacho tungeweza kutumia katika maendeleo mengine, lakini ni mradi ambao ni unganishi kwa kuendeleza pia Makaa ya Mchuchuma na chuma cha Liganga,

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa maana hiyo, kulikuwa na mpango sahihi kabisa wa kuzalisha megawati 600 ambazo nyingine zingetumika kuchenjua chuma na megawati nyingine 400 zingeingizwa katika njia ya msongo wa kilovoti 400 pale Makambako ili uweze kuingia kwenye Gridi ya Taifa kwa hiyo, ni mradi muhimu kwa ustawi na maendeleo ya nchi.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Mwanyika, Taarifa hiyo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana kaka yangu kwa kuendelea kunifilisi nilichotaka kuongea, lakini niseme mradi huu ni *special*. Mradi huu ukiuangalia kwa haraka upande mmoja ni mradi wa kiuchumi, lakini ni mradi wa kiundombinu; tunaongelea ujenzi mkubwa wa reli katika mradi huu ambao utaiunganisha Bandari ya Mtwara, inakuja mpaka Manda inapata mchepuko inakuja kwenye huu mradi. Kwa hiyo, ajira ngapi zitazalishwa katika hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuangalie kitu kingine, tunatumia fedha nyingi sana nnchi hii katika masuala ya chuma; ujenzi wa maghorofa, ujenzi wa madaraja, ujenzi wa *SGR*, ujenzi wa *towers*. Mheshimiwa Naibu Waziri hapa ameongea kwamba hatuna *towers*, nchi hii ina *towers* za simu zaidi ya 10,000; hivi hiyo miradi yote hiyo ya *towers* ni chuma na sisi chuma tunacho hapa na tunaliallia kwamba, hakuna *towers* za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia ni mengi, miradi hii itapunguza gharama nyingi sana ya vitu vingi. Kwa mfano, tunaongelea uzalishaji wa gesi, nani anafahamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungashio cha gesi unachokiona, unakiita *cylinder*, asilimia karibu 50 ya ile gesi, gharama...

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumpa Taarifa kaka yangu Mheshimiwa Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kuhusu suala la Liganga-Mchuchuma sio tu itasaidia hayo anayoyasema, lakini pia itasaidia kuanzisha viwanda vya magari katika nchi yetu. Kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hiyo, itaongeza na kukuza uchumi kwa zaidi ya asilimia 100. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante. Taarifa hiyo.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali taarifa na mambo ni mengi ni mengi sana ambayo chuma kingetusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumalizia kwa kusema wenzetu Serikalini watusaidie. Mheshimiwa *Engineer Chiwelesa amesema* huyu mwekezaji kama hawezi basi aondolewe, lakini tunachoambiwa ni kwamba kuna tatizo la *tax incentives* au vivutio.

Sasa mimi nimeangalia vivutio vinavyoongelewa, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, hivi vivutio vinavyoongelewa kwa mradi mkubwa wa aina hii tuangalie maslahi makubwa kwamba tukijenga hii *infrastructure* ambayo ni Liganga – Mchuchuma, *powerna steel*, tukajenga na hizi reli, uchumi mkubwa wa eneo zima la Kusini utasisimka na tunaweza tukapata hii kodi ambayo tunaweza tukaisamehe hapa mwanzoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata ukiziangalia hizi kodi zinazoongelewa hapa tulifuliza swali hivi tunazipata leo? Kwa hii chuma kuwa bado hazijachimbwa? Tunazipata hiso kodi? Hatuzipati.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Mwanyika.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Kwa hiyo, tuliangalie kwa karibu nashukuru muda ni mfupi lakini naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mwijage ajiandae Mheshimiwa Juma Usonge.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia taarifa za Kamati hizi mbili kwa sababu ya muda nitachangia taarifa ya Kamati inayoshughulika na sekta ya kiuzalishaji ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ndiyo sekta za kiuzalishaji na kwa mtazamo wangu mimi ni kwamba naangalia ustawi wa ndani ya nchi, uzalishaji wa chakula na naangalia uwezo wa sekta hizi kuuza nje. Tunapata chakula Tanzania, hatujapata njaa kwa miaka sita au saba na watu wanafurahi, lakini nataka niwaambie Watanzania tunakula chakula cha bei ghali, tunazalisha bila tija, tungetegemea watu wale nyama kwa shilingi 5,000 kwa kilo, wale samaki kwa shilingi 3,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nchi yetu ina *export* thamani ya dola bilioni sita lakini bahati mbaya 2/3 inatokana na madini na zaidi dhahabu, tunapaswa tu *export* tutikegemea hizi sekta za kiuzalishaji kwa sababu zina nguvu ya kujumuisha, zinashirikisha watu walio wengi. Lakini ukisikiliza wataalamu ikiwepo Wizara husika hizi, hawa watu wakiwezeshwa Serikali ikiwekeza katika sekta hizi tutaweza ku-*export* zaidi ya bilioni 10 kutoka kwenye sekta hizi, lakini madhara yake ni kwamba wananchi walio wengi watakuwepo wataachana na hizi tabia za kushukuru vitu vidogo vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze kitu kimoja na nimshauri Mheshimiwa Spika aiambie Serikali iletwe semina na Wabunge tukae kama Kamati tujadili hizi sekta mbili kwa kifupi bila kutafuta maneno mimi sijadili pesa walizopewa, hizi sekta hazijapewa pesa yaani Serikali hajaweweza kwenye sekta hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape jambo moja la kuangalia, fursa ya samaki wa kufuga *world potential*/ni bilioni 284; hakuna zao tunalima Tanzania kwenye soko la dunia lina kiasi hicho. Lakini ngoja niwaeleze Tanzania sisi tunasifikasi kwa kuwa na maji mengi, sasa niwaambie aibu, uwekezaji

wa Serikali ya Uganda samaki wa kufuga wanaauza tani 118,000; sisi tunauza samaki tani 12,000 nasema tani 12,000 lakini nini wenzenetu hawa wamewekeza sitaki kuwaaletea historia za mzee wangu za Brazil nawaeleza Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Egypt wana samaki tani milioni 1.4; kwa hiyo ujanja ni kwamba kwa sababu tuna *water bodies* nydingi Tanzania Serikali muwekeze kule na uzuri wa sekta hizi tatu nilizozungumza ukiweka pesa leo, kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati inalipa na tusitegemee benki zetu za *commercial* mambo ya CRDB na asilimia tisa au TBBA hakuna, twende tukakope kwenye benki za kimataifa, zinazotoza riba ndogo, tuweke mamlaka za Serikali tuwape Watanzania. Sekta binafsi mnayoisema siwezi kukubali sekta binafsi ya kutoka nje hayo ni ya kumlisha mtoto wa kwale wakati watoto wa kuku wanakufa, tuchukue pesa tuwape watoto wetu Watanzania, tuwasimamie waingie kwenye uchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwetu watu wanasema ziwa liliuzwa kwa sababu hawawezi kuvua kama watu wanaokuja na*technology*, sasa watu wangu mimi lazima tuwatengenezee vizimba, tuwatengenezee miundombinu waweze kushiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nisaidie nizungumze hoja ya Tume ya Mipango; kuna kitendawili kimoja, kuna Wizara ina shughulikia maji ya binadamu, nyininge maji ya kilimo, nyininge maji ya mifugo, nyininge inazuia mafuriko ya miundombinu tungakuwa na Tume ya Mipango hili suala lingeratibiwa kwa pamoja. Lakini unakuta sasa kuna Wizara sita zinashughulika na kitu kile kile halafu mtu anakwambia eti uchimbe kisima unyweshe ng'ombe huo umeme utautumia kutoka wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tungakuwa tumeratibiwa pamoja tungetengeneza kitu kinaitwa *mini leg* hawa wa ndugu zangu wa Kaskazini wasingakuwa wanalia, wangakuwa majosho yao.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo niungane na kamati na niungane na mzungumzaji wa kwanza lazima Tume ya Mipango iweze kurudishwa tuweze ...keki ya Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Juma Usonge, ajiandae Mheshimiwa Polepole.

MHE. JUMA USONGE HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kunipatia fursa hii ya kusimama kwenye Bunge lako yukufu. Lakini pia na mimi niungane na wenzangu kukupongeza kwa kushinda kwa kura nyngi sana. (*Makofii*)

Baada ya kusema hayo naomba njikite zaidi kwenye ripoti ambayo iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, lakini zaidi nitajikita kwenye maeneo ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mjumbe katika mifuko ya kimataifa yanayohusu masuala ya mazingira duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nitaje baadhi ya wadau ambao wanachangia sana kwa ajili ya nchi yetu ya Tanzania ikiwemo *list of Development Countries Fund*, kuna mfuko wa *Adaptation Fund*, kuna *Global Environment Facility* ambayo ni ikolojia hiyo kuna mfuko ambao unaitwa *Green Climate Fund*, kuna mfuko ambao unaitwa *UN Environmental Program*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifuko hii inapofadhili nchi zetu hizi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana kwamba Zanzibar pamoja na Jamhuri ya Tanzania ambayo ni Tanzania tatizo linakuja kwenye ugawaji wa fedha. Zanzibar miaka yote fedha hizi hazifiki ipasavyo, kwa mfano na nikupe mfano mzuri kuna mradi ambao unatekelezwa wa *Global Environment Facility* wa ikolojia ambayo kwa ajili ya

kunusuru hizi kaya maskini pamoja na vijiji ambavyo viko hatarini kwa ajili ya kuharibika na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fedha ambazo zimetoka zaidi ya bilioni 17 lakini cha kushangaza Zanzibar tumepata 18% na miradi hiyo mpaka hii leo haijakamilika na mradi huu ukomo wake ni ifikapo mwezi Julai, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza miradi mingine ambayo tayari inafanyika huku Tanzania Bara miradi hiyo inafanyika kwenye Wilaya nne na yote tayari ishakamilika na fedha zote zimeenda lakini changamoto zile za Zanzibar mpaka leo hii miradi haijakamilika na zimetoka shilingi 402,792,000 basi hizo ndiyo zilitotoka utashangaa nini tatizo; ukiwaliza Zanzibar wanasema fedha zimeganda huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo lazima tuwe wa wazi kabisa Mheshimiwa Waziri nakuomba sana na Serikali yako hii miradi ya fedha zinapokuja Zanzibar tuzisimamie kwa pamoja. Leo hii kuna blah blah nydingi, leo hii tumechonganisha wananchi kati ya Serikali na wananchi wenyewe, leo hii wananchi tumewaambia fedha hizi tunaenda kununua maboti, tunaenda kuwasaidia wajasiriamali, lakini kuna miradi ambayo tayari tumeikita pale kwa ajili ya kupanda miti ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Lakini leo hii miradi hii imefanyika asilimia moja asilimia 90 bado haijakamilika ukomo wa mradi huu uanenda kukamilika kesho kutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa tunaenda wapi? Tukae tujitafakari hii mifuko wenzetu wanatusaidia kwa Imani. Leo hii miradi hii haikamiliki kwa muda upasavyo, tunaweka picha gani huko mbele? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii inatekelezwa kwenye Wilaya ya Kaskazini A - Unguja kwenye vijiji zaidi ya vine, wananchi wa kule sasa hivi wameweka kasumba kubwa dhidi ya Serikali yao, Serikali ya Zanzibar ukiwaliza Zanzibar...

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. SOUD MOHAMED JUMAH: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa

T A A R I F A

MHE. SOUD MOHAMED JUMAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Juma Usonge uratibu kama alivyozungumza wa fedha ambazo zinakwenda Zanzibar ambaao Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio masuuli kwa kweli haliko vizuri; kuna mradi ambaao ulikuwa wa *African Development Bank* na ulikuwa na pesa kidogo tu *just dola 350,000* lakini kutokana na uratibu mbaya mradi ule muda umemalizika na zimetumika fedha kama 30% tu na zilizobakia fedha zimeenda halijojo yaani fedha hazikutumika tena mradi umefungwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tungeliomba tu uratibu huu tukaupitia na ingewezekana ukaunda tume maalum ya kuweza kuratibu hizi fedha ambazo zinakwenda Zanzibar na mifuko yote hii matumizi yakoje na changamoto ziko wapi? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante endelea Mheshimiwa; taarifa umeipokea?

MHE. JUMA USONGE HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa nimeipokea kwa mikono miwili. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama alivyozungumza mtoaji taarifa Mheshimiwa Waziri nakuomba sana kwenye fedha hizi ambazo zinaenda Zanzibar tuzisimamie ipasavyo lakini siyo hilo tu pia kuna Mifuko hii ya Jimbo ambayo mnayotupa kila siku tukiwalizia wenzetu wa Tanzania Bara fedha tayari zimeshaingia, kwa Zanzibar kule kuna urasimu ambaao tayari hauna majawabu. Hii ni tatizo tunaumia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Zanzibar kama tunafanya tathmini Zanzibar ndio inahitajika zaidi kupeleka

zile fedha. Kuna visiwa sasa hivi vinaanza kupotea, kuna miradi mbalimbali haifanyi kazi sababu ya fedha haiziingizwi, juzi Mheshimiwa Waziri ulikuja Zanzibar umefika mpaka eneo Nungwi umeona maeneo ya *beach* kule yanavyoharibika na maji kupanda juu. Lakini siyo hilo tu *almost* Zanzibar nzima kisiwa kinapotea, fedha tunazipata lakini mwisho wa siku urasimu ndiyo ambao tayari unaofanya kazi. Kwa hiyo hatuvi wa wazi, wala hatuvi *active* kwa ajili ya kuisimamia hii miradi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono ripoti ya Kamati. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Polepole ajiandae Neema Lugangira. Mheshimiwa Polepole bado uko kwenye darasa au? (*Kicheko*)

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, unisamehe.

Mheshimiwa NaibU Spika, kwanza nikupongeze sana kwa kuchaguliwa kwa kishindo na ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Nipongeze sana Wenyeviti wa Kamati wamesema mambo makubwa sana yaliyonipelekea kubadilisha kidogo mtiririko wa namna ambavyo ningependa kuchangia na ningependa kwanza kusema kama ifuatavyo:-

Kwa maana njema kabisa kama Serikali isiposikiliza mapendekezo ya Kamati hizi mbili kwa umakini, tutaelekea kubaya na mimi ningesema jambo moja ambalo labda linaweza likaonekana lisieleweke, lakini kama tusipoweka dhamira ya dhati kwenye mradi mmojawapo tu wa chuma tunatumia pesa nyngi kuleta chuma hapa na inaathiri kitu kimoja kwenye uchumi kinaitwa *balance of payment* yaanitunatumia pesa nyngi sana kuagiza bidhaa kutoka nje kuja ndani kuliko ambavyo tunauza bidhaa za ndani kwenda nje, kiuchumi unapokuwa na nakisi kwenye *balance of payment* si afya kwenye uchumi na ni kitu ambacho kinaweza kikatufikisha siku moja tukashindwa kuwa na fedha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya nje ya kutosha kuweza kufanya majukumu yetu mengine ikiwemo kulipa madeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa niseme katika hili la kuweka nidhamu ya namna ambavyo tunazalisha ndani, ifike pahala tukubaliane kama Taifa yako mambo tuweke sera za ulinzi (*protection policies*) katika nchi yetu kwamba bidhaa hii na hii hatuta agiza kutoka nje tutaizalisha kutoka ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano mafuta ya kula yanatuongezea nakisi kwenye *balance of payment*, mbolea inatuongezea nakisi kwenye *balance of payment*, hiyo chuma nimeisema, sukari inatuongezea nakisi kwenye *balance of payment*, mchele unalimwa hapa Tanzania lakini bado tunaagiza inatuongezea nakisi kwenye *balance of payment*, ngano/shairi ambayo inaweza kulimwa hapa Tanzania inatuongezea nakisi kwenye *balance of payment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nakisi kubwa nikipitia pitia nyaraka hapa za Wanakamati na nini inaonekana bado ni tatizo baadhi yenu mtafahamu ya kwamba dhamira nzuri ya Mheshimiwa Rais kwenda kukopa kule *IMF* pamoja na mambo mengine ilikuwa ni kuweza kushughulika na nakisi kubwa inayoongezeka kwenye *balance of payment*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Serikali ziko bidhaa ambazo tukiwekeza vya kutosha hapa hapa nyumbani tutajitosheleza na tukijitosheleza fedha nyingi itabaki hapa hapa nyumbani na hapo ndiyo inapokuja kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani kote wale wanaitwa *micro small and medium enterprises* ndiyo wanashika zaidi ya asilimia 90 ya chumi zote. Hapa Tanzania hawa *micro small and medium enterprises* ndiyo ambao wanashikilia viwanda vingi vidogo na vya katika ambavyo vina jukumu la kuchakata mazao mbalimbali na huduma na bidhaa ambazo zinahitajika hapa nyumbani. Ifike pahala

hawa *micro small and medium enterprises* yaani biashara ndogo sana, ndogo na za kati ziwezeshwe kwa makusudi na Serikali yenye, mabenki hayawazi kuweka pesa kule kwa sababu watasema hakuna usalama. Lakini Serikali ndiyo baba yao, ndiyo mama yao na hapa katika Wizara ya Fedha na Mfuko ule wa Uwezeshaji iko mifuko zaidi ya 50 ya kuwezesha wananchi kiuchumi haisomani, hajiuani, malengo yake hayashabihiani, sasa unapokuwa una mifuko zaidi ya 50 yenye fedha za mamia ya mabilioni ambayo haisomani nafahamu yaliwahi kutoka maelekezo hapa kwamba mifuko hii ihiushwe, lipatikane fuko moja kubwa la kwetu la ndani ambalo tatalitumia kuwawezesha wajasiriamali wadogo ambao hawa kimsingi ndiyo *engine* ya uchumi wetu. Tukifanya hivyo hata wigo wetu wa kodi na mapato utaongezeka. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Lugangira.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na mimi niungane na wenzangu kukupongeza sana kwa kupata nafasi hii na tunakutakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mimi nitajikita katika eneo la usalama wa chakula kwa maana ya *food safety*. Nasema hivi kwa sababu duniani kote masuala mazima ya usalama wa chakula kwa maana ya *food safety* yanaratibiwa chini ya Wizara ya Afya kwa maana ya kuwa chini ya mamlaka ya Kudhibiti Ubora wa Chakula na Dawa na hata Tanzania miaka ya nyuma ndivyo ambavyo tulikuwa tunafanya chini ya *TFDA*, na hata nchi za Afrika Mashariki zilikuja kwetu kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini miaka ya karibuni Serikali iliamua kuivunja *TFDA* na badala yake kuunda *TMDA* na jukumu la usalama wa chakula kwa maana ya *food safety* wakaliweka chini ya Shirika la Viwango (*TBS*). Sasa jambo hili mtaniwia radhi sana kusema Iakini limeweka maisha na afya za watanzania rehani.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa naibU Spika, nasema hivyo kwa sababu *TBS* ina jukumu la kuangalia ubora wa matairi, ubora wa mabati, ubora wa misumari mabati na kadhalika na hapo hapo iweje tena *TBS* hiyo hiyo ipewe jukumu la kuratibu na kudhibiti ubora wa usalama wa chakula kwa maana ya *food safety*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa hawa *TBS* ndiyo wanaotoa vibali kwa wazalishaji wa chakula, halafu hao hao tena waende waangalie kama ule ubora kile kibali walichotoa kimekidhi, tayari hapo kuna *conflict of interest*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo mahsusini ambalo lilijitokeza ambalo linadhihirisha kabisa *TBS* haiwezi kuendelea kubeba jukumu la usalama wa chakula kwa maana ya *food safety*. Mwaka jana kwenye tarehe 13 au 14 Oktoba, 2021 Shirika la Chakula na Madawa la Kenya lilitangaza kwamba linarudisha *juice* aina ya *Ceres* ya *apple* ambazo zilikuwa na aina moja ya sumukuvu ambayo ni hatari kwa maisha ya wanadamu. Mpaka siku hiyo kwa huku Tanzania *TBS* ilikuwa hajasema kitu chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, gazeti la Mwananchi likawatafuta *TBS* na nakumbuka Mkurugenzi mwenye Idara husika alisema kwamba mpaka muda ule wa kwenye tarehe 14 Oktoba *juice* aina ya *Ceres* ilikuwa hajiaingia nchini na wanaendelea kufuatilia na pale ambalo zitaingia nchini basi watazizua na watatoa taarifa na watafanya uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya tarehe 16 Oktoba *TBS*katoa taarifa ya umma kuelezea kwamba wamejiridhisha *juice* zile hazijaingia nchini *juice* aina ya *Ceres* na *barcode* ambazo zilikuwa zimewekwa wakasema na waiambia umma kwamba kila kitu kiko sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa masikitiko makubwa TBS walitudanganya Watanzania kwa sababu kwenye tarehe 22 mimi kwenye kiosk kimoja hapa Dodoma nilikuwa zile *juice* za *Ceres* aina ya *apple* zikiwa zinazuwa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nilichukua jukumu la kupiga picha na kumtumia Waziri mwenye dhamana wa wakati ule wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambaye akapokea akasema atalifanyia kazi. (*Makofii*)

Kwa hiyo, moja kwa moja inaonesha kwamba kwanza *TBS* hawachukulii *serious* jambo la usalama wa chakula kwa maana ya *food safety*; *TBS* hawana muda wa kuangalia masuala ya usalama wa chakula na *TBS* wanaendelea kuhatarisha maisha ya Watanzania kwa kuendelea kulimbikiza mambo mengi ambayo hayaendani pia na mambo ya usalama wa chakula. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi kwa unyenyekevu mkubwa sana naiomba Serikali ipitie upya uamuzi wake wa kuondoa masuala ya usalama wa chakula kutoka Wizara ya Afya na kuyapeleka kwenye eneo la mambo ya Viwanda, Biashara na kadhalika turudi kwenye *basic practice*. Hii haitakuwa mara ya kwanza ya Serikali kufanya mapitio na maboresho ya uamuzi wake kadri ambavyo itaonekana inafaa.

Kwa hiyo, mimi kwa kumalizia na kwa unyenyekevu mkubwa sana na kwa maslahi mapana ya kulinda afya za Watanzania, kulinda mzigo mkubwa ambao Wizara ya Afya unao, kulinda mzigo mkubwa wa ongezeko kubwa la magonjwa ya kansa ambayo hayaeleweki, suala la usalama wa chakula kwa maana ya *food safety* lirudi ndani ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Haya, Mheshimiwa Nusrat. Hayupo, yuko wapi?

Hapa (Mhe. Nusrat S. Hanje) aliingia ukumbini

NAIBU SPIKA: Ulikuwa wapi?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nilikuwa *washroom*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kuhusiana na hotuba ya Kamati ya Viwanda na Bishara lakini pia Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuna vitu tunavikosea sana, mathalani...

(Hapa Mhudumu wa Bunge alimkabidhi nyaraka zake)

MBUNGE FULANI: Hajajipanga huyo.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, na samahani kwa hicho kilichotokea, maana ni kama nimekuwa *ambushed*, na pia sijawahi kuchangia kutoea upande huu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza leo tarehe 11 Februari ninachangia, itakumbukwa kwamba leo ni Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi. Na jana imesomwa taarifa ya Kamati ya Sayansi na Teknolojia, lakini ninyi nyote ni mashahidi kwamba sayansi, teknolojia na ubunifu, suala la ubunifu ni suala ambalo kama halitambuliwi vizuri na Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi tunavyozungumza Taifa hili linatambua sayansi na teknolojia ambayo kuna Sera ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996, lakini pia kuna Wizara ya Teknolojia na Mawasiliano ambayo ina teknolojia, halafu kuna Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, zote hazina neno ubunifu, kwa maana ya *innovation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninyi nyote ni mashahidi, nchi zote ambazo tunazitolea mfano kwenye Taifa hili, kwamba ni nchi ambazo zimefanya vizuri kwenye masuala ya viwanda na biashara, kama nchi ambazo zimefanya vizuri

kwenye biashara na kwenye maendeleo, kwa maana ya nchi ambazo zimeendelea wote wamefanya vizuri katika masuala ya sayansi na teknolojia, lakini pia na ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi kama Taifa tuna Wizara nyingi, yaani kama kuna Wizara ambazo hazihusiani na masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu (*STI*) hazizidi tano, hazipo. Wizara yenewe ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inahitaji *innovation science and technology*. Pia Wizara ya Afya inahitaji *science innovation and technology*, Wizara ya Elimu, Wizara ya Kilimo yenewe pia, zote zinahitaji *science, technology* na ubunifu kwa maana ya *innovation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hatutapiga hatua kama taifa kama hatutakuja kuharakisha na kufanikisha mchakato wa sera itakayoitwa Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Kwa sababu mpaka sasa hivi tunavyozungumza sera hiyo ina miaka 28. Tumeanza kuipigia kelele tangu tuko nje, hatujaingia kwenye Bunge hili mpaka sasa hivi. Itakapokuja kufika hatua kwamba sera inaletwa itakuwa *outdated* kwa sababu tunakusanya maoni leo. Tutakaa miaka 10 ijayo ndipo tuje tulete sera ambapo maoni yamekuswanywa leo, maana yake hatutakuwa tumefanikiwa. Kwa hiyo, ili tufanikiwe tunahitaji kuwa Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye viwanda na biashara Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ina miaka 19, ni ya mwaka 2003. Lakini pia Sera ya Taifa ya Biashara ina miaka 19; ni ya mwaka 2003, iko *outdated*. Waheshimiwa Wabunge mkumbuke kwamba *life span* ya sera ni miaka kumi. Kwa hiyo, tuna sera ambayo tunategemea ituletee maendeleo kama Tanzania ya Viwanda, sera ambayo ina miaka 19 hatuwezi kufanikiwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa mpaka sasa hatuna Sera ya Taifa ya Ubora, hatuwezi kufanikiwa. Watanzania wenye biashara ndogo ndogo na biashara ndogo sana hawajui kuhusiana na *blue print*, sisi tunajua *blue*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

print. Hatuwezi kufanikiwa kama Taifa, na ni lazima tuvuke hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kufanikiwa hata kama tuna Tume ya Ushindani (*Fair and Competition Commission*) kwa sababu hatuna *innovation*. Vitu vyote vinahitaji watu wafikiri, sasa sisi kama nchi hatujajipanga kuhakikisha kwamba tunasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nitoe ushauri kwa Serikali, umefika muda sasa iundwe wizara maalum iitwe Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Kenya, Rwanda, Burundi, Uganda, Malaysia pamoja *South Africa* wamefanya hivyo na wamefanikiwa, ukiachana na China na nchi nyingine ambazo zinaonekana ni *first world...*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante, muda wako umekwisha. Unaweza kukaa hapo hapo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Gambo, dakika tatu.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wenzangu kwanza kabisa kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika, na ninakutakia kila la kheri kwenye kazi zako.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaongeleza jambo moja tu kwa sababu ya changamoto ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba malengo makubwa tuliyo nayo ni kuhakikisha kwamba tunaongeza ajira kutokana na llani yetu ya Uchguzi ya CCM; tuliahidi ajira milioni nane mpaka mwaka 2025, lakini pia kuongeza na mapato. Na kwa kuititia Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvubi ndiko kwenye uwezekano mkubwa wa kutoa ajira nyingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukiangalia, taarifa yam waka 2019 inaonesha kwamba sekta ya *horticulture* imeweza kuchangia asilimia 38 ya fedha zote za kigeni ambazo zinatokana na mapato ya kilimo. Ukiangalia kwa mujibu wa *data* zilizopo pia kwa nchi za Tanzania, Kenya na Ethiopia tunaona kwamba Tanzania tunatumia eka zisizozidi 120 kwa ajili ya *horticulture*, wenzetu wa Ethiopia eka 1,450 na Kenya 2,800; na ukizingatia kwamba sisi kule Arusha tuna mashamba 11 ambayo yamefungiwa, hayafanyi tena shuhguli zile ambazo zilikuwa zimeusudiwa. Mashamba hayo ni kama vile *Kiliflora*, *Meru Flowers* na mashamba mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kufungiwa kwa mashamba haya tumejata changamoto nyingi sana. Changamoto ya kwanza tumejeteza fedha za kigeni kiasi cha dola za Kimarekani 42,450,000, tumejeteza pia ajira kama 4,010, na hizi ni ajira za moja kwa moja, ukiacha nyingine ambazo zinatokana na sekta yenye. Tumejeteza pia fursa kutokana na mnyororo wa thamani, kwa sababu kutokana na kilimo kile kuna ambao walikuwa wanauza pembejeo, kuna ambao walikuwa wanafanya biashara za usafiri pamoja na shughuli nyingine. Lakini pia tumeondoa imani kwa wawekezaji, kwa sababu mashamba yale 11 yalikuwa chini ya wawekezaji, kitendo cha kuchukuliwa na Serikali imetoea hofu kwa wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto hizo mimi nilikuwa na mapendekezo yafuatayo.

Kwanza, nilikuwa nashauri kwamba kama wawekezaji waliokuwepo wameshindwa kuwekeza na ushahidi upo kwa sababu alikuwa anadaiwa na Serikali kuititia benki yatu ya *TIB*, lakini bado dhana na tija ya uwekezaji wa sekta ya bustani (*horticulture*) kwenye yale maeneo bado iko pale pale. Kwa hiyo tunashauri kwamba Serikali baada ya kuchukua mashamba yale sasa watafutwe wawekezaji wengine wakafanye uwekezaji ili tuweze kupata zile fursa ambazo tunazikosa, kama vile ajira pamoja na fursa ya mapato.

Lakini pia tulikuwa tunashauri kuwa...

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Gambo mengine andika.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Tunakwenda kwa Mawaziri, Mheshimiwa Jaffo, ajiandae Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Kigahe na Mheshimiwa Ndaki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nikupongeze sana, wewe unaweza sana, hongera sana mkubwa wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hapa leo kazi yetu ni kuchangia Kamati. Naomba niipongeze Kamati yetu ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kazi kuwa wanayoifanya ya kutushauri; na kwa ufupi ni kwamba sisi kama Serikali tutachukua mapendekezo yote ya Kamati kwa ajili ya kuyafanya kazi, hilo ndilo jukumu letu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika Waheshimiwa Wabunge wanafahamu kuwa ajenda ya mazingira nip ana, na tuna kila sababu kwa kila mmoja wetu kuhakikisha kwamba tunashirikiana vizuri katika mpango wa mazingira. Tumeshuhudia wazi hivi karibuni kwamba Taifa letu liliingia katika changamoto kubwa sana ya mgao wa maji, ni changamoto ya kimazingira. Ukiachia hapa Dodoma, ukienda pale Morogoro watu wa Morogoro walikuwa katika hali mbaya sana. Ukienda Dar es Salaam hali ni ile ile. Changamoto yam aji iliathiri sana vilevile hata upatikanaji wa nishati ya umeme ambapo naamini hata baadhi ya viwanda vilishindwa kufanya kazi vizuri na hatima yake, hata hatuwezi kujua, inawezekana pengine wakapoteza ajira. Hiyo yote ni *chain* ya mazingira. Kwa hiyo tuna kila sababu kuhakikisha kwamba tunalinda mazingira. Wenzetu

wa kule Kiteto na Simanjiro hali ilikuwa mbaya sana kiasi cha mifugo kufa, yote ni changamoto ya kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwashukuru sana wadau wote kwa pamoja. Hivi sasa Serikali tuko katika ajenda ya kuhakikisha tunapambana na mazingira, na tumeshuhudia kwamba katika utekelezaji wa miti, na niwapongeze sana Wabunge wote katika maeneo yenu; na kwa kweli hali ya upandaji wa miti ni nzuri na hamasa imekuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa sababu kesho tunazindua Sera yetu ya Mazingira ya mwaka 2021, ni Imani yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wadau wengine tutashirikiana kwa pamoja katika suala la utekelezaji wa seria hiyo. Lakini pia nishukuru kwa sababu hapa Mwenyekiti ndiye atatoa *response* kwa michango yote, niwashukuru sana Wabunge katika Kamati mbalimbali, hasa Kamati yetu ya Mazingira kwa kutoa ushauri mbalimbali na hasa kwa upande wa Wabunge waliotoka Zanzibar tunafahamu kwamba katika Wizara yetu tuna-deal na mambo ya Muungano kwa upande wa Muungano lakini pia mazingira upande wa Tanzania Bara. Kule Zanzibar ni Wizara iliyo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Dada yangu Saada ndiye anayehusika eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kuna miradi mingine ambayo tuna-scale up mpaka maeneo ya Zanzibar, kwa mfano Kaskazini A; nishukuru sana, lakini bahati mbaya miradi hii tukiwa tunafanya sisi huku kule Zanzibar maana yake hatuna mkono wa moja kwa moja. Mheshimiwa Mbunge unafahamu, mradi wako ule ndio unaotekelawa kwa Mheshimiwa Comrade Ole-Sendeka pale. Ukienda kwa Ole-Sendeka zaidi ya ng'ombe 10,000 wanakunywa maji kupitia mradi ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pesa hizi zinashuka kwenye Halmashauri ambazo ndizo zinazosimamia. Katika Halmashauri ya Mheshimiwa Ole-Sendeka (Simanjiro) mradi umekwenda vizuri 100% na wananchi watasema huyu mwaka 2025 kitaleweka vizuri sana. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bahati mbaya na fedha hizi zilienda katika Halmashauri ya Kaskazini A, kwa hiyo, Mkurugenzi na timu yake ndio wanaoratibu mambo hayo. Mmeshauri mambo ya uratibu, tutauangalia ushauri wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nishauri; kule nako tuna wawakilishi ambao pia wanaingia kwenye vikao vya ndani na Mkurugenzi yuko pale. Niwaomba Mheshimiwa Mbunge wakati mwingine tuwashauri wenzetu katika vile vikavyo wanavyokaa, maana kuna Kamati inayoendeshwa katika Halmashauri husika, basi tushauri kwamba zile fedha zikifika, kwa mfano ununuzi wa boti au uchimbaji wa visima; ni kweli, lakini Ofisi ya Makamu wa Rais huku yeye kazi yake inahakikisha inatoa zile fedha halafu uratibu ni wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmeshauri hapa kwamba suala la uratibu tulifanye vizuri. Tunaomba kuchukua ushauri huu kwa ajili ya kuona namna ya kufanya, miradi hii, kama ya mafanikio yaliyopatikana kule Kishapu, Mpwapwa, Simanjiro pamoja na Mvomero basi halikadhalika Halmashauri ya Kaskazini A ifanye vilevile utekelezaji kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme ushauri huu ni mzuri; na kwa kweli suala la mazingira sasa hivi limekuwa changamoto kubwa na ndiyo maana tuna jukumu la kujitahidi sana kwa kushirikiana na upande wa pili kule, japo suala la mazingira lipo upande huu, kwa ajili ya kuvinusuru visiwa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwenda pale Nungwi kwa rafiki yangu *comrade* pale, hali ni mbaya, maeneo mengine yanalika kabisa. Ukienda kwa dada yangu pale, Mbunge wa Pandani hali ni changamoto kubwa kule kwake, ukienda Chakechake kule hali ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuseme kwamba suala la mazingira kwa sasa hivi ni suala gumu sana. Naomba niwaambie kwamba ofisi yetu itajitahidi kufanya kila

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

liwezekanalo ili fursa za kimataifa zinazoweza kupatikana,tuzitafute kwa nguvu zote kwa kushirikiana, kwa sababu suala la mazingira halina mipaka na linaenda mbali zaidi; tutashirikiana upande wa Bara na Zanzibar, mimi na dada yangu Saada Mkuya tutafanya kazi kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kushirikiana, ninabeba ajenda moja ya Wabunge, suala la uratibu liwe vizuri, hili ninalichukua. Kwa sababu kama tusipoweka misingi mizuri ya uratibu, hata fedha ikitoka huku ikienda kule kama mambo hayataenda vizuri itakuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nishukuru sana, tuatekeleza maelekezo ya Bunge. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Bashe, ajiandae Mheshimiwa Kigahe na baadaye Mheshimiwa ndaki.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza nikupongeze na nikutakie kila la kheri katika kutimiza wajibu wako na kutuongoza katika Bunge ukimsaidia Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa ushauri waliotupa na maoni waliyoyatoa. Nataka tu niwaahidi kwamba sisi kwetu maoni, ushauri na mapendekezo yao ni *working tool*, tutajitahidi ndani ya Serikali kuhakikisha yale ambayo ni kwa maslahi ya nchi tunayafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kweli, *concerns* za Waheshimiwa Wabunge zipo, na sisi kama Wizara na Serikali tunazitambua hasa kwenye eneo la umwagiliaji, pembejeo na gharama za pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la umwagiliaji, nilitaka tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na kuwaambia kwamba mapendekezo ya kuiwezesha Tume ya Umwagiliaji ni jambo ambalo halikwepeki. Tumeanza maongezi na wenzetu wa Wizara ya Fedha na kwa uwezo

wa Mwenyezi Mungu tutapata fedha nyingi sana ambazo zitaenda Tume ya Umwagiliaji na tumekubaliana na Wizara ya Fedha, hivi sasa kuna miradi 19 ya umwagiliaji ambayo Tume ya Umwagiliaji imeshasaini na kupata wakandarasi, na tunaamini kwamba tutakopofika mwisho wa mwaka fedha zitatoka kwa ajili ya *ku-facilitate* hiyo miradi ambayo tumetangaza *tender* na kuwapa wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la ugani Wizara tayari sasa hivi imepatiwa fedha kwa ajili ya kuwapatia vitendea kazi Maafisa Ugani, na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu mwezi wa nne tutagawa pipipiki kwa ajili ya Maafisa Ugani, na sasa hivi tuko kwenye mazungumzo na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuwapatia Maafisa Ugani vitendea kazi. Mara ya kwanza *allocation* ilikuwa ni kwa ajili ya Maafisa Ugani 1,500 lakini tunawenza kufikia maafisa ugano wote 6,300 wallioko nchini ili waweze kupatiwa vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba tunabadili muundo wa Tume yetu ya Umwagiliaji ili kuhakikisha kwamba *representation* ya Tume ya Umwagiliaji itakuwepo mpaka katika Ofisi za Wilaya, kwa hiyo, itakuwa katika *structure* kama ilivyo *TARURA* na taasisi nyingine. Kwa hiyo kutakuwa na ma-*engineer* wa umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya ili kuleta usimamizi wa karibu kwenye eneo la umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakinji jambo lingine ambalo halikwepeki, nia kwamba tunatambua Watanzania wengi wako katika sekta ya kilimo. Sekta hii inatakiwa kufanyiwa mabadiliko ya kuwepo kwa sheria inayotu-*guide*, kwa hiyo tutaleta mabadiliko ya Sheria ya Ushirika, tutaleta Sheria Mpya ya Kilimo katika nchi yetu ambayo itatoa *legal framework* ya kuisimamia sekta kwenye masuala ya *resources, financing* na masuala yote yanayohusu mifumo ya kodi ili kuondoa matatizo tuliyo nayo katika sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Arusha kwamba kuhusu *subsector ya horticulture*, kwamba tuko kwenye hatua za mwisho na Wizara ya Fedha

na mashamba yale yatarudi na watawekeza Watanzania kwa *priority* na watapewa nafasi wawekezaji wa Kitanzania ili wawekeze katika *subsector* ya *horticulture*. *Subsector* ya *horticulture* ni sekta ambayo tunaipa jicho la karibu sisi kama Serikali kwa sababu ni sekta ambayo inakua na ni lazima tuendane na hali ya dunia inavyokwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba tunashukuru kwa maoni na tahadhari zilizotolewa. Niwahakikishie tu kwamba sisi upande wa Serikali, suala la majadiliano juu ya kuifanya Wizara ya Kilimo ipate fedha ya kutosha yameshafika katika nafasi nzuri na Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo. Tunafanya mazungumzo na Wizara ya Fedha ili Wizara hii iweze kupata fedha inazostahili kwenda kuwashudumia wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuhusu kilio cha mbolea na mwelekeo wa dunia unavyokwenda, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge hili litakuwa ni jambo la mwisho la kujadili katika nchi yetu. Ni lazima tu-*subsidize* kwenye *inputs* za kilimo, na huo ndio mwelekeo kwa sababu wakulima wetu ni wakulima wadogo; na hili tunalitengenezea *legal framework* na *financing model* ambayo tutakapoenda kutoa ruzuku basi ruzuku hiyo iweze kuwafikia wakulima, na tusifanye makosa ambayo tumekuwa nayo huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nimalizie kuwashukuru Kamati, na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maoni waliyoyatoa. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Kigahe, ajiandae Mheshimiwa Ndaki.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru sana na kukupongeza kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Naibu Spika wetu katika Bunge hili tukufu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara nipende kwa namna ya pekee kushukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Wajumbe wote kwa vile ambavyo wanatupa ushirikiano katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza mipango ya Serikali, na hivyo basi imekuwa desturi ya Kamati hii kutushauri kwa umakini mkubwa kwa nia ya kuhakikisha kwamba tunatekeleza masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inathamini sana ushauri wa Kamati hii, na tutandelea kufanya nao kazi kwa ukaribu kuhakikisha yale ambayo wanatuelekeza tunayatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tunaendelea kuptitia sera zetu, kuanzia Sera ya Uwekezaji, Sera ya Viwanda Vidogo (*SMEs*) na biashara ndogo na biashara ili ziendane na mazingira ya sasa ikiwa ni pamoja na kujumuisha vipaumbele na mipango ya maendeleo ya Taifa kwa ajili ya mabadiliko yanayoendelea katika dunia ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tunatekeleza mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunatekeleza *blue print*. Baadhi ya vitu ambavyo vimelalamikiwa sana ni kuwa na sehemu moja ya kuhudumia wawekezaji. Tanzania tunatengeneza sasa kitu inaitwa *Tanzania Electronic Investment a single window* ambayo hiyo itawezesha sasa wawekezaji kuwa na sehemu moja ambako watapata huduma nyingi ambazo zinatolewa na taasisi zetu. Kwa kuanzia tutaanza na *BRELA*, *TIC* na *TRA* ambazo zitaunganishwa pamoja katika mfumo huo ili kupunguza usumbufu kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunaendelea pia kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo kwa maana ya kuwa na kungani za viwanda ambazo zitasaidia sana, unajua sekta kubwa ya viwanda ni viwanda vidogo, vyakati, lakini pia hatusahau viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali tunaendelea kuhakikisha tunaweka mazingira wezeshi ili kuwe na ujenzi wa viwanda katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunaangalia pia kwa namna ya pekee kuona mifuko ya kuwezesha wajasiriamali inaongezewa fedha, lakini kuhakikisha pia inaboreshwu kwa kuunganishwa ile ambayo inawezekana ili iweze kuwa na tija kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa hili muhimu sana la utekelezaji miradi ya kimkakati ambayo imeongeleta sana. Nia ya Serikali hasa ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan, ameelekeza tuone sasa namna ya kukwamua miradi hii mikubwa ambayo itakuwa na *impact* kubwa sana katika maeneo ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie tutaenda kuishughulikia kwa haraka iwezekanavyo, lakini kwa kuangalia kwa weledi ili kuhakikisha tija na manufaa ya nchi nzima kwa kizazi hiki na vizazi vijavyo ili utajiri huu na maliasili hii tuliyonayo katika hii miradi ya kimkakati ambayo iko chini ya sekta hii ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inakuwa na tija kwa ajili ya maendeleo endelevu ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini pia nashukuru Kamati na Wabunge wote ambao wametushauri, ushauri wao tunaenda kuufanya kazi ili kuhakikisha tunaendelea kuhakikisha tunajenga uchumi wa viwanda kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ndaki, mjiandae watoa hoja.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kwa kura nydingi sana na Waheshimiwa Wabunge, ila nikutakie mema kwenye kazi zako kama Naibu Spika wa Bunge letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushauri wao na maelekezo yao mengi ambayo sio kwenye taarifa hii tumeyasikia, lakini pia kila wakati tunapokutana nao wanatupa maelekezo, wanatupa mapendekezo, wanatupa maoni ambayo ni ya kujenga kwa kweli, wao hawakai kwenye mstari wa kukosoa tu kama Serikali, lakini pia wanaonesha changamoto tulizonazo, lakini pia na kutuonesha njia ya kutoka kwenye hizo changamoto. Namshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati na Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa ambacho kimezungumzwa kwenye taaarifa ni upatikanaji wa fedha lakibi bajeti ya Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi. Nipende kukubaliana na maoni ya Kamati, kwamba inawezekana kweli hapa tunachangamoto kubwa lakini wote tumekwisha kusikia *commitment* ya Serikali kuhusiana na sekta hizi za uzalishaji, kilimo, mifugo, uvuvi, maliasili na sekta zinazozalisha. Tumemsikia Mheshimiwa Rais mwenyewe alipokuwa akihitubia Bunge kwamba tunataka kuangalia na kuona ni namna gani tunaziwezesha sekta hizi za uzalishaji ili ziweze kujikita sawasawa kwenye kuzalisha ajira, lakini kuzalisha mazao yale ambayo yanazalishwa na hizi sekta. Lakini pia Mheshimiwa Rais amerudia jambo hili tulipokuwa kwenye ziara pamoja naye Mkao wa Mara kwamba sasa ni zamu ya kuziangalia sekta hizi za uzalishaji kuona ni kwa namna gani zinapewa kipatumbele kibajeti ili ziweze kuzalisha na kutoa mchango wake unaotakikana kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi, pia tumekuwa na jithada hizo tukisaidiana kwa karibu sana na Wizara ya Fedha na Mipango. Hivi karibuni tumekwisha kupeleka maandiko yetu yote mawili la mifugo pamoja na andiko la uvuvi kuonesha ni kwa namna gani tunataka pesa kwenye *components* mbalimbali ili tukipatiwa zile pesa tuweze kuzalisha kwa wingi, tuweze kuzalisha ajira zinazotakiwa, lakini sekta hizi ziweze kutoa mchango wake mkubwa ambao kwa kweli unategemewa na Watanzania kwa ujumla.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaamini kama maandiko haya tuliyopeleka na tuliyoji-*engage* pamoja na Wizara ya Fedha yatakapopita, tunaamini mchango wa sekta yangu ya Mifugo na Uvuvi itaweza kutoa mchango wake unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna maeneo mengi ambayo nisingependa kuyataja hapa ambayo tumeyaainisha kwa upande wa mifugo, lakini pia hata upande wa uvuvi tumeainisha na baadae kukubaliana na hivi karibuni tu kuna dalili njema sana kuhusiana na malisho ya mifugo yetu, Serikali ya China iko tayari na imekwisha iko kwenye hatua za mwisho kutupatia dola za Kimarekani milioni tatu kwa ajili ya malisho ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huo ni mfano mmoja tu wa jambo ambalo tayari Wizara ya Fedha na sisi tumeji-*engage* pamoja na kwamba kuna dalili nzuri ya jambo hilo kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia bado kuna mambo yanayohusiana na mabwawa, bado kuna mambo yanahusiana na maji, na suala la maji pia bado tuna *engage* pamoja na Wizara ya Maji, kwa sababu na wenyewe wana fedha za maji, lakini sisi pia tunatafuta fedha za maji pamoja na kwamba tumeshauriwa na Bunge lako kwamba angalau kuwe na namna ya kupanga pamoja, lakini tunakaa pamoja na Wizara ya Maji ili kwamba miradi yetu ya maji iliyopo Wizara ya Mifugo na itakayokuwepo Wizara ya Maji isiweze kuingiliana au tusiweze kuiweka mahali pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali iko na *commitment* ya kutosha kuhusiana jambo la kubajeti kuhusiana na sera hizi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha malizia malizia sekunde kumi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana, lakini nilihakikishie tu Bunge lako kwamba Serikali imekwisha kuona kwamba kuna haja ya kuongeza bajeti kwenye sekta hizi za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kihenzile. (*Makof*)

MHE. DAVID M. KIHENZILE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja ya Kamati yangu, lakini na mimi niungane na Wabunge wenzangu kukupongeza kwa ushindli mkubwa uliouopata kwa nafasi ya Naibu Spika wetu. (*Makof*)

Niwapongeze na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia kwenye hoja yangu, kwa uchache Mheshimiwa Cecil Mwambe, *Engineer Ezra Cheweleesa*, Mheshimiwa Maryam Omar Said, Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mheshimiwa Juma Usonge, Mheshimiwa Humphrey Polepole, Mheshimiwa Neema Lugangira, Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Exaud Kigahe, Mbunge na Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Mheshimiwa Dkt. Suleiman Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja mbalimbali zimezungumzwa katika kuchangia kwenye hoja zetu, lakini pamoja mambo mengine kwa kirefu sana imezungumziwa hoja ya Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hoja zingine tunaamini Serikali imechukua na kwa uzito mkubwa itakwenda kufanya kazi hoja hizo kwa maslahi makubwa ya Watanzania. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kukubali maoni ya Kamati yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

NAIBU SPIKA: Mwenyekiti hongera. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. (*Makof*)

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kwa mara nyingine ya pili nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kupata nafasi hiyo, nakutakia majukumu mema. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yetu ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao yapata kama Wabunge tisa ambao wamechangia. Pia nawapongeza Mawaziri ambao wametoa ufanuzi, Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Ndaki bila kumsahau Mheshimiwa Aweso ambaye na yeye yuko kwenye Kamati yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio lazima wote niwataje majina ila Mheshimiwa Profesa Muhongo, Mheshimiwa Profesa Manya, Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, Mheshimiwa Kunti, Mheshimiwa Mwijage; na Mheshimiwa Polepole amepongeza na yeye kuwa mapendekezo yote yaliyopendekezwa na Kamati yaweze kuchukuliwa. Mheshimiwa Neema Lugangira na yeye kwa sababu usalama wa chakula ni mtambuka uko pia kwenye upande wa kilimo,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa hiyo na yeye amechangia pamoja na Mheshimiwa Nusrat amesema ubunifu kwenye sayansi na hasa tunaposema kuwa ubunifu wa chakula, Mheshimiwa Gambo kwenye upande wa ajira ambao ni llani ya Chama cha Mapinduzi, pamoja na mambo ya maua tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yaliyoongeleta sana ni mengi ya kuhusu Tume ya Umwagiliaji, mambo ya pembejeo na mambo mengine yote yaliyoongeleta. Nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri kama mmekubali kuwa mtachukua ushauri wetu na mapendekezo yetu na tumekuwa pamoja, naamini tutaendelea vizuri kama tulivyokuwa tunaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yetu yote iweze kuungwa mkono na mapendekezo yote pamoja na Wabunge wote waliomo humu ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja ya Kamati. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, toa hoja.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Wanaoafiki taarifa ya Kamati.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

NAIBU SPIKA: Wote mmeafiki hakuna aliysema siyo. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru tena kuwa na imani na mimi, naishukuru Kamati kwa kazi nzuri mlizofanya, naishukuru Serikali na Mawaziri wote kwa majibu mazuri, majibu ya imani, majibu ambayo nchi yetu itakwenda mbele na kwa muda mfupi sana itafikia malengo ambayo tunataka tuyafikie kabla ya 2025.

Baada ya maneno hayo, naahirisha Kikao hiki mpaka Jumatatu saa nane mchana.

*(Saa 12:30 Jioni Bunge Lillahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 14 Februari, 2022 Saa Nane Mchana)*